Kiswahili

Shule za Sekondari

Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita

Fasihi



Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kiswahili

Shule za Sekondari

Kitabu cha Mwanafunzi

Kidato cha Tano na Sita

Fasihi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita - Fasihi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-024-2

Taasisi ya Elimu Tanzania

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN 978-9987-09-024-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar-es-Salaam

Simu: +255-22-2773005/ +255 22 2771358
Faksi: +255-22-2774420
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Dibaji

Kitabu hiki cha *Kiswahili Kidato cha Tano na Sita Fasihi* kina jumla ya sura tano. Sura hizo ni Fasihi kwa ujumla, Maendeleo ya fasihi simulizi, Maendeleo ya fasihi andishi, Uhakiki wa fasihi, na Usanifu wa maandishi.

Kitabu hiki kimezingatia muhtasari wa somo la Kiswahili Kidato cha Tano na Sita wa mwaka 2009. Mada zote zimeandikwa kwa kina na zinamshirikisha mwanafunzi kikamilifu. Kuna mazoezi ya kutosha kila mwisho wa mada ndogo na maswali ya marudio kila mwisho wa mada kuu. Maswali ya mazoezi na maswali ya marudio yameandaliwa kwa lengo la kumfikirisha na kumjengea mwanafunzi umahiri katika somo. Hali kadhalika, lugha iliyotumika katika kitabu hiki ni rahisi na itakayomwezesha mwanafunzi kujifunza somo la Fasihi vizuri.

Taasisi ya Elimu Tanzania

For Online Use Only

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

Waandishi: Prof. Mugyabuso M. Mulokozi, Dkt. Janeth Barongo, Dkt. Rehema Stephano, Dkt. Edith B. Lyimo, Mwl. Lameck E. Mpalanzi, Mwl. Saumu L. Mahanda, Mwl. Amani Mgheni & Mwl. Adelgot J. B. Mapunda

Wahariri: Prof. Fikeni M.E.K Senkoro, Dkt. Shani Omari & Dkt. Athumani S. Ponera (Mwenyekiti wa jopo)

Msanifu: Bi. Rehema H. Maganga

Wachoraji: Alama Art and Media Production Co. Ltd.

Mratibu: Mwl. Adelgot J. B. Mapunda

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandishi wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 4 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Yaliyomo

Ukurasa

Dibaji iii

Shukurani iv

Orodha ya vielelezo vii

Vifupisho viii

Sura ya Kwanza: Fasihi kwa ujumla 1

Mitazamo ya fasihi 1

Dhana ya sanaa 3

Usanaa wa fasihi 4

Aina za fasihi 6

Dhima za fasihi 8

Chimbuko la fasihi 12

Maendeleo ya fasihi katika mifumo ya maisha ya jamii 14

Uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi 17

Udhamini 20

Athari za udhamini 23

Uandishi wa kazi za kifasihi 25

Sura ya Pili: Maendeleo ya fasihi simulizi 31

Dhana ya fasihi simulizi 31

Tanzu za fasihi simulizi 31

Utunzi wa kazi za fasihi simulizi 64

Athari za sayansi na teknolojia katika fasihi simulizi 71

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 5 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tatu: Maendeleo ya fasihi andishi 74

Dhana ya fasihi andishi 74

Maendeleo ya fasihi andishi kabla ya uhuru 74

Maendeleo ya fasihi andishi baada ya uhuru 77

Tanzu za fasihi andishi 79

Sura ya Nne: Uhakiki wa kazi za fasihi 114

Uhakiki wa kazi za fasihi 114

Dhana ya uhakiki 114

Dhima za mhakiki wa kazi za fasihi..115

Uhusiano wa fani na maudhui 117

Sura ya Tano: Usanifu wa maandishi 172

Usanifu wa maandishi... 172

Mambo ya kuzingatia wakati wa kutathimini maandishi 172

Tathimini ya matini 175

Faharasa 184

Marejeleo teule 190

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 6 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Orodha ya vielelezo

1.1 Maumbo ya sanaa 3

2.1 Tanzu na vipera vya fasihi simulizi 32

3.1 Tanzu na vipera vya fasihi andishi 79

4.1 Vipengele vya uhakiki 143

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 7

17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vifupisho

BAKITA	-	Baraza la Kiswahili la Taifa
DUP	-	Dar es Salaam University Press
EAEP	-	East African Education Publishers
EALB	-	East African Literature Bureau
EAPH	-	East Africa Publishing House
EPD	-	Educational Publishers and Distributors Ltd
ITV	-	Independent Television
KAUTTU	-	Kampuni ya Utamaduni Tafsiri na Uchapishaji
Kur	-	Kurasa
MEP.	-	Mture Educational Publishers Ltd
Mf.	-	Mfasiri
Mh.	-	Mhariri
Mhe.	-	Mheshimiwa
MPP	-	Moccony Printing Press
OUP	-	Oxford University Press
S.P.C.K	-	Society for the Promotion of Christian Knowledge
TATAKI	-	Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili
TBC	-	Tanzania Broadcasting Corporation
TET	-	Taasisi ya Elimu Tanzania
THT	-	Tanzania House of Talent
TPH	-	Tanzania Publishing House
TUKI	-	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UKIMWI	-	Upungufu wa Kinga Mwilini
UKUTA	-	Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania
UWAVITA	-	Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania
Wah.	-	Wahariri

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 8
17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Kwanza

Fasihi kwa ujumla

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza juu ya mitazamo ya fasihi, dhana ya sanaa, usanaa wa fasihi, aina, dhima na chimbuko la fasihi. Vilevile, utajifunza kuhusu maendeleo ya fasihi katika mifumo ya maisha ya jamii, uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi, dhana ya udhamini, aina, sababu na athari za udhamini. Aidha, utajifunza juu ya uandishi wa kazi za kifasihi.

Mitazamo ya fasihi

Dhana ya fasihi ni pana. Dhana hii imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kupitia mitazamo mbalimbali. Tunaweza kuigawa mijadala hiyo katika mitazamo mitano kama ifuatavyo:

Mtazamo wa kwanza unadai kuwa fasihi ni jumla ya maandishi yote katika lugha fulani. Mtazamo huu umeelezewa na Wellek na Warren (1986) wakisema kuwa njia mojawapo ya kuielezea fasihi ni kuichukulia kuwa ni jumla ya machapisho yote.

Changamoto ya mtazamo huu ni kuupanua mno uwanja wa fasihi na kujumuisha dhana ambazo si za kifasihi. Kwa mtazamo huu, maandishi yoyote, yakiwamo matangazo ya biashara, mafunzo ya historia, jiografia ama sayansi, yanaweza kujumuishwa humo. Aidha, mtazamo huu unabagua fasihi simulizi ambayo kimsingi haipo katika maandishi.

Mtazamo wa pili unadai kuwa fasihi ni hisi ambazo zinajifafanua kwa njia ya lugha. Wafuasi wa mtazamo huu ni John Ramadhani (1973), May Balisidya, (1973) Tigiti Sengo na Saifu Kiango (1973). Hawa wanadai kuwa lazima pawe na mguso ndipo mwanafasihi aweze kuandika au kueleza jambo kifasihi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 1 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wataalamu hao wanasema kuwa, hisi ni kama kuhisi njaa, baridi, joto, uchovu au kuumwa. Wataalamu kama vile Mugyabuso Mulokozi (2017) wanaeleza kuwa, mtazamo huu unachanganya mambo matatu ambayo ni fasihi yenyewe, mambo yaelezwayo na fasihi, na mtindo wa kifasihi.

Changamoto ya mtazamo huu ni kwamba, fasihi inaweza kuelezea hisi, kupitia mtindo wa fasihi, lakini fasihi yenyewe si hisi. Aidha, fasihi huweza kuelezea mapenzi lakini fasihi yenyewe si mapenzi.

Mtazamo wa tatu unaitazama fasihi kama sanaa ya lugha yenye ubunifu bila ya kujali kama imeandikwa au la. Mtazamo huu unaafikiwa na Peter Kirumbi (1975), Aldin Mutembei (2006) na F.E.M.K Senkoro (2011). Kwa mujibu wa mtazamo huu, hata nyimbo na masimulizi ya kisanaa ni fasihi, ijapokuwa hayakuandikwa. Kwa mfano, Kirumbi anasema kuwa fasihi ni taaluma ya sanaa inayowasilishwa kwa njia ya lugha katika muundo wa maandishi au matamshi. Mtazamo huu ndio unaotawala katika taaluma ya fasihi. Inadaiwa kuwa neno fasihi limetokana na neno "*fasuh*" la Kiarabu lenye maana ya ufasaha au uzuri wa lugha. Hivyo, istilahi "fasihi" katika taaluma ya Kiswahili inatofautiana na istilahi ya "*literature*" inayotumika katika Kiingereza. Kwa sababu hii, neno fasihi halihusiani na maandishi wala vitabu, bali linahusiana na ufasaha wa kauli. Hivyo, dhana hii katika Kiswahili inazingatia aina zote za fasihi, yaani fasihi simulizi na andishi. Mtazamo huu umehusisha fasihi na sanaa itumiayo lugha ya maandishi au mazungumzo. Hata hivyo, tatizo lake ni kutokuonesha uhusiano wa fasihi na jamii.

Mtazamo wa nne unadai kuwa fasihi ni maandiko bora ya kisanaa yenye manufaa ya kudumu. Akizungumzia mtazamo huu, Hollis Summers (1989) anasema kuwa fasihi ni sanaa inayojumuisha zaidi maneno yaliyoandikwa. Mtazamo huu unaupa uzito ufundi wa kubuni lakini unafinya mawanda ya fasihi kwa kuhusisha mawazo yaliyo bora tu.

Mtazamo wa tano unaona kuwa fasihi ni tokeo la matumizi ya lugha kwa njia isiyo ya kawaida ili kuleta athari maalumu. Kwa mujibu wa Mugyabuso Mulokozi (2017), waasisi wa mtazamo huu ni Roman Jakobson, Boris Tomashevsky na Viktor Shklovsky. Kwa maelezo ya wataalamu hawa, fasihi hukiuka taratibu za kawaida za matumizi ya lugha katika sarufi, maana na sauti ili kumvutia na kumuathiri msikilizaji au msomaji.

Changamoto ya mtazamo huu ni kuwa humfanya msomaji aitafakari lugha yenyewe badala ya kuutafakari ujumbe unaowasilishwa na lugha hiyo. Vilevile, fasihi inaonekana kuelemea zaidi upande wa fani na kupuuza maudhui, maana na muktadha wa kazi za fasihi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 2 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa ujumla, mijadala hii inaonesha kuwa kila mtazamo una ubora na udhaifu wake. Mitazamo hiyo inaeleza kwamba fasihi ni sanaa itumiayo lugha kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Zaidi, inaonesha kwamba kuna aina mbili za fasihi kutokana na namna ya uwasilishaji. Aina hizo ni fasihi simulizi na fasihi andishi. Kimsingi, fasili hizi zote zinahusisha fasihi, maisha na jamii. **Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiufundi kuwasilishia masuala mbalimbali yanayomhusu mwanadamu na maisha yake.** Tunaposema "lugha" hatuna maana ya usemaji wa kutumia sauti tu, bali hata mawasiliano ya kutumia ishara na vitendo. Kwa kuwa neno sanaa limejitokeza katika fasili za fasihi, ni vyema tukajua maana ya sanaa.

Dhana ya sanaa

Sanaa ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililosanifiwa, umbo ambalo msanii hulitumia katika kuelezea hisia zinazomgusa kwa kutoa kielelezo au vielelezo vyenye dhana maalumu. Sanaa ni matokeo ya kazi za mikono na akili ya mtu, nayo, aghalabu, huwa na umbo dhahiri lenye maana au dhana maalumu. Sanaa huweza kutokana na mwigo ambao hujengwa na kanuni au mbinu za uzuri na hata ubaya. Sanaa hujitokeza katika maumbo tofautitofauti kama inavyoonekana katika kielelezo kifuatacho:



Kielelezo namba 1.1 Maumbo ya sanaa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 NA 6 (KIWANDANI).indd 3
17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maumbo haya ya sanaa yanaweza kuwekwa katika makundi makuu matatu ambayo ni sanaa za uonesho, sanaa za ghibu na sanaa za vitendo (Penina Muhando na May Balisidya, 1976). Ufuatao ni ufafanuzi mfupi wa makundi hayo:

(a) ***Sanaa za uonesho:*** Ni sanaa ambazo uzuri wake hujitokeza katika umbo la kudumu, umbo ambalo linaweza kuhifadhiwa na uzuri wake ukaoneshwa muda wowote. Sanaa hizi ni kama vile ufinyanzi, uchoraji, utarizi, ususi, uchongaji na ufumaji.

(b) ***Sanaa za ghibu:*** Ni sanaa ambazo uzuri wake umo katika ufundi wa kutumia lugha kiasi cha kugusa hisia za mtu. Uzuri wa uimbaji au upigaji muziki na usimuliaji au usomaji wa fasihi umo katika hisia. Kwa mfano, msikilizaji anaposikia sauti tamu za wimbo, shairi au muziki, au kusoma kazi ya kisanaa hupata hisia au msisimko utakaomwezesha kupata yale yaliyokusudiwa na msanii. Aina hii ya sanaa hujumuisha kazi zote za fasihi, kama vile ngano, riwaya, ushairi na tamthiliya.

(c) ***Sanaa za vitendo***: Ni sanaa ambazo uzuri wake umo katika matendo. Msanii hana budi kuonesha matendo ya jambo alilokusudia au analokusudia mbele ya hadhira yake. Pia, hadhira sharti iwepo ili kushuhudia uzuri wa sanaa husika. Ili sanaa nyingi za aina hii zikamilike, huhitaji dhana inayotendeka, jukwaa, hadhira na wahusika.

Kwa mantiki hiyo, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya sanaa za uonesho, za ghibu na za vitendo. Sanaa zote zina dhima mbalimbali katika maisha ya mwanadamu. Mifano ya dhima hizo ni kuburudisha, kuelimisha, kukosoa na kuadibu. Vilevile, kumsaidia mwanadamu huyo kupambana na mazingira yake kwa njia ya ubunifu.

Usanaa wa fasihi

Usanaa wa fasihi hujitokeza katika vipengele vifuatavyo:

(a) Mtindo

Katika fasihi, sanaa hujionesha katika namna ya kueleza jambo. Jambo linaweza kuelezwa kwa mkato. Aghalabu, methali nyingi hutolewa kwa lugha ya mkato. Kwa mfano, "Mla ni mlaleo, mla jana kala nini? /alileni?" *Alileni* ni alikula nini? Methali hii imefupisha taarifa ambayo ingeweza kutolewa hivi, mtu anayekula leo ndiye mlaji wa kweli, aliyekula jana hajulikani. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba mtu mwenye uwezo au mali leo ndiye atakayeheshimiwa wala si yule aliyekuwa na uwezo au mali jana.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 4 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Muundo

Kazi ya fasihi hupangiliwa katika muundo maalumu ili iweze kuwasilishwa vyema kwa jamii husika. Kila utanzu wa fasihi una muundo wake. Kwa mfano, shairi la kimapokeo huundwa na vipande, mishororo, beti, urari wa vina na mizani. Aidha, utanzu kama vile methali huundwa na pande mbili; upande wa kwanza huanzisha kauli na upande wa pili hukamilisha kauli hiyo. Pande hizi hutegemeana na kukamilishana. Muundo ndio unaotoa umbo au sura ya kazi husika.

(c) Matumizi ya lugha

Kazi za fasihi huwasilishwa kwa lugha ya kisanaa. Lugha ya kisanaa ni ile ambayo husheheni vipengele kama vile nahau, misemo, methali, tamathali za semi, taswira na picha mbalimbali. Lugha ndio msingi wa fasihi; bila lugha hakuna fasihi. Hii yatokana na ukweli kuwa lugha hutumika kiufundi kuunda vipengele vingine vya kazi ya fasihi kama vile wahusika, mandhari, dhamira na matukio. Matumizi ya lugha ya kisanaa huibua hisia za hadhira. Hivyo, lugha inatakiwa kutumika ipasavyo katika kazi za fasihi ili kufanikisha dhima hii ya kuwa kiungo muhimu.

(d) Wahusika

Katika fasihi, wahusika ni vitu, watu au viumbe wengine waliokusudiwa kuwasilisha dhana, mawazo au tabia za watu. Usawiri wa wahusika na majukumu ya uhusika wao hufanywa katika namna inayoleta mvuto wa kisanaa. Kwa mfano, wahusika wasio binadamu kama vile mti au sungura wanapopewa uwezo wa kuongea huleta mvuto wa namna fulani.

(e) Mandhari

Mandhari ni dhana inayorejelea mahali na wakati kazi ya fasihi inapotendeka. Hiki ni kipengele cha kisanaa kwa sababu kinadokeza muktadha wa utokeaji au utendekaji wa tukio la kifasihi. Uteuzi na uumbaji wa mandhari hufanywa kwa ufundi; hivyo, kutoa mchango mkubwa katika kujenga mvuto wa kazi. Kazi za fasihi huweza kutumia mandhari halisi au za kubuni. Kwa mfano, riwaya za *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971), *Utubora Mkulima* (Shaaban Robert, 1968) zimetumia mandhari halisi; ilhali riwaya za *Kufikirika* (Shaaban Robert, 1967) na *Ziraili na Zirani* (William Mkufya, 1999) zimetumia mandhari ya kubuni.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 5 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) **Uwasilishaji**

Uwasilishaji wa kazi za fasihi hufanywa kwa njia ya mdomo, vitendo au maandishi. Uwasilishaji huo hufanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile mpangilio wa matukio, ucheshi, na taharuki ili kuleta mvuto katika kazi husika. Mbinu nyingine katika fasihi simulizi huhusisha namna ya utamkaji wa maneno na sentensi, uchezaji, matumizi ya viungo vya mwili, matumizi ya ala mbalimbali, matumizi ya maleba, uigizaji, kubadili muundo wa simulizi, pamoja na uhusishaji wa kazi husika na miktadha iliyo karibu na ufahamu wa hadhira. Katika kazi za fasihi andishi, ufundi wa uwasilishaji hufanywa kwa kutumia mbinu kama vile uumbaji wa wahusika, matumizi ya lugha na uumbaji wa mandhari.

Aina za fasihi

Fasihi simulizi

Hii ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya mdomo. Fasihi simulizi ina umbo maalumu, kwa wakati maalumu, kwa kuzingatia misingi mbalimbali ya tanzu ziundazo aina hii ya fasihi. Aidha, ni tukio ambalo huambatana na mwingiliano wa mambo manne ambayo ni dhana, muktadha, watu na mahali. Mambo haya ndiyo yanayoamua fani ya fasihi simulizi ichukue umbo lipi, iwasilishwe vipi, kwa hadhira gani, kwa wakati na mahali gani. Kwa mfano, hadithi inaweza kugeuzwa wimbo na utendi unaweza kuwa hadithi, kutegemea dhana inayowasilishwa katika muktadha, watu na mahali. Maelezo zaidi kuhusu fasihi simulizi yatatolewa katika sura ya pili katika mada ya maendeleo ya fasihi simulizi.

Fasihi andishi

Fasihi andishi ni aina ya fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi. Msingi mkuu wa fasihi andishi ni mwandishi kwani ndiye anayetunga na kuandika kiubunifu kazi ya fasihi. Maelezo zaidi kuhusu fasihi andishi yatatolewa Sura ya Tatu katika mada ya maendeleo ya fasihi andishi.

Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Fasihi simulizi na fasihi andishi huingiliana na kutofautiana katika vipengele mbalimbali. Wakati mwingine fasihi andishi huweza kutendwa kama fasihi simulizi, kwa mfano tamthiliya na mashairi. Tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi huweza kuoneshwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo kama vinavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 6 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jedwali **Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi**

Na.	Kigezo	Fasihi simulizi	Fasihi andishi
1.	Utunzi	Huweza kutungwa mapema na kukaririwa kabla ya uwasilishaji. Huweza pia kutungwa papo kwa papo wakati wa utendaji.	Hutungwa kwa kipindi kirefu kabla ya kuwasilishwa kwa hadhira.
2.	Uwasilishaji	Huwasilishwa kwa njia ya mdomo, ishara na vitendo. Uwasilishaji huo hutumia viambato kama vile maleba, miondoko na sauti.	Huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
3.	Umri	Ni kongwe kwa sababu ilianza kabla ya ugunduzi wa maandishi.	Ilianza baada ya mwanadamu kugundua maandishi.
4.	Umiliki	Tanzu nyingi za fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima.	Ni mali ya mtunzi na mdhamini wake.
5.	Uhifadhi	Huhifadhiwa kichwani na kuendelezwa kwa njia ya kupokezana, ijapokuwa kutokana na maendeleo ya teknolojia, huweza kuhifadhiwa katika vinasa sauti, kompyuta na hata maandishi	Huhifadhiwa katika nyaraka au kwa njia za kidijiti.
6.	Tanzu na vipera	Idadi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi ni kubwa kuliko ilivyo katika fasihi andishi. Aidha, huwa na mwingiliano mkubwa wa vipera.	Idadi ya tanzu na vipera vya fasihi andishi ni ndogo. Aidha, vipera vyake havina mwingiliano mkubwa.
7.	Mabadiliko	Hubadilika kwa haraka kutegemeana na mahitaji ya hadhira, tukio la kijamii na wakati.	Haibadiliki kwa haraka kwa sababu ipo katika hali ya kudumu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI f.5 & 6 (KIWANDANI).indd 7 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8.	Hadhira	Hadhira hai ambayo hushiriki katika utendaji kama kuitikia, kupiga vigelegele na makofi).	Ni wasomaji; hivyo hawashiriki katika utendaji, isipokuwa katika tanzu chache zinazowasilishwa kiutendaji kama vile mashairi na tamthiliya.
9.	Wahusika	Hutumia wahusika mchanganyiko (kwa mfano binadamu, wanyama, mimea na vitu visivyo na uhai).	Hutumia zaidi wahusika binadamu. Wahusika wasio binadamu hutumika mara chache.
10.	Muundo	Huwa na muundo wa moja kwa moja aghalabu bila utata.	Huweza kuwa na muundo wa moja kwa moja au changamani kutegemeana na utanzu.

Dhima za fasihi

Fasihi ina dhima mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kuelimisha jamii

Kazi kubwa ya fasihi ni kuelimisha jamii. Fasihi huufumbua macho umma na kupiga vita mazingira ya njaa, maradhi, umaskini na matatizo mengine. Aidha, fasihi huipa jamii maarifa na stadi za kukabiliana na mazingira ambamo jamii inaishi. Kwa mfano, wimbo wa "Kachiri" humfundisha mtoto wakike kustahimili shida wakati mumewe anaposafiri:

Kachiri

Kachiri kachiri *saga*
Mume wangu kasafiri *saga*
Kaniachia ukili *saga*
Upatao pima mbili *saga*
Na kipande cha hariri *saga*
Kachiri *saga*
kachiri *saga*

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 8 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kuburudisha jamii

Dhima nyingine ya fasihi ni kuburudisha jamii. Katika kutimiza jukumu hili, fasihi hustarehesha, huliwaza na kutuliza mwili na akili ya hadhira. Kwa mfano, watu wanapotazama vichekesho na maigizo ya "Mizengwe" (katika ITV Tanzania) hufurahia vituko, kejeli na mizaha inayoigizwa.

(c) Kuadibu na kunasihi jamii

Mara nyingi, kazi za fasihi hutumika katika kuasa na kuadibu kuhusu mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Kwa mfano, tamthiliya ya *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (Edwin Semzaba, 1988) inawaadibu na kuwaasa watu kufanya kazi kwa nidhamu. Kwa ufupi, tamthiliya hiyo inatoa funzo kwamba mtaka yote kwa pupa, hukosa yote. Katika fasihi simulizi, nyimbo hutumika kukamilisha jukumu hili. Kwa mfano, wimbo wa *bongo fleva* wa Naseeb Abdul (maarufu kama Diamond) uitwao "Nitarejea." Ifuatayo ni sehemu ya wimbo huo:

Aah vipi mizigo umeweka tayari? ii ihii,
Nisije chelewa nikaachwa na gari, aa ahaa,
Basi jikaze usilie mpenzi, aahaa,
Mimi nitarudi niombee kwa Mwenyezi, aahaa,
Zile taabu na njaa msimu mzima mavuno hakuna,
Huwa nakosa raha mkikosa cha kutafuna,
Roho yangu inauma sana, sema nitafanya nini fedha sina aaahaa,
Nakuonea huruma, bora niende mjini kusaka chuma aaahaa.

Kiitikio:
Kama mtoto akinililia, mwambie kesho nitarejea x2
Wadanganye na vibagia, waambie pipi nitawaletea,
Na usichoke kuvumilia, na kila siku kuniombea.

Katika wimbo huu, mume anamnasihi mkewe avumilie na awalee watoto vizuri wakati yeye (mume) akiwa katika pilikapilika za kusaka maisha.

(d) Kutia hamasa jamii

Fasihi hutia hamasa kuhusiana na mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii. Mathalani, riwaya ya *Pepo ya Mabwege* (Harrison Mwakyembe, 1980) inatia hamasa kwa vijana, kusimamia kile wanachokiamini. Mhusika Kalenga alisimama kidete kufichua uozo uliomo kwenye jamii na, hatimaye, alipandishwa cheo kutokana na kazi nzuri aliyoifanya. Vilevile, kazi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 9 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nyingine za fasihi kama nyimbo zimekuwa zikitumika kutia hamasa. Wimbo wa "Gezaulole" ulioimbwa na bendi ya Urafiki Jazz ulikuwa unahamasisha wanajamii waishio mijini bila kazi kuhamia vijijini ili kujishughulisha na kilimo. Katika kipindi cha miaka ya 1970 kilimo kilionekana kuwa ndio uti wa mgongo wa maisha na kwamba kila mtu anaweza kulima.

(e) Kukomboa jamii

Dhima nyingine ya fasihi ni kupiga vita mambo mbalimbali yanayokwamisha maendeleo ya jamii kama vile ujinga, maradhi na umaskini. Tamthiliya ya *Hawala ya Fedha* (Amandina Lihamba, 1985), kwa mfano, inaeleza mambo yanayosababisha umasikini ambayo ni ujinga na uvivu. Aidha, wakati wa harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika, bendi za muziki zilipiga nyimbo za kuwaunganisha watu kwa ajili ya ukombozi. Wimbo mmojawapo ni "Mwenyekiti Mwalimu Nyerere" ulioimbwa na bendi ya Urafiki Jazz miaka ya 1970. Ufuatao ni wimbo huo:

Mwenyekiti wa nchi tano zilizo mstari wa mbele,
Tunakuomba uzidishe mapambano ya Kusini mwa Afrika,
Kwani, maadui wa Afrikaaa wanalisumbua sana bara letu hili la Afrika,
Rais Kaunda na Samora wa Msumbiji, Seretse Khama, na Neto wa Angola, tunawaambia *aluta continua.*

Kiitikio:
Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere Baba, imarisha ukombozi wa Afrika x2

Uhuru wetu hauwezi kuwa safi mpaka Afrika yote imekuwa huru, Mwalimu eeh!

Kiitikio:
Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere Baba, imarisha ukombozi wa Afrika x2

Maadui wa bara la Afrika wameanza kuwahujumu viongozi, Mwalimu eeh!

Kiitikio:
Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere Baba, imarisha ukombozi wa Afrika x2

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 10 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Murtala Mohammed wa Nigeria na Marien Nguabi wa Kongo wamepotea, Mwalimu eeh!

Kiitikio:
Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere Baba, imarisha ukombozi wa Afrika x2.

Uhuru wetu hauwezi kuwa safi mpaka Afrika yote imekuwa huru, Mwalimu eeh!

(f) Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii

Fasihi husaidia kutunza amali na kumbukumbu nyingine za jamii. Mifano ya amali hizo za kijamii ni mila, desturi, historia na sanaa. Tamthiliya za Kiswahili kama vile *Kinjekitile* (Ebrahim Hussein, 1969) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Emmanuel Mbogo, 1988) zimebeba vyema jukumu hili la kuhifadhi na kurithisha amali za jamii. Pia, zinafafanua masuala ya kijadi kama vile imani, uganga na uchawi.

(g) Kukosoa jamii

Fasihi ina dhima ya kukosoa jamii katika mambo mbalimbali ya maisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufikirika* (Shaaban Robert, 1967) mwandishi anakosoa tabaka tawala linalotumia rasilimali nyingi kwa manufaa ya watu wachache ilihali wanajamii wengine wanateseka. Hali kadhalika, methali katika fasihi hutumika kukosoa au kuonya jamii. Methali kama vile "Mkataa pema, pabaya panamwita" inakosoa mtu anayekataa wosia mzuri kwani kuna madhara yanaweza kumpata. Aidha, methali kama "Tamaa mbele, mauti nyuma" imekusudiwa kuwaonya wanajamii kuwa mtu mwenye tamaa anaweza kukabiliwa na madhara.

(h) Dhima ya kifalsafa

Falsafa ni mwelekeo wa kimawazo ambao unadhihirika katika kazi ya kifasihi. Kwa hiyo, falsafa ni busara ya kimawazo iliyofikiwa baada ya mtu au watu kutafakari kwa kina kuhusu maisha na masuala ya kiulimwengu. Mathalani, falsafa huuliza maswali kama ifuatavyo: Kwa nini tupo duniani? Kwa nini tunakufa? Hatima ya maisha ni nini? Ulimwengu ulitoka wapi na hatima yake ni nini? Je, kuna Mungu? Kwa jicho la kifalsafa, fasihi huwachochea wasomaji au wasikilizaji kuyatafakari masuala hayo kwa umakini zaidi. Katika fasihi ya Kiswahili, baadhi ya kazi za kifalsafa ni

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 11 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nagona (1990) na *Mzingile* (1991) zote za Euphrase Kezilahabi na *Bin-Adamu* (Kyallo Wamitila, 2002).

(i) **Kukuza na kuhifadhi lugha**

Kutokana na ukweli kwamba fasihi hutumia lugha, lugha haiwezi kudumaa kwa sababu inakuwa kwenye matumizi. Mwanafasihi hutumia maneno kuibua na kueleza dhana mbalimbali katika utunzi wa kazi zake. Uandishi wa kazi za fasihi huibua misemo mipya mara kwa mara; kwa njia hii lugha huweza kukua. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika* (Shaaban Robert, 1951) kuna uibuaji wa msamiati kama vile 'ali ali' (tukufu) 'azali' (asili au kiini) 'kitali' (mapigano) na 'mlizamu' (chemchem).

Ingawa fasihi ina dhima hizi chanya tulizozieleza, huweza kuwa na dhima hasi kwa baadhi ya watu na nyakati. Hii ni kwa kuwa fasihi ni zao la harakati na mivutano ya kijamii. Aidha, huweza kutumiwa na dola au kundi moja kukandamiza au kudhalilisha kundi jingine. Kwa mfano, fasihi ya wakoloni iliyofasiriwa kwa Kiswahili ilikuwa inahalalisha ukoloni kwa kumkweza Mzungu na kumtweza Mwafrika. Mifano ya kazi hizo ni *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Ridder Haggard, 1929) na *Allan Quartermain* (Ridder Haggard, 1934). Zipo pia kazi za fasihi zinazosifia na kutukuza wauaji na madikteta badala ya kuwakemea.

Chimbuko la fasihi

Kuna mitazamo miwili inayohusu chimbuko la fasihi: mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu.

(a) **Mtazamo wa kidhanifu**

Msingi wa mtazamo huu ni mawazo ya kudhani yasiyotokana na uhalisi. Waasisi wa mtazamo huu ni wanafalsafa wa Kiyunani wakiwamo Plato na Sokrate. Waasisi wa mtazamo huu wanaamini kuwa fasihi na sanaa vimetoka kwa Mungu. Hivyo, mwanafasihi huipokea sanaa ikiwa tayari imeivishwa na Mungu. Wachambuzi wengine wenye mtazamo wa kidhanifu ni Felician Nkwera na John Ramadhani.

Katika insha yake kuhusu fasihi, Felician Nkwera (1976) anasema "Fasihi ni sanaa ambayo huanzia kwa Muumba, humfikia mtu katika vipengele mbalimbali... (ni) hekima ambayo mtu ameshirikishwa apate kumtambua

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 12 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muumba wake". Akiunga mkono mtazamo huu, Ramadhani (1975) anadai kwamba, ingawa fasihi ni hisi, kitendo cha mtu kuibuni kazi ya sanaa ni uigaji wa Mungu ambaye ndiye mfalme wa sanaa zote. Mawazo ya wanafalsafa wa mtazamo huu hayana uthibitisho wowote zaidi ya kumtenga msanii na jamii yake kwa kumkweza na kuonekana yuko karibu na Mungu kuliko wanajamii wengine. Aidha, waumini wa mtazamo huu wanaamini kuwa mwanafasihi hawezi kubuni kitu chochote zaidi ya kuiga sanaa ambayo tayari Mungu ameitengeneza.

(b) Mtazamo wa kiyakinifu

Wafuasi wa mtazamo huu wanadai kuwa chimbuko la sanaa na fasihi ni mazingira halisi ya jamii, hususani sanaa ya mwanzo iliyofungamana na kazi za uzalishaji mali. Hii inamaanisha kwamba binadamu (jamii) na mazingira yake ndio chanzo cha fasihi na sanaa. Katika harakati za kukabili mazingira yake, ilimlazimu binadamu kufanya kazi. Binadamu wa mwanzo waliishi katika mazingira yasiyo rafiki. Hivyo, iliwalazimu kutumia silaha ili wapambane na mazingira hayo. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutafuta njia za kurekebisha silaha zao (mawebutu) kwa kuyachonga ili yawe na ncha kali.Uchongaji huo ndio ulikuwa sanaa yenyewe. Kwa hiyo, hisia za kisanaa zimefungamana na maendeleo ya mtu katika kupambana na mazingira yake na katika kufanya kazi. Mtazamo huu una mwelekeo zaidi kwani unakubaliana na fikra kuwa, wanadamu walianza mawasiliano kupitia kazi zao. Kwa mantiki hiyo, chimbuko la sanaa ni kazi.

Kadiri binadamu alivyozidi kuendelea, alikuwa na mahitaji mengine zaidi ya mahitaji ya msingi. Mahitaji hayo yaliamsha hisia za kuchora vielelezo vya shughuli zake za kujikimu. Michoro ya mapangoni iliyopo Kondoa (Tanzania) ni mifano mizuri ya vielelezo hivyo. Kuzuka kwa lugha kuliongeza aina nyingine ya sanaa ambayo ni fasihi. Fasihi hii haikutoka kwa Mungu wala haikutokana na hisi tu.

Fasihi, kama zilivyo sanaa nyingine, ilitokana na kazi alizofanya binadamu katika kupambana na mazingira yake. Fasihi ilianzia katika wimbo wa kazi. Baadaye, tanzu nyingine za fasihi zilitungwa na kusimuliwa kwa madhumuni ya kufunza, kukosoa, kuadibu, kuchokoza fikra na kuliwaza jamii baada ya kazi. Kadiri maendeleo ya uzalishaji mali yalivyoongezeka, binadamu akapata muda wa kupumzika na kustarehe kwa njia ya sanaa, fasihi ilianza kutengana na kazi za uzalishaji. Fasihi ikawa shughuli maalumu ya jamii katika matukio mbalimbali, kama vile sherehe na ibada. Fasihi na sanaa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 13 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nyingine zilirithishwa kizazi hadi kizazi kwa njia ya masimulizi mpaka maandishi yalipogundulika.

Maendeleo ya fasihi katika mifumo ya maisha ya jamii

Fasihi hubadilika kulingana na mabadiliko ya mwanadamu. Kadiri binadamu anavyobadili mifumo yake ya maisha ndivyo fasihi inavyobadilika. Hii inajidhihirisha kupitia mifumo mbalimbali ya uzalishaji mali aliyoipitia binadamu ambayo ni ujima, utumwa, ukabaila, ubepari na ujamaa kama ifuatavyo:

(a) Mfumo wa ujima

Mfumo wa awali kabisa wa jamii ya binadamu baada ya kutoka katika usokwe ulikuwa ni ujima. Katika mfumo huo watu waliishi katika makundi kwa usawa, wakimiliki kila kitu kwa pamoja, na wakishirikiana kupambana na mazingira kama vile ukame na wanyama wakali. Kila walichokipata waligawana.

Fasihi ya kipindi hiki ilihusu uzalishaji mali na uwindaji. Fasihi hii ilifungamana na haja ya kukidhi mahitaji ya lazima. Ilitumika kama chombo cha kazi. Binadamu wa kipindi hicho alitumia nyimbo katika shughuli zake za kilimo kwa lengo la kufanya kazi kwa muda mrefu pasipo kuchoka. Pia, fasihi ya wakati huo ilikuwa na lengo la kuwaunganisha watu pamoja kwa lengo la kufanya kazi, hasa kilimo. Vilevile, binadamu alitumia fasihi simulizi kama chombo cha kusifu na kupongeza watemi au mashujaa waliokuwa wanajitokeza katika jamii zao. Mashujaa hao walitungiwa nyimbo za kuwasifu au walijitungia nyimbo za kujisifu mbele ya jamii zao. Kimsingi, fasihi ya kipindi hiki haikuwa ya kitabaka kwa sababu jamii ilikuwa haijagawanyika katika matabaka mbalimbali. Kwa hiyo, fasihi iliwanufaisha watu wengi katika jamii.

(b) Mfumo wa utumwa

Mfumo huu haukuenea sana hapa Afrika bali ulitamalaki zaidi huko Ulaya na Asia. Katika mfumo huu, matajiri walimiliki ardhi, migodi na watumwa, na kuwatumia watumwa hao kuzalisha mali. Kwa minajili hii, iliibuka fasihi ya tabaka tawala ya kutukuza wamiliki wa watumwa na mali zao na kuwatweza watumwa. Fasihi ya watumwa iliyopinga mfumo huo ilienezwa kwa siri; watunzi hao walipogunduliwa waliadhibiwa vikali. Pamoja na masaibu yote hayo, baadhi ya watumwa hawakuacha kutumia fasihi katika kujitetea au kuelezea ubaya wa mfumo huo kwa lengo la kujikomboa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Mfumo wa ukabaila

Katika mfumo huu, mtaji mkubwa wa uzalishaji ulikuwa ardhi. Uhusiano wa utwana na ubwana ulifikia hatua mpya ambapo tabaka tawala lilitawala njia zote za kiuchumi na kiutamaduni. Mbinu mojawapo ya kutawala uchumi ni kukodisha mashamba. Kabaila hukodisha (ma) shamba, ambapo mtwana hutoa fungu kubwa kwa mwinyi wakati wa mavuno. Fasihi ilitawaliwa na falsafa zilizohalalisha uhusiano wa mabwana (makabaila) na watwana (waishio kwa jasho lao). Mfumo huu ulikuwa na uozo mwingi. Uozo mmojawapo uliojitokeza katika mfumo huu ni kusisitiza starehe na mapambo yasiyo na maana. Pia, kazi za fasihi ziliathiriwa na uozo huu na zilisisitiza mapambo. Kazi za fasihi kama zile za *Al-Inkishafi* (Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir, 1800) na *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona bint Mshamu, 1858) ni mifano mizuri ya kazi za wakati huo.

Kazi za fasihi katika mfumo huu ziliathiri sana nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke alisawiriwa kama pambo la mwanamume kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo:

Nawe ipambe libasi,
Ukae kama arusi,
Maguu tia kugesi,
Na mikononi makoa.

Na kidani na kifungo,
Sitoe katika shingo,
Muili siwate mwengo,
Kwa marashi nadalia.

Nyumba yako inadhifu,
Mumeo umsharifu,
Wakutanapo sufufu,
Msifu na kumtaya.

Mume wako mtukuze,
Sifa zake zieneze,
Wala simsharutize,
Asichoweza kutoa.

("Utenzi wa Mwanakupona" katika *Tenzi Tatu za Kale*, (Mugyabuso Mulokozi [Mh.], 1999: 129-130)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 15 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Beti za hapo juu zinasisitiza umuhimu wa mapambo kwa wanawake. Mwanakupona anamuusia binti yake akubali kuwa pambo kwa mume wake. Fasihi katika mfumo huu ilitumiwa kumuasa mwanamke aelekeze akili yake katika kumsifu, kumfurahisha na kumhudumia mumewe.

(d) Mfumo wa kibepari

Baada ya mfumo wa kikabaila kuanguka, uliibuka mfumo wa kibepari. Msingi mkuu wa mfumo wa kibepari ni mtaji. Kila jambo huamuliwa kwa nguvu ya fedha. Katika mfumo huu kila kitu kinachofaa kuwa bidhaa hufanywa kuwa bidhaa. Kwa hiyo, fasihi pendwa ndiyo inayouzika zaidi kuliko fasihi dhati. Fasihi katika mfumo huu huegemea zaidi katika kuburudisha kuliko kuwafanya watu wafikirie maisha halisi. Watunzi wa kazi za fasihi hutumia vipaji vyao ili kujipatia fedha. Aidha, katika mfumo wa kibepari, mara nyingi fasihi husawiri maisha ya mtu mmoja mmoja badala ya jamii nzima. Mfano mzuri wa kazi za fasihi za mfumo huu ni riwaya za *Mzimu wa Watu wa Kale* (Mohammed Said Abdulla, 1957) na *Simu ya Kifo* (Faraji Katalambula, 1965); hizi ni riwaya za kipelelezi ambazo zimejishughulisha na matatizo ya watu binafsi badala ya matatizo yanayoikumba jamii nzima.

(e) Mfumo wa kijamaa

Mfumo mwingine unaoakisi maendeleo ya fasihi ni mfumo wa kijamaa. Huu ni mfumo wenye kujali usawa na utu wa mtu. Ni mfumo ambao kila mtu anatakiwa kufanya kazi na kufaidi matunda ya jasho lake kwa kugawana kulingana na kazi aliyoifanya. Nchini Tanzania, mfumo huu ulishadidiwa na Azimio la Arusha lililoanzishwa mwaka 1967 kwa lengo la kuondoa ubepari na kujenga ujamaa. Baadhi ya kazi za fasihi zenye kuakisi mfumo huu ni *Ufunguo Wenye Hazina* (Paul Ugula, 1969), *Ngonjera za UKUTA* (Mathias Mnyampala, 1970) *Shida* (May Balisidya, 1975) *Ndoto ya Ndaria* (John Ngomoi, 1976), *Mtu ni Utu* (George Mhina, 1977), *Gamba la Nyoka* (Euphrase Kezilahabi, 1978), *Lina Ubani* (Penina Mhando, 1984), *Kaptula la Marx* (Euphrase Kezilahabi, 1999), *Mashairi ya Azimio la Arusha* kilicho haririwa na Farouk Topan na Kamenju (Longman 1971) na kwa upande mwingine, kulikuwa na kazi nyingine za fasihi zilizokosoa ama kuhakiki mfumo huu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 16 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1

(i) Eleza dhana ya fasihi kama ilivyojadiliwa na wanafasihi mbalimbali.

(ii) Eleza tofauti kati ya fasihi na vipengele vingine vya sanaa.

(iii) Jadili mitazamo kuhusu chimbuko la fasihi kwa kuzingatia ubora na udhaifu wa kila mtazamo.

(iv) Fasihi ina umuhimu gani katika maisha ya mwanadamu?

(v) Kwa kutumia mifano, jadili kauli kwamba "Fasihi hubadilika kulingana na jamii inavyobadilika."

Shughuli ya kufanya

Iandaliwe ngonjera fupi kuhusu "utumwa," miongoni mwa wahusika wakuu wa ngonjera hiyo wawe "mtumwa" na "bwana". Kisha ighanwe darasani.

Uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi

Mtunzi wa kazi za fasihi ni mtu anayetunga kazi kama vile nyimbo, mashairi, ngonjera, riwaya au tamthiliya. Mtunzi anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(i) Awe mbunifu ili aweze kutoa kazi ya kifasihi yenye mvuto;

(ii) Ajue vizuri utamaduni wa jamii anayoitungia kazi ya fasihi. Pia, ajue mabadiliko yanayotokea katika mifumo mbalimbali ikiwamo ya kisiasa na kiuchumi;

(iii) Awe na ujuzi wa lugha anayotumia kutunga kazi yake ili aweze kuteua msamiati, nahau, misemo na methali ambazo zinaendana na kile anachokitunga;

(iv) Awe na ujuzi wa utanzu husika. Mathalani, kama anatunga shairi, ni lazima ajue kanuni na mbinu za utunzi wa mashairi. Kwa hiyo, ni muhimu mtunzi asome kazi mbalimbali zinazohusu utanzu husika ili kuongeza ujuzi na kubaini mambo ambayo hayajaandikiwa. Kama ni mtunzi simulizi ajue kanuni za utunzi simulizi wa fani inayohusika; na

(v) Awe na uwezo wa kupanga matukio kwa sababu mpangilio mzuri wa matukio hufanya kazi ya fasihi ivutie

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 17 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Fasili ya uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi

Ili mtunzi aweze kufanya kazi yake barabara, sharti awe na uhuru. Uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi ni dhana pana sana. Inajitokeza ndani na nje ya nafsi ya mtunzi. Kwa mujibu wa Euphrase Kezilahabi (1993) uhuru wa mwandishi uko katika mambo manne yafuatayo:

(i) Utashi ambao humfanya mtunzi kufanya mambo yake bila kuyumbishwa na mtu au kikundi cha watu.

(ii) Falsafa inayoendana na maisha halisi ya jamii husika. Hata hivyo, mwandishi anaweza kuwa na falsafa yake mwenyewe inayopingana na falsafa ya watu wengine.

(iii) Kuimudu lugha anayoitumia ili aweze kujieleza vizuri kwa hadhira yake na kutoa kazi zinazokubalika katika jamii.

(iv) Kuitawala kazi anayoishughulikia; kwani mtunzi anayejua vema misingi na taratibu za sanaa anayoishughulikia, mara nyingi, hutoa kazi ambazo huvutia hadhira yake kifani na kimaudhui.

Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kusema kuwa uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi ni hali inayomfanya mtunzi kufanya kazi yake pasipo kuingiliwa na mtu, kikundi cha watu, au taasisi yenye nguvu.

Tathmini ya uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi

Wataalamu wa fasihi wanasema kuwa ili mtunzi awe na uhuru katika jamii yoyote, inatakiwa iwepo demokrasia ya kweli itakayomfanya mtunzi atoe mawazo yake bila kubanwabanwa kwa njia ya sanaa. Vilevile, anatakiwa kuwa na uwezo fulani wa kiuchumi kwani kutokuwa na fedha kunamfanya mtunzi kuyumbishwa na wenye fedha kiasi cha kumfanya kikaragosi chao. Hali kadhalika, uhuru wa mtunzi unahitaji kuwapo machapisho mbalimbali ya kusoma. Kwa hiyo, studio na maktaba vinatakiwa kuwapo ili kumwezesha mtunzi kupata machapisho na sidii mbalimbali zenye kumjengea uwezo wa kutunga kazi bora.

Hata hivyo, jambo la kujiuliza ni kuwa je, kuna uhuru wa mtunzi nchini Tanzania? Kimsingi, swali hili linahitaji majibu makini kutokana na ukweli kuwa mtunzi ni mwanajamii na jamii ina miiko na mipaka yake. Hivyo, mtunzi anapokiuka mipaka hiyo, anakumbana na matatizo. Hali hii inapotokea, huibua hisia za kutokuwapo kwa uhuru wa mtunzi. Mjadala wa uhuru wa mtunzi si kwa Tanzania tu bali unajitokeza hata nchi nyingine duniani. F.E.M.K Senkoro (1984:18) akimnukuu Karl Marx (1899) anasema: "Sheria inaruhusu kuandika

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

lakini kwa sharti moja kuwa niandike kwa mtindo usio wangu. Ninayo haki ya kuonesha undani wa mambo, lakini nalazimishwa niuoneshe undani huo kwa kupitia katika kauli isiyo yangu. Mimi ni mcheshi, lakini sheria inaniamrisha niandike bila mzaha wowote; mimi hupenda kusema mambo bila kuficha, lakini sheria hainitaki niandike hivyo."

Kauli hii ya Marx inaonesha walakini kuhusu dhana ya uhuru wa mtunzi wa kazi za fasihi. Uhuru wa mwandishi umebanwa na sheria zilizowekwa na watu wenye mamlaka ambazo mtunzi hatakiwi kuzikiuka. Katika kipindi cha utumwa na ukabaila hali haikuwa tofauti. Tunaambiwa kuwa katika kipindi cha utumwa, baadhi ya wasanii walioonekana kuwatetea wenzao kwa kulaani mfumo huo kwa kutumia nyimbo, walitenganishwa na wenzao au walikatwa ndimi zao au kuuawa. Lengo lilikuwa ni kuwanyima wasanii uhuru wa kujieleza kuhusu dhambi za mfumo husika ili wasije wakawapa wenzao maarifa ya kuepukana na mfumo huo.

Katika kipindi cha ukoloni, vitabu vilivyotukuza uzungu kama vile *Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Allan Quatermain* (Richard Haggard 1948), ndivyo vilivyochaguliwa kutumika shuleni.

Waandishi wa Kiafrika waliojitokeza kuulaani na kuupinga ukoloni, waliandika kazi zao kwa kificho sana. Mfano wa waandishi hao ni Shaaban Robert aliyeandika riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1967).

Baada ya kupata uhuru, baadhi ya serikali za Kiafrika ziliendeleza tabia ya kuwafunga midomo watunzi. Kazi zote za kifasihi zilizoonekana kwenda kinyume na mwelekeo wa kisiasa na kijamii zilipigwa marufuku. Mfano mzuri ni riwaya ya *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971) ambayo inasawiri maovu yaliyomo ndani ya jamii ambapo watu wazima wenye dhamana ya kuwalinda watoto wa kike wako mstari wa mbele kuwaharibu. Kazi yake nyingine iliyowahi kufungiwa ni *Kaptula la Marx* (1999) iliyokosoa mienendo ya baadhi ya viongozi wa serikali. Kwa upande wa fasihi simulizi, mfano wa nyimbo zilizofungiwa ni "Wapo" (Elibariki maarufu kama 'Ney wa Mitego', 2018). "Wapo" ulifunguliwa kwa idhini ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya tano baada ya kuona maudhui yake hayajakiuka maadili ya jamii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 19
17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mbali na serikali, pia udhibiti wa watunzi wa kazi za fasihi umekuwa ukifanywa na wafadhili, mashirika ya uchapishaji, taasisi za elimu na mashirika mbalimbali ya kidini. Wasanii wamekuwa wakidhibitiwa kwa kutumia nguvu za kimamlaka au fedha ili waandike yale yanayotakiwa na vyombo hivyo.

Hata hivyo, kazi mbalimbali za fasihi zimekuwa zikitolewa mara kwa mara. Hali hii inaweza kuwa kiashiria kwamba watunzi wa kazi za fasihi hapa nchini wana uhuru wa kutosha. Jambo muhimu la kujiuliza ni je, hizi kazi za watunzi zinazotolewa mara kwa mara zinaakisi mawazo ya watunzi pasipo kuingiliwa na watu wengine? Inawezekana, watunzi wengi wa kazi za fasihi hapa nchini wamekuwa wakitoa kazi pendwa ndio maana kazi hizo hazifungiwi.

Ikumbukwe kuwa kunapokuwa na uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi, kuna ukosoaji wa jamii au tabaka lolote lile linaloenda kinyume cha sheria na taratibu zilizopo kama vile wala rushwa, wanyonyaji, wezi, wakwepa kodi na wahujumu uchumi. Hali kadhalika, uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi utasaidia kuikomboa jamii kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kupitia fasihi. Pia, utasaidia kutokomeza mawazo ya kikasuku yaliyomo vichwani mwa baadhi ya watu. Vilevile, utasaidia kutoa elimu kuna mwongozo wa maendeleo ya jamii. Msanii atakuwa huru kutoa elimu kuhusu mambo mbalimbali katika jamii yake ili iwe ya kisasa na ya kimaendeleo. Zaidi ya hayo, utasaidia kuchochea jamii iondokane na matatizo yanayoikumba, ikiwa ni pamoja na mtu kuwa na msimamo unaoeleweka katika kutetea jamii yake. Kwa hiyo, ni muhimu wasanii kuzingatia maadili na utamaduni wa jamii husika.

Zoezi la 2

(i) Kwa kutumia mifano, fafanua jinsi uhuru wa mtunzi unavyoweza kuhusishwa na utamaduni wa jamii.

(ii) "Uhuru wa mwandishi ni wa kitabaka zaidi kuliko wa mtu binafsi." Jadili.

Udhamini

Udhamini ni moja ya dhana muhimu zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Katika fasihi, udhamini ni hali ya mtu, kundi, shirika au asasi fulani kutoa fedha,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 20 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mali au huduma kwa ajili ya kugharamia kazi ya fasihi. Mdhamini hutoa mali zake kwa malengo maalumu ambayo huyapa kipaumbele. Kwa ujumla, lengo la mdhamini ni kuona udhamini huo unamsaidia kupata faida au matokeo aliyokusudia. Athari za udhamini huo huweza kuwa hasi au chanya.

Aina za udhamini

Kuna udhamini wa aina kuu nne wa kazi za fasihi. Aina hizo ni udhamini wa jamii, udhamini wa ushawishi, udhamini wa nguvu na udhamini wa mtunzi mwenyewe.

(a) Udhamini wa jamii

Udhamini mkubwa kuliko wote ni ule wa jamii. Walengwa wa kazi ya sanaa, ikiwemo fasihi ni wanajamii. Wao ndio wasomaji wa mashairi, riwaya au tamthiliya na ndio wanunuzi wa kazi za sanaa. Mwandishi na msanii hujitahidi kuwaridhisha wanajamii ili waipende na kuinunua kazi yake.

(b) Udhamini wa ushawishi

Katika udhamini huu mdhamini hutumia fedha, mali na uzoefu wake katika fasihi kwa lengo la kuwavuta wasanii mbalimbali. Udhamini wa aina hii umejikita zaidi katika fedha au mali aliyo nayo mdhamini. Mdhamini hutumia vitu vyenye kuwavuta wasanii kwa lengo la kukamilisha mahitaji yake.

Mdhamini anaweza kumshawishi msanii kwa kumpa fedha za kuzalisha na kusambaza kazi zake. Wamiliki wa vyombo vya habari kama vile runinga na redio hurusha kazi za wasanii mara kwa mara ili kuwatumia katika matamasha makubwa kwa gharama ndogo. Pia, udhamini wa aina hii hutumiwa na mashirika ya uchapishaji vitabu na baadhi ya asasi za serikali na zisizo za serikali hasa kupitia mashindano mbalimbali ya utungaji wa kazi za kifasihi.

Kupitia umaarufu wa mdhamini, msanii anaweza kulazimika kupitia kwenye mgongo wa mdhamini huyo ili aweze kufanikiwa katika kazi zake za kisanii. Hii ni kwa sababu msanii anakuwa na imani na mdhamini au anakosa uwezo wa kujidhamini yeye mwenyewe.

(c) Udhamini wa nguvu

Udhamini wa aina hii hutegemea zaidi mamlaka aliyo nayo mdhamini dhidi ya mdhaminiwa au msanii. Mara nyingi, udhamini wa aina hii

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 21 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hufanywa na vyombo vya tabaka tawala kama vile serikali inayomiliki vyombo vyote vya dola. Serikali, kwa mfano, inaweza kuwatumia wasanii katika shughuli za maadhimisho ya sherehe za kitaifa. Hapa, msanii hulazimika kuandika au kutunga kazi ya kisanaa kwa kufuata matakwa ya chombo chenye mamlaka. Msanii huwa kama kasuku; hana sauti katika kile anachokiandika au kukitunga.

(d) Udhamini wa mtunzi mwenyewe

Mtunzi wa kazi za kifasihi anaweza kujidhamini yeye mwenyewe wakati wa uchapishaji wa kazi zake. Wakati mwingine hutumia fedha zake katika kuhakikisha kuwa kazi yake inazalishwa kupitia usimamizi wake. Wakati mwingine, anaweza kusambaza kazi zake yeye mwenyewe au kupitia kwa wasambazaji mbalimbali ambao wanakuwa kama mawakala wake. Katika udhamini huu mtunzi huandika au kutunga kazi za fasihi zenye ujumbe anaoutaka yeye mwenyewe kwa sababu hafuati matakwa ya mtu mwingine. Msanii anayeweza kujidhamini ana uwezo wa kutetea tabaka lolote analolitaka.

Sababu za udhamini katika kazi za fasihi

Kuna sababu mbalimbali za udhamini katika kazi za fasihi. Sababu hizo ni pamoja na:

1. Kutojiamini: Baadhi ya wasanii ni waoga na hawajiamini katika kufanya kazi zao. Wanafikiri kuwa bila mtu fulani hawawezi kufanikiwa kisanaa. Kwa hiyo, huwalazimu kutafuta mdhamini ili wafanikiwe.

2. Uhaba wa fedha: Baadhi ya watunzi wa kazi za fasihi hawana fedha za kutosha kuendesha shughuli zao za sanaa. Hali hii huwafanya watafute wadhamini.

3. Tamaa ya kupata fedha za harakaharaka: Baadhi ya wasanii hudhaminiwa na wadhamini wanotaka kupata fedha za harakaharaka. Hii hutokana na umaarufu wa mdhamini katika uwanja wa fasihi. Wasanii wa aina hii hulazimika kutunga yale anayoyataka mdhamini hata kama hayana mchango katika maendeleo ya jamii.

4. Kujipendekeza kwa baadhi ya wasanii kwa wadhamini: Baadhi ya wasanii wana tabia ya kujipendekeza kwa wadhamini ili kulinda na kutetea maslahi yao na ya wadhamini wao mbele ya jamii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 22 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Kulazimishwa: Hii inatokea pale ambapo tabaka moja katika jamii lina nguvu za kisiasa na kiuchumi kiasi cha kuwa na nguvu juu ya matabaka mengine. Katika hali hii, msanii apende asipende atadhaminiwa na tabaka lenye nguvu. Iwapo msanii atakataa kudhaminiwa na tabaka hilo, kazi zake zinaweza kupigwa marufuku au kudhibitiwa.

6. Kutafuta umaarufu: Baadhi ya wasanii hudhaminiwa kwa lengo la kuwafanya wajulikane kwa watu. Wasanii wa aina hii wanapenda kutumia umaarufu wa mtu au shirika fulani ili na wao wajulikane angalau hata robo ya mdhamini wao. Wanaona ufahari kujulikana bila kujali athari mbaya wazipatazo au izipatazo jamii.

7. Mgawanyo wa kazi: Jamii imegawanyika katika "makundi kazi" mbalimbali yakiwamo ya wasanii na wadhamini. Ili makundi haya yaendelee kuwapo, hayana budi kutegemeana na kuendelezana hata kama kuna athari zake.

Athari za udhamini

Udhamini una faida na hasara katika kazi za kifasihi. Zifuatazo ni faida na hasara hizo.

Faida za udhamini

1. Husaidia baadhi ya wasanii kufanya tafiti za masuala mbalimbali yanayohusu jamii. Baada ya tafiti hizo, wasanii huwasilisha masuala hayo kwa njia ya sanaa.

2. Husaidia jamii kupata kazi mbalimbali za fasihi, hasa fasihi andishi ambayo inahitaji fedha nyingi ili ikamilike. Kupitia msaada wa wadhamini, mwandishi hapati shida ya kuzalisha na kusambaza kazi yake kwa umma. Kazi hizi zote hufanywa na wadhamini na, hivyo, kuwafikia walengwa kiurahisi.

3. Udhamini husaidia kuibua na kuendeleza vipaji, hasa vya wasanii chipukizi ambao hawana fedha za kutosha ili kukamilisha kazi zao na kuonesha vipaji vyao kwa jamii. Kwa mfano, mashindano ya uandishi wa kazi za fasihi kwa shule za sekondari yaliyodhaminiwa na Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) miaka ya 1970 yalisaidia kuibua na kuendeleza vipaji vya waandishi chipukizi ikiwa ni pamoja na kuchapisha

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kazi zao. Kadhalika, mashindano ya ushairi ya "Tuzo ya Ebrahim Hussein" yamesaidia kuibua vipaji vya washairi chipukizi. Pia, *Bongo Star Search* ya TBC1 na *Tanzania House of Talents* (THT) ambayo ipo chini ya *Clouds Media Group* hudhamini wanamuziki wachanga. Wadhamini hawa huweza kuibua na kuendeleza vipaji vya washiriki.

4. Baadhi ya wasanii hujipatia fedha kutokana na kudhaminiwa. Hii inatokana na mgao (mrabaha) wanaoupata baada ya kazi zao kuuzwa. Vilevile, wasanii hutajirisha wadhamini kutokana na mauzo ya kazi zao.

5. Udhamini husaidia kuleta ushindani wa ubora wa kazi katika soko la kazi za fasihi. Kuwapo kwa wadhamini wengi husababisha kuwapo kwa wasanii wengi na, hivyo, kuwa na kazi za kutosha. Matokeo yake huleta ushindani wa bei katika soko. Hili pia husaidia kuinua kiwango cha ubora wa kazi husika kwani kazi duni hukosa wanunuzi hata kama zitauzwa kwa bei ya chini.

Hasara za udhamini

1. Humtenga msanii na jamii yake; kwani msanii hutunga kazi zenye maudhui yanyotakiwa na mdhamini au mamlaka zilizopo hata kama yamepotoka.
2. Udhamini humnyima msanii uhuru. Kazi za fasihi hutawaliwa na mwelekeo wa mdhamini kifani na kimaudhui. Hivyo, msanii hukosa uhuru wa kutunga kazi yenye maudhui ayatakayo;
3. Mara nyingi, kazi ya sanaa huwa mali ya mdhamini ambaye huwa na mamlaka kuliko msanii, hasa kama msanii huyo hana hakimiliki.
4. Udhamini husababisha utegemezi miongoni mwa wasanii. Hata kama msanii anajitosheleza kifedha, bado atahitaji mkono wa mdhamini ili kazi yake ikamilike.
5. Udhamini husababisha wasanii wengi kupenda fedha kuliko wajibu wao wa kuelimisha jamii. Kutokana na kupenda fedha, wasanii hutunga kazi pendwa ambazo baadhi haziusawiri vizuri uhalisi.
6. Udhamini hukuza utabaka kati ya mdhamini na mdhaminiwa.
7. Udhamini huifanya sanaa kuwa na mwelekeo wa aina moja; na hivyo,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 24 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huwafanya wasanii kushindwa kueleza hali halisi. Hii inatokana na ukweli kuwa kazi za fasihi hazina budi kuendana na itikadi ya mdhamini.

Zoezi la 3

(i) Fafanua dhana ya udhamini wa kazi za fasihi.

(ii) "Udhamini wa ushawishi ni sawa na udhamini wa nguvu." Jadili.

(iii) Fafanua athari za udhamini wa kazi za fasihi kwa jamii.

(iv) Eleza ni kwa namna gani jamii nzima ni mdhamini wa kazi ya fasihi. Toa mifano muafaka.

Uandishi wa kazi za kifasihi

Uandishi wa kazi za fasihi ni mchakato wa kiubunifu unaotumiwa na mtunzi wa kazi za fasihi katika kutunga kazi yake. Katika kuandika kazi za fasihi, msanii anatakiwa kujiuliza maswali kadha wa kadha. Baadhi ya maswali hayo ni: Anaandika kuhusu nini? Anamwandikia nani? Anaandika kwa kutumia mandhari ipi? Lengo lake ni nini? na, anaandika kwa namna gani? hii inatokana na ukweli kuwa mwandishi huandika kazi yake ili isomwe na watu wengine. Hivyo, mwandishi hana budi kuzingatia mahitaji na mitazamo ya wasomaji wake ili aweze kuwapeleka anakotaka huku wakiendelea kufurahia kusoma kazi husika.

Waandishi wa fasihi huandika kazi zao kwa malengo tofautitofauti. Miongoni mwa malengo hayo ni kusawiri uhalisi wa kijamii kwa lengo la kuurekebisha au hata kuubadili ikibidi. Hii ina maana kuwa mwandishi sharti aibuke na vitu vipya ambavyo vitawavutia wasomaji katika kuwahabarisha yale yanayotokea katika jamii yao. Vilevile, waandishi wa kazi za fasihi huandika kazi zao kwa lengo la kuelezea hisia zao ambazo wanaamini kuwa zitawavutia wasomaji wao ili wayaone maisha kama wanavyoyaona wao. Pia, waandishi wanaandika kazi zao ili kuwaburudisha wasomaji wao. Hii inatokana na ukweli kuwa katika mchakato wa usomaji, msomaji hupata maarifa na burudani. Hali kadhalika, waandishi huandika kazi zao ili kuwashawishi wasomaji wao wakubali ukweli na namna ya kutafsiri mambo mbalimbali kama wanavyofanya wao. Mbali na hayo, waandishi huandika kazi zao kwa lengo la kuonesha na kuendeleza vipaji

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vyao ambapo hujipatia fedha kutokana na mauzo ya kazi hizo ikiwa ni pamoja na kutambuliwa na jamii zao.

Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa kazi za kifasihi

Kazi za kifasihi huwa na mtiririko wa hoja, mawazo na msuko wa visa kisanaa. Kazi hizi huweza kuwasilishwa katika maumbo manne ambayo ni hadithi fupi, riwaya, tamthiliya na ushairi. Yafuatayo ni mambo ya msingi ya kuzingatia katika kuandika kazi za kifasihi.

Wazo au dhamira

Mwandishi hufikiria masuala na athari ambazo zinafaa kuifikia hadhira yake. Mawazo ya mwandishi hutokana na uzoefu wake katika maisha kwani mwandishi huwa haandiki vitu kutoka hewani. Kwa hiyo, dhamira hutokana na uhalisi wa maisha ya binadamu. Mwandishi huchagua dhamira zinazoigusa zaidi jamii na kuandika kazi yake ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Mifano ya mambo yanayoigusa jamii ambayo mwandishi anaweza kuyatungia kazi ya fasihi ni ukombozi wa mwanamke, ajira kwa watoto, mapenzi, umaskini na upelelezi wa matukio ya kisiasa na kiuchumi. Mtunzi huchagua utanzu wa kutolea kazi yake. Utanzu huu huweza kuwa ushairi, hadithi fupi, riwaya na tamthiliya. Mtunzi mwenye wazo la kuonesha kuwapo kwa matabaka katika jamii anaweza kuwasilisha wazo lake kwa njia ya ushairi kama ifuatavyo:

Watoto wawili

1. Mtoto wa tajiri akilia hupewa mkate,
   Mtoto wa tajiri akilia hupewa picha kuchezea,
   Mtoto wa tajiri akilia huletewa kigari akapanda,
   Akiendelea kulia hupanda mgongo wa yaya,
   Akikataa kunyamaza ulimwengu mzima hulaumiwa.

2. Mtoto wa masikini akilia hula mchanga,
   Mtoto wa masikini akilia hupewa mti kuchezea,
   Akilia mtoto wa masikini huvutwa kashani,
   Akiendelea kulia hupanda mgongo wa mama ulio uchi,
   Akikataa kunyamaza wazazi husikitika kimya kimya.

Euphrase Kezilahabi, *Kichomi* (1974)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hapa mtunzi ametumia mbinu ya usawiri sambamba ili kumfanya msomaji ajione mwenyewe na kulinganisha tofauti za kitabaka baina ya watoto hao wawili. Wazo hili linaweza kuelezwa katika umbo la riwaya au tamthiliya pia.

Wahusika

Wahusika ni viumbe wenye kubeba maudhui yanayotokana na jamii husika. Wahusika hupewa vitendo na lugha kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Mwandishi huwapa wahusika sifa na tabia ambazo hadhira huziona kama za watu wanaoishi katika jamii zao. Wahusika hawa hupewa majukumu mbalimbali ambayo huwapambanua kama wahusika wakuu au wahusika wadogo.

Wahusika wakuu sharti wapewe nafasi kubwa katika kazi ya fasihi husika kwa kuwa wanawakilisha wazo kuu la mwandishi. Mwandishi anaweza kumfanya mhusika mkuu kuwa mwenye akili, nguvu, huruma na mbunifu.

Wahusika wadogo hupewa nafasi ndogo na hubeba mawazo madogo kwenye kazi ya fasihi. Hata hivyo, wahusika hawa wote sharti wajengwe katika migogoro inayoibua dhamira na hatimaye, ujumbe. Wahusika hawa sharti waakisi waziwazi au kimafumbo uhalisi wa maisha ya kila siku ya jamii. Matumizi ya wahusika lazima yazingatie muktadha, mwonekano, sifa na uwezo wa mhusika. Idadi ya wahusika hutegemea urefu wa kisa na idadi ya visa vidogo vidogo ndani ya kisa kimoja. Mara nyingi, wahusika wa namna hii ni wahusika wa riwaya na tamthiliya. Katika ushairi, si kila mara mwandishi huonesha mhusika mkuu isipokuwa kama atachanganya mtindo wa riwaya au tamthiliya katika utungo wake. Matumizi mazuri ya wahusika huifanya kazi ya kifasihi kuwa nzuri.

Matumizi ya lugha ya kisanaa

Lugha ya kisanaa ndiyo msingi wa kazi yoyote ya fasihi kwa sababu huitofautisha kazi ya kifasihi na kazi nyingine zisizokuwa za kifasihi. Hivyo, mwandishi wa kazi za fasihi anatakiwa kutumia lugha yenye kumvutia msomaji. Lugha ya kisanaa hujumuisha, pamoja na vipengele vingine tamathali za semi, taswira, methali na nahau kulingana na maudhui husika ili kuvuta hisia za wasomaji.

Kwa upande wa ushairi, mwandishi anatakiwa kuzingatia uteuzi wa msamiati wenye mnato, ambao unaweza kujenga picha na taswira. Aidha, anapaswa kujua kwamba hafungwi na kanuni za kisarufi, hivyo anaruhusiwa kutumia maneno ya mkato na hata kubadili mpangilio wa sentensi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 27

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muundo

Muundo ni umbile au mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi. Mwandishi anaweza kuandika kazi yake kwa kutumia muundo wa moja kwa moja, ambapo kisa cha kwanza hufuatwa na cha pili hadi cha mwisho. Pia, mwandishi anaweza kuandika kazi yake kwa kutumia muundo rejeshi au changamani, ambapo visa na matukio huchangamana au hurejeleana. Mathalani, mtunzi wa riwaya anaweza kujenga muundo wa hadithi kwa kutumia sehemu au sura mbalimbali. Ndani ya sura au sehemu hizo kunatakiwa kuwe na msuko wa matukio ambao unaleta mgogoro miongoni mwa wahusika. Kwa maneno mengine, kazi za kifasihi hujengwa na migogoro baina ya wahusika. Aidha, upangaji wa kazi za fasihi katika sura hurahisisha usomaji.

Mtunzi wa hadithi fupi anatakiwa kuwa na visa vichache na kutumia wahusika wachache. Kwa kawaida, hadithi fupi huwa na kisa kikuu kimoja, na wahusika wakuu wawili wanaokinzana. Wahusika hao wanaweza kuwa na wafuasi wao wachache wasiokuwa watendaji wakuu. Mgogoro wa hadithi fupi huwa mkali, na unaposuluhishwa hadithi humalizika. Hadithi fupi haipaswi kuwa na mawanda mapana ya kiwakati na kijiografia.

Mtunzi wa tamthiliya anatakiwa kujenga kazi yake kwa kutumia, Vitendo, Sehemu au Maonesho, na kutoa maelezo ya jukwaa kwa hadhira yake. Maelezo ya jukwaa husaidia kufafanua mandhari, vifaa na matendo ya wahusika.

Mtunzi wa ushairi azingatie idadi ya mishororo katika ubeti, na urari wa vina na mizani katika kila ubeti, hasa kama ni mwanamapokeo. Mathalani, anaweza kutunga shairi lenye muundo wa mishororo minne au mitano kadiri atakavyoona inakidhi kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo. Kwa upande wa wana usasa, uteuzi wa muundo haufungwi na sheria bali huongozwa na maudhui, lengo la mtunzi na mbinu za uwasilishaji.

Mtindo

Mtindo ni namna ambavyo msanii hutunga kazi yake na kuipa upekee tofauti na kazi nyingine. Kwa vile mtindo huonesha upekee wa mwandishi, ni vema mwandishi akachagua mtindo utakaowavutia wasomaji. Mitindo ya uandishi wa kazi za kifasihi ni mingi kwa mfano katika hadithi, ushairi na tamthiliya zilichota vipengele kutoka katika fasihi simulizi. Ni jukumu la mwandishi kuhakikisha kuwa kazi yake inakuwa katika ubora na upekee ili kuifikishia hadhira yake yale aliyoyakusudia kwa njia ya kuvutia.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 28 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mandhari

Mandhari ni mahali ambapo visa na matukio ya ndani ya kazi ya fasihi hufanyika. Aidha, mandhari hujumuisha wakati na muktadha ambao visa na matukio hutendeka. Mandhari huweza kuwa ya kubuni au halisi. Mwandishi ni lazima atumie mandhari inayoakisi matukio na visa vya kazi husika. Iwapo, kwa mfano kazi ya fasihi inahusu maisha ya kijijini, mtunzi atumie mandhari ya kijiji ili kuijengea hadhira dhana inayoelezwa kwa urahisi. Mathalani, mtunzi hawezi akawa anaeleza kisa cha kijijini halafu akasema: "Wahusika walipokuwa ofisini ghorofa ya saba, lifti ikagoma kufanya kazi." Vijiji vyetu vingi havina mandhari ya namna hiyo.

Mandhari iliyobuniwa vizuri husaidia kufikisha ujumbe na kuaminika kwa masimulizi. Uhalisi wa matukio na visa, katika kazi za kifasihi, hutegemea zaidi mandhari na muktadha wake.

Hadhira

Mwandishi huandika kazi yake ili iweze kusomwa na watu wengine. Kwa hiyo, hana budi kujua aina ya watu anaowaandikia kazi husika. Mwandishi anatakiwa kujua mahitaji ya wasomaji wake, ikiwa ni pamoja na mitazamo yao kuhusu kile anachokiandika. Kwa mfano, kama mwandishi anawaandikia watoto, anatakiwa kuandika hadithi fupi yenye lugha nyepesi ili watoto waweze kuvutiwa kusoma na kuelewa maudhui ya hadithi hiyo kwa urahisi. Aidha, anaweza kuweka picha au michoro yenye rangi mbalimbali ili kuwavutia watoto na kuwajengea kumbukumbu.

Ujumbe

Ujumbe ni taarifa au funzo linalotokana na kazi ya fasihi. Kazi moja inaweza kuwa na ujumbe zaidi ya mmoja. Mathalani, kazi ya kifasihi inaweza ikawa inatoa ujumbe kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii, kujikinga na maradhi, kuepuka tamaa, uaminifu na utii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 4

(i) Kwa nini mtunzi wa kazi za kifasihi hutakiwa kuzingatia mandhari?

(ii) Linganisha vipengele vya muundo wa shairi la kimapokeo na muundo wa riwaya.

Maswali ya marudio

(i) Eleza mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi.

(ii) Jadili mitazamo miwili ya chimbuko la fasihi.

(iii) Eleza dhima chanya na hasi za fasihi.

(iv) Fafanua dhima ya wahusika katika kazi za fasihi.

(v) Jadili uhusiano uliopo kati ya tabaka tawala, dola na uhuru wa mwandishi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 30

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Pili: Maendeleo ya fasihi simulizi

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu dhana, tanzu, utungaji, usimulizi, uwasilishaji, uenezaji na uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi. Aidha, utapata ujuzi wa kutunga, kusimulia na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

Dhana ya fasihi simulizi

Fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa kichwani kabla ya uwasilishaji, au papo kwa papo, na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo, vitendo na/au ishara. Fasihi simulizi ina tanzu nne. Kila utanzu una vipera anuwai. Katika madarasa ya chini, ulijifunza kuhusu tanzu hizo za fasihi simulizi. Sura hii inafafanua kwa ufupi sifa, umuzi, dhima na maendeleo ya tanzu hizo.

Sifa za fasihi simulizi

Fasihi simulizi ina sifa mahususi zifuatazo:

(i) Huwasilishwa kwa mdomo, vitendo na ishara;

(ii) Ufanisi wake kisanaa hutegemea uwezo wa fanani au wahusika;

(iii) Masimulizi yake huweza kuathiriwa na mazingira, hisia na hali;

(iv) Kwa kiasi kikubwa, huwa ni mali ya jamii;

(v) Huweza kubadilika kutoka kizazi hadi kizazi au katika mazingira mbalimbali kutegemea ufundi na kumbukumbu ya fanani.

Tanzu za fasihi simulizi

Fasihi simulizi imegawanyika katika tanzu mbalimbali kufuatana na wataalamu walivyoainisha. Baadhi ya hizo ni hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonesho. Kila utanzu umegawanyika katika vipera mbalimbali kama inavyoonekana katika kielelezo kifuatacho:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 31 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo Namba 2.1 Tanzu na vipera vya fasihi simulizi

Chanzo: (Kyallo Wamitila, 2010)

Kwa ujumla, fasihi simulizi kugawanyika katika tanzu kadhaa kulingana na uchanganuzi wa wataalamu mbalimbali, na tanzu hizo zimegawanyika katika vipera. Pia kuna mwingiliano mkubwa wa tanzu na vipera hivyo. Ni nadra kukuta kazi moja ya fasihi inayobebwa na utanzu au kipera kimoja. Tanzu zinaainishwa kwa kupewa jina fulani kutokana na siafa zake za kifani na maudhui. Sasa tuangalie maendeleo ya tanzu na vipera hivyo.

1. Hadithi

Ni utungo unaotumia lugha ya mjazo (nathari). Hadithi hueleza kisa fulani kwa mpangilio wa matukio unaotumia wahusika ambao ndio watendaji wa matukio hayo. Hadithi huwa na kisa kinachofululiza tangu mwanzo hadi mwisho ili kukamilisha muundo wake.

Hadithi huwasilishwa na msimuliaji mbele ya hadhira katika mandhari maalumu kama vile chini ya mti mkubwa, sebuleni, darasani au uwanjani. Aghalabu, masimulizi hufanyika katika muda maalumu, hususani baada ya kazi. Kama inavyoonekana hapo juu katika kielelezo namba 2.1, utanzu wa hadithi una vipera sita ambavyo ni ngano, tarihi, visasili, vigano, soga na visasuli.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 32 17/05/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Ngano

Ngano ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu. Ni kipera cha mwanzo kabisa katika utanzu wa hadithi. Kwa kawaida, mtunzi wa ngano hajulikani; ngano hupokezanwa na kuendelezwa kutoka kizazi hadi kizazi. . Maudhui yake hujikita katika maadili, mahusiano na mwenendo ndani ya jamii. Aghalabu, ngano ni hadithi za maadili na burudani ambazo husimuliwa katika mazingira ya starehe na mapumziko. Ngano ina vipera vidogo kadha; baadhi yake ni **hurafa**, **hekaya** na **istiara**.

Hurafa ni ngano zenye wahusika wanyama tu. Wanyama hao huwakilisha tabia na matendo ya binadamu kwa kurejelea masuala yanayopatikana katika jamii. Mafunzo katika hurafa huweza kuhusu tabia nzuri au mbaya za binadamu, kama vile woga, ulafi na tamaa. Katika hurafa, wanyama wanaotumiwa ni kama vile sungura, fisi na kobe. Sungura huwakilisha ujanja, kutokata tamaa na kutochoka. Fisi huwakilisha tamaa, ulafi, woga, uzembe na ujinga. Kobe huwakilisha ukimya, busara na utulivu; ni mhusika ambaye hufanya vitu kimya kimya lakini huibuka mshindi.

Hekaya ni ngano zenye visa visivyo vya kawaida vinavyoambatana na masaibu na pengine hata ujanja wa mhusika mkuu ambaye huweza kuwa mtu au mnyama. Hekaya hujengwa na visa vingi tofautitofauti. Mhusika mkuu katika hekaya hupitia misukosuko mingi hadi kukaribia kushindwa. Hata hivyo, katika hatua za mwisho kabisa, mhusika huyu huweza kuibuka mshindi kwa namna isiyotarajiwa. Lengo la hekaya ni kumtia mtu moyo asikate tamaa anapopitia changamoto za aina mbalimbali. Kimsingi, kinachohimizwa ni kutumia akili kutatua matatizo ya maisha. Kwa kumtumia mhusika sungura, kwa mfano, tunahimizwa kuwa wajanja na kutokujidharau hata kama ni wadogo. Umbile dogo linaweza kuwakilisha pia uwezo wa kiuchumi kama vile kuwa na mtaji mdogo. Mtu anaweza kutumia mtaji mdogo akafanya biashara mpaka kufikia kiwango cha kuwa mfanyabiashara mkubwa. Ufuatao ni mfano wa hekaya:

Hapo zamani, kulitokea mfanyabiashara mmoja aliyekuwa na mali nyingi sana. Basi alioa mke na baadaye akaongeza Bi. Mdogo (mke mdogo). Wakaishi hivyo. Alitokea kumpenda zaidi Bi. Mdogo na kumnyanyasa Bi. Mkubwa (mke mkubwa).

Siku moja alikuwa na safari ya kwenda kununua bidhaa za duka lake. Basi akamwambia Bi. Mdogo ataje mahitaji yote ambayo angependa aletewe kama zawadi. Bi. Mdogo akataja vitu vingi. Naam, kwa vile mfanyabiashara yule

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 33 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

alikuwa akimpenda sana, hakusita kumhakikishia kwamba atamletea. Kwa shingo upande, alimwendea vilevile Bi. Mkubwa na kumwambia ataje zawadi ya kumletea. Yule Bi. Mkubwa akamwambia mumewe asisumbuke ila amletee pete na kipande cha akili. Basi, kwa dharau yule bwana akakubali.

Basi tajiri akafunga safari akafika huko, akanunua vifaa vyake vyote alivyovihitaji kwa ajili ya duka lake. Vilevile, akanunua vitu vyote kama vile nguo ambazo Bi. Mdogo alimtuma, pamoja na pete ya Bi. Mkubwa. Sasa akakwama wapi apate kipande cha akili. Akazunguka maduka yote, asipate. Mwishowe, akaona ni upuuzi kuendelea kutafuta kipande hicho.

Basi, katika ghadhabu yake, akawa anamtukana huyo Bi. Mkubwa, jinsi alivyo mpumbavu. Ikatokea kwamba Bi. Kizee mmoja akamsikia alivyolalamika na kuapiza. Yule Bi. Kizee akamuuliza kwa nini analalamika. Yule bwana akamsimulia kisa chote. Bi. Kizee akamwambia yule bwana kuwa asipate taabu kwani kipande hicho anacho nyumbani. Wakafuatana kuelekea nyumbani kwa huyo Bi. Kizee. Kufika karibu na kule nyumbani, Bi. Kizee akamweleza kwamba kipande hicho kiko nyumbani kwa yule bwana, ila tu akitaka kukipata sharti ni kwamba atakapokaribia nyumbani kwake ajipake mavi, halafu aone jinsi wake zake watakavyompokea.

Basi tajiri akafanya kama alivyoagizwa. Alipokaribia nyumbani kwake, akajipaka mavi mwili mzima, akawa hovyo kabisa kisha akapiga hodi kwanza nyumbani kwa Bi. Mdogo. Bi. Mdogo kufungua mlango katika harakati za kumlaki, akaona mumewe kajaa mavi mwili wote. Bi. Mdogo akafoka sana na kumwambia asithubutu kuingia mle ndani hadi ameoga vizuri.

Basi yule bwana katika hali hiyohiyo, akaenda kwa Bi. Mkubwa. Bi. Mkubwa akamwona mumewe katika hali ile, akasikitika sana. Akamvua nguo zenye mavi, akamwosha, akamvika nguo nyingine.

Ndipo yule bwana akamwambia mke wake, "Pete na kipande cha akili vyote nimepata. Isipokuwa kipande cha akili nimekipata hapahapa." Akachuka zawadi zote hata zile za Bi. Mdogo, akampa yule Bi. Mkubwa, na kumfukuza Bi. Mdogo.

Wakaishi raha mustarehe.

Hadithi inapatikana katika kitabu cha *Riwaya ya Kiswahili* (Joshua Madumulla, 2009 kurasa 94-95)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 34 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Istiara ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana iliyofichika. Kwa hiyo, maana huwasilishwa kwa njia ya mafumbo. Kwa mfano, hadithi mashuhuri ya zimwi linalovamia kijiji na kuwameza wanakijiji wote isipokuwa mwanamke mmoja mjamzito ni istiara. Katika hadithi hiyo, mama huyo mjamzito baadaye anajifungua mtoto na kumlea akiwa mafichoni. Mtoto anapokua anamuuliza mama yake kwa nini wako peke yao kijijini, wakazi wengine walikwenda wapi. Mama yake anamweleza kuwa watu wote walimezwa na zimwi ambalo linaishi katika msitu ulio karibu na kijiji hicho. Mtoto anaamua kwenda kupambana na zimwi hilo hadi analiua, analipasua tumbo na kuwatoa watu wote liliowameza wakiwa bado hai. Watu wanafurahi na kumfanya mtoto huyo kuwa kiongozi wao. Kiistiara, hadithi hii huweza kuwakilisha ukoloni na mapambano ya kujikomboa. Zimwi linamwakilisha Mkoloni, na mtoto ni mkombozi. Ufuatao ni mfano mmojawapo wa Istiara.

Kisa cha Shemakumbi

Hapo zamani za kale katika kijiji kimoja, palitokea nyoka aina ya nondo. Nondo huyu aliitwa Nungu. Yeye mwenyewe alijiita Shemakumbi. Nyoka huyu alikuwa ana vichwa saba. Watu wengi walimuogopa; kila mtu alijitahidi kuwa mbali naye kwa sababu ya umbile na tabia yake ya kuwashambulia watu.

Siku moja, kulizuka uvumi kuwa nondo amekuwa hatari na tishio kubwa kwa wananchi. Alimshambulia kila aliyemkuta. Watu wa kijiji hiki waliogopa sana hata wakashindwa kuamua kuwa wafanye nini. Kila mtu alijitetea mwenyewe; kwanza, kwa kujaribu kumuua nondo, pia kukimbia. Ingawa watu wote walijitahidi kumkimbia nondo, walikamatwa na kuuawa isipokuwa mwanamke mmoja aliyekuwa mjamzito.

Mara baada ya kusikia maafa yaliyosababishwa na nondo, mama huyu alikimbia haraka haraka mpaka akafika nyumbani kwao. Hapo alipanda hadi ghalani na huko alijificha ndani ya mtungi mkubwa. Alijiingiza humo ili ajinusuru yeye pamoja na mwanawe mtarajiwa. Mama aliishi ndani ya mtungi ule kwa muda wa siku nyingi akiwa amezongwa na upweke, kwani watu wote walishamezwa na nondo. Naye nondo baada ya kujiridhisha kuwa hakukuwapo na mtu yeyote aliyebakia, alienda kuishi katika jangwa na nyika iliyokuwa pembezoni mwa kijiji hicho.

Akiwa katika lindi la upweke na woga, mama alijifungua mtoto wa kiume. Taratibu, hofu yake ilianza kupungua. Kadri mtoto alivyokuwa mkubwa, upweke na woga

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 NA 6 (KWANDANI).indd 35 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

viliendelea kuihama kaya ya mama yule. Hata mtoto alipokuwa mtu mzima, mama alikuwa na matumaini kuwa angalau kwa wakati huu, yeye pamoja na mwanawe wanaweza kushirikiana kupambana na hatari yoyote itakayojitokeza. Siku moja wakiwa wamepumzika mtoto alimuuliza mama, "Mama, mbona katika maeneo yanayotuzunguka kuna magofu mengi, inaelekea kulikuwapo na watu wakiishi kwenye maeneo haya. Tafadhali, nieleze nini kilitokea hata hali ikawa hivi?" Mama yake akamjibu bila hamaki:

"Ni kweli mwanangu, hapo zamani za kale katika kijiji hiki, palitokea kuishi watu wengi. Tena wengi sana, wake kwa waume, watoto kwa vikongwe, lakini yaliyotokea siku hizo sitakueleza leo hii. Subiri utakapokuwa mtu mzima nitakusimulia habari yote. Kwa sasa wewe bado u mtoto. Si vizuri kukuambia suala hili. Tafadhali subiri, kwani subira yavuta kheri."

Ingawa mwana alimbembeleza mama yake amuelezee kisa hiki, mama alikataa katakata kusimulia habari ya maangamizi ya kijiji hicho kwa kuhofia kuwa bado mwanawe si mtu mzima, na kumuahidi kuwa atakapokuwa mtu mzima atamueleza. Kila siku na kila mara mwana alijitahidi kuwa karibu na mama yake akijaribu kumshawishi amsimulie lakini mama hakufanya hivyo mpaka ulipofika wakati muafaka wa kufanya hivyo. Siku ilipowadia mama alianza kisa chake:

"Mwanangu sasa umekuwa mtu mzima na yanipasa nikueleze habari za kijiji chako. Basi katika ukao wao hapo zamani, wakazi hao pamoja na mimi nikiwamo walifikwa na dhoruba ya nondo mla watu. Nondo huyu alikuwa ana vichwa saba, na aliazimia kummeza kila mwanadamu katika kijiji hiki. Dhoruba hii ilipotokea, kila mtu alihaha.Wengine walijaribu kumuua lakini walishindwa. Wengine walilia lakini vilio vyao viliishia kwenye kimya kirefu; na wengine walikimbia lakini mbio zao ziliishia sakafuni. Wote waliishia kwenye midomo saba ya nondo mla watu isipokuwa mimi mama yako, kipindi hicho nilikuwa mjamzito wa uzao wako."

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 36 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mama alipofika hapa, mtoto alihema kama chatu na kutokwa na kijasho chembamba kama mtu aliyekuwa akikwea mlima mrefu. Licha ya hivyo, mtoto alibaki kinywa wazi kwa mshangao na hamaki kwa yale aliyohadithiwa. Baada ya kitambo, mtoto alipata nguvu za kuuliza. Alisema:

"Ehe, wewe ulitumia mbinu gani? Na huyo nondo alienda wapi?" Mama akaendelea kuhadithia, "Basi, kwa msaada wa Mungu, mimi nikatumai kuwa ningeweza kujiokoa pamoja na kuiokoa nafsi ya kile kilichokuwa tumboni mwangu kwa kuingia kwenye mtungi. Nilikimbia mpaka nyumbani kwetu, nikapanda ghalani, nikajificha kwenye mtungi. Kwa muda wote huo nilikula akiba za vyakula vya wanakijiji wenzangu. Kila mara nilitoka mara moja na kisha mara baada ya kumaliza shida zangu nilirudi kwenye mtungi. Humo nilijificha mpaka siku ulipozaliwa wewe, ukakua na hata sasa wewe u mtu mzima. Nondo alipodhani kuwa amemaliza kazi yake, alienda kuishi katika nyika na msitu ulee unaouona pembezoni mwa kijiji hiki. Sijawahi kumuona tena nondo katika kijiji hiki, lakini hata wewe nakusihi endelea na shughuli zako kwa uangalifu na wala usijisumbue kumtafuta."

Alipomaliza kuhadithia, kijana alitabasamu kidogo ingawa kwa namna fulani alijawa na huzuni na woga. Alimwambia mama yake:

"Kuna sababu gani ya kuendelea kuishi ikiwa watu wote katika kijiji hiki walishamezwa na nondo? Mimi nitaenda kumtafuta nondo, ama nitamuua au ataniua."

Mama yake alimsihi mwanawe asifanye hivyo, lakini mtoto wake alikataa. Hata mwisho mama akasema, "Haya mwanangu, kama umedhamiria kufanya mapambano na nondo, nadhani mimi nitaendelea kuishi peke yangu, lakini angalia hali yangu kwa sasa, mimi sina nguvu. Nishakuwa mzee. Je, nitawezaje kujitafutia mahitaji yangu bila wewe? Mimi nakuhitaji sana wewe mwanangu. Kwa nini usikubali kuachana na nondo?"

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwana akajibu, "Ikiwa nondo ataniua mimi, bila shaka atakuua hata wewe. Pia, kama mimi nitamuua nondo, wewe, wanakijiji waliomezwa siku nyingi na mimi tutakuwa salama. Hakuna haja ya wewe kumhofia nondo aliyeweza kuwameza wanakijiji wote. Mimi naondoka sasa hivi."

Basi, mtoto akachukua silaha za namna mbalimbali kama vile shoka, panga, kisu, upinde na mishale. Alipofika pembezoni mwa ile nyika, alizikumbatia vizuri silaha zake kisha akaanza kumuita nondo kwa kuimba wimbo:

Kisambaa	Tafsiri ya Kiswahili
Nungu ee kwea, nungu kwea, *Uko nyika kwea, nungu kwea,* *Nungu ee kwea, nungu kwea,* *Uko nyika kwea, nungu kwea.*	Nungu panda, nungu panda, Huko mjini panda, nungu panda, Nungu panda, nungu panda, Huko mjini panda, nungu panda.

Aliendelea kuukariri wimbo huu mara kadhaa, hata yule nondo aliposikia sauti ya mwanadamu aliamka akanyanyua shingo yake. Nondo alijiuliza, "Ni nani huyo ambaye bado yungali hai katika kijiji hiki?" Lakini hakupata jibu. Mwisho kabla hajaja kuona nani anayemuita naye alianza kuimba:

Kisambaa	Tafsiri ya Kiswahili
Shemakumbi niani enilanga, *Shemakumbi niani enilanga,* *Vintu vyooshe nzaja nzabinda,* *Shemakumbi niani enilanga.*	Shemakumbi ni nani hapo juu, Shemakumbi ni nani hapo juu, Vitu vyote nimekula nimemaliza, Shemakumbi ni nani hapo juu.

Mara baada ya kusikia sauti hii yule kijana alikariri tena ule wimbo wake kwa sauti nzuri. Kila alivyoimba naye nondo aliimba na kuzidi kusogea karibu na mahali alipo yule kijana Alipofika karibu yake, kijana aliamua kuwa hatamkata Nondo

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa kutumia panga, kisu wala kumchoma mshale. Ila atanyamaza na kukumbatia silaha zake, ili atakapomezwa amezwe pamoja na silaha hizo.

Kama alivyokuwa amepanga, kijana alijikunyata kama mtu mnyonge sana. Naye nyoka alimmeza kijana akiwa na silaha zake. Mara baada ya kumezwa, yule kijana alianza kumchanachana nondo. Alichana kila sehemu ya mwili wa nondo, nondo akatokwa na damu nyingi isiyo kifani na mwishowe akafa.

Lo! Damu iliyokuwa inatiririka kutoka mwilini mwa nondo ilipokatika palionekana miili ya watu wengi ajabu. Wengine walikuwa wamekufa na wengine walikuwa wazima. Walikuwamo wanaume na wanawake, vichwa vyao vilijawa na nywele zenye mvi. Mvi mvi mvi kila mahali. Wale waliokuwa hai, walifurahi sana kutokea tena katika ulimwengu wa dunia. Waliuliza kwa sauti moja:

"Ni nani aliyetuamsha toka katika usingizi wetu mwanana?" Kwa urefu na kwa kina mama wa yule mtoto akasimulia yote yaliyotokea. Alipofika mwisho, wanakijiji wote wakaazimia kumuita mtoto yule jina la kishujaa la "Nondo Mlawatu-Shemakumbi." Si hivyo tu, pia walimtawaza yeye awe kiongozi na mfalme wao na wakaishi raha mustarehe.

(*Hadithi ilikusanywa na* Ramadhan Thomas, 2011).

Kwa kawaida, ngano huwa fupi kwa sababu ya muundo wake wa kuwa na kisa kimoja.Wahusika wa ngano ni bapa kwa maana kwamba mhusika akiwa mwema ni mwema mwanzo hadi mwisho wa hadithi, vivyo hivyo kwa mhusika mwovu. Lengo kuu la ngano, mbali na kuburudisha, ni kuadibu, kuadili na kuelimisha jamii. Hujaribu kujenga utu bora kwa kueleza wema na ubaya.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 39 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Tarihi

Tarihi ni hadithi zinazohusu matukio muhimu ya kihistoria. Msingi wa hadithi hizi ni matukio ya kihistoria. Matukio haya yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni au mchanganyiko wa ukweli na ubunifu. Aghalabu, wahusika wa hadithi hizi ni binadamu. Mifano maarufu ya tarihi ni *Tarihi ya Kilwa* na *Tarihi ya Pate* (Whiteley,1969:34) Tazama mfano ufuatao:

Habari za mji wa Kisaki

Awali kabisa, aliyejenga Kisaki ni Jamitambo aliyekuwa Sultani mkubwa. Kazi ya sultani huyu ilikuwa ni kulima mtama na mpunga pamoja na kuwinda ndovu, huku akiuza pembe za ndovu hao. Wakati wa utawala wake, Jamitambo alipigana na Wakamba ambao hatimaye waliondoka. Baada ya muda, Jamitambo naye alifariki na utawala ukatwaliwa na mtu aliyejulikana kama Mwinyi Mgeni. Kazi ya Mwinyi Mgeni ilikuwa kulima mpunga, mtama, mahindi na ufuta. Katika utawala wake, Mwinyi Mgeni alipigana pia na Sultani aliyejulikana kama Makobe. Baada ya kufa kwa Mwinyi Mgeni, mwanawe aliyejulikana kama Abdalah alichukua uongozi wa makao makuu ya ufalme huo; yeye vilevile, kazi yake ilikuwa kulima mahindi, mtama na ufuta, na alikuwa pia na mazoea ya kwenda porini kuwinda ndovu kwa ajili ya pembe zake (Kyallo Wamitila, 2008).

(c) Visasili

Visasili ni hadithi zinazoelezea chimbuko au asili ya jamii, ukoo, au kundi fulani. Huelezea pia tamaduni mbalimbali na namna jamii fulani ilivyofika katika eneo fulani. Kadhalika, visasili huelezea na kufafanua masuala ya kimaumbile na kiimani yanayomhusu na kumsumbua binadamu kama vile maradhi na kifo. Visasili hueleza pia maana ya maisha na hatima ya mwanadamu kulingana na imani za jamii inayohusika. Kwa kawaida, visasili huheshimiwa na kuaminiwa na wanadamu, na huhusishwa na kuwa vielelezo vya miviga na ibada zao. Mfano wa kisasili ni hadithi za mataifa mbalimbali kuhusu kuumbwa kwa ulimwengu na vilivyomo. Mfano mzuri ni hadithi ya Wakikuyu ya "Gikuyu na Mumbi" (ambayo inapatikana katika kitabu cha *Naushangilia Mlima Kenya*, (Kenyatta na Kibui, 1966) na simulizi ya "Adamu na Hawa" ambayo inapatikana katika *Biblia* na *Kurani*.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Vigano

Vigano ni hadithi fupifupi. Mafunzo yake hutolewa kwa kutumia lugha ya picha kama ilivyo kwa methali. Hadithi hizi zina hadhi ya methali ingawa hutumia taswira pana kuliko methali. Kimsingi, hadithi za namna hii hutolewa kama vielelezo hasa wakati wa mazungumzo au maongezi. Lengo kuu huwa ni kumkanya na kumfunza anayesikiliza.

Kigano, kwa mfano, kinaweza kueleza kuhusu mzazi aliyempenda mno mtoto wake wa pekee. Kwa hiyo, hakuthubutu kumkemea au kumrudi yule mtoto. Hatimaye, mtoto alijenga tabia mbaya. Basi, msimulizi husema kwa methali: *Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe*.

Vigano, aghalabu, hutokea katika mazungumzo na, wakati mwingine, hutungwa papo hapo. Kwa mantiki hiyo, vigano vingi huwa havienei kwa sababu hufungamanishwa na muktadha wa maongezi na hutungwa kwa ajili ya mada husika tu. Kwa hiyo, hupotea baada ya mada kuwasilishwa.

(e) Soga

Soga ni hadithi fupifupi za utani na ucheshi. Hadithi hizi husimuliwa kwa mfuatano wa matukio yanayochekesha. Soga hujengwa juu ya tukio moja tu. Tukio hilo, aghalabu, hulenga kuchekesha kwa kubeza na kukejeli. Pia, hueleza mambo ya ukweli unaoumiza kwa njia ya ucheshi ili kupunguza ukali wa ukweli huo. Soga hupatikana au hufanywa na watu wa jamii zenye historia ya kufanyiana utani kama vile jamii za Wanyaturu na Wakurya, Wahaya na Waha, Wachaga na Wapare. Kwa ujumla, soga hujikita katika kuburudisha na kuelimisha jamii. Tazama mfano wa soga inayowahusu Wamakonde hapa chini:

Kisa cha Mmakonde na Ngedere

Mmakonde mmoja alikwenda shambani kwake, akakuta ngedere anakula mahindi yake. Ngedere alipomwona Mmakonde akakimbilia juu ya mti. Mmakonde akamwona kule alikojificha, akamwambia: "Wee ngedere *nimechakuona, uchijifanye n'janja, telenka* hapa chini nikupige *nchale* ili upate adhabu moja tu. Vinginevyo, *n'kupige nchale* ukiwa hukohuko juu ya *nti*, upate adhabu mbili: Adhabu ya kupigwa *nchale*, na adhabu ya kuanguka kutoka juu ya *nti* baada ya kupigwa *nchale*. Je, wewe ungekuwa ngedere ungefanyaje?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Visasuli

Kisasuli ni hadithi yenye kueleza usuli na sababu za jambo, tukio au hali. Visasuli havina uzito mkubwa kama visasili, na si lazima viaminiwe na wanajamii. Mathalani, zipo hadithi zinazoeleza kwa nini mnyama fulani anapenda kushirikiana na wanadamu, au ameumbika kwa namna fulani. Mfano wa kisasuli ni hadithi ya "Kwa nini nyoka hana miguu?"

Kwa nini nyoka hana miguu?

Siku moja nyoka pamoja na wanyama wengine walialikwa kwenye sherehe nyumbani kwa mfalme. Kule walikula na kunywa! Baadaye mfalme aliwaita wapewe zawadi. Nyoka, kwa sababu ya uroho, hakusikia wito. Alipozinduka, alikuta miguu yote, hata ile hafifu ya tandu na buibui, imeshatolewa; akabakia anajiburuza kwa tumbo lake. Mpaka leo hii nyoka hana miguu (May Balisidya, 1987)

2. Semi

Semi ni tungo fupifupi za fasihi simulizi, na aghalabu, hutumia picha, tamathali na ishara. Semi hutumika kutoa mafunzo, nazo zimegawanyika katika vipera mbalimbali kama vile methali, misemo, nahau, mafumbo, lakabu, mizungu, misimu na vitendawili.

(a) Methali

Methali ni semi za kimapokeo zenye hekima na busara zinazoelezea falsafa na uzoefu wa jamii fulani kwa muhtasari. Semi hizi hubeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Methali hutumika kusisitiza, kuelimisha, kuonya au kupongeza kwa njia za busara. Aghalabu, methali hujengwa kwa sitiari. Sitiari hizo hujitokeza katika pande mbili za methali ambazo hubainishwa kwa mkato. Angalia mifano ifuatayo:

(i) Mtaka yote kwa pupa / hukosa yote.
(ii) Usipoziba ufa / utajenga ukuta.
(iii) Aisifuye mvua / imemnyea.
(iv) Chanda chema / huvikwa pete.
(v) Mtaka cha uvunguni / sharti ainame.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 42 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mifano ya hapo juu inaonesha kuwa methali hubeba dhima mahususi. Kwa mfano, methali (i) inawaasa wanajamii kutofanya mambo mengi kwa wakati mmoja. Ni vema kumakinikia jambo moja ili kulifanya kwa ufanisi, ndipo uanze jambo jingine. Katika mfano (ii), jamii inaaswa kurekebisha tatizo katika hatua za mwanzo, yaani kabla madhara makubwa hayajatokea.

(b) Misemo

Misemo ni tungo zitumiazo picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi ili kuelimisha au kuadilisha. Misemo hufananisha maisha na matukio au vitu. Wakati mwingine, misemo hutumika kutambulisha mazingira maalumu au kujulisha hadhira wakati au mahali fasihi hiyo ilipotungwa. Angalia mifano ifuatayo:

(i) Bendera hufuata upepo.

(ii) Elimu ni bahari.

(iii) Ukubwa jalala.

Mfano (i) unaonesha hali ya maisha, ambapo wapo watu ambao hufuata mkumbo bila kufikiria au kuhoji kwa nini wanafanya jambo fulani na, hatimaye, kujikuta kwenye matatizo. Katika mfano (ii) elimu inafananishwa na bahari. Bahari ni kubwa, na haina mwisho, vivyo hivyo na elimu. Elimu hutupatia maarifa na ujuzi wa aina mbalimbali. Pia, elimu haina ukomo. Binadamu hujifunza kila siku. Mfano (iii) unalinganisha hali ya mtu kuwa mkubwa wa umri au cheo, na kutupiwa lawama hata kama hajatenda kosa, kama lilivyo jalala ambapo watu hutupa taka.

(c) Nahau

Nahau ni fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana za kawaida za maneno hayo. Kwa kawaida, nahau huanza na kitenzi wakati misemo huanza na nomino. Mifano ya nahau ni:

(i) Kujikaza kisabuni (kuvumilia)

(ii) Piga kikumbo (sukuma)

(iii) Kula bakora (kupewa adhabu ya viboko)

(iv) Tia chumvi (shadidia kupita kiasi)

Ukichunguza mifano hiyo hapo juu, utaona kwamba nahau huhitaji ujuzi wa maarifa ya kiutamaduni na kimazingira ya lugha husika ili kuzielewa. Nahau hutumika kupunguza ukali wa maneno, kupamba lugha na kuhifadhi amali za jamii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 43 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Mizungu

Ni kauli zenye mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio. Mbali na vitendawili vya kawaida, kuna vitendawili vingine vijulikanavyo kama mizungu. Hii hutumia zaidi mafumbo. Kwa mfano inaelezwa kwamba mtu hawezi kumwoa ndugu wa damu. Ukinzani huu umetumika kuonya ndugu wasiwe na uhusiano wa kimapenzi. Mizungu hutumia mafumbo ya hali ya juu, hivyo, hutumiwa na watu wazima katika miviga ili kueleza dhana na mawazo mbalimbali kwa maongezi au nyimbo. Mizungu hutumia lugha ya picha inayoonesha ukinzani wa fikra. Ukinzani husaidia kumfikirisha msikilizaji na kumpa changamoto ya kutafuta jibu. Mifano mizuri ya mizungu ni:

(i) Ua zuri sana limeota kwenye miiba; hivyo, huwezi kulichuma.

(ii) Papai limeiva nyumbani, ila siwezi kulila.

(e) Mafumbo

Mafumbo ni kauli au maelezo yanayoficha maana ambayo humtaka msikilizaji kuyafumbua. Kwa mfano, watu wanamteta mtu, mtetwaji akawa anakuja mahali walipo, mmoja wao anaweza kusema *wifi kaja* au *shangazi kaja*. Hii huwasaidia kubadilisha maongezi baada ya kufumbua *wifi* au *shangazi* kuwa ndiye mtu anayetetwa ingawa mtu huyo si wifi wala shangazi wa mtu yeyote katika kundi hilo.

Aidha, kwenye mazingira ambapo watu wanaongea lakini hawataki mmoja wao ajue maongezi yao, labda kwa sababu ni domokaya, mmoja wao anaweza kuwatahadharisha kwa kusema hivi, *Ooho! Mkorosho umeanguka!* Inabidi waelewe kwamba "mkorosho ulioanguka" ni mmoja wao. Hivyo, wataongea kwa tahadhari kubwa. Aghalabu, mafumbo mengi huwa ni kejeli dhidi ya watu wenye tabia mbaya.

Mafumbo yana malengo ya kuelimisha, kuburudisha, kukosoa na kuonya kuhusu mambo yanayotendeka miongoni mwa wanajamii.

(f) Lakabu

Lakabu ni majina ya kupanga (ambayo sio halisi) ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipa kutokana na sifa zao za kimaumbile, kinasaba, kitabia, kiujuzi au kimatendo. Majina haya huwa na maneno yenye maana iliyofumbwa, yaani maana ya kisitiari. Majina haya huwa na dhima ya kusifia, kukosoa au hata kudhalilisha. Angalia mifano ifuatayo:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 44 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) *Baba wa Taifa* - J. K. Nyerere (Rais wa Kwanza wa Tanzania)
(ii) *Simba waVita* - Mzee Rashid Kawawa
(iii) *Komandoo* - Dkt. Salmin Amour
(iv) *Kulakulala* - Mvivu
(v) *Jembe* - Mchapakazi

Wasanii wengi hujipa majina ya kilakabu. Mathalani, Mrisho Mpoto (*Mjomba*), Naseeb Abdul (*Diamond/Simba*), Judith Wambura (*Binti Machozi/Lady Jay Dee*) na Joseph Mbilinyi (*Mr. II/ Sugu*). Pia, waganga wa tiba mbadala hutumia majina ya namna hii, mfano Steven Ngonyani (*Prof. Maji Marefu*).

(g) Misimu

Misimu ni semi ambazo huzuka mahali au kipindi fulani kisha hutoweka. Misimu huambatana na matukio au shughuli zinazotokea katika jamii. Aghalabu, misimu hutumiwa na makundi mahususi ya kijamii, hususani yanayoendana kikazi, kirika au kimasomo. Misimu mingi haina maisha marefu. Ikidumu, husanifiwa na kuingizwa katika matumizi ya lugha husika. Tazama mifano ifuatayo:

(i) *Fataki* - mtu mzima anayefuata watoto/vijana kwa nia ya kufanya nao mapenzi.
(ii) *Marioo* - vijana wanaoishi kwa kuwategemea wanawake wanaowazidi kipato.
(iii) *Kutema ngeli* - kuongea Kiingereza vizuri.
(iv) *Bodaboda* - pikipiki inayotumiwa kusafirisha watu/mizigo kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa malipo.

Ijapokuwa misimu katika mifano (ii) na (iii) inatumika katika jamii, haijaingizwa katika matumizi rasmi. Mifano (i) na (iv) inaonesha misimu ambayo imesanifiwa na kuingizwa katika matumizi rasmi.

(h) Vitendawili

Vitendawili ni semi fupi fupi za mafumbo zenye kutumia lugha ya picha, tamathali na ishara kueleza jambo lililofichika. Jambo hilo ndilo jibu la fumbo. Kwa kawaida, kitendawili hupewa jibu kwa neno moja au zaidi au maelezo. Kama ilivyo katika kazi nyingine za fasihi, vitendawili hutumika

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 NA 6 (KWANDANI).indd 45 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuburudisha, kuelimisha, kupamba lugha, kukosoa au hata kukejeli. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Pango langu limejaa mawe–**kinywa**.

(ii) Nyumba yangu ina nguzo moja - **uyoga/mwavuli.**

(iii) Blanketi la babu lina chawa - **mbingu na nyota.**

(iv) Bibi amejitwisha machicha ya nazi - **mvi**.

Uundaji wa vitendawili hutegemea mazingira ambako kitendawili hicho hutumika. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Watoto wa sultani wamevaa kofia.

(ii) Nimenunua sungura nimemvika kofia.

(iii) Nikune kichwa nikupe moto.

Jibu la vitendawili hivi vyote ni **njiti ya kiberiti**.

Tofauti ya vitendawili (i), (ii) na (iii) inatokana na mazingira. Kitendawili (i) kimeundwa katika mazingira ambayo sultani aliwahi kuishi. Kitendawili (ii) kimeundwa katika sehemu yenye wafugaji au pori lenye sungura. Kitendawili (iii) kimeundwa katika mazingira yanayoakisi udugu, ambapo ni rahisi mtu kuomba kukunwa kichwa.

3. Ushairi

Ushairi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao huwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya uimbaji au ughani badala ya usemaji wa kawaida. Ushairi hujipambanua na tanzu nyingine za fasihi simulizi kutokana na matumizi ya mizani, lugha ya mkato, lugha ya mafumbo na uimbaji au ughani. Ushairi una vipera vitano; vipera hivyo ni nyimbo, mashairi, ngonjera, maghani, na tenzi.

(a) Nyimbo

Nyimbo ni tungo za kishairi zinazowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi na melodia, na inayozingatia mapigo ya kiurari. Mahadhi au tuni ni sauti mahususi ya uimbaji wa wimbo fulani, na melodia ni mpangilio na mwendo wa uimbaji wenye kuzingatia urari wa mapigo au ridhimu. Nyimbo huweza kuimbwa na kuchezwa pamoja na ala za muziki. Nyimbo huimbwa na mtu mmoja au kundi la watu. Wakati mwingine, kikundi cha waimbaji huwa na kiongozi na wafuasi wake. Kiongozi huanzisha wimbo, halafu wafuasi huitikia mkarara. Kiongozi wa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 46 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nyimbo huitwa manju. Nyimbo zinaainishwa kwa kuzingatia dhima, hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana nazo. Kutokana na vigezo hivyo, tunapata baadhi ya aina kama ifuatavyo: tumbuizo, bembea, kongozi, nyimbo za dini na wawe. Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu aina hizi:

(i) *Tumbuizo* ni nyimbo za furaha ziimbwazo katika matukio mbalimbali kama vile harusini na ngomani.

(ii) *Bembea* ni nyimbo za kubembeleza watoto.

(iii) *Kongozi* ni nyimbo za kuaga na kukaribisha mwaka.

(iv) *Nyimbo* za dini ni nyimbo zinazoimbwa kwa lengo la kumsifu Mungu au miungu.

(v) *Wawe* ni nyimbo za kilimo; zinapatikana karibu katika makabila yote ya Tanzania.

(b) Mashairi

Mashairi ni tungo zenye kuelezea au kuonesha kwa ufupi wazo au jambo au hisi fulani kuhusu binadamu na mazingira yake. Mambo hayo huelezwa katika mpangilio maalumu wa maneno fasaha yenye muwala, aghalabu kwa lugha ya kitamathali yenye kugusa moyo. Tunaposema mpangilio wa maneno tunamaanisha kuwa mpangilio wa maneno katika shairi hufuata kanuni tofauti na ule wa nathari. Si lazima shairi kufuata kanuni za miundo ya sentensi inayotumika katika lugha husika. Mathalani, badala ya kuandika *usikate tamaa maishani* tungo hii inaweza kuandikwa *maisha usikate tamaa*, mpangilio ambao unakubalika katika shairi. Mbali na kuzingatia mambo hayo yanayohusu ushairi kwa jumla, ushairi simulizi una sifa ya kutungwa papo kwa papo na kufungamana na muktadha au tukio mahususi. Wakati mwingine, ushairi simulizi huambatana na ala za muziki. Kwa mfano, baadhi ya tungo za taarabu ni ushairi simulizi. Ufuatao ni mfano wa beti za wimbo wa taarabu:

Macho yanacheka, moyo unalia

Macho yanacheka, moyo unalia x4
Nikimkumbuka, wangu maridhia x4
Chozi hunitoka, kwa zake tabia x4
La la la la la oooh!

Nenda nateseka, nalia na njia x3
Siku zikifika, kukugeukia x4

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 47 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Waja hangaika, ulie na njiax4
La la la la la oooh!

(Shakila Said, miaka ya 1960)

(c) Ngonjera

Ngonjera ni neno la Kigogo lenye maana ya "twende pamoja" au "tuambatane." Baadhi ya wataalamu wanasema kipera hiki kilikuwapo toka zamani na kina historia ndefu. Ila kilihuishwa mwishoni mwa miaka ya 1960 na Mathias Mnyampala katika harakati zake za kuelezea siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Ngonjera ni mazungumzo au majibizano ya kishairi kuhusu mada fulani. Kwa maana hii, ngonjera haziimbwi, husemwa bila kutazama karatasi au kitabu chochote. Aghalabu, majibizano hayo huwa na washiriki wa pande mbili, upande wa wanaopinga na upande wa wanaotetea hoja. Wahusika hawa hutumia lugha ya ishara pamoja na miondoko ya mwili kama vile mikono, macho na midomo. Kutokana na wahusika kutumia miondoko, ngonjera huitwa ushairi wa maigizo. Katika ngonjera, suluhisho hupatikana mwisho wa majibizano, ambapo pande mbili zinazopingana hukubaliana. Ingawa ngonjera za Mathias Mnyampala ni fasihi andishi, lakini ngonjera hupatikana pia katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Mfano mzuri ni majibizano ya Amiri Andanenga (Sauti ya Kiza) na Abdallah Matawa (Mbwenzi) ambayo yalifanywa kishairi, ubeti kwa ubeti, papo kwa papo (Tazama *Elimu ya Bahari ya Ushairi* (Amiri Andanenga, 2002:117-119)

(d) Maghani

Maghani ni tungo za ushairi zinazotongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji. Maghani hutongolewa kwa kutumia mapigo ya mwendo na kasi inayokubalika. Kiimbo cha sauti hupangiliwa ili kuleta ladha na maana katika maghani. Wakati mwingine, kiimbo cha kati (ambacho si cha juu wala cha chini) hutumiwa. Kina cha juu na cha chini cha sauti katika kiimbo hurudiwa ili kuburudisha na kuweka uzito katika maana. Mfano mzuri wa maghani ni utambaji wa majigambo na tendi simulizi, kama zile za *nanga* (Ukanda wa Ziwa) na *zeze*.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 48 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Tenzi

Tenzi ni tungo ndefu zinazoeleza tukio fulani linalotokea au lililowahi kutokea katika jamii; au zinazofafanua jambo au fikra fulani. Tenzi huwa na kisa kimoja kinachoelezwa kwa kina. Kisa hicho kinaweza kuwa ni maelezo kuhusu wasifu wa mtu fulani, jambo fulani la kihistoria au jambo lolote. Sifa ya kusimulia au kuelezea jambo kwa urefu ndio husababisha tenzi kuwa na beti nyingi kuliko mashairi au aina nyingine za ushairi. Tenzi za wasifu au matukio ya kishujaa huitwa tendi.

Utendi ni utenzi wa matendo wenye masimulizi kuhusu mashujaa. Kimuundo, tenzi simulizi huwa na muundo wenye kufungamana na mahadhi ya ala ya muziki inayotumika au melodia ya uimbaji. Kwa kawaida, hazina urari wa vina na mizani. Tenzi zenye urari wa vina na mizani ni zile zenye kufuata kanuni za ushairi andishi wa Kiswahili japo chimbuko au utungaji wake ni wa kisimulizi. Mifano ni *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (Mugyabuso Mulokozi, 1997) na *Utendi wa Fumo Liyongo* (Muhammad Kijumwa, 1913) katika *Tenzi Tatu za Kale* (Mh. Mugyabuso Mulokozi, 1999). Katika tenzi hizo, mishororo haikugawanywa katika vipande viwili. Kila ubeti huwa una mistari minne; mistari mitatu ya kwanza ikiwa na vina vyenye urari sawa na ule wa mwisho ukiwa na kina tofauti. Pamoja na vina hivyo kuwa na urari sawa, hubadilika toka ubeti mmoja hadi ubeti mwingine. Kina kinachorudiwa katika mstari wa mwisho, huitwa kina bahari. Ufuatao ni mfano wa beti za *Utendi wa Fumo Liyongo* ambao unatokana na utendi simulizi:

Niweleze kwa utungo,
Hadithi yake Liyongo,
Niweleze na mazingo,
Mambo yalomzingiya.

Liyongo kitamakali,
Akabarighi rijali,
Akawa mtu wa kweli,
Na haiba kaongeya.

Kimo kawa mtukufu,
Mpana sana mrefu,
Majimboni yu marufu,
Watu huya kwangaliya.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 49 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ni mwanamume swahihi,
Kama simba unazihi,
Usiku na asubuhi,
Kutembea ni mamoya.

Kisa katiti kutuwa,
Mkobani akatowa,
Zitu alizotukuwa,
Nyumba ndima nisikiya

Katowa kinu na mti,
Na jiwe na kupaza kuti,
Na zunguze si katiti,
Na mawe ya kupikiya.

Mohammed Kijumwa katika *Tenzi Tatu za Kale* Mugyabuso Mulokozi [Mh] (2012)

Beti hizi ni sehemu ya masimulizi ya kiutendi yanayomhusu Fumo Liyongo. Masimulizi haya yanaakisi maudhui ya kipindi cha miaka ya 900-1500 BK. Hivyo, lugha iliyotumika ni ile inayoakisi kipindi hicho. Masimulizi hayo yanahusu masuala kama vile nguvu za kimwili, kiakili, kisihiri, kivita na kiume (urijali).

4. Sanaa za Maonesho

Sanaa za maonesho zinajumuisha sanaa ambazo huwasilisha wazo ana kwa ana kwa kutumia usanii wa utendaji. Utanzu huu hujumuisha kipera chochote chenye mambo yafuatayo:

(i) Dhana ya kutendeka (tendo)
(ii) Mtendaji (fanani)
(iii) Uwanja wa kutendea (jukwaa)
(iv) Watazamaji (hadhira)
(v) Kusudio la kisanaa (maudhui).

Hivyo, sanaa za maonesho huwa kwenye umbo linalotendeka. Sanaa za maonesho huweza kugawanyika katika makundi mawili ambayo ni sanaa za maonesho za jadi na sanaa za maonesho mamboleo. Sanaa za maonesho za jadi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni zile zilizochipuka katika jamii za Kiafrika (Tanzania). Sanaa hizi hujumuisha ngoma, matambiko, majigambo na miviga. Ingawa miviga kama vile ibada, sherehe, jando na unyago ni matukio ya kijamii au kimila yenye kuvuka mipaka ya kisanaa, lakini inajumuishwa hapa kwa kuwa sanaa hutawala utendaji na uwasilishaji wa maudhui yake. Wakati wa uwasilishaji wa shughuli hizi, watu hufanya vitendo vya kisanaa kama vile uigizaji wa visasili, uchezaji ngoma, uimbaji na utongoaji mashairi, vikiambatana na matendo ya mwili. Kwa njia hii, watu huweza kuwasiliana wao kwa wao au kuwasiliana na miungu. Ijapokuwa dhima ya sanaa hizi hufanana kwa namna ya jumla, huwa kuna tofauti mahususi katika vipengele vya utendaji kati ya jamii au kabila moja na jingine.

Wakati wa ukoloni, sanaa za jadi, hasa zile zilizohusiana na imani za dini, zilipigwa vita. Hali hii ilisababisha sanaa kama vile matambiko kupotea katika baadhi ya jamii. Sanaa nyingine zimedumu mpaka leo kutokana na wito wa kitaifa wa kudumisha utamaduni wa Kitanzania.

Sanaa za maonesho mamboleo ni zile zilizotokana na athari za ujio wa wageni. Sanaa za namna hii ni vichekesho na maigizo. Vipera vya sanaa za maonesho za jadi ni majigambo, miviga, vichekesho, ngomezi, tambiko, utani, maigizo na michezo ya watoto.

(a) Majigambo

Majigambo ni masimulizi ya kujisifia au kujikweza kwa mtu kuhusu mambo aliyowahi kufanya. Mambo hayo huwa ni ya kishujaa kama vile kupigana vita na kuua wanyama wakali. Kwa kawaida, majigambo husimuliwa katika lugha ya kishairi. Mjigambi hufanya matendo mbalimbali. Aghalabu, mjigambi hubeba silaha kama vile mkuki na ngao au upinde na mishale. Kama mjigambi ametoka kuua simba, kwa mfano, ataonesha matendo ya jinsi alivyopambana na simba hadi kumshinda.

Makabila yenye sanaa za majigambo ni yale ya Ukanda wa Ziwa (kama vile Wakurya, Wasukuma na Wahaya), yale ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania, hususani Wahehe, na ya Kaskazini mwa Tanzania, hasa Wamasai. Majigambo hufanyika wakati wa sherehe za harusi na za kuwapokea au kuwapongeza mashujaa. Pia, hufanyika kwenye mikutano inayoitishwa na watawala. Majigambo huambatana na ngoma na nyimbo za kusifu. Mjigambi hutokea katika kikundi kinachocheza na kujigamba; amalizapo, mjigambi mwingine hufuata. Mara nyingi, mjigambi wa mwisho huwa ni

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 51 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yule aliyetenda jambo la kishujaa kuliko wote au yule anayeijua vizuri sanaa ya majigambo.

Lengo kuu la majigambo ni kujenga ari ya ushujaa, ukakamavu na ujasiri. Mtu anayefanya kitendo cha kishujaa, hushangiliwa na kupewa heshima kubwa katika jamii yake. Kwa msingi huu, vijana huhamasika kuwa jasiri na wakakamavu ili kulinda hadhi na heshima ya jamii zao. Ikumbukwe kuwa, kwa kawaida, wanaojigamba ni wanaume tu; katika jamii nyingi mwanamke haruhusiwi kujigamba hata akifanya kitu cha kishujaa. Hii inatokana na ukweli kwamba, katika jamii nyingi washiriki wa ngoma za kujigamba huwa wanaume. Aidha, katika mazingira mengine yaliyotumika kujigamba, wanawake hawakuruhusiwa kuwapo, mathalani, kwenye vikao vya pombe. Kwa ujumla, majigambo ni sanaa ya wanaume ambayo inalenga kudumisha utu na heshima yao katika jamii. Ufuatao ni mfano wa majigambo kutoka katika wimbo wa "Ndiyo Mzee":

Ok ok naitwa **Joseph Haule mwana Msolopagazi**
Nadhani nimeletwa kuokoa hiki kizazi
Mimi ni mwanasiasa niliyebarikiwa na Mungu
Nimeletwa kwenu waungwana niwapunguzie machungu
Mimi ni mteule **Kusini mwa jangwa la Sahara**
Ndio maana nimetunukiwa cheti cha juu cha utawala
Nina hekima kuliko mfalme Sulemani msiwe na wasi
Na hii nitadhihirisha pindi mtakaponipa nafasi
Actually, nimedhamiria kuwasaidia
Taifa lenye nguvu duniani liwe Tanzania

Haule 'Profesa Jay', *Machozi, Jasho na Damu* (2001)

Katika dondoo hili, msanii anajigamba kuwa anatoka katika nchi ya Kusini mwa Jangwa la Sahara. Zaidi, anajigamba kwamba anatoka katika ukoo wa Msolopagazi (*Umslopogaas*). Kwa mujibu wa Samwel (2012), Msolopagazi ni mhusika wa Kizulu katika riwaya ya *Allan Quatermain* iliyoandikwa na (Ridder Haggard). Katika riwaya hiyo, Msolopagazi anaambatana na Wazungu (Sir Henry Curtis na John Good). Anamsaidia rafiki yake, Allan Quatermain, katika safari zake barani Afrika. Katika wimbo huu, Joseph Haule, ambaye ni Mngoni, anajinasibisha na chimbuko lake la Afrika Kusini kama historia inavyotufundisha. Kwa hiyo, katika majigambo haya, msanii anahifadhi historia hiyo ya jamii yake.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 52 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Matambiko

Matambiko ni ibada zinazoambatana na utoaji wa sadaka kwa Mungu, miungu na mizimu. Tangu zamani, jamii mbalimbali zilifanya matambiko ili kutoa shukrani, kusifu, kuomba msamaha na kutatua matatizo. Tambiko ni tukio halisi ambalo hutendwa kisanaa, ndiyo maana linaingizwa katika kundi la sanaa za maonesho. Usanii wa tambiko hutokana na uzingatizi wa vipengele vifuatavyo: maleba, umri, mandhari, malengo, hatua na namna (ya kunena na kutenda). Kwa kawaida, matambiko hufanywa na watu maalumu katika jamii zao. Matambiko hufanyika katika mandhari maalumu. Kwa mfano, watambikaji katika baadhi ya jamii za Kanda ya Ziwa huelekeza maombi yao kwa *Namhanga* (Mungu Mkuu), *Mugasa* (mungu wa wavuvi) au *Kalungu* (mungu wa wawindaji). Utendaji wa tambiko hili huenda sanjari na matumizi ya maleba, vyungu na pembe maalumu. Sadaka zinazotolewa hujumuisha kuku, mbuzi, kondoo, ng'ombe, vyakula vya nafaka na pombe iitwayo na Wakerewe *empahe*.

(c) Miviga

Miviga ni sherehe au shughuli zinazofanywa na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka au katika muktadha maalumu. Sherehe hizo zinaweza kuwa za jando na unyago, kutawazwa kwa Mtemi au harusi. Miviga huwa ni sherehe zihusuzo mtu kutoka katika kundi au wadhifa fulani na kuingia katika wadhifa mwingine. Mathalani, anaweza kutoka katika rika la utoto kwenda ujana (jando na unyago) na ujana kwenda utu uzima (kuoa au kuolewa). Kadhalika, miviga ni matendo ya kimila ambayo wakati mwingine huhusisha sehemu kubwa ya jamii.

Miviga huambatana na maigizo na nyimbo zinazoendana na tukio husika. Katika harusi, nyimbo zinazoimbwa ni za ndoa na katika mazishi nyimbo zinazoimbwa ni za maombolezo. Katika miviga, ngoma mbalimbali huchezwa. Aghalabu, wazee hutoa mafunzo na mawaidha, hususani kwa watoto na vijana.

(d) Vichekesho

Vichekesho ni aina ya sanaa ya fasihi simulizi ambayo watu hutoa vihadithi vifupi ambavyo huwafanya wasikilizaji na watazamaji wacheke. Vichekesho vinahitaji ubunifu mkubwa ili kupata jambo litakaloibua hisia na kuvunja mbavu. Lugha inayotumika katika vichekesho ni nyepesi na iliyojaa picha ambazo watazamaji wana uwezo wa kuzitambua. Hii ni kwa sababu hutumia

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 53 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mifano ya vitu vinavyojulikana wazi kwa hadhira au vinavyopatikana katika mazingira yao. Aidha, vichekesho hutumia mbinu ya kejeli na chuki.

Kama ilivyodokezwa katika maelezo ya sanaa za maonesho kwa ujumla, vichekesho ni mojawapo ya sanaa mamboleo; vichekesho vimetokana na kuletwa kwa tamthiliya za kizungu. Tamthiliya hizi zilibeba na kuongelea utamaduni wa kizungu. Baadhi ziliongelea matatizo ya kijamii ya wakati wa ukoloni, mathalani suala la mgongano kati ya miji na shamba, na uzuzu au ushamba wa Mwafrika anayetoka kijijini na kuingia mjini kwa mara ya kwanza. Maigizo hayo hayakuwa na maana kubwa kwa Waafrika zaidi ya kuwachekesha kupitia katika vitendo vilivyofanywa kwenye jukwaa. Kwa hiyo, Waafrika wakadhani kuwa jambo muhimu katika vichekesho ni kuchekesha.

Kimsingi, dhima ya vichekesho si kuchekesha tu, bali vichekesho huelimisha pia. Mifano ya vichekesho ni kama ile inayopatikana katika vipindi vinavyorushwa na vituo vya redio na televisheni. Mifano ya vipindi vya kwenye televisheni ni *Mizengwe* (ITV), *Ze Comedy* (EATV) na *Vitimbi Show* (Channel Ten).

(e) Ngomezi

Hii ni sanaa ya kuwasiliana kupitia midundo ya ngoma. Baadhi ya makabila huweza kupeana taarifa za matukio mbalimbali kupitia ngoma. Aghalabu, taarifa hizo huwa katika hali ya mafumbo, kiasi kwamba, wenyeji wa jamii husika tu huweza kubaini maana ya midundo husika. Hii yatokana na ukweli kuwa midundo katika sanaa hii hufuata kanuni maalumu zinazojulikana na wanajamii hao tu. Kanuni hizo hubebwa kupitia vipengele vya aina ya ngoma zinazotumika, muda wa kupigwa kwa ngoma pamoja na kasi au mwachano wa upigaji. Kanuni hizi huwasaidia wanajamii kupata ujumbe unaowasilishwa. Kwa mfano, katika jamii ya Wayao kuna ngoma ya Ngulantwe inayopigwa kwa ajili ya kutoa ujumbe kuhusu matukio mbalimbali ya kitanzia. Ujumbe huo huweza kuwa: "Simba amevamia na kuua mifugo", "Simba amejeruhi mtu ila hajamuua", "Simba ameua mtu", au "Kesho wanaume wote wanatakiwa kwenda kwenye msako wa simba mvamizi."

(f) Utani

Ni hali ya kufanyiana mizaha au masihara baina ya watu ambapo hali hii ni tofauti na desturi za kutokuheshimiana. Wanajamii wenye uhusiano wa kutaniana, hutaniana mahali popote wakutanapo kama vile msibani,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 54 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

harusini, hata kwenye sehemu za kazi. Utani huweza kuwa kati ya mtu na mtu, ukoo na ukoo au kabila na kabila. Utani kati ya mtu na mtu huwa ni kati ya babu/bibi na wajukuu, mtu na shemeji au wifi na wifi. Kadhalika, utani kati ya kabila na kabila, aghalabu, huwa kati ya makabila yenye asili ya kuishi katika eneo moja au yaliyokuwa na maingiliano ya muda mrefu. Makabila yote ya mkoa wa Mara, kwa mfano, ni watani wa Wanyaturu na Wanyiramba (Singida) na Wahaya (Kagera).

Utani hujenga uhusiano na ushirikiano mzuri baina ya wanajamii. Vilevile, utani hutunza historia ya jamii zinazotaniana. Aidha, utani huwafunza watoto upendo na majukumu, mathalani, utani wa mjukuu wa kike na babu anapomwita mke wake na kuomba amfanyie jukumu fulani, mtoto huyo hujifunza jukumu lake atakalolitekeleza akiwa mkubwa.Vilevile, utani hukumbusha wanajamii majukumu yao. Mathalani, katika misiba, watani hutumia tukio kukumbusha watu kujuliana hali wanapokuwa wazima na kusaidia kazi zihusuzo msiba. Kama zilivyo dhima nyingine za fasihi, utani huburudisha kwenye matukio ya furaha na huzuni. Ikumbukwe kwamba, utani unaweza kusababisha ugomvi endapo mhusika hajui kuwa anayemfanyia mzaha ni mtani wake.

(g) Maigizo

Maigizo ni sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha au kutoa ujumbe fulani. Maigizo haya yanapoletwa jukwaani na kuoneshwa kwa hadhira huitwa drama. Mara nyingi, maigizo ya Kiafrika huambatana na utambaji wa hadithi, vichekesho, nyimbo, matendo ya kijadi kama vile harusi, jando na unyago. Wahusika hutakiwa kutumia lugha ya kifasihi inayoendana na hadhira. Zipo aina mbalimbali za maigizo zikiwamo: maigizo ya misibani na mivigani, maigizo ya watoto na ya burudani.

(h) Michezo ya watoto

Watoto hucheza michezo mingi yenye kuambatana na usanii. Michezo hiyo hutofautiana majina kulingana na mahali. Katika michezo hiyo, kuna kuimba, kucheza, kurukaruka, kukimbia, kughani, kujigamba na kuigiza. Baadhi ya michezo hiyo ni: *kiota*, *ukuti*, *pembea* (*bembea*), *kitikiti*, *kibuzi* na *kombolela*. Michezo hiyo inawekwa hapa kwa sababu aghalabu huambatana na nyimbo, majibizano, vitendo na maigizo. Kwa mfano, katika mchezo wa *kiota*, watoto hunyanyuka pale walipoketi na kuanza kutangatanga huku na

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huku ilihali wakiimba mpaka kila mmoja anapopata mahali pake na kukaa. Watoto huimba hivi:

Kiota

Sisi ndege twaruka
Twatafuta kiota
Kiota
Kiota
Kiota
Ta la la la la la
Kiota

Wimbo wa mchezo huu umetumia mbinu za takriri, urari na uimbaji mbali na kuambatana na vitendo vya kutembea na kuzunguka. Michezo mingi ya watoto huunganisha sanaa ya uimbaji na vitendo.

Mchezo mwingine ni wa kubembea kwenye kamba. Mchezo huu huambatana na wimbo wa "Pembea". Ufuatao ni wimbo huo uliorekodiwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita:

Pembea

Pembea iyo pembea
Pembea iyo pembea
Wewe Maasisi
Kalaga hasi pembea
Mtama ukigwa pembea
Tule tuta pembea
Tuta kaya pembea
Ya mgambo pembea

Amiri Andanenga, *Bahari ya Elimu ya Ushairi* (2002: 168)

Pia, kuna mchezo wa "Kibe." Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike na wa kiume ambao hujipanga katika mistari miwili inayotazamana. Uchezaji wake huambatana na wimbo. Wachezaji huongozwa na kiongozi kuimba na kucheza. Kiini cha uchezaji wake hubebwa na vitendo vya kila mmoja kuchagua mwenza kutoka mstari wa wachezaji wa jinsi tofauti. Ufuatao ni wimbo wenyewe:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 56 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wimbo wa "Kibe"

Kiongozi: Kibee mama kibeeex2
Wote: Hayaaa
Kiongozi: Nilikwenda matembezi
Wote: Hayaaa
Kiongozi: Nikamkuta msichana mrembo
Wote: Hayaaa
Kiongozi: Akaniuliza wenda wapi?
Wote: Hayaaa
Kiongozi: Nikamwambia naenda kurithi matanga
Wote: Hayaaa

Kiitikio:
Haya msichana wa sawa.
Chagua mumeo sawa.
Mumeo akikuita nenda.
Usije ukatonesha donda.

Maigizo ya watoto ni aina nyingine ya michezo ya watoto. Watoto huigiza michezo inayoakisi mazingira yanayowazunguka kama vile nyumbani, shuleni, shambani, hospitalini, barabarani, kanisani, msikitini na porini. Pia, watoto huigiza mambo wanayoyaona kwenye runinga, hasa watoto waishio mijini, mfano michezo ya kivita, sherehe mbalimbali, vikundi vya nyimbo, miziki na michezo ya kuigiza.

Maigizo ya watoto, kama ilivyo kwa kazi nyingine za fasihi, yana vipengele vya fani na maudhui. Maudhui ya michezo ya watoto, kwanza, huhusu maisha ya nyumbani kwa sababu ndiyo maisha wanayoyaona mara kwa mara.Watoto huigiza maisha ya nyumbani kwa kuakisi maisha halisi ya familia, hususani yale wanayoyaona kwenye familia zao. Mathalani, kama baba ni mkali, mtoto atakayeigiza kama baba, ni lazima atakuwa mkali, pengine kuzidi ukali anaouona kwa baba; vivyo hivyo, kama baba ni mpole na mkarimu basi muigizaji ataigiza upole na ukarimu. Kwa upande mwingine, watoto waigizao nafasi ya mama, huakisi tabia ya mama. Ikiwa mama ni mchapakazi, basi muigizaji atakuwa na tabia hiyo; kama ni nadhifu, mwigizaji naye atajitahidi kuwa nadhifu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

Watoto waigizapo sherehe za harusi, hujumuisha matendo kama vile ufungaji wa ndoa. Baada ya kufunga ndoa, huigiza kwenda ukumbini au eneo lolote ambapo sherehe za harusi hufanyika. Tukio hili huambatana na nyimbo mbalimbali. Nyimbo hizo ni kama:

(i) *Kiongozi*: Anameremeta
Wote: Anameremeta
Kiongozi: Bwana Harusi anameremeta
Wote: Anameremeta
Kiongozi: Bibi Harusi anameremeta
Wote: Anameremeta

(ii) Aiya iya kuolewa, utarudi nyumbani kutembea,
Kwa heri ndugu zangu, kuonana majaliwa
Kwa heri majirani, kuonana majaliwa.

Nyimbo hizi husaidia kuburudisha, kupamba na kuupa mchezo wao hadhi ya kuwa fasihi simulizi. Aghalabu, watoto hupenda kuigiza maisha ya vitimbi na ubabe kuliko kuigiza maisha ya kawaida.

Maigizo ya watoto hubuniwa pale wanapokutana, hakuna matini inayokuwa imeandaliwa kabla ya mchezo. Watoto wanapokutana hukubaliana aina ya mchezo na kugawana uhusika na majukumu ya kila mhusika; wakati mwingine, watoto wenyewe huchagua nafasi watakazoigiza. Uigizaji wa michezo ya watoto huambatana na ubunifu ambapo kila mtoto (mhusika) hubuni uigizaji wa sehemu yake anayoigiza. Maigizo ya watoto huwa na muundo wa moja kwa moja.

Wahusika katika maigizo hayo ni watoto wenyewe ambao hupanga nafasi zao za uhusika kulingana na mchezo wanaoigiza. Katika maigizo yanayohusisha wanyama, kwa mfano, kama igizo lina mhusika Simba, mtoto anayeigiza kama simba, ni lazima awe na sifa za ubabe, sauti nzito na nguvu. Hali kadhalika, atakayeigiza kama jogoo, awe na sauti kali, ili atakapowika isikike.

Aidha, watoto huchagua nafasi kulingana na jinsi zao na jinsi jamii ilivyogawa majukumu ya jinsi hizo. Mathalani, watoto wa kike huchagua nafasi za kuigiza kutokana na kazi ambazo hufanywa na wanawake katika jamii kama vile uuguzi, uyaya,upishi,ufanyaji usafi na ukatibu muhtasi.Vivyo hivyo, watoto wa kiume

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huchagua nafasi za kuigiza kutokana na kazi ambazo hufanywa na wanaume kama vile udereva, urubani, kuchinja na kuuza nyama, uaskari na kazi nyingine ngumu. Kupitia michezo hii, ndimo ndoto za watoto huchomoza na watoto wengine huanza kuishi na ndoto zao. Maigizo ya watoto hayahitaji maleba mahususi.

Dhima za michezo ya watoto

Michezo ya watoto ina dhima nyingi kwa watoto wenyewe. Zifuatazo ni baadhi ya dhima hizo:

(i) *Kuchochea ubunifu miongoni mwa watoto*

Michezo ya watoto huwa na sifa za kisanaa kama vile ubunifu, urari wa matukio, uigizaji na matumizi maalumu ya lugha na sauti. Mambo haya huhitaji kiasi fulani cha ubunifu na usanii. Kwa njia hii, watoto hujifunza kuwa wabunifu.

(ii) *Kujenga uwezo wa usimulizi na usemaji wenye ufundi*

Michezo ya watoto huwa na wahusika wanaohusiana ili kuumba mtiririko wake. Uhusiano huu hujengwa kwa njia ya mazungumzo yenye uhalisi. Mathalani, "mama" anapaswa aongee kama mama kweli; hali kadhalika, "baba" aongee kama baba, na wanapoongea waoneshe uhusiano wa "mke" na "mume." Kadhalika, usimuliaji wa matukio na maelezo uwe na ushawishi.

(iii) *Kuchochea umahiri wa lugha*

Baadhi ya michezo hutumia lugha. Maongezi, majibizano na maelezo ya wahusika hujenga uwezo wao wa kutumia lugha kwa njia mbalimbali kulingana na muktadha. Uzoefu huo hatimaye huwajengea umahiri wa kutumia lugha katika maisha halisi.

(iv) *Kuchochea udadisi*

Uumbaji wa mchezo huwafanya wahusika wahoji na kudadisi mambo mbalimbali na kuyatafutia ufumbuzi. Udadisi huo hatimaye huweza kutumika katika maisha halisi.

(v) *Kuburudisha watoto na kuwafanya wawe wachangamfu*

Watoto hufurahi na kucheka wanapokuwa wakitunga na kuigiza au kucheza mchezo wao, kwa mfano *Kachiri* au *Ukuti*. Hizi ni shughuli zinazopumzisha akili na miili yao baada ya shughuli zao za kawaida ambazo, wakati mwingine, ni ngumu na zinachosha.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 59 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) *Kuhimiza umuhimu wa kazi*

Ndani ya michezo ya watoto huwa kuna vitendo vinavyoiga kazi na amali mbalimbali zifanywazo na watu wazima. Kwa njia hii, watoto hujifunza umuhimu wa kazi.

(vii) *Kuibua vipaji mbalimbali vya watoto*

Uigizaji huibua vipaji vilivyolala kwa watoto wenye uwezo wa kuongoza, wengine wana vipaji vya kuongea, kuimba, kukimbia, kuruka kamba na vinginevyo. Vipaji hivyo huweza kujidhihirisha wakati wa michezo hiyo.

(viii) *Kujenga kumbukumbu*

Michezo ya watoto hubuniwa kichwani bila maandishi; kila mhusika hupaswa kutunga maneno au hotuba zake mwenyewe, kukumbuka maelezo ya wenzake, na kuwajibu bila kusahau au kukosea. Kwa njia hii, watoto hujifunza kuwa na kumbukumbu.

(ix) *Kuchochea na kujenga ujasiri*

Baadhi ya michezo huhitaji kiwango cha ujasiri na uthubutu. Kwa mfano, hujenga ujasiri wa namna ya kumkabili mtu mwenye nguvu anayemzidi, anayetaka kumuonea, pamoja na kutoogopa kushindwa.

(x) *Kufundisha watoto majukumu ya baadaye katika maisha*

Kama ilivyoelezwa hapo juu, watoto huchukua uhusika wa watu wazima katika michezo yao. Wengine huwa waume, wake, walezi wa watoto, wakulima, wawindaji, viongozi wa mtaa au kijiji na mengineyo. Kwa njia hii, watoto hujiandaa kuyabeba majukumu hayo pindi watakapokuwa watu wazima.

(xi) *Kujenga uhusiano mwema miongoni mwa wanafamilia*

Michezo ya watoto, mbali na kujenga uhusiano mwema miongoni mwa wanafamilia wenyewe, huweza kuwapanua upeo kuhusu uhusiano unaopaswa kuwapo katika familia au ukoo kwa jumla. Mathalani, kati ya watoto na wazazi, na wazazi na wanandugu.

(xii) *Kujenga moyo wa ushirikiano*

Watoto wanapoigiza au kucheza pamoja hujenga urafiki na hujifunza kushirikiana katika kufanya mambo mbalimbali yenye umuhimu kwao na kwa jamii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(xiii) *Kujenga afya njema kwa watoto*

Michezo ya watoto ni vitendo vinavyotumia mwili na akili. Watoto wanapoigiza huchakarika na kushughulika: husimama, huketi, hulala, huamka, hukimbia na kutembea. Shughuli zote hizi huwajengea afya kimwili na kiakili.

Changamoto za michezo ya watoto

Pamoja na dhima zilizoelezwa hapo juu, michezo ya watoto ina changamoto zifuatazo:

(i) Kupoteza muda wa kufanya shughuli nyingine, hasa kwa watoto wenye umri wa miaka saba na kuendelea. Watoto wa umri huu, wana majukumu mengine kama vile kazi za shule na kazi ndogo ndogo za nyumbani.

(ii) Kusababisha mmomonyoko wa maadili, hasa kwa watoto wenye umri mkubwa kidogo, kuiga tabia na matendo yasiyoendana na umri wao.

(iii) Michezo mingine husababisha kupotea kwa watoto, hasa kwa watoto waishio mijini, endapo watacheza michezo inayowapeleka mbali na nyumbani kwao.

(iv) Kusababisha migogoro kati ya watoto na watoto, wazazi na wazazi; pamoja na migogoro ya namna hii kutodumu, huweza kusababisha hasara fulani kama kuwekeana vinyongo.

(v) Kuibua tabia za ukatili, hasa watoto wakishiriki michezo yenye ubabe.

(vi) Kuhatarisha maisha ya watoto na kusababisha ajali hata kifo.

(vii) Maudhui yake huweza kuendeleza unyanyasaji na ubaguzi wa kijinsia.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 61 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1

(i) Eleza tofauti kati ya ngano na vigano.

(ii) Kwa kutumia mifano anuwai, tofautisha sanaa za maonesho na maigizo.

(iii) Fasili dhana zifuatazo kwa mifano hai:

- (a) hadithi
- (b) misemo
- (c) ushairi
- (d) miviga
- (e) matambiko
- (f) ngoma
- (g) ngomezi

(iv) Jadili athari za utani unaofanyika katika jamii yako.

(v) "Si kila mchezo wa watoto ni fasihi simulizi." Jadili kauli hii kwa hoja maridhawa.

(vi) Kwa namna gani miviga na matambiko ni sanaa au si sanaa za maonesho?

Kazi ya kufanya

Soma mfano ufuatao wa ngonjera iitwayo "BAKITA" kutoka katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* (Amiri A.S. Andanenga, 2002: uk 117-119), kisha tunga ngonjera simulizi yenye beti zisizopungua sita.

BAKITA
Baraza la Kiswahili, lililokuja Dodoma,
Eti kuja kujadili, mambo ya leo na nyuma,
Mnalaumiwa kweli, mliyotenda si mema,
Msizikwepe lawama.
(Mbwezi)

Matawa ukome gubu, kwa tungo zenye viroja,
Ni Muhamedi Khatibu, ufunguzini kutaja,
Bakita ni mahabubu, kwa Lugha ni yenye tija,
Mbwenzi wacha kubwabwaja.
(Andanenga)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 62 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nyote mlokokotwa, kimbelembele kizima,
Nikipi mlichokutwa, kimyakimya kijitoma,
Dhamiri zenu zasutwa, imepungua heshima,
Hata kama washairi
(Mbwezi)

Kamwe hatukuburutwa, donge linakusogoja,
Kwa barua tuliitwa, za kupandishwa daraja,
Wewe Mbwenzi umepetwa, tungo zako ni harija,
Walia kwa kukuchuja!
(Andanenga)

Kumuenzi Mathias, Mzee wetu wa zama,
Pasi kutujuza sisi, washairi wenye dhima,
Ni ukuu wa utusi, ni dalili ya dhuluma,
Mliyotenda si haki.
(Mbwenzi)

Una dhima gani wewe, mambo ungaliyafuja,
Mathias ni wanawe, kizuka chake pamoja,
Walikuwa ndo wenyewe, tungefikwa na mauja,
Ungenusa tafrija.
(Andanenga)

Mngefanya huko huko, katu tusingeloloma,
Yanini malalamiko, mngekutana Kigoma,
Hamuepi maepuko, za haki hizi shutuma,
Mnashutumiwa hasa.
(Mbwenzi)

Matawa siyo mzima, Kichwa chako kinavuja,
Mathias wa Dodoma, Mgogo si Muunguja,
Isingekuwa hekima, kumuenzia Miteja,
Kwa udaku wewe Meja.
(Andanenga)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 63 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mnadhiki ya akili, dira zetu zikipima,
Vipimo vya maadili, utu na tabia njema
Dodoma si mafidhuli, hatuogopi kusema,
Hatuogopi kusema.
(Mbwenzi)

Asodhiki ya akili, pekee Mola mmoja,
Siwo nyinyi ngurumbili, mlao na wenda haja,
Mbogo zenu zimedhuli, kwenye uzembe wateja,
Wewe Mbwenzi ni Meneja.
(Andanenga)

Kitu gani kongamano, upuuzi na unyama,
Wa kupeana mikono, na mgeni wa heshima,
Beti sita ya mabano, na hii ni kaditama,
Tutawaponda daima.
(Mbwenzi)

Waziri kwa zake hima, kwa kufungua akaja,
Na Isdori Shirima, kwa kufunga alikuja,
Wawavunjia heshima, tutosheleze kwa hoja,
Mbwenzi kesi yakungoja.
(Andanenga)

Utunzi wa kazi za fasihi simulizi

Katika mada ndogo ya sifa za fasihi simulizi, ulijifunza kwamba, kwa kawaida, kazi nyingi za fasihi simulizi ni mali ya jamii. Kazi za fasihi ni kazi za kisanaa; hivyo, utunzi wake unahitaji kuzingatia kanuni za sanaa inayohusika. Kwa hiyo, katika mada hii ndogo, utajifunza kanuni mbalimbali za utunzi wa baadhi ya kazi za fasihi simulizi.

Utunzi ni kazi inayohitaji umakini sana. Ni muhimu kwa mtunzi kujua jamii anayoitungia kazi husika. Mtunzi ni mhakiki wa jamii yake katika masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Faida mojawapo ya utungaji wa kazi za fasihi simulizi ni kusawiri na kuhakiki uhalisi wa maisha ya jamii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 64 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba utunzi wa fasihi simulizi hutofautiana na utunzi wa fasihi andishi. Fasihi andishi hutungwa na mwandishi mahususi kwa kutumia kalamu na karatasi (au vifaa bora zaidi kama kompyuta). Mwandishi huyo hujiwekea malengo na kuamua maudhui anayotaka kuyatoa. Akishaandika mswada wake, huweza kuusoma tena kwa makini na kuudurusu au kuusahihisha ili ufikie kiwango anachokitaka. Huweza pia kumpa mtu mwingine amsomee na kumpa maoni au kupendekeza marekebisho. Kwa upande mwingine, mtunzi wa fasihi simulizi ana fursa finyu ya kufanya hivyo. Hivyo, kazi yake hufungamana na muktadha wa utendaji au uwasilishaji. Baadhi ya kazi za fasihi simulizi zinazopata umaarufu huendelea kutumika katika jamii huku zikirekebishwa na kubadilishwa kulingana na wakati.

Utunzi wa fasihi simulizi hutofautiana kwa kutegemea kipera kinachotungwa. Mathalani, utunzi wa nyimbo mara nyingi hutokea wakati wa ngoma au tukio mahususi. Manju huibua wimbo kulingana na muktadha na mahitaji ya wakati huo. Utunzi wa fani nyingine za kishairi, kama tendi na majigambo, huweza kuwa na michakato mirefu zaidi inayoongozwa na kanuni za utunzi simulizi. Utendi au majigambo huweza kuandaliwa kwa kipindi fulani na kufanyiwa mazoezi kabla, na hatimaye kuwasilishwa hadharani.

Kwa upande wa ngano, ni vigumu kujua wakati zinapotungwa. Nyingi hupokewa kutoka vizazi vilivyotangulia, na hubadilika kidogo wakati wa kusimuliwa kulingana na mahitaji ya muktadha huo. Vilevile, semi hupokewa kutoka kwa wahenga na kurekebishwa kidogo kidogo kutegemea muktadha. Semi mpya, zikiwamo methali na vitendawili, huibuka wakati wowote; lakini ni vigumu kujua mtunzi kwa kuwa hazitungwi kwa kukusudia, yaani hakuna tukio mahususi la utungaji wa methali au vitendawili, japo linaweza kuwapo tukio la utambaji wa vitendawili. Methali ni fani tegemezi ambayo huegemezwa kwenye fani nyingine kama hotuba, simulizi na nyinginezo.

Kanuni za utunzi wa kazi za fasihi simulizi

Katika utunzi wa kazi za fasihi simulizi, mtunzi ni lazima awe na jambo linalomgusa kwa kumfurahisha au kumkera. Baada ya kuwa na jambo linalomgusa, mtunzi huliweka jambo hilo hadharani kwa kutunga kazi ya fasihi simulizi. Mtunzi huamua kuhusu fani inayofaa kutumika. Aidha, uamuzi wa fani ya kutumia hutegemea ujuzi na kipaji cha mtunzi katika fani inayohusika.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 65 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Utunzi wa hadithi

Hadithi ni masimulizi yaliyopangiliwa katika mfuatano fulani wa matukio yanayoambatana na matendo ya wahusika. Hadithi hutoa ujumbe fulani katika jamii. Kwa kawaida, hadithi huwa katika lugha ya njazo. Mtunzi wa hadithi ni lazima azingatie kanuni mbalimbali katika utunzi wake. Takribani hadithi zote, ziwe simulizi au andishi, huwa na mambo yafuatayo:

(a) Mfuatano wa matukio yaliyopangiliwa kiwakati au bila kufuata wakati na yenye ukamilifu wa kimasimulizi na kiujumi.

(b) Muundo wenye mwanzo, kati na mwisho. Mpangilio wa matukio yanayosimuliwa kwa namna inayodhihirisha usababishano na hivyo kujenga mgogoro na taharuki.

(c) Wahusika wenye kuwakilisha pande mbili au zaidi za mgogoro wa hadithi na ambao mahusiano na matendo yao ndiyo husukuma mbele hadithi kuelekea kileleni.

(d) Matumizi ya lugha ya masimulizi na maelezo ili kusawiri matukio na migogoro ya hadithi.

(e) Maudhui (mawazo, dhamira, mafunzo na falsafa) yanayoibuliwa na muundo, msuko na lugha inayotumika.

Haya ni mambo ya jumla yanayotarajiwa kuwamo katika hadithi, iwe simulizi au andishi. Kwa kuwa hapa tunazungumzia utunzi wa fasihi simulizi, ni muhimu pia kuzingatia mambo mahususi yanayohusu utunzi simulizi tu. Mambo hayo ni:

(i) Kutokuandikwa;
(ii) Utungaji kichwani kabla ya tukio au papo kwa papo;
(iii) Ufungamano na muktadha; na
(iv) Upokezi na urithishwaji.

Ni vigumu kutunga ngano au hekaya papo kwa papo. Kinachoweza kufanyika ni kuandaa mazingira ya uwasilishaji au utambaji wa hadithi hadharani kutokana na kumbukumbu za watambaji. Kufuatia kutamba ngano hizo, watambaji watakuwa wanatunga kwa maana ya kuziunda upya kwa maneno yao wenyewe, huku wakizihusisha na muktadha husika. Utambaji huo unapaswa kuzingatia taratibu zake zinazofahamika katika jamii husika. Taratibu hizo ni pamoja na: namna ya kuanza (mianzo). Mwanzo huweza kuwa:

(i) *Mtambaji*: Paukwa
Hadhira: Pakawa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 66 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mtambaji: Paukwa
Hadhira: Pakawa
Mtambaji: Hapo zamani za kale…

(ii) *Mtambaji*: Hadithi hadithi
Hadhira: Hadithi njoo, uongo njoo, utamu kolea…
Mtambaji: Hapo zamani za kale
Hadhira: Eeeh!

(iii) *Mtambaji*: Alitokeani…
Hadhira: Naam twaib!
Mtambaji: Alitokeani…
Hadhira: Naam twaib

(iv) Kaondokea chanjagaa
Kajenga nyumba kakaa
Mwanangu Mwanasiti
Kijino kama kijiti
Cha kujengea kikuta
Na vilango vya kupita.

(v) Hapo kale alikuwako/walikuwako…

Na, mwisho unaweza kuwa:

(i) Wakaishi raha mustarehe…..
(ii) Ndiyo maana mpaka leo… (Paka na panya hawapendani au mbwa na mwanadamu ni marafiki, n.k.)
(iii) Na hadithi yangu imeishia hapo…

Utunzi wa ushairi

Ushairi simulizi una vipera vya nyimbo, mashairi, ngonjera na maghani. Vipera vyote hivi vinapotungwa kisimulizi, hutungwa kichwani bila kuandikwa na kuwasilishwa hadharani kwa kusemwa, kuimbwa, kutambwa au kughanwa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 67 17/09/2019 13:20

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Watunzi wa vipera hivi walioathiriwa na ushairi andishi huweza kutunga kwa kufuata kanuni za urari wa vina na mizani, na bado tungo zao zikawa simulizi endapo hazitaandikwa.

Kwa kuwa ushairi simulizi hautungwi kwa kuandikwa, inabidi ufanywe darasani au shuleni kwa vitendo. Mathalani, wakati wa sherehe za shule au darasa, wanafunzi wanaweza kuhamasishwa kutunga na kutamba ngonjera, shairi au maghani mbele ya wenzao. Kama kuna uwezekano, ala za muziki au muziki wa ala uliorekodiwa kabla, unaweza kutumika. Katika utunzi simulizi, matumizi ya lugha, hasa tamathali, ishara na mafumbo hupewa uzito. Vilevile, msanii hujizoeza kuongea au kuimba mbele ya watu, na namna ya kushirikisha hadhira katika utambaji wake.

Mtunzi wa maghani kama majigambo na tendi huongozwa na kaida za sanaa hiyo katika jamii inayohusika. Kwa mfano, muundo wa majigambo katika jamii ya Wahaya hutakiwa uzingatie yafuatayo: jina halisi au la sifa (lakabu) la mjigambi; nasaba na mbari yake upande wa baba; jina la mama yake na nasaba yake; matendo ya ushujaa aliyoyafanya na namna alivyoyatekeleza; hitimisho na kujikabidhi kwa mtemi au kiongozi.

Mtunzi wa tendi sharti afanye utafiti kidogo kuhusu tukio au historia anayotaka kuisimulia. Baada ya kupata taarifa za kutosha, hujaribu kuzisimulia (bila maandishi) kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kulingana na jamii inayohusika.

Utunzi wa maigizo (sanaa za maonesho)

Maigizo ni kipera muhimu cha sanaa za maonesho. Kuna maigizo ya watoto na maigizo ya watu wazima. Maigizo yote hayo ni faraguzi; hutungwa kichwani na hayaandikwi. Kwa kawaida waigizaji hujitungia maneno yao wenyewe wawapo jukwaani. Jambo la muhimu ni kuwa na hadithi au tukio la kuigiza lenye wahusika, mwanzo, kati na kilele. Waigizaji huchagua uhusika wao na kufanya mazoezi hadi wanapojiridhisha kuwa igizo liko tayari kuoneshwa hadharani. Igizo linaweza kuhusu jambo lolote linalowagusa, kuwakera au kuwafurahisha watu. Kwa mfano igizo kuhusu tatizo la utoro shuleni, uhalifu na kadhalika.

Mbali na utaratibu wa kifaraguzi, igizo simulizi lina sifa kadhaa za igizo andishi la kitamthiliya, kama vile wahusika wanaokinzana, mgogoro, mazungumzo na vitendo. Mambo haya sharti yazingatiwe.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Utunzi wa semi

Kama ulivyokwishajifunza, semi ni tungo fupifupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara ili kutoa ujumbe. Ni mafumbo yanayosawiri mandhari kulingana na kipera husika. Semi hueleza mambo kwa muhtasari.

Semi zinazozungumziwa hapa ni za aina mbili: methali na vitendawili. Tunazitumia kuwakilisha semi zote kwa jumla. Kanuni ya msingi katika utungaji wa semi ni kwamba hakuna utaratibu rasmi wa kutunga, bali huibuka katika miktadha mahususi au hupokewa kutoka kwa wahenga. Mathalani, methali huwa katika kumbukumbu za wanajamii kwa muda mrefu na hujitokeza katika matumizi pale tu zinapohitajika. Ifuatayo ni mifano ya methali zinazoweza kukumbukwa na kutumiwa katika miktadha mbalimbali:

(i) Uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti.

(ii) Mwenda tezi na omo, marejeo ni ngamani.

(iii) Ng'ombe akivunjika mguu malishoni, hujikokota zizini.

(iv) Simba mwenda kimya, ndiye mla nyama.

Vilevile, vitendawili huibuka au kukumbukwa wakati wa utendaji wake, maana vyenyewe vina fursa za kutendwa. Mara nyingi, utendaji wa vitendawili hufanywa na watoto, na huwa ni aina ya chemshabongo. Ifuatayo ni mifano ya vitendawili.

(i) Hawapandi wala hawatafuti chakula lakini wanashiba - **mdomo na tumbo**

(ii) Adui mpenzi -**moto**.

(iii) Mgonjwa wa ndui ananing'inia mtini–**fenesi**.

(iv) Tunda langu la ajabu; juu nyama, katikati ngozi, ndani mchanga **firigisi.**

Njia za uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi

Fasihi simulizi huwasilishwa na kuenezwa kwa njia ya mdomo na utendaji. Hii ndiyo njia ya mwanzo kabisa kutumika. Katika njia hii, masimulizi huhifadhiwa kichwani, kisha huwasilishwa kwa hadhira kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano masimulizi ya hadithi, hufanyika kwa jamii au familia. Watu wazima hasa babu au bibi, hukaa pamoja jioni sehemu yenye moto kutegemea na mazingira na kuwasimulia watoto hadithi mbalimbali. Utendaji mbele ya hadhira ndiyo njia kuu ya kuwasilisha na kueneza fani za fasihi simulizi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 69 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesaidia sana katika uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi. Maendeleo haya yamewezesha kuwapo kwa vyombo mbalimbali vya uwasilishaji kama redio, runinga na simu. Redio na runinga zimekuwa na mchango mkubwa katika uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. Redio Tanzania (kwa sasa TBC Taifa) imekuwa na vipindi ambavyo vimesaidia sana fasihi simulizi kuwafikia watu wengi. Kipindi kama vile *Mama na Mwana* kilipendwa na watu wengi, hasa watoto, kwa sababu ya masimulizi ya hadithi mbalimbali. Kipindi kingine ni *Cheichei Shangazi* ambacho kimekuwa na masimulizi ya hadithi, vitendawili na nyimbo. Aidha, kuanzishwa kwa vituo vingine vya redio kumeongeza mawanda ya uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano Redio One Stereo, hurusha kipindi cha *Watoto Wetu* ambacho hupambwa na wimbo maarufu wa *Watoto Wasafi Moyoni.* Kipindi hiki hurushwa kila Jumamosi, ambapo watoto walioko studio na nyumbani huweza kushiriki katika uwasilishaji wa hadithi, methali, vitendawili, mafumbo na nyimbo.

Pamoja na watoto kutoonana ana kwa ana wanaweza kushiriki kwa njia ya kusikiliza. Hivyo, hadithi ambazo awali zilisimuliwa kwa watu wachache, zinaweza kujulikana kwa wote wanaosikiliza. Mbali na vipindi vya watoto, redio zimekuwa zikirusha vipindi vingine vya fasihi simulizi. Baadhi ya vipindi hivyo ni *Mkoa kwa Mkoa*, *Malenga Wetu*, *Ngoma Zetu*, *Zilipendwa*, *Salamu kwa Wagonjwa*, *Mchana Mwema* (TBC Taifa), *Hizi Nazo* (Redio One Stereo), *Kwa Raha Zetu* (Redio Clouds FM) na *Mitikisiko ya Pwani* (Times FM).

Kwa upande wa runinga, uwasilishaji umekuwa tofauti kidogo. Katika runinga washiriki wana fursa ya kuona matendo yanayotendwa. Kama ilivyo kwenye redio. Pia katika runinga kuna vipindi vya watoto ambamo kazi za fasihi simulizi huwasilishwa. Mfano wa vipindi hivyo ni *Bongo Kids* (TBC1) ambacho kinahusu somo la hisabati lakini huwa na matumizi ya nyimbo na wahusika ambao ni wa fasihi simulizi. Aidha, kituo cha ITV hurusha kipindi cha *Watoto Show* ambacho hujuimusha nyimbo, ngoma, methali, vitendawili na hadithi. Hali kadhalika, runinga zimekuwa zikirusha vipindi kama vile, *Mizengwe*, *Sanaa na Msanii*, *Mashamushamu ya Pwani* na *Hawavumi lakini Wamo* (ITV); *Futuhi*, *Bongo Beats* na *Msanii Wetu* (Star TV) *Fataki*, *Ngoma Zetu*, *Mchikicho wa Pwani Club Raha Leo Show* (TBC1) na *Mirindimo ya Pwani* (Channel Ten). Vipindi vyote hivyo vimekuwa vikisaidia uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi.

Matumizi ya simu nayo yana mchango mkubwa katika jamii. Watu wengi hutumia simu kwa mawasiliano ya mazungumzo. Kuwapo kwa mawasiliano

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 70 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya mitandao ya kijamii kwa kutumia simu kumewezesha uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi. Baadhi ya simu zina uwezo wa kurekodi na kutuma nyimbo, masimulizi na picha. Pia, zina uwezo wa kunasa vituo mbalimbali vya redio na runinga na, hivyo, kuwawezesha watumiaji wake kusikiliza kazi za kifasihi.

Matamasha mbalimbali yamesaidia kukuza na kueneza fasihi simulizi. Kwa mfano, Tamasha la *Sauti za Busara* ambalo hufanyika kila mwaka visiwani Zanzibar, hujumuisha washiriki wa fani mbalimbali za fasihi simulizi kutoka ndani na nje ya Tanzania. Kupitia tamasha hili, kazi mbalimbali za fasihi simulizi huwasilishwa na kuenezwa.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, fasihi simulizi pia imekuwa ikiwasilishwa kwa njia ya maandishi. Hii inatokana na fasihi kuhifadhiwa katika vitabu na machapisho mbalimbali, hivyo kuifikia hadhira kwa njia ya maandishi. Njia hii ya uwasilishaji huwatenganisha fanani na hadhira. Mifano ya vitabu vya fasihi simulizi ni: *Kuku, Njiwa, Kicheche na Hadithi Nyinginezo* (Abasi, 1996), *Mkia wa Chura* (Baitu Richard, 2002) na mfululizo wa *Fasihi Simulizi ya Mtanzania -Hadithi*, *Methali* na *Vitendawili* (TUKI, 1976).

Pia, baadhi ya magazeti, yamekuwa na makala maalumu za watoto ambazo, mara nyingi, huwa na kipengele cha fasihi simulizi, hususani hadithi. Kwa njia hiyo, fasihi simulizi huwasilishwa na kuenezwa.

Athari za sayansi na teknolojia katika fasihi simulizi

Kama ilivyoelezwa katika kipengele kilichotangulia, kuna njia mbalimbali za uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi. Njia ambazo zimetokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia zina athari kwa fasihi simulizi. Uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi kwa njia ya redio hauwawezeshi wasikilizaji kuona matendo yanayotendeka kwa sababu fanani na hadhira hawaonani ana kwa ana.

Katika njia ya runinga na simu, watazamaji hushindwa kushiriki ana kwa ana. Watazamaji hushindwa kuuliza maswali, hasa kwa wale ambao hawana simu. Kuna changamoto ya gharama kwani si kila mtu ana uwezo wa kununua runinga na simu. Vilevile, matumizi ya runinga huhitaji kifaa kijulikanacho kama kisimbuzi. Kifaa hiki huhitaji fedha kulipia huduma za vituo mbalimbali. Hata hivyo, pamoja na changamoto hizi, fasihi simulizi imepata sura mpya katika uwasilishaji na ueneaji wake tofauti na awali ilipokuwa inawasilishwa kwa njia ya mdomo tu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 71 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi

Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi una manufaa makubwa kwa jamii. Kazi za fasihi zilizohifadhiwa kwa njia mbalimbali kama sidii na machapisho huwasaidia wanajamii kujifunza kuhusu fasihi simulizi. Pia, kazi hizo hutunza kumbukumbu za jamii; hivyo, huwawezesha wanajamii kujifunza historia ya jamii yao. Kutokana na uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi, watafiti hupata data ambazo husaidia kufikia mahitimisho na kupata matokeo ambayo hutumika katika shughuli za maendeleo. Hivyo, ni vema kuhifadhi na kutunza kazi mbalimbali za fasihi simulizi.

Mbinu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi

Kuna mbinu mbalimbali za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. Zifuatazo ni miongoni mwa mbinu hizo:

(a) **Kuhifadhi kiamali**

Njia kuu na bora zaidi ya kuhifadhi fasihi simulizi ni kuitenda na kuitumia katika maisha ya kawaida ya kila siku. Huko ndiko kunaitwa kuhifadhi kiamali, yaani kuifanya iwe sehemu ya maisha. Hii ni kwa kuwa uhai wa fasihi simulizi hutegemea muktadha na matumizi. Fasihi simulizi hukua na kudumu inapohitajika na kutumika katika jamii, vinginevyo hufifia na hatimaye hufa.

(b) **Kuhifadhi kichwani**

Njia hii ni kongwe kuliko njia zote kwani ilianza tangu fasihi simulizi ilipoanza. Katika njia hii, fanani huhifadhi yale anayoyajua kichwani mwake. Baadaye, huyasimulia kwa wengine. Kwa kutumia njia hii, fasihi simulizi imekuwa ikisimuliwa kizazi hadi kizazi. Njia hii humpa fanani ujuzi wa kuhifadhi mambo anayoyajua. Kwa upande mwingine, usimuliaji huweza kubadilika kama fanani atapoteza uwezo wa kutunza kumbukumbu na kusimulia.

(c) **Kuhifadhi katika maandishi**

Fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa katika maandishi baada ya fanani kusimulia. Njia hii inasaidia kuhifadhi kazi kwa muda mrefu. Njia hii ni ya gharama kwa sababu huhitaji vitendea kazi wakati wa kuandika, mahali pa kuhifadhi na msomaji ni lazima anunue kazi hizo. Aidha, njia hii huifanya kazi ya fasihi simulizi kuwa mali ya mtu binafsi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 72 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kuhifadhi katika vinasa sauti

Hizi ni mbinu ya kutumia vifaa vya kurekodi sauti. Njia hii huruhusu kurekodi sauti za ala zinazotumika katika kazi husika. Kwa mfano nyimbo, huambatana na mlio wa ngoma. Ubora wa mbinu hii ni kuwawezesha watu kusikia sauti hata kama hawaoni vitendo. Njia hii ina gharama ya kununua vinasa sauti pamoja na vifaa vya kusikilizia kama vile redio.

(e) Kuhifadhi katika sidii, diski au kinyonyi

Mbinu hii huhifadhi sauti au vitendo vilivyorekodiwa kwa kutumia vifaa kama sidii, diski, kompyuta na kinyonyi. Njia hii ina ubora kwa sababu huruhusu utendekaji kuonekana na sauti kusikika. Pamoja na hayo, njia hii ina gharama katika kupiga picha, kusambaza na kununuliwa na watumiaji wa fasihi. Njia hii inahitaji runinga, kompyuta na deki ili kuweza kutazama kilichohifadhiwa katika vifaa hivyo. Njia hii ya uhifadhi huifanya kazi ya fasihi simulizi kumilikiwa na mtu binafsi. Kwa mfano Lukas Mkenda (maarufu kama Mr. Nice), amechota nyimbo za watoto katika tungo zake na kutoa albamu ambayo yeye ndiye mmiliki. Baadhi ya nyimbo hizo ni "Kidali Po" na "Fagilia."

Zoezi la 2

(i) Jadili jinsi utanzu wa semi unavyosaidia katika kujenga na kuimarisha tanzu nyingine za fasihi simulizi.

(ii) Eleza namna unavyoweza kutunga hadithi simulizi.

(iii) Ni kanuni gani ambazo humwongoza mtunzi wa ushairi kujenga taswira?

Kazi ya kufanya

Wanafunzi wajigawe katika vikundi wakiongozwa na mwalimu, kisha wabuni na kuandaa:

Igizo simulizi.

Maghani (kama vile majigambo au tendi).

Utegaji wa vitendawili.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 73 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tatu

Maendeleo ya fasihi andishi

Utangulizi

Sura hii inahusu maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru. Lengo la kujifunza sura hii ni kupata maarifa kuhusu maendeleo ya fasihi andishi katika vipindi mbalimbali.

Dhana ya fasihi andishi

Fasihi andishi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha na kuwasilishwa kwa njia ya maandishi. Msingi wa utunzi na uwasilishaji wa sanaa hii upo katika maandishi. Fasihi andishi ni changa ikilinganishwa na fasihi simulizi kwa sababu fasihi simulizi imekuwapo kabla ya uvumbuzi wa teknolojia ya uandishi, uchapaji na uchapishaji.

Sifa za fasihi andishi

Fasihi andishi ina sifa zifuatazo:

1. Ni changa kuliko fasihi simulizi.
2. Huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
3. Ni mali ya mtu binafsi.
4. Haiwezi kubadilishwa kirahisi ikishaandikwa.
5. Baadhi ya tanzu zake, kama riwaya, hutungwa kwa muda mrefu.

Maendeleo ya fasihi andishi kabla ya uhuru

Fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi kama ilivyokwisha elezwa. Tanzu za fasihi simulizi ni ushairi, hadithi, semi na sanaa za maonesho. Tanzu hizi zina uhusiano wa moja kwa moja na fasihi andishi. Baada ya ugunduzi wa maandishi, fasihi andishi ilizaliwa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 74

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika jamii za Afrika Mashariki, fasihi andishi ilianza pale jamii hizo zilipoanza kuweka amali zao kama vile historia na tamaduni katika maandishi. Hati za maandishi zili🙂letwa na wageni waliotoka Bara la Asia na Ulaya. Wageni hao ni Waajemi, Wareno, Waarabu, Wajerumani na Waingereza. Wageni walioleta elimu ya kigeni walikuwa na athari katika maandishi. Hati ya Kiarabu ilianza kutumiwa kuandika Kiswahili tangu karne ya 9 (inakisiwa miaka ya 800 BK). Maandiko ya kale ya Kiswahili, hasa tendi, tenzi na tarihi yaliandikwa kwa hati hiyo. Mifano ni *Utendi wa Tambuka* (Bwana Mwengo, 2019) na *Al-Inkishafi* (Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir, 1800). Kuanzia karne ya 19, hati ya Kirumi ilianza kutumiwa kuandika fasihi ya Kiswahili. Wakati wa ukoloni wa Kijerumani na Kiingereza, hati hiyo ya Kirumi ilienezwa na kutumika zaidi kupitia mfumo wa elimu ya kishule. Hati hiyo inaendelea kutumika hadi leo na ndiyo imekuwa hati ya uandikaji wa fasihi andishi ya Kiswahili.

Maendeleo ya fasihi andishi kabla ya uhuru yana uhusiano mkubwa na wageni (wamisionari na watawala). Wageni hawa walipofika Pwani ya Afrika Mashariki kuanzia karne ya 16, waliwakuta wenyeji wakiwa na fasihi yao. Tunaona kuwa baadhi ya tenzi za zamani kama vile *Fumo Liyongo* zilikuwapo kabla ya maandishi na ziliwekwa katika maandishi baadaye. Pia, tenzi hizi zilitokana na nyimbo zinazosemekana kuwa ndizo fasihi ya awali. Aidha, chimbuko la riwaya za Kiswahili ni ngano na hekaya simulizi.

Kulikuwa na wanafasihi wenyeji waliokuwa wakiandika mashairi na fani nyinginezo kama tarihi na masimulizi ya wasafiri. Pia, kulikuwapo na ngano na hekaya mbalimbali. Ngano na hekaya hizi ndizo zilitafsiriwa na kuwa msingi wa riwaya za Kiswahili. Miongoni mwa hadithi hizo ni *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870) zilizotafsiriwa na Edward Steere. Ngano nyingine zimechapishwa katika kitabu cha *Prosa und Poesie der Suaheli* (1907) kilichohaririwa na Carl Velten pamoja na *Mazungumzo ya Alfu Lela Ulela* Juzuu (1-4) (1928) kilichotafsiriwa na Edwin Brenn na kuhaririwa na Frederick Johnson. Vilevile, kulikuwa na riwaya za kutoka nje zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Baadhi ya riwaya hizo ni *Mashujaa: Hadithi za Wayunani* (Charles Kingsley, 1889), *Hadithi za Esopo* (John Bunyan, 1925), *Hekaya za Abunuwasi* (Samwil Chiponde, 1928), *Kisiwa chenye Hazina* (Frederick Johnson, 1929), *Safari za Gulliver* (Jonathan Swift, 1932), *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Ridder Haggard, 1937) na *Safari ya Msafiri* (John Bunyan, 1925).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 75 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kadiri muda ulivyokwenda, Waafrika walianza kuandika kazi za kinathari. Miongoni mwa kazi hizo ni *Habari za Wakilindi* (Abdalla Hemed el Ajjemi, 1972), *Maisha ya Hemed bin Muhamed el Murjebi au Tippu Tip* (Wilfred Whiteley, 1902) (Mhariri), (1950), *Uhuru wa Watumwa* (James Mbotela, 1934), *Tulivyofanya na Tulivyoona Uingereza* (Martin Kayamba, 1932) na kazi nyingine ni *Mwaka katika Mnyororo* (Samwil Sehoza, 1921).

Kuanzia miaka ya 1940 hadi 1960, riwaya nyingi zilifuata mkondo wa hekaya na ngano. Kimaudhui, riwaya nyingi zilielezea mambo ya mila na desturi kama njia ya kutunza maadili. Baadhi ya riwaya hizi zilitokana na fasihi ya Kiarabu kwa mfano: *Msafiri katika Nyumba ya Sultani* (David Diva, 1949) na *Kisa cha Mwana wa Mfalme Mohamed bin Suleiman* (Akida Waziri, 1944).

Aidha, fasihi zilizoandikwa na Waafrika zilihusu mila na desturi za jamii. Maandiko hayo pia yalihusu maadili mbalimbali na changamoto zilizohusu jamii ya wakati huo. Vilevile, baadhi ya maandiko hayo yalisisitiza utu wa mtu kama njia mojawapo ya kukomesha manyanyaso yaliyokuwa yakifanywa na wakoloni. Miongoni mwa kazi hizo ni *Adili na Nduguze* (Shaaban Robert, 1952), *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali* (Aniceti Kitereza, iliandikwa 1945 na kuchapishwa 1980), na *Kurwa na Doto* (Mohamed Saleh Farsy, 1960).

Hali kadhalika, kulikuwa na kazi mbalimbali za fasihi zilizokuwa zimeathiriwa na tamaduni za Kizungu, ingawa ziliandikwa na wazawa wa nchi za Afrika Mashariki. Kazi hizi zilikuwa na maudhui yanayohusu upelelezi na ujambazi wa kutumia silaha. Miongoni mwa kazi hizo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* (Mohammed Said Abdulla, 1957).

Kazi nyingine zilizoandikwa miaka ya 1940-1960 zilikuwa na mwelekeo wa kupinga ukoloni. Kazi hizi zilionesha madhara ya kutawaliwa na wakoloni. Miongoni mwa hizo ni *Kufikirika* (1951) na *Kusadikika* (1952) za Shabaan Robert. Pia, walikuwapo waandishi wengine kama vile Saadan Kandoro, Mathias Mnyampala na Kaluta Amri Abedi walioandika kupinga ukoloni. Ijapokuwa baadhi ya kazi za waandishi hawa ziliandikwa miaka ya mwanzo baada ya uhuru, zina maudhui yanayohusu kudai uhuru.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 76 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maendeleo ya fasihi andishi baada ya uhuru

Baada ya uhuru, fasihi andishi iliendelea kupata sura mpya kulingana na mahitaji ya wakati huo. Kazi nyingi za fasihi za wakati wa uhuru zilikuwa za kushangilia uhuru uliopatikana. Kazi hizi zilijitokeza katika magazeti ambapo mashairi na hadithi nyingi zilionesha hoihoi za kushangilia uhuru. Pamoja na kushangilia uhuru, wanafasihi waliandika pia kazi za kusisitiza ukombozi wa wanyonge.

Kwa upande wa Tanzania Visiwani, kufuatia mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, kuliibuka kazi za fasihi ambazo zilihusu ukombozi wa mnyonge. Baadhi ya hizo ni *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Shafi Adam Shafi, 1978), *Nyota ya Rehema* (Mohamed Suleiman Mohamed, 1978), *Kuli* (Shafi Adam Shafi, 1979), *Dunia Mti Mkavu* (1980), '*Sikate Tamaa* (1983) na *Utengano* (1980) za Said Ahmed Mohamed, na *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* (Muhammed Seif Khatib, 1978).

Mnamo mwaka 1967, yapata miaka sita baada ya uhuru, Azimio la Arusha lilitangazwa. Falsafa kuu ya Azimio la Arusha ilikuwa ni Ujamaa na Kujitegemea. Pamoja na mabadiliko mengine, fasihi andishi pia ilipata sura mpya. Fasihi ya kipindi hicho ililenga kutukuza maadili na amali zilizotokana na tamko la Azimio la Arusha. Kazi nyingi za fasihi andishi za wakati huo zilisifu Azimio la Arusha. Miongoni mwa kazi hizo ni *Matunda ya Azimio* (Wah. Lucas Honero, Shaaban Ngole, na Tigiti Sengo, 1980) *Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha* (UKUTA, 1977), na *Ngonjera za UKUTA* (Mathias Mnyampala,1970).

Kutokana na Azimio la Arusha kusisitiza vijiji vya ujamaa pamoja na shughuli za kilimo, kazi za fasihi andishi zilisawiri ubora wa maisha ya vijijini ikilinganishwa na yale ya mjini. Kazi zenye maudhui ya aina hiyo ni kama vile *Mtu ni Utu* (George Mhina, 1971) *Kijiji Chetu* (Ngalimecha Ngahyoma, 1975), *Ndoto ya Ndaria* (John Ngomoi, 1975) na *Njozi za Usiku* (William Seme, 1975), *Shida* (Ndyanao Balisidya 1975) na *Hatia* (Penina Muhando 1972)

Pamoja na kuwapo kwa kazi zilizosifu Azimio la Arusha, zipo kazi nyingine ambazo zilikosoa. Baadhi ya kazi zilionesha kushindwa kwa Azimio la Arusha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya viongozi kushindwa kulielewa Azimio hilo; hivyo, kushindwa kusimamia utekelezaji wake. Miongoni mwa kazi hizo ni *Njozi Iliyopotea* (Claude Mung'ong'o, 1979) na *Lina Ubani* (Penina Muhando, 1984). Nyingine ni *Dunia Uwanja wa Fujo* (1978), *Gamba la Nyoka* (1978) na *Kaptula la Marx* (1999) za Euphrase Kezilahabi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 77 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika miaka ya 1970-1980, liliibuka wimbi la riwaya na hadithi fupi za upelelezi na za mapenzi. Waandishi wengi wa mkondo huu waliandika ili kuchuma fedha. Kazi zao zilisisimua wasomaji kutokana na fani yake ya kuvutia. Kwa upande mwingine, kazi hizi zilitimiza masharti ya mfumo wa kibepari kwa sababu hazikujishughulisha na matatizo halisi ya watu wa kawaida. Hata pale zilipoyashughulikia, zilipotosha ukweli na uhalisi wake. Hii ni kwa sababu zilitoa majibu ya mkato ambayo hayakulenga kutoa suluhisho la matatizo zaidi ya kusisitiza kutatua matatizo kwa kutumia polisi, mahakama na jela.

Pamoja na kuzuka kwa riwaya pendwa, wapo waandishi walioandika kazi zao kueleza hali halisi ya maisha ya Mtanzania. Mifano ya kazi hizo ni *Fungate ya Uhuru* (Muhammed Seif Khatib 1974), *Raha Karaha* (Theobald Mvungi,1982), *Chungu Tamu* (Theobald Mvungi,1985) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi, 1982).

Mwishoni mwa miaka ya 1980, ziliibuka riwaya za kimajaribio zinazokiuka au kutengua baadhi ya kaida za uandishi wa riwaya. Kwa mfano, zilikosa msuko ulio dhahiri, zilikosa mhusika mkuu, na zilikwenda nje ya wakati (kama vile kuonesha mtu wa karne ya 16 akimtembelea mtu wa karne ya 20). Mara nyingi, riwaya za aina hiyo huwa na maudhui mazito ya kifalsafa yenye uchangamani mkubwa. Mifano ni riwaya za Euphrase Kezilahabi za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), *Babu Alipofufuka* (Said Ahmed Mohamed, 2001) na *Bin-Adamu* (Kyallo Wamitila, 2002).

Kwa jumla, maendeleo ya fasihi andishi yanaonekana kufuata mwelekeo wa mifumo ya maisha ya wakati ambao kazi husika zinaandikwa; na baadhi zimekwenda mbele ya wakati.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 78 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1

(i) "Fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi." Thibitisha kauli hii kwa mifano.

(ii) Jadili maendeleo ya fasihi andishi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru.

(iii) Tathmini jinsi kazi za fasihi ya Kiswahili zilizochapishwa kuanzia miaka ya 1970 hadi sasa zinavyofungamana na uhalisi wa maisha nchini Tanzania.

Tanzu za fasihi andishi

Kama ilivyo kwa fasihi simulizi, fasihi andishi pia ina tanzu zake. Tanzu za fasihi andishi ni nne; nazo ni ushairi, hadithi fupi, riwaya na tamthiliya. Tazama kielelezo kifuatacho:



Chanzo: Kyallo Wamitila, (2002).

Kielelezo namba 3.1 Tanzu na vipera vya fasihi andishi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Ushairi

Ushairi ni usawiri wa mawazo, hisi au tukio kwa muhtasari katika mpangilio maalumu wa lugha teule ya kitamathali yenye urari. Kwa hiyo, ushairi hutofautiana na tanzu nyingine za fasihi andishi katika umbo na matumizi ya lugha. Tanzu nyingine hutumia lugha ya mjazo ya kinathari, lakini ushairi hutumia lugha ya mkato, yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari; na aghalabu, huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara.

Ushairi, ambao ndio utanzu wa kwanza kabisa wa fasihi, ulianza wakati binadamu alipoanza kufanya kazi. Kupitia lugha, binadamu alibuni nyimbo za kazi. Nyimbo hizo ndizo msingi wa fasihi simulizi. Nyimbo za kazi zilitungwa kwa kuzingatia mapigo ya zana za kazi ili ziweze kukumbukwa kwa urahisi.

Historia fupi ya ushairi wa kiswahili

Kwa mujibu wa Mugyabuso Mulokozi (2017), tarehe mahususi za kuanza kwa ushairi wa Kiswahili, hususani umbo la ushairi linaloonekana leo, ni za kukisia. Kilicho bayana ni kwamba, kabla ya karne ya 10 ushairi wa Waswahili ulikuwa ukitungwa na kughaniwa kwa ghibu bila kuandikwa. Hali ilibadilika kuanzia karne ya 10 wakati Uislamu ulipoanza kuenea Uswahilini; na hivyo, kueneza hati ya Kiarabu. Kuanzia wakati huo, baadhi ya Waswahili walianza kutunga mashairi, hasa tenzi na tendi, kwa kutumia hati ya Kiarabu. Wataalamu hugawa maendeleo ya ushairi wa Kiswahili katika mihula mbalimbali. Kwa mfano, Euphrase Kezilahabi (1983) anabainisha mihula ifuatayo: muhula wa urasimi, muhula wa utasa, muhula wa urasimi mpya, na muhula wa sasa.

Muhula wa Urasimi ni kipindi maalumu kinachochukuliwa kuwa msingi wa kuwekwa kwa sheria au kanuni ya jambo fulani. Urasimi wa ushairi wa Kiswahili ulipata mashiko mnamo karne ya kumi na nane (1700-1800). Katika kipindi hicho, kulikuwa na tungo kama vile *Utenzi wa Hamziyya* (Sayyid Aidarusi bin Uthman, 1690), *Utenzi wa Tambuka* (Bwana Mwengo, 1728), *Utenzi wa Al-Inkishafi* (bin Nasir, 1800) na *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona bint Mshamu, 1858). Tungo hizi zilitanguliwa na tungo zilizohusu simulizi za Fumo Liyongo, na zikafuatiwa na tungo za Muyaka bin Haji. Baada ya hapo, ulifuatia ukame wa tungo kwa kipindi cha takribani miongo mitano (1885-1945). Kulikuwa na tungo chache; ndiyo maana muhula wa pili unaitwa **muhula wa utasa**. Sababu za ukame huu ni pamoja na matukio ya vita yaliyotokea ulimwenguni. Baada ya hapo, ukafuatia **muhula wa urasimi mpya** ambapo kulikuwa na watunzi kama vile Shaaban Robert, Kaluta Amri Abedi na Mathias Mnyampala. Huu ni muhula ulioshuhudia kuimarishwa kwa kanuni za utungaji wa ushairi wa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 80 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kiswahili. Kwa mfano, *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (Kaluta Amri Abedi, 1954). Kisha, ulifuatia **muhula wa sasa**. Muhula huu ulianza wakati mataifa ya Afrika Mashariki yalipopata uhuru kutoka kwa wakoloni. Hiki ni kipindi kilichokuwa na wasomi wengi wa ngazi ya chuo kikuu waliojihusisha na utungaji, uhakiki na utafiti kuhusu masuala ya fasihi, ukiwamo ushairi. Hali hii mpya ilisababisha kuwapo kwa fikra mpya katika ushairi wa Kiswahili; ndipo mjadala kuhusu ushairi wa vina na mizani usiofuata utaratibu huo ulipoibuka. Mjadala huo hujulikana kama **Mgogoro wa Ushairi.**

Hivyo, ushairi wa Kiswahili umepitia katika hatua kadhaa zilizoambatana na mabadiliko fulani. Ulianza ushairi wa kutungwa na kughanwa bila kuandikwa. Kisha, ukafuatia ushairi ulioandikwa kwa kutumia hati ya Kiarabu kwa Kiswahili. Halafu ukaja ushairi wa kuandikwa kwa hati ya Kirumi.

Dhana muhimu katika ushairi andishi

Kuna dhana muhimu zinazotumika katika taaluma ya ushairi andishi. Nazo ni mshororo au mstari, kibwagizo au kituo, ubeti, mizani, urari na vina.

Mshororo ni mstari katika ubeti wa kazi yoyote ya kishairi. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja, viwili, vitatu au zaidi kulingana na mtindo wa shairi husika. Istilahi "mshororo" hutumika katika ushairi simulizi na ushairi andishi. Istilahi "mstari" hutumika zaidi katika ushairi andishi.

Kibwagizo au kituo ni mshororo wa mwisho katika ubeti, ambao, kwa kawaida, hujirudiarudia. Kibwagizo au kituo huweza kuwa na majina mbalimbali kutokana na matumizi yake. Huweza kuitwa kibwagizo, kiini au kibwagizo bahari, yaani ni kile kinachojirudiarudia katika kila ubeti. Pia, kuna kibwagizo kawaida, hiki hubadilika katika kila ubeti. Kwa jumla, kibwagizo hutumika kusisitiza dhamira au wazo kuu la shairi husika.

Ubeti ni fungu la mishororo au mistari iliyopangwa pamoja katika shairi. Fungu hili hujenga maana kamili au inayojitosheleza. Pia, ubeti huweza kujengwa na mshororo mmoja au zaidi. Mshororo wa kwanza katika ubeti huitwa *mwanzo*, mshororo wa pili huitwa *mloto*, mshororo wa tatu huitwa *mleo* na mshororo wa nne huitwa *kibwagizo*, *kimalizio*, *kituo*, *mkarara* au *kipokeo*. Vipande mstari pia vina majina yake. Kipande mstari cha kwanza huitwa *ukwapi*, kipande mstari cha pili huitwa *utao* na kipande mstari cha tatu huitwa *mwandamizi*.Tazama mfano ufuatao:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 81 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kinda ningali mtini, sina mama kunilea
Mama yangu simuoni, naambiwa kakimbia,
Sina furaha moyoni, mama nilimzowea,
Nimebaki ukiwani, ninalia na dunia,
Kinda ningali mtini, sina mama kunilea.

Ufafanuzi

MWANZO → Mama yangu simuoni, naambiwa kakimbia,
MLOTO → Sina furaha moyoni, mama nilimzowea,
MLEO → Nimebaki ukiwani, ninalia na dunia,
KIBWAGIZO → Kinda ningali mtini, sina mama kunilea.

↑ UKWAPI ↑ UTAO

(*Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*, Kaluta Amri Abedi, 1954:68)

Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo. Mara nyingi, mashairi ya kimapokeo huwa na mizani kumi na sita (16); ukwapi unakuwa na mizani nane, na utao unakuwa na mizani nane.

Urari ni ulingano au uwiano wa mizani na vina katika mashairi. Katika mashairi ya kimapokeo, urari huzingatiwa kwa sababu husaidia kuimbika kwa shairi.

Vina ni silabi zenye sauti zinazofanana zinazowekwa kati au mwishoni mwa mshororo. Mashairi ya kijadi huwa na vina vya kati na mwisho. Utenzi huwa na kina cha mwisho pekee. Vina huleta mvuto katika kughani na kusisitiza maudhui ya shairi. Husaidia kuhifadhi au kutunza kumbukumbu kwa urahisi kutokana na kujirudiarudia kwake.

Vipera vya ushairi andishi
Ushairi andishi umegawanyika katika vipera vitatu. Vipera hivyo ni mashairi, tenzi na ushairi wa maigizo.

For Online Use Only

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Mashairi

Dhana ya mashairi ni ngumu kufasilika kutokana na washairi kutofautiana mitazamo, hususani katika muundo wa shairi. Kuna mitazamo miwili inayohusu mashairi: Mtazamo wa kimapokeo na mtazamo wa kisasa.

Mtazamo wa kimapokeo

Huu ndio mtazamo wa awali kuhusu mashairi ya Kiswahili.Wafuasi wa mtazamo huu wanasisitiza kufuata kanuni za urari wa vina na mizani. Zaidi ya uzingatizi wa kanuni hizi, wanaeleza kwamba shairi halina budi kuwa na ufasaha wa lugha, maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata, nyoofu, tamu na laini. Kwa upande wa mizani, wanamapokeo, ambao wanasisitiza uimbikaji wa shairi, wanaona kwamba, ili shairi liimbike ni lazima liwe na mizani na urari wa vina. Mizani ni lazima iwe linganifu kwa kila mstari, vina vifanane na mistari iwe na idadi sawa kwa kila ubeti. Mtazamo huu ndio unaotupatia mashairi ya kimapokeo. Tazama mfano wa beti zifuatazo:

Maisha

Maisha kitendawili, kitegue kwa busara,
Uitulize akili, huku ukiwa tohara,
Uhimili kila hali, yaweza kwako kung'ara,
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

Maisha kama bahari, yenda mpera mpera,
Vyovyote uwe tayari, kwa kujiweka imara,
Na kumuomba Kahari, akunyooshee dira,
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

Maisha ni kujituma, ili upate tira,
Ushughulike kulima, au kuunda minara,
Mwiko kujiweka nyuma, utakumbwa na idhara,
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

Maisha kuhangaika, usafe kama sangara,
Vuka mabonde na nyika, ili upate stara,
Bila ya kushughulika, hali yako itajura,
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 83 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maisha kwa mwenye pupa, yatamtoa kafara,
Na pabaya humtupa, achomwe kama sigara,
Au aliwe na papa, atangulie ahera.
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

Maisha uvumilivu, na wala siyo papara,
Zitumie zako nguvu, ikiwa huna safura,
Huo ndio uerevu, na siyo kuuza sura,
Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.

(Juma Muhunzi Juma (Mwana wa Nyasa), katika *Diwani ya Tunzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein* (Mkuki na Nyota 2016: 83:84)

Shairi hili lina mizani linganifu. Kila mshororo una mizani kumi na sita na vina vinavyofanana mwishoni mwa kila mshororo kwa shairi zima.Vina vya kati vinafanana katika kila ubeti. Kila ubeti umeundwa na mistari minne, ambapo huu ni muundo wa *tarbia*.

Mtazamo wa kisasa au masivina
Huu ni mtazamo wa wanamabadiliko wanaodai kwamba si lazima shairi liwe na urari wa vina wala ulinganifu wa mizani. Mtazamo huu ulianza mwishoni mwa miaka ya 1960 na kushadidiwa mwanzoni mwa miaka ya 1970. Wafuasi wa mtazamo huu ni Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi na Jared Angira.Wafuasi wengine ni Mugyabuso Mulokozi, Kulikoyela Kahigi, Said Ahmed Mohamed na Theobald Mvungi. Kulikoyela Kahigi na Mugyabuso Mulokozi wameandika *Mashairi ya Kisasa* (1973), *Malenga wa Bara* (1976) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1982), Said Ahmed Mohamed ameandika diwani kadhaa zikiwamo '*Sikate Tamaa* (1983) na *Kina cha Maisha* (1986).

Wafuasi wa mtazamo huu wanaamini kuwa maudhui yanaweza kuwasilishwa bila kujikita katika sheria za vina na mizani. Wanadai kuwa, kama ambavyo mabadiliko yanatokea katika nyanja nyingine, ni lazima pia yatokee katika ushairi. Kwa hiyo, ushairi wa Kiswahili huyakubali mabadiliko hayo, hasa katika fani inayotumiwa na washairi katika kuelezea maudhui. Ikumbukwe kwamba, wenye mtazamo huu hawapingi kabisa kanuni za wanamapokeo, ila wanaamini katika mabadiliko. Kwa mfano, zaidi ya nusu ya mashairi yaliyomo katika *Diwani ya Malenga wa Bara* (Kulikoyela Kahigi, na Mugyabuso Mulokozi, 1976) ni ya kimapokeo. Wanausasa wanatilia mkazo matumizi ya lugha kuliko muundo wa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 84 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shairi. Tazama mfano wa shairi la kisasa la "Kuchambua Mchele":

Habari zilifika kutoka Arusha,
Tukaanza kuchambua mchele wa Ujamaa,
Macho mbele, macho pembeni tukitoa mchanga,
Tukafanya kaburi dogo la mchanga.

Tukaanza kutoa chenga, moja moja,
Vidole vikafanya kazi kama cherehani,
Usiku na mchana; macho yakauma,
Tukafanya kichuguu kidogo cheupe.

(Euphrase Kezilahabi, *Kichomi* 1974)

Ukichunguza beti hizi mbili, utaona kwamba hakuna mizani linganifu wala urari wa vina. Kilichozingatiwa ni uteuzi wa maneno wenye kujenga picha na kumvutia msomaji au msikilizaji.

Wanausasa wanasisitiza uhuru katika kutunga mashairi, yaani mshairi awe huru kueleza mawazo yake bila kubanwa na kanuni za wanamapokeo. Kitu cha msingi katika shairi ni mpangilio wa maneno, lugha ya picha au taswira, tamathali za semi, hisia za kishairi na ujumbe.

(b) Tenzi

Dhana ya tenzi imekwishaelezwa katika sura ya pili. Mambo machache ya kuyaongezea katika sura hii ni kwamba, mara nyingi, tenzi huanza na dua, ambapo mwandishi humwomba Mungu amwongoze katika uandishi wake. Kwa kawaida, tenzi huwa na beti nyingi kuliko shairi, lakini tenzi nyingi ni fupi kuliko tendi.

Beti za utenzi zinatakiwa ziwe hamsini na kuendelea. Hata hivyo, urefu wa utenzi hutegemea uzito wa maudhui na ujuzi wa mwandishi. Aghalabu, mstari wa utenzi huwa ni nusu ya mshororo wa shairi la kimapokeo. Hivyo, utenzi huwa na mizani minane. Vilevile, vina katika mishororo mitatu ya kwanza, hufanana; mshororo wa mwisho huwa na kina tofauti. Kina hiki hakibadiliki katika utenzi mzima. Kina hiki huitwa kina bahari. Tazama mfano katika baadhi ya beti za utenzi ufuatao:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ewe Mama mpenzi

(1) Baba akamuadhari,
Bwana puliza tunguri,
Ziambae mbali shari,
Pasiwe la kutokea.

(2) Simike vipembe vyako,
Kandoni pa nyumba huko,
Vizuilike vituko,
Pasiwe pa kupitia.

(3) Nimetengeneza nyuzi,
Bwana nivike hirizi,
Iwe kingo la mzazi,
Kumkinga na balaa.

(4) Nichanje chanja za paja,
Na za ubavuni chanja,
Nami heri nitaonja,
Mwanangu nikimzaa.

(5) Tumia wote uganga,
Kama ngao ya kukinga,
Mungu atujalie mwanga,
Mwana vyema kutokea.

(Francis Semghanga, *Tenzi za Nafsi*, 1988)

Beti za hapo juu zinaonekana wazi kuwa zimeundwa na nusu mishororo minne. Kina cha mshororo wa mwisho "a" ni tofauti na vina vya nusu mishororo mingine mitatu inayobaki katika beti zote.

(c) Ushairi wa maigizo

Hii ni fani mojawapo ya ushairi wa Kiswahili. Fani hii tunaweza kuiweka katika michepuo miwili ambayo ni ushairi wa ngonjera na ushairi wa kidrama.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 86 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Ushairi na ngonjera

Kama ulivyojifunza katika mada ya fasihi simulizi, ngonjera huhusisha mazungumzo na malumbano kati ya pande mbili. Mahojiano na malumbano haya yanaweza kuwa baina ya mtu na mtu, mtu na watu au watu na watu. Kwa kawaida, ngonjera hughanwa, haziimbwi. Aghalabu, ngonjera huwa na pande mbili zinazosigana, upande unaofahamu na usiofahamu jambo. Kazi ya upande unaofahamu ni kuuelimisha upande usiofahamu. Hatimaye, upande usiofahamu hukiri kwamba umeelewa jambo hilo. Pande zinapokubaliana, ngonjera huwa imefika kileleni na ujumbe kudhihirika. Wahusika wa ngonjera hutumia lugha ya kisanaa pamoja na miondoko ya mwili kama vile mikono, macho au midomo. Kutokana na wahusika kutumia miondoko, ngonjera pia huitwa *ushairi wa maigizo*.

Tazama mfano wa ngonjera ya "Sielewi Azimio" katika *Ngonjera za UKUTA* (Mathias Mnyampala, 1970).

Mwana

Baba tafadhali sana, nakuomba kwa hisani,
Mimi ningali kijana, mengi sijayabaini,
Sijaelewa maana, ni mgeni duniani,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

Nambie lieleweke, niondoke ujingani,
Taratibu yatamke, mimi ni mwanao duni,
Lau ni mwana mteke, yataningia moyoni,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

Nielewe Azimio, unambie kwa makini,
Liniondoke pumbao, mimi na dada nyumbani,
Wajue sisi wanao, tuondoke ujingani,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

Baba

Ahsante ewe mwana, maneno yako matamu,
Utakayo yana maana, una akili timamu,
Lau ungali kijana, takwambia ufahamu,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 87 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Laneemesha taifa, laondoa madhalimu,
Wale wajipao sifa, kula mali ya kaumu,
Wameangushwa vifafa, kama walikula sumu,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Limeleta mambo mengi, Azimio hilo zuri,
Halikubagua rangi, akiwa mtu wa heri,
Ila wawe wasarangi, wanyonyaji mabepari,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Mwana
Ala, hivyo baba kweli, mabepari ni mirija?
Hujikusanyia mali, kwa sababu ya ujanja,
Uongo huzusha kweli, haki zetu kutupunja?
Azimio la Arusha, limeleta haki kweli.

Baba
Azimio lenye heri, mkono ninaliunga,
Alijalie Kahari, Rabi Mola Mwenye anga,
Tukayafyeke mapori, shoka mundu na mapanga,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio ni jeupe, linameta sura njema,
Mwanangu tusiwe kupe, tujitegemee vema,
Na uzembe tuutupe, na tuwe raia wema,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio limenena, elewa mwanangu hasa,
Ni haramu kunyonyana, papa kummeza kasa,
Baba mama hata mwana, tuondoe hivyo visa,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio ni azizi, kwa kila Mtanzania,
Tusifanye upuuzi, tuzikaze zetu nia,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 88 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tuwakabe mabazazi, watupotezao njia,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Mwana
Baba Azimio tamu, mwanao nimesikia,
Sasa nami naazimu, mjini kujihamia,
Nao wale madhalimu, wote watuangamia,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Nanyi ndugu ikhiwani, mlio pwani na bara,
Tulinde yetu Amani, tusimame kwa imara,
Na wale watu haini, wabaki wahangarara,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Wito wako twafurahi, ewe Baba wa Taifa,
Waovu tumewawahi, waharibifu wa sifa,
Wamekuwa majeruhi, wameona bora kufa,
Azimio la Arusha, ufunguo wa faraja.

Mfano wa hapo juu unaonesha wazi washiriki wa ngonjera ambao ni Baba na Mwana. Baba anamfafanulia Mwana kuhusu uzuri wa Azimio la Arusha, hatimaye, Mwana anaelewa na kuazimia kutekeleza matakwa ya Azimio.

(c) Ushairi wa kidrama

Huu ni ushairi unaotumiwa katika baadhi ya tamthiliya. Ni mtindo mmojawapo wa kuandika mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya. Hivyo, hauwezi kutenganishwa na fani hiyo ya tamthiliya (Mugyabuso Mulokozi, 2017). Ufuatao ni mfano wa ushairi huu:

Mwanamke: Ndugu zangu, pulikeni ndugu zangu
Sasa si kama zamani
Sasa umetawala uwazi
Uwazi na utambuzi
Tusipigwe na bumbuwazi
Tusijisabilie kirahisi
Kwa ndoa yenye wasiwasi!

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 89 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bikisiwa: Nilikuomba baba unipe nafasi
Mume mwenyewe kumwakisi
Bali hukufanya kisisi
Ukanipa mchumba mwenye ukakasi…

Mfalme: Mwenzako lakini kakukosa nini?
Mwenzako kakufanya nini?
Mimi bado sijaamini
Kwa kweli baya mimi sijalibaini

Basi jambo hilo lanikata maini
Na kunivunjia matumaini
Mbona unaivunja ihsani
Yake sisi tul'omwamini

Said Ahmed Mohamed, *Posa za Bikisiwa* (2013)

Kwa jumla, vipera vya ushairi ni mashairi, tenzi na ushairi wa maigizo. Huwa na sifa mbalimbali za kisanaa zinazoutofautisha ushairi na tanzu nyingine za riwaya pamoja na tamthiliya. Sifa hizo ni:

(a) Mpangilio maalumu wa maneno ambao wakati mwingine, hukiuka kanuni za kisarufi za lugha inayohusika na kufuata kanuni za miundo inayowezekana.

(b) Matumizi ya picha ambazo hujumuisha matumizi ya dhana mbalimbali ndani ya dhana moja ili kuleta taswira na athari maalumu katika mawazo ya msomaji au msikilizaji. Aghalabu, msomaji au msikilizaji huzipata athari hizi kwa kutumia milango ya fahamu.

(c) Ridhimu inayotokana na mlingano wa mapigo ya lugha au sauti; huweza kupishana kidogo katika mashairi ya kisasa au masivina.

(d) Uwezo wa kufikisha hisia za kishairi kwa msomaji au msikilizaji kupitia lugha, yaani kupitia uchaguzi wa maneno, mpangilio wa maneno, sauti, picha na ridhimu. Hisia hizo hutakiwa kuwa za dhati ili ziweze kumgusa na kumzindua msomaji au msikilizaji.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 2

Soma kauli hizi mbili kisha jibu maswali yanayofuata:

(a) "Katika kitabu hiki, tungo za Euphrase Kezilahabi, Kulikoyela Kahigi, Mulokozi na wengineo watungao tungo tutumbi zisizokuwa na sanaa yoyote nimezitupa pembeni ... Muundo wa mashairi yote yaliyomo kitabuni humu ni ya asili ya Kibantu. Kila utungo wa shairi umefungika upande wa mistari; umefungika upande wa vina; ni lazima mistari iwe na vina; umefungika upande wa mizani; ni lazima kila mstari uwe na idadi sawa ya mizani. Mashairi yote yaimbwe; yaweza pia kusomwa au kusemwa tu. Tungo zisizotimiza yote hayo si mashairi."

(Jumanne Mayoka, *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*, 1986)

(b) Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lala salama
katika mionzi hafifu, ya jua machweoni
Na mahadhi yaguagaa, juu ya bahari ya utenzi
Yameshindwa chini kuzama, kwenye kina cha urazini
Nao wahenga vibandani, nje tena hawatoki
Hakuna tena ngoma, ya kugeana kani
Na ushairi umehama, umerudi upeponi
Lakini majani makavu, sasa hayatingishiki,
Nayo madirisha ya nyumba, imara yamefungwa
waliomo ndani wahofu, hasira ya mizimu.
(Euphrase Kezilahabi, *Kichomi*, 1988)

Maswali

(i) Toa maoni yako kuhusu hoja ya kuwa ili utungo uitwe shairi, sharti ukidhi vigezo vya kauli (a).

(ii) Tathmini ukweli wa kinachosemwa katika kauli (b) katika hali halisi ya sasa ya ushairi wa Kiswahili.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 91 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Hadithi fupi

Ni simulizi za kubuni zinazosawiri tukio, tabia, mgogoro au kipengele cha maisha kwa ufupi. Hadithi za namna hii huwa na tukio moja au mawili na hutumia mawanda finyu. Kwa kawaida, hadithi fupi haiwi na uchangamano mkubwa wa matukio, na hutumia wahusika wachache ikilinganishwa na riwaya.

Historia ya hadithi fupi

Chimbuko la hadithi fupi ni hadithi simulizi na andishi zinazopatikana katika lugha nyingi duniani. Baadhi ya fani zilizochangia kuchipuka kwa hadithi fupi ni ngano, hekaya, visa, michapo na tendi. Kuzuka kwa fani ya hadithi fupi huko Marekani na Ulaya katika karne ya 19 kulisaidiwa sana na kuchipuka kwa utamaduni wa kusoma magazeti, kwani visa vingi vilichapishwa katika magazeti hayo. Uhusiano huu kati ya hadithi fupi na magazeti au majarida bado upo hadi leo.

Kwa mujibu wa Mugyabuso Mulokozi (2017), historia ya hadithi fupi haitofautiani sana na historia ya riwaya ya Kiswahili. Visa vya mwanzo vilivyochapishwa kwa Kiswahili ni mkusanyiko wa hekaya na ngano. Baadhi ya hadithi hizo ni *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870), *Hadithi za Wayunani* (1889), *Hekaya za Abunuwasi* (1928) na *Alfu Lela Ulela* (1928). Hadithi hizi zilikuwa za kimapokeo na zenye kuingiliana na fasihi simulizi. Visa halisi vya kwanza katika hadithi za lugha ya Kiswahili vilianza miaka ya 1950 katika magazeti ya *Mamboleo, Mwafrika, Baraza, Nyota Afrika* na *Kiongozi*. Katika miaka ya 1960, visa hivi vilianza kuchapishwa kwenye vitabu. Baadhi ya watunzi mashuhuri wa hadithi fupi za Kiswahili ni Gabriel Ruhumbika, Alex Banzi, Joseph Kiimbila, Kyallo Wamitila na Owen Onyango. Baadhi ya mikusanyiko ya hadithi fupi iliyochapishwa ni *Misingi ya Hadithi Fupi* (Mbunda Msokile, 1992), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (Mwenda Mbatia, 2000), *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine.* (Owen Onyango, 2006), *Mizungu ya Manabii na Hadithi nyingine* (John Habwe, 2010), *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (Kyallo Wamitila, 2010) .

Sifa za hadithi fupi

Hadithi fupi huwa na sifa au kaida zinazoitofautisha na riwaya. Nazo ni hizi zifuatazo:

(i) Huwa na urefu wa kusomeka kwa mkao mmoja. Kwa kawaida hadithi fupi haizidi maneno 10,000.

(ii) Ina muundo sahili.

(iii) Ina wahusika wachache; aghalabu mhusika mkuu mmoja au wawili. Wahusika hawa hawakui kitabia wala hawakui kulingana na maendeleo ya kisa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 92 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Huwa na dhamira chache ikinganishwa na riwaya. Aghalabu, huwa na dhamira kuu moja katika kisa kikuu kimoja.
(v) Huwa na mawanda finyu ya kiwakati na kijiografia.

Aina za hadithi fupi

Hadithi fupi huainishwa katika makundi mawili: *hadithi fupi dhati* na *hadithi fupi pendwa*. Hadithi fupi dhati huwekwa katika makundi yafuatayo: hadithi fupi za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kifalsafa.

Hadithi fupi za **kijamii** huzungumzia masuala mbalimbali ya kijamii kama vile ndoa, jinsia, mapenzi na malezi. Mifano ya hadithi fupi za kijamii ni: "Uwike Usiwike Kutakucha" (Gabriel Ruhumbika, 1992), "Siri ya Bwanyenye" (Mugyabuso Mulokozi, 1992) katika Mbunda Msokile, "Damu Nyeusi" (Ken Walibora, 2007), Kijana Yule (Mohamed Mohamed, 2010) katika Kyallo Wamitila.

Hadithi fupi za **kisiasa** ni zile zinazohusu masuala ya kisiasa. Mifano ya hadithi za kisiasa ni "Wali wa Ndevu" (Gabriel Ruhumbika, 1974), "Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani", "Magwanda Kubilya na Vyama Vingi" na "Mayai Waziri wa Maradhi" (Euphrase Kezilahabi katika Mbunda Msokile, 1992).

Hadithi fupi za **kiutamaduni** zinahusu masuala ya mila na desturi. Mifano ya hadithi fupi za kundi hili ni *Tamaa Mbele* (Alex Banzi, 1970) na "Siku ya Mganga" (Chesi Mpilipili, katika Kyallo Wamitila 2012).

Hadithi fupi za **kifalsafa** huzungumzia tafakuri kuhusu masuala mazito yanayomzunguka mwanadamu na ulimwengu wake. Mifano ya hadithi fupi za kifalsafa ni "Wasubiri Kifo" (Euphrase Kezilahabi, katika Mbunda Msokile, 1992) na "Mchakamchaka wa Maisha" (Serapius Komba, 1978).

Hadithi fupi **pendwa** huhusu masuala yanayosisimua kama vile mapenzi, mauaji na upelelezi.

Pamoja na uainishaji wa hadithi fupi uliofanywa hapo juu, ni vema ifahamike kuwa ni vigumu kuwa na hadithi fupi yenye maudhui ya mwelekeo mmoja. Hivyo, hadithi fupi moja yaweza kubeba maudhui ya aina mbalimbali.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 93 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Tamthiliya

Tamthiliya ni mchezo ulioandikwa ili utendwe jukwaani au usomwe, lengo likiwa ni kutoa maudhui na ujumbe. Tamthiliya hujengwa na wahusika na migogoro iliyomo katika mchezo. Migogoro ndiyo inayokuza mwendo wa igizo kwa kutumia visa ambavyo hutendwa na wahusika mbalimbali. Wahusika ndio huzungumza na kutenda matendo mbalimbali kisanii.

Tamthiliya haikuwapo nchini Tanzania kabla ya ujio wa Waingereza; wao ndio walioleta drama ambayo inaaminika kuwa chanzo cha tamthiliya. Drama iliingizwa shuleni na Waingereza kwa lengo la kuwaburudisha na kuwakumbusha utamaduni wao, hasa baada ya saa za kazi ambapo wengi wa walimu walikuwa Waingereza. Ilikuwa rahisi kuanzisha vikundi vya drama shuleni kwa sababu shule nyingi zilikuwa za bweni; hivyo, wanafunzi walipatikana kwa wingi. Vilevile, wanafunzi hao walifahamu vizuri lugha ya Kiingereza. Tamthiliya nyingi zilizoigizwa ni zile zilizoandikwa na Waingereza. Miongoni mwa tamthiliya hizo ni *The Merchant of Venice* (William Shakespeare, 1596) na *Julius Caesar* (William Shakespeare, 1599). Kwa kuwa tamthiliya hizi hazikuwa na uhusiano na mazingira ya Kitanzania, Watanzania walioziigiza waliona ni kiburudisho tu; yaani tamthiliya hizo hazikuwa na maana kubwa kwao. Kadiri muda ulivyopita, baadhi ya Watanzania walivutika kutumia vipaji vya kisanaa kuonesha tamthiliya. Kwa bahati mbaya, hawakuwa na ujuzi wa kuandika tamthiliya kama zile za Waingereza. Miaka ya mwanzo baada ya uhuru, maudhui hayakubadilika mpaka lilipotangazwa Azimio la Arusha mwaka 1967. Maudhui ya tamthiliya ya baada ya Azimio la Arusha yalichukua sura mpya kwa kutangaza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Tamthiliya za mwanzo ziliathiriwa sana na vichekesho. Pia, ziliathiriwa na drama za Kiingereza. Watunzi walitunga tamthiliya zilizofanana kimaudhui na zile za akina Shakespeare. Kwa mujibu wa Mazrui (2007) na Mugyabuso Mulokozi (2017), tamthiliya za mwanzo za Kiswahili zilitungwa nchini Kenya. Mifano ya tamthiliya hizo ni *Mgeni Karibu* (Graham Hyslop, 1957), *Nakupenda Lakini* (Henry Kuria, 1957) na *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (Gerishon Ngugi, 1961). Kwa upande wa Tanzania, miaka ya 1960, tamthiliya za Kiingereza zilitafsiriwa. Miongoni mwa tamthiliya hizo ni zile za Shakespeare za *Juliasi Kaisari* (Julius Nyerere, 1964) *Mabepari wa Venisi* (Julius Nyerere, 1969), *Tufani* (Samwel Mushi, 1969) na tamthiliya ya Kiyunani ya *Mfalme Edipode* (Samwel Mushi, 1969). Tamthiliya zilizotafsirwa kutoka lugha za Kiafrika ni *Mtawa Mweusi* (Ngugi wa Thiong'o, 1970), *Masaibu ya Ndugu Jero* (Abdulhakim Yahaya, 1974) na *Nitaolewa Nikipenda* (Ngugi wa Thiong'o na Ngugi wa Mirii, 1982).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 94 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuanzia miaka ya 1960, watunzi wa Kitanzania walianza kutunga tamthiliya kwa Kiswahili kwa ajili ya Watanzania. Tamthiliya ziligusa maisha ya kisiasa yaliyodumisha Utanzania. Kwa upande wa fani, walifuata nyayo za tamthiliya za Waingereza. Hii ni kwa sababu wengi wa watunzi hawa ni wale waliopitia mfumo wa elimu, hasa waliofika chuo kikuu na kupata ujuzi wa utunzi kupitia somo la fasihi kwa Kiingereza na sanaa za maonesho. Watanzania wengine waliopata ujuzi wa utunzi ni wale walioshiriki katika maigizo ya tamthiliya.

Vilevile, baada ya uhuru nchini Tanzania, kulikuwa na mashindano ya utunzi na uigizaji kupitia *Youth Drama Association*. Mashindano haya yaliwezesha watunzi chipukizi kujitokeza katika kutunga na kushiriki katika mashindano. Miongoni mwa watunzi waliojitokeza ni Ebrahim Husein, (1969) ambaye tamthiliya yake ya kwanza, *Wakati Ukuta*, ilishinda na kupata tuzo katika mashindano hayo. Tamthiliya nyingi zilizotungwa miaka ya 1960 ziliigizwa tu shuleni na katika kumbi za maonesho lakini hazikuchapishwa.

Tamthiliya nyingi za Kiswahili zilichapishwa kama matokeo ya kuhitimu kwa watu wengi katika fani ya sanaa za maonesho katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, yalikuwa ni matokeo ya kuanzishwa kwa mashindano ya uigizaji miaka ya 1970 - 1990. Baadhi ya tamthiliya zilizochapishwa ni *Kinjekitile* (Ebrahim Hussein, 1969), *Mashetani* (Ebrahim Hussein, 1971), *Hatia* (Penina Muhando, 1972), *Tambueni Haki Zetu* (Penina Muhando, 1973), *Aliyeonja Pepo* (Farouk Topan, 1973) na *Pambo* (Penina Muhando, 1975). Nyingine ni *Sundiata* (Emmanuel Mbogo, 1975), *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (Ebrahim Hussein, 1976), *Machozi ya Mwanamke* (Ibrahim Ngozi, 1977), *Mukwava wa Uhehe* (Mugyabuso Mulokozi, 1979), *Arusi* (Ebrahim Hussein, 1980), *Tendehogo* (Edwin Semzaba, 1980), *Giza Limeingia* (Emmanuel Mbogo, 1980). Vilevile, kulikuwa na *Njia Panda* (Henry Muhanika, 1981) *Tone la Mwisho* (Emmanuel Mbogo, 1981), *Nguzo Mama* (Penina Muhando, 1982), *Lina Ubani* (Penina Muhando, 1984), *Kwenye Ukingo wa Thim* (Ebrahim Hussein, 1988), *Pungwa* (Said A. Mohamed 1988), *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (Edwin Semzaba, 1988) *Kivuli Kinaishi* (Said Mohamed 1990) na *Morani* (Emmanuel Mbogo, 1993).

Baadhi ya tamthiliya hizi zilichotarisha tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi. Dhana ya uchotarishaji ina maana ya uchanganyaji wa fani na mbinu za fasihi simulizi na fasihi andishi kuibua fani na maudhui mapya. Kwa mfano, katika *Lina Ubani* (Penina Muhando, 1984) kuna matumizi ya hadithi ndani ya hadithi,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 95 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ambapo mtambaji anasimulia, vivyo hivyo na Bibi anasimulia hadithi nyingine. Pia, katika tamthiliya hii, kuna matumizi ya wahusika kama vile Zimwi na Joka ambao wanapatikana katika ngano.

Vilevile, tamthiliya za *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (Ebrahim Hussein, 1976) zina masimulizi kuhusu ukombozi na utambulisho. Mathalani, katika *Ngao ya Jadi* kuna joka lenye vichwa saba. Joka hili linapouawa, bado sumu yake inabaki na kuathiri jamii nzima, hasa watemi. Matumizi ya nyoka ambaye ni mhusika anayepatikana katika fasihi simulizi yanaonesha uhusiano uliopo kati ya tamthiliya na fasihi simulizi. Pia, tamthiliya ya *Arusi* (Ebrahim Hussein, 1980) imejengwa katika misingi ya fasihi simulizi, hasa kitendawili. Aidha, kuna matumizi ya ngano ya arusi ya Bukini na Mwanaheri. Arusi hii inaonesha uhusiano wa mataifa yenye siasa tofauti.

Tamthiliya zimeendelea kutungwa zikiakisi mabadiliko ya mifumo ya maisha ya jamii ya wakati huo. Mathalani, tamthiliya kama *Kilio Chetu* (Medical Aid Foundation, 1995) imejadili suala la ugonjwa wa UKIMWI na athari zake katika jamii.

Maelezo haya yanaonesha kuwa ingawa tamthiliya andishi ya Kiswahili ilipata msukumo kutoka kwa Waingereza, lakini mizizi yake ilijikita katika fasihi simulizi kutokana na uchotarishaji wa vipengele vya fasihi simulizi unaofanywa na waandishi wa tamthiliya. Tamthiliya za awali za Kiswahili kama vile *Kinjekitile* (1969) na *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (1976) za Ebrahim Hussein, kama tulivyokwishaona, zimechota vipera vya fasihi simulizi. Hii inathibitisha kwamba tamthiliya imeathiriwa na fasihi simulizi. Waingereza walisaidia kuipa umbo na kuiweka katika maandishi.

Miaka ya karibuni tamthiliya ya kihistoria imeanza kushamiri tena baada ya kupotea kwa takribani miongo mitatu tangu enzi za *Kinjekitile* na *Mukwava wa Uhehe*. Mtunzi aliyejipambanua zaidi katika mkondo huu ni Emmanuel Mbogo ambaye ametoa tamthiliya sita miaka ya karibuni. Tamthiliya hizo ni *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Sundiata* (1994), *Fumo Lyongo* (2009), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Tamthiliya hizo, mbali na kupevua mkondo wa tamthiliya ya kihistoria, zinadhihirisha namna historia inavyoweza kutumika kisanaa kusawiri migogoro na masuala yenye umuhimu katika jamii ya leo.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 96 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sifa za tamthiliya

Tamthiliya huwa na sifa mbalimbali kama vile kutawaliwa na majibizano, kugawika katika vitendo na maonesho na kuwa na maelekezo. Tamthiliya huhusisha mazungumzo ya wahusika. Mara nyingi, tamthiliya huundwa na vitendo vyenye maonesho kadhaa kulingana na matakwa ya mtunzi. Hata hivyo, tamthiliya nyingine huundwa kwa maonesho pekee. Baadhi ya waandishi hutenga vitendo au maonesho kwa kuyapa majina kama vile kijito, vijito, mto, jito, bahari (katika *Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe*, (Edwin Semzaba, 1988). Tamthiliya huwa na maelekezo yanayofafanua mambo mbalimbali kama vile wahusika, mandhari na mwongozo wa uigizaji.

Aina za tamthiliya

Tunaweza kuainisha tamthiliya kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile kigezo cha maudhui, kusudio, dhima, muktadha wa utendaji, hadhira lengwa na mbinu za kisanii. Kila kigezo hutupatia aina mahususi za tamthiliya. Mathalani, kigezo cha hadhira lengwa kinapotumika, huweza kutupatia aina zifuatazo: tamthiliya ya watoto, tamthiliya ya vijana, tamthiliya ya watu wazima, tamthiliya ya wanawake, tamthiliya ya wanaume, tamthiliya ya miungu na tamthiliya ya waumini wa dini fulani. Uainishaji uliotumika katika kitabu hiki umetumia kigezo cha mbinu za kisanaa. Kwa kuzingatia kigezo hicho, tunapata aina zifuatazo: tanzia, ramsa, tanzia ramsa, melodrama, majaribio na bubwi.

(a) Tanzia

Tanzia ni tamthiliya zenye tukio au matukio ya kuhuzunisha. Tanzia inahusika na mambo yenye uzito, kifikra na kihisia, katika maisha ya binadamu. Mhusika mkuu ambaye kwa kawaida ni mtu maarufu na hupewa sifa nyingi zinazovutia, hukabiliwa na shida au tatizo. Tatizo hilo ni kama lile linaloweza kumkabili mtu yeyote. Hujitahidi kulitatua tatizo hili hata hivyo, hali ya ulimwenguni na tabia ya kibinadamu humfanya asiweze kufaulu na mwishowe hushindwa. Kwa hiyo, mwisho wa tamthiliya hizi ni masikitiko, maanguko na hasara kwa mhusika mkuu au jamii. Mfano wa tanzia ni tamthiliya ya *Kifo kisimani (*Kithaka wa Mberia, 2001).

(b) Ramsa

Ramsa hujulikana pia kama komedia au futuhi. Ramsa hukusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema. Sifa ya kufurahisha na kuchekesha haimaanishi kwamba tamthiliya za aina hii hazina maudhui mazito. Tamthiliya hizi hushughulikia masuala mbalimbali ya msingi kama vile uzembe, uzalishaji mali, siasa, mapenzi na ndoa. Utani, mzaha na kejeli

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hutumika katika kuchekesha. Kupitia uchekeshaji huo, jamii, watawala na watu binafsi hukosolewa. Mhusika mkuu wa ramsa si lazima awe mtu maarufu. Anaweza kuwa mtu wa kawaida au anaweza kuwa mtu wa nasaba duni, lakini hubeba matendo ya ucheshi. Mhusika huyu akifanikiwa, wasomaji au watazamaji hufurahi. Mfano mzuri wa ramsa ni tamthiliya ya *Mfalme Juha* (Farouk Topan, 1971).

(c) Tanzia ramsa

Hii ni tamthiliya yenye mseto wa maudhui ya kuhuzinisha na kufurahisha. Mifano ya tamthiliya hizi ni *Kaptula la Marx* (Euphrase Kezilahabi, 1999), *Pambo* (Penina Muhando, 1975), *Masaibu ya Ndugu Jero* (Wole Soyinka, [mf.] Abdulhakim Yahaya, 1974), *Mabepari wa Venisi* (William Shakespeare [mf.] Julius Nyerere, 1969) na *Wakati Ukuta* (Ebrahim Hussein, 1969).

(d) Melodrama

Melodrama hujulikana pia kama vichekesho. Hii ni tamthiliya yenye matumizi mengi ya uimbaji wa nyimbo. Inafanana sana na tanzia ingawa, mara nyingi, nguli wa melodrama huibuka na ushindi. Dhamira za melodrama huzungumzia mvutano kati ya wema na uovu au ubaya. Matukio yake husisimua sana na mwendo wa msuko wake huwa ni wa harakaharaka. Wahusika wake huvutia lakini hawana sifa za kishujaa. Mwishoni, mhusika mwema hupata ushindi.

(e) Majaribio

Ni tamthiliya zinazotumia mbinu zinazokiuka kaida zilizozoeleka. Tamthiliya za kimajaribio za Kiswahili hutumia mbinu za jadi na za Ki-Aristotle. Kwa mfano, *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (Ebrahim Hussein, 1976) na *Harakati za Ukombozi* (Amandina Lihamba, May Balisidya, na Penina Muhando, 1982).

(f) Bubwi

Ni tamthiliya inayotumia vitendo na ishara bila maneno.

Tofauti baina ya michezo ya fasihi simulizi na tamthiliya za fasihi andishi

(a) Utunzi wa maonesho

Mtungaji wa mchezo na mwigizaji katika tamthiliya ya fasihi andishi mara nyingi huwa ni watu tofauti. Maneno ya mtunzi ni lazima yakaririwe na waigizaji jinsi yalivyo au kama madokezo ya lazima. Kwa upande wa fasihi simulizi, watunzi wa mchezo ndio wachezaji. Maneno na vitendo ni vyao wenyewe tena hubuniwa hapo hapo.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 98 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Maandalizi

Tamthiliya ya fasihi andishi hupitia maandalizi kadhaa kama vile kufanya mazoezi mengi kabla ya kuigizwa jukwaani. Pia, jukwaa na vyombo vitakavyotumika ni sharti viandaliwe mapema. Kwa upande wa maigizo ya fasihi simulizi, karibu kila mahali panafaa kuwa jukwaa. Kadhalika, kitu chochote kama vile ardhi, vifuu na matawi ya miti huweza kuwa nyenzo muhimu katika utendaji.

(c) Shabaha

Shabaha kuu katika tamthiliya ya fasihi andishi ni kuelimisha, kuburudisha na biashara kwa sababu watu hununua tamthiliya. Maigizo ya fasihi simulizi hukusudiwa kuburudisha na kufundisha; mara nyingi, si kazi ya ujira. Hata hivyo, baadhi ya vipera vya fasihi simulizi siku hizi ni sehemu ya kujipatia vipato.

Zoezi la 3

(i) "Tamthiliya za Kitanzania za sasa ni zao la tamthiliya za Kimagharibi." Jadili.

(ii) Eleza kwa ufupi namna dhana ya utendekaji inavyojitokeza katika tamthiliya.

(iii) Kwa kutumia mifano, eleza aina za tamthiliya na namna zinavyotofautiana.

4. Riwaya

Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni itumiayo lugha ya kinathari (lugha ya mjazo) pamoja na uchanganamani wa visa, wahusika, mandhari na dhamira. Vipengele hivyo hubuniwa kutokana na uhalisi wa maisha ya jamii inayohusika. Hivyo, riwaya huweza kutoa picha ya jumla ya maisha ya mtu kutoka nyumbani (mtu binafsi) hadi kiwango cha taifa na hata dunia nzima (Said Ahmed Mohamed, 1995; Joshua Madumulla, 2009).

Sifa za riwaya

Riwaya ina sifa zifuatazo:

(a) Huwa ni ndefu ukilinganisha na tanzu nyingine. Urefu wa riwaya ya *Hiba ya Wivu* (Zainabu Mwanga, 1984) kwa mfano ni tofauti na ule wa hadithi fupi ya *Uwike Usiwike Kutakucha* (Gabriel Ruhumbika, 1978).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 99 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Huwa na visa changamani, yaani huwa na visa zaidi ya kimoja, ambapo kisa kikuu hujengwa na visa vidogo.

(c) Huwa na wahusika wengi na waliokuzwa. Kutokana na riwaya kuwa na visa vingi, huwa na wahusika wengi ambao humwezesha mwandishi kukidhi haja hii.

(d) Huwa na mandhari pana na huendelezwa kikamilifu. Kwa kuwa riwaya hushughulikia mawazo mengi, hujishughulisha na vipengele vingi vya maisha ambavyo hupatikana katika nyakati na mahali tofauti kama vile shuleni, mijini, vijijini, nyumbani na barabarani. Ili kushughulikia mazingira mapana, simulizi hutumia kipindi kirefu cha wakati ikilinganishwa na kazi kama vile hadithi fupi ambayo huweza kuchukua kipindi kifupi tu kukamilika.

(e) Huwa na migogoro iliyokuzwa zaidi kwa sababu mwandishi ana uhuru mkubwa wa kuiibua na kuieleza kwa kina.

(f) Hutumia lugha ya kisanii ya kinathari (lugha ya mjazo).

(g) Huwa na uwezo wa kubeba au kutomelea tanzu nyingine (kama vile barua, insha, shairi, wimbo au igizo) bila matatizo kwa sababu ya urefu na upana wake. Mathalani, katika riwaya ya *Kiu ya Haki* (Zainabu Mwanga, 1983) mwandishi ametumia hadithi ndani ya hadithi. Hadithi mojawapo ni ile ya Mzee Fundisha, anayesimulia yaliyompata alipovamiwa na polisi nyumbani kwake na kulazimishwa kutoa rushwa ya Sh. 2,000 ingawa hakuwa na hatia. Vilevile, kuna hadithi ya Sikujua, anayesimulia yaliyompata miaka kumi iliyopita wakati yeye na Pondamali wakifanya biashara ya kubadilisha fedha.

Historia ya riwaya

Riwaya ni utanzu wa hivi karibuni zaidi ukilinganishwa na ushairi na tamthiliya. Inadaiwa kwamba riwaya ilipata umbo ililo nalo hivi sasa katika karne ya 18 huko Ulaya. Riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kiutamaduni na viwanda. Ukoloni na uvumbuzi viliumba hali zilizohitaji kuelezwa kwa mawanda mapana kuliko ilivyowezekana katika ngano na hadithi fupi. Uchangamano wa maisha katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, utamaduni na uchumi ulihitaji kuwa na utanzu wa fasihi ulio na uchangamano kifani na kimaudhui pia. Kupanuka kwa usomaji, hasa wakati wa mapinduzi ya viwanda huko Uingereza kuliwafanya waandishi waandike maandiko marefu kwa sababu walikuwapo wasomaji, hasa wanawake, waliokuwa wakibaki majumbani wakati waume zao wakiwa viwandani (Njogu na Chimera, 1999; Joshua Madumulla, 2009).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 100 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Afrika ni moja ya mabara yenye historia fupi zaidi ya riwaya, ambapo maandiko ya riwaya yalianza kujitokeza mwishoni mwa karne ya 19. Katika eneo la Afrika ya Mashariki, kazi za kinathari za kwanza hazikukidhi ubora wa usanii na ubunifu. Baadhi ya maandiko ya awali ni *Habari za Wakilindi* (Abdalla Hemed el Ajjemi, 1885, 1907), *Tulivyoona na Tulivyofanya Uingereza* (Martin Kayamba, 1932), *Mwaka katika Minyororo* (Samwil Sehoza, 1921) na *Uhuru wa Watumwa* (James Mbotela, 1934). Vyote hivi vinaangukia katika kundi linaloendana na tawasifu au masimulizi ya wasafiri; na, kwa hakika, kiwango cha usanifu wa vitabu hivi ni cha chini.

Nchini Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazoendelea, nathari andishi ya kibunifu ni fani ambayo imechelewa kuja. Nathari bunifu simulizi, kama vile hadithi, hekaya na ngano iliyosimuliwa kwa mdomo ndiyo ambayo ilitawala ndani ya jamii.

Kwa upande wa fasihi andishi, kwa kipindi kirefu, maandiko ya fani ya ushairi, hususani tenzi za Kiswahili katika hati ya Kiarabu, ndiyo yaliyotamba katika eneo la Pwani ya Afrika ya Mashariki. Maandiko ya kinathari yalianza baada ya ujio wa wamisionari. Nathari simulizi inayojulikana kuandikwa na wenyeji ni *Habari za Mrima* (Sheikh Ali bin Hemed, 1880) ilichapishwa mwaka 1935 katika *Mambo Leo*, gazeti la Kiswahili lililovuma wakati huo. Nathari nyingine ni ile ya *Habari za Wakilindi* ambayo juzuu ya kwanza ilichapishwa mwaka 1894, ya pili mwaka 1904 na ya tatu mwaka 1907 na Abdallah bin Hemed bin Ali el Ajjemy mzaliwa wa Zanzibar kwa baba wa Kiarabu na mama wa Kihehe. Kitabu hiki kilihusu masimulizi ya Wasambaa. Kumbukumbu nyingine ni zile zilizohusu Lamu na ambazo zinasadikiwa kuwa ziliandikwa na Shaibu Faraji, na kuchapishwa na William Hichens (1928). Maandiko haya yalitokea wakati wa kipindi cha Wajerumani (Njogu na Chimera, 1999).

Baada tu ya Vita vya Kwanza vya Dunia, Waingereza walijishughulisha zaidi na kuandika na kufasiri vitabu vya shule vya kiada na ziada. Baadhi ya vitabu hivyo ni: *Hadithi ya Allan Quartermain* (Ridder Haggard [mf.] Frederick Johnson, 1934), *Safari za Gulliver* (Nathanael Swift, [mf.] Frederick Johnson, 1932), *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Ridder Haggard, [mf.] Edwin Brenn, 1929) na *Alfu Lela Ulela* ([Waf.] Frederick Johnson na Edwin Brenn 1929), *Kisiwa Chenye Hazina* (Robert Stevenson [mf.] Frederick Johnson, 1929), *Hadithi za Esopo*

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 101 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(John Bunyan, 1925 [mf.] David Diva). Maandiko haya yalikuwa maarufu hadi kufika mwaka wa 1950 ambapo waandishi wazawa walianza kujitokeza kuandika nathari za kibunifu (bunilizi) kwa mfuatano wa kimikondo (Joshua Madumulla, 2009).

Riwaya ya Kiswahili iliendelea kukua na kubadilika sambamba na vipindi mbalimbali vya kihistoria nchini Tanzania. Katika kipindi cha miaka 1940 mpaka 1970, riwaya za aina mbalimbali ziliandikwa, zikiwamo za kitawasifu, kimaadili, kiethnolojia, na za kihalifu au kikachero. Riwaya za kimaadili, kwa mfano, zina sifa za kifasihi simulizi ambazo ni matumizi ya dialojia, kutofungwa na wakati pamoja na matumizi ya mubalagha (chuku), ambayo hukipatia kitu sura, uwezo na nguvu isiyokuwa ya kawaida. Mifano ya riwaya hizi ni *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguze* za Shabaan Robert.

Riwaya nyingine za kipindi hiki zilisheheni maudhui yaliyosawiri tamaduni za jamii mbalimbali. Mfano mmojawapo ni riwaya ya *Kurwa na Doto* (Mohamed Saleh Farsy, 1960) inayosawiri maisha ya watu wa visiwa vya Unguja. Hali kadhalika, kuna riwaya ya *Mzishi wa Baba ana Radhi* (Felician Nkwera, 1967), inayoelezea maisha ya Wapangwa wa Ziwa Nyasa. Vilevile, kuna riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka, Ntulanalwo na Bulihwali* (Aniceti Kitereza, 1981). Riwaya hii inasawiri mila na desturi za jamii ya Wakerewe kabla ya kuja kwa wageni kutoka ng'ambo.

Aidha, kipindi hiki kilitamalakiwa na riwaya zenye maudhui ya kiuhalifu na kipelelezi. Mfano mzuri ni riwaya za Muhammed Said Abdulla ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Kosa la Bwana Msa* (1984).

Baada ya uhuru, na hatimaye Azimio la Arusha kutangazwa, ziliibuka riwaya zenye maudhui yenye kuhusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kipindi hiki, makundi mawili ya waandishi yalijitokeza kuandika riwaya kuelezea Azimio la Arusha. Kundi la kwanza liliuona ujamaa kwa jicho la ujadi. Kundi hili liliandika kazi zao kwa kusawiri maisha yaliyopita. Mfano wa riwaya za kundi hili ni *Mtu ni Utu* (George Mhina, 1971) na *Njozi za Usiku* (William Seme, 1976). Kundi la pili ni lile lililouona ujamaa kwa jicho la matarajio kwamba kuna ujenzi wa jamii mpya itakayoishi vizuri kuliko jamii iliyokuwapo. Kwa hiyo, kundi hili liliandika kazi kwa shauku ya kueleza mabadiliko yatakayoletwa na vijiji vya ujamaa. Mfano wa riwaya hizo ni *Shida* (May Balisidya, 1975) na

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 102 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ndoto ya Ndaria (John Ngomoi, 1976). Riwaya hizi zililenga kuonesha ubora wa maisha ya vijijini. Muundo wa riwaya hizi ni wa moja kwa moja, lugha nyepesi na wahusika wasio tata.

Pia, katika kipindi hiki, walijitokeza waandishi walioandika riwaya kwa jicho la kiyakinifu. Riwaya za namna hii ziliyachanganua na kuyasawiri masuala ya kijamii kipembuzi. Mifano ya riwaya hizo ni *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Shafi Adam Shafi, 1978), *Kuli* (Shafi Adam Shafi, 1979) na *Dunia Mti Mkavu* (Said Ahmed Mohamed, 1979). Waandishi wa riwaya hizi wanaeleza mapambano dhidi ya umwinyi na ubepari. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, kwa mfano, kuna mvutano baina ya mamwinyi, watwana na watumwa. Pande hizi mbili zinakinzana na hatimaye, mikinzano inazaa mapinduzi. Kwa kiasi, waandishi hawa waliathiriwa na fikra za Ki-Marx (F.E.M.K Senkoro, 1984).

Katika miaka ya 1980 kuliibuka wimbi la uandishi wa riwaya pendwa. Riwaya hizi zilizuka kutokana na sababu za kiuchumi, ambapo uchumi wa Tanzania uliyumba kutokana na Vita vya Kagera, majanga kama ukame, pamoja na masharti magumu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia. Waandishi wengi walianza kuandika riwaya pendwa kwa lengo la kujipatia fedha za haraka. Pia, zilizuka kampuni nyingi za uchapishaji nchini. Kampuni hizo zilirahisisha uchapishaji wa riwaya pendwa kwa haraka na kwa gharama nafuu. Soko la riwaya pendwa lilikuwa kubwa kutokana na maudhui yake kupendwa na watu wa rika zote. Aidha, waandishi ndio walikuwa wachapishaji na wauzaji wakuu wa riwaya hizo. Miongoni mwa riwaya hizo ni *Tutarudi na Roho Zetu* (Ben Mtobwa 1987), *Roho Mkononi* (Hammie Rajab,1984), *Dimbwi la Damu* (Ben Mtobwa, 1984), *Njama* (Aristablas Elvis Musiba, 1981), *Kikomo* (Aristablas Elvis Musiba, 1980) Nyingine ni *Kijasho Chembamba* (Eddie Ganzel, 1980), *Ufunguo wa Bandia* (Hammie Rajab, 1974), *Jeraha la Moyo* (Saifu Kiango, 1974) na *Kwa Sababu ya Fedha* (John Simbamwene, 1972).

Pia, katika kipindi hiki waandishi wengi waliandika riwaya zilizohakiki jamii. Riwaya hizi zilitokana na Azimio la Arusha kutokidhi matarajio ya Watanzania. Wasanii waliandika riwaya kueleza maoni kuhusu viongozi walioaminika kuwaongoza wananchi kuyafikia malengo ya vijiji vya ujamaa.Viongozi waligeuka wasaliti, waroho, wazembe huku wakiendekeza rushwa, uvivu, ulevi na ubadhirifu wa mali ya umma. Mfano wa riwaya za kipindi hicho ni *Nyota ya Huzuni* (George Liwenga, 1978), *Njozi Iliyopotea* (Claude Mung'ong'o, 1979), *Sudi ya Yohana* (Chachage Seithy Chachage 1981), *Kivuli* (Chachage Seithy

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 103 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chachage, 1981), *Harusi* (Abdalla Safari, 1984) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Gabriel Ruhumbika, 1992).

Riwaya hizo za kihakiki zimeendelea kuandikwa mpaka miaka ya 2000. Riwaya hizi zimejadili upokezi na athari za soko huria lililotokana na sera za ubinafsishaji. Katika mfumo huu, njia kuu za uchumi zinamilikiwa na watu binafsi, wengi wao wakiwa si wazawa. Kwa hiyo, wazawa wameendelea kuishi maisha magumu kinyume na matarajio waliyokuwa nayo, baada ya uhuru, hususani baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Mifano ya riwaya zenye maudhui yanayohusiana na ubinafsishaji na soko huria ni *Almasi za Bandia* (Chachage Seithy Chachage 1991) na *Makuadi wa Soko Huria* (Chachage Seithy Chachage, 2002).

Ikumbukwe kwamba hakuna mpaka bayana katika vipindi vilivyotajwa hapo juu. Kuna kazi za fasihi andishi zenye maudhui yanayohusu vipindi tofauti katika kipindi kimoja. Hivyo, si ajabu kukuta riwaya za kiuhakiki katika kipindi cha Azimio la Arusha; vivyo hivyo, riwaya pendwa zinajitokeza katika vipindi vyote. Pia, hali hii inaweza ikatokana na mhamo wa kutoka kipindi kimoja kwenda kipindi kingine. Katika kipindi cha mpito, kunakuwa na kazi za fasihi zinazozungumzia kipindi ambacho kinaelekea kufikia mwisho na nyingine zinakuwa na maudhui ya kipindi kilichopo au hata kijacho.

Aina za Riwaya

Riwaya hugawanywa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Vigezo vilivyo maarufu ni vya kutazama fani na maudhui. Kifani, riwaya huainishwa kwa kuzingatia jinsi vipengele vya fani vinavyojitokeza. Kadhalika, kimaudhui, mgawanyo hutazama mambo yanayoongelewa katika riwaya inayohusika. Kigezo hiki cha maudhui ndicho kinachotumika katika kitabu hiki. Kwa kutumia kigezo hiki, kuna makundi makubwa mawili ya riwaya: riwaya dhati na riwaya pendwa.

1. Riwaya dhati

Riwaya dhati ni zile zinazochambua matatizo au masuala mazito ya kijamii, kutafuta sababu zake, athari zake na ikiwezekana ufumbuzi wake. Riwaya hizi hukusudiwa kumfikirisha msomaji kuhusu masuala mazito na si kumstarehesha tu. Riwaya dhati zimegawanyika katika aina mbalimbali. Aina hizo ni: riwaya za kijamii, kisaikolojia, sira, kiistiara, kingano, teti, chuku, kihistoria, kimaadili, kimapinduzi na kifalsafa. Pia, kuna riwaya za barua na vitisho.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 104 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Riwaya za kijamii

Hizi ni riwaya zinazosawiri maisha na matatizo ya kawaida ya kijamii. Matatizo hayo huweza kuwa ya kifamilia, kimahusiano, kitabaka, kisiasa na kiutamaduni. Maudhui mengine ni mgongano kati ya ukale na usasa, kati ya maisha ya mjini na ya shamba na migogoro ya kifamilia. Wahusika wake, aghalabu, huwa halisi ambao wanapatikana katika jamii. Hivyo, huifanya riwaya iwe inaishi wakati wote, yaani haichuji. Aina hii ndiyo yenye idadi kubwa ya riwaya. Mifano ya riwaya za aina hii ni *Siku ya Watenzi Wote* (Shaaban Robert, 1968). *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971), *Titi la Mkwe* (Alex Banzi, 1972) na *Nyota ya Rehema* (Mohamed, 1978).

(b) Riwaya za kisaikolojia

Hizi ni riwaya zinazododosa nafsi ya mhusika. Inadodosa fikra, hisia, mawazo, imani, hofu, mashaka, matumaini na matamanio yake binafsi. Vilevile, hudodosa athari za mambo hayo kwa mhusika na labda jamii yake. Hueleza mikinzano ya ndani ya mhusika kinafsi, kiakili na kijinsia. Baadhi ya riwaya za aina hii ni: *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971), *Kiu* (Mohamed Said Mohamed, 1972), *Ukiwa* (Katama Mkangi, 1973), *Kichwa maji* (Euphrase Kezilahabi, 1974). *Tata za Asumini* (Said Ahmed Mohamed, 1990), na *Mhanga Nafsi Yangu* (Said Ahmed Mohamed, 2012) .

(c) Riwaya za sira

Hizi ni riwaya ambazo husimulia habari za mhusika au wahusika tangu kuzaliwa hadi pale inapokomea au anapo fariki. Riwaya za aina hizi zimegawanyika katika makundi mawili: ambayo ni riwaya za kitawasifu na za kiwasifu.

Riwaya za kitawasifu

Riwaya za kitawasifu ni zile zinazotumia nafsi ya kwanza, yaani mwandishi anajielezea mwenyewe tangu kuzaliwa kwake hadi muda wa kuandika riwaya husika. Mwandishi hueleza matukio ambayo huona yanasisimua na huenda hayatokei kwa wengine. Kwa kuyaeleza, anadhani yanaweza kuwasaidia wasomaji. Pia, inaweka kumbukumbu au historia ya maisha ya mtu binafsi. Mifano ya riwaya za aina hizi ni *Mbali na Nyumbani* (Shafi Adam Shafi, 2013) na *Nasikia Sauti ya Mama* (Ken Walibora, 2015).

Riwaya za kiwasifu

Riwaya za kiwasifu ni zile zinazotumia nafsi ya tatu, yaani mwandishi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 105 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

husimulia maisha ya mtu mwingine. Mfano wa riwaya za wasifu ni *Wasifu wa Siti Binti Saad* (Shaaban Robert, 1967).

(d) Riwaya za Istiara

Ni riwaya za mafumbo ambazo umbo lake la nje ni ishara au kiwakilishi tu cha jambo jingine. Mifano mizuri ni riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* za Shaaban Robert ambazo huenda ni istiara kuhusu utawala wa mabavu wa kikoloni.

(e) Riwaya za kingano

Hizi ni riwaya zenye umbo na mtindo wa ngano. Mathalani, huweza kuwa na wahusika wanyama, visa vya ajabu ajabu, mandhari ya kubuni na visa vyenye kutendeka nje ya wakati wa kihistoria. Mfano wa riwaya za kingano ni *Adili na Nduguze* (Shaaban Robert, 1952) na *Lila na Fila* (Kiimbila, 1966).

(f) Riwaya teti

Hizi ni riwaya zinazosimulia vituko na masaibu ya maayari (watu wapuuzi walaghai, wajanja, na kadhalika) kwa njia inayosisimua na kuchekesha. Aghalabu maayari hao huwa ni watu wanaovutia (si wahusika wawi/ waovu), wa tabaka la chini, na bapa. Matukio ya riwaya hii hayana msuko ulioshikamana vizuri. Mfano wa riwaya hizi ni *Hekaya za Abunuwasi.*

(g) Riwaya barua

Hizi ni riwaya ambazo sehemu yake kubwa husimuliwa kwa njia ya barua wanazoandikiana baadhi ya wahusika. Mfano ni riwaya ya *Barua Ndefu kama Hii* (Mariama Bâ, 1980).

(h) Riwaya chuku

Hizi ni riwaya za vituko na masahibu yasiyokuwa ya kawaida na yasiyozingatia uhalisi. Mara nyingi, masahibu ya riwaya chuku huambatana na mapenzi ya kindugu. Katika fasihi ya Kiswahili, riwaya za Shaaban Robert kama vile *Adili na Nduguze* na *Kusadikika* (Shaaban Robert,1967) zinaingia katika kundi hili.

(i) Riwaya za kihistoria

Riwaya hizi huchanganya historia halisi na ubunifu ili kutoa maudhui fulani. Mara nyingi, riwaya hizi zinajikita kwenye matukio makuu ya kihistoria yaliyoathiri mwenendo na mwelekeo wa jamii au taifa linalohusika. Riwaya ya kihistoria huchanganya wahusika wa historia na wa kubuni, matukio ya

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 106

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kweli na ya kubuni. Hata hivyo, riwaya hizo huzingatia zaidi namna matukio makuu ya kihistoria yalivyomwathiri mtu binafsi aliyeyashiriki. Riwaya ya kihistoria ina dhamira zinazogusa watu wengi, ni muhimu kwa sababu masimulizi yake yanahusu mambo yaliyotokea, na inawezekana yaliwahi kuwapata hata wasomaji. Ni kumbukumbu nzuri ya kipindi kilichopita. Baadhi ya riwaya mashuhuri za kihistoria ni *Uhuru wa Watumwa* (James Mbotela 1934), *Kuli* (Shafi Adam Shafi 1979), *Zawadi ya Ushindi* (Ben Mtobwa, 1987), *Kwa Heri Iselamagazi* (Bernard Mapalala, 1992) na *Pambazuko Gizani* (Karumuna Mboneko 2004). Pia, kuna riwaya za Mugyabuso Mulokozi za *Ngome ya Mianzi* (1990), *Ngoma ya Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996). Nyingine ni *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992) na *Wachamungu wa Bibi Kilihona* (Gabriel Ruhumbika, 2014) .

(j) Riwaya za kimaadili

Hizi ni riwaya zenye nia ya kufundisha maadili fulani yahusuyo mwenendo mwema katika maisha. Hii ni riwaya inayowapa watu maadili, na mara nyingi, maadili hayo huwa ya kidini. Wahusika wakuu huwa na sifa na tabia nzuri bila udhaifu. Sifa hizo ni za kudumu; kama ni mwenendo mwema huwa mwema tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mabadiliko yakitokea, huwa ni ya kimaadili na hutokea ghafla. Mifano ya riwaya za aina hii ni *Adili na Nduguze* (Shaaban Robert, 1952) *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili* (Mathias Mnyampala, 1961) na *Mtu ni Utu* (George Mhina, 1971).

(k) Riwaya za kimapinduzi

Hizi ni riwaya zinazojadili matatizo yanayosababisha ukinzani fulani katika jamii kwa lengo la kuleta mabadiliko. Mabadiliko hayo huweza kuwa ya kisiasa, kiutamaduni au kiuchumi. Aghalabu, lengo la riwaya hizi ni kuuwezesha umma kushika hatamu kwa njia ya mapambano. Mifano ya aina hii ya riwaya ni *Ubeberu Utashindwa* (Joseph Kiimbila, 1971), *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Shafi Adam Shafi, 1974), *Kabwela* (Abdalla Saffari, 1976), *Dunia Mti Mkavu* (Said Ahmed Mohamed, 1979) na *Kuli* (Shafi Adam Shafi, 1979).

(l) Riwaya ya kifalsafa

Riwaya za kifalsafa ni zile zinazojadili masuala mazito kuhusu maisha. Aghalabu, masuala hayo ni yale yanayohitaji tafakuri ya kina ili kuyaibua na kuyapatia ufumbuzi. Hii inamaanisha kuwa riwaya hizi zinajadili kwa kina na kwa kufanya tafakuri makini kuhusu mambo ambayo hayaonekani

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa urahisi. Muundo wa riwaya hizi ni changamano. Riwaya hizi hujadili maswali kama vile: Ukweli ni nini? Maisha ni nini? Kifo ni nini? Kuwapo na kutokuwapo ni nini? Mifano ya riwaya za kifalsafa ni *Mzingile*, *Kichwa maji* (Euphrase Kezilahabi, 1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (Euphrase Kezilahabi, 1978), *Mafuta* (Katama Mkangi, 1984), *Kiza katika Nuru* (Said Ahmed Mohamed, 1988), *Nagona* (Euphrase Kezilahabi, 1989), *Ziraili na Zirani* (William Mkufya, 1999), na *Babu alipofufuka* (Said Ahmed Mohammed, 2001).

(m) Riwaya ya vitisho

Hii ni riwaya yenye visa vya kutisha na kusisimua. Mara nyingi, visa hivyo huambatana na mambo ya ajabu au miujiza. Mambo hayo ni kama vile mauaji ya kishirikina, uchawi, uganga na vita. Mifano ya riwaya hii ni *Mbojo Simba Mtu* (Kuboja, 1971), *Mirathi ya Hatari* (Claude Mung'ong'o, 1977) na *Janga Sugu la Wazawa* (Gabriel Ruhumbika, 2002). Riwaya ya *Mirathi ya Hatari*, kwa mfano, imeeleza visa na mikasa ya kishiri katika jamii za Njombe. Msanii amemtumia Gusto ambaye anarithishwa mirathi ya hatari (uchawi) kutoka kwa baba yake, Kazembe. Mirathi hiyo inasababisha vifo visivyokuwa vya kawaida. Miongoni mwa vifo hivyo ni kile cha mama yake Gusto, dada yake (Nandi) na mjomba wake Gusto (Kapedzile). Kuwapo kwa matukio mengi ya kichawi kunaleta hofu kwa wasomaji wa riwaya hii. Zaidi, matendo yanayotendeka wakati Gusto akila kiapo cha uchawi yanatisha mno.

2. Riwaya pendwa

Riwaya pendwa ni zile ambazo hutumia fani inayojichomoza na kusisimua zaidi kiasi cha kuweza kufunika maudhui. Hali hii huifanya riwaya hizi zionekane kuwa na lengo la kustarehesha au kuburudisha wasomaji tu. Mambo yanayosawiriwa sana na waandishi wa riwaya za kundi hili ni mapenzi, upelelezi, ujasusi, ugaidi, ujambazi na mauaji. Waandishi wa riwaya pendwa huyasawiri mambo hayo kwa ufundi mkubwa; na hupangilia visa na vituko kwa namna inayosisimua. Nchini Tanzania, aina hii ya riwaya iliandikwa kwa mara ya kwanza na Muhamed Said Abdulla (MSA) alipoandika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957). Mifano mingine ya riwaya hizi ni *Simu ya Kifo* (Faraji Katalambula, 1965), *Kisima cha Giningi* (Mohammed Said Abdulla, 1968) na *Njama* (Aristablas Elvis Musiba, 1981).

Katika miaka ya 1980, uandishi wa riwaya za aina hii uliongezeka maradufu kutokana na matatizo ya kiuchumi. Hali mbaya ya maisha iliyokuwapo hapa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 108 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nchini miaka ya 1980 iliwafanya waandishi waandike riwaya pendwa ili waweze kujikwamua kiuchumi. Kwa ujumla, maandishi yao ni mwigo au mwendelezo wa maandishi ya Kimagharibi pamoja na filamu za Kizungu na Kiasia zinazohusisha uhalifu na mapenzi.

Sifa za riwaya pendwa

Riwaya pendwa ina sifa zifuatazo:

(a) Hutumia taharuki kwa kiasi kikubwa

Taharuki ni hamu kubwa anayokuwa nayo msomaji kutaka kujua mambo yatakayotokea na yatakavyotokea katika hadithi. Taharuki hutumiwa kwa kiasi kikubwa katika riwaya pendwa kupitia matukio ya kusisimua yanayojibainisha kwa njia ya mikinzano iliyosukwa kwa ufundi. Taharuki inafikia kilele wakati fumbo linapofumbuliwa kwa kujibiwa maswali kadhaa yaliyojitokeza akilini mwa msomaji. Kwa mfano, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* (Mohammed Said Abdulla, 1957) swali linalojitokeza ni: nani amemuua Bwana Ali Bomani? Mbinu za awali za msanii za kumfanya msomaji awatuhumu watu wasiohusika ndizo zinazojenga maswali akilini mwa msomaji.

(b) Hutumia wahusika wale wale

Riwaya pendwa ina sifa ya kutumia wahusika wale wale; hivyo, huwa na uwezo wa kujiendeleza katika vitabu kadhaa. Karibu kila mwandishi maarufu wa riwaya pendwa ameandika vitabu zaidi ya kimoja. Sifa hiyo ya kuwatumia wahusika wale wale hufanya kitabu kimoja katika mfuatano wa vitabu kadhaa vya mwandishi mmoja kionekane kama tukio linalojitegemea katika mfululizo wa matukio. Mifano ya watunzi waliowatumia wahusika wa jinsi hii ni Aristablas Elvis Musiba. Huyu amemtumia mhusika *Willy Gamba* katika riwaya zake kama vile *Kufa na Kupona* (1974) *Kisasi* (1979), *Uchu* (2000), *Kikomo* (1980), *Njama* (1981) na *Hofu* (1988). Pia, kuna Muhammed Said Abdulla ambaye amemtumia mhusika Bwana Msa katika riwaya za *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957), *Kisima cha Giningi* (1973) *Duniani Kuna Watu* na *Kosa la Bwana Msa* (1984). Mwandishi mwingine ni Ben Mtobwa ambaye amemtumia mhusika *Joram Kiango* katika riwaya za *Pesa Zako Zinanuka* (1984), *Tutarudi na Roho Zetu?* (1984) na *Salamu Toka Kuzimu* (1987).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 109 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Huwa na mhusika mkuu mkwezwa

Mhusika wa riwaya pendwa mara nyingi hupewa sifa zisizo za kawaida kitabia na kiutendaji. Mhusika mkuu wa riwaya pendwa hukwezwa juu ya wahusika wengine; hivyo, anawatawala na ana sifa ya ubabe. Wahusika hawa huwa na sifa ya kuwa kielelezo chenye ukamilifu, yaani kutokuwa na dosari. Mifano mizuri ya wahusika wa namna hii ni Bwana Msa, Willy Gamba na Joram Kiango. Mara kwa mara, mhusika mkuu ndiye mshindi; hata atakapopitia katika taabu na mashaka ya aina gani, tunajua, hatimaye ataibuka kuwa mshindi katika mapambano yake. Wahusika hawa wakuu hutenda na kuendesha mambo yao kama miungu wadogo pasi na kukosea. Huwa hodari sana katika kutenda mambo yao. Mambo hayo ni kama vile kuchunguza, kufanya mapenzi, kuwindana, kupigana kwa silaha na kwa mikono mitupu. Kwa hiyo, ufundi wa utendaji unaojitokeza humo huwa unaziteka nafsi za wasomaji, na wakati mwingine, kuwasahaulisha hata maudhui. Mfano mzuri ni riwaya ya *Njama* (Aristablas Elvis Musiba, 1981). Msomaji anapoendelea kuisoma riwaya hii, anajikuta anamezwa na ufundi wa kupeleleza na kupambana unaooneshwa na Willy na wenzake kiasi cha kupoteza kiini cha simulizi yenyewe, ambacho kinahusu ukombozi wa nchi za Afrika. Hali hii inasababishwa na hali ya kukwezwa kwa wahusika wa riwaya, hususani Willy Gamba, katika tabia na matendo yao.

(d) Masimulizi yake yanapendwa na watu wengi

Riwaya hizi zina wasomaji na wapenzi wengi, hasa vijana. Hii ni kwa sababu wasanii wake wameupatia vizuri utunzi wa kisasa ambao umeletwa na utamaduni wa kigeni unaofuatwa kwa makini na vijana na baadhi ya watu wazima. Kwa hiyo, watu wanaposoma riwaya hizi, wanasisimka na kuburudishwa.

(e) Hutumia mandhari ya mijini

Wasanii wa riwaya pendwa hutumia mandhari halisi au ya kubuni, ila hujikita sana katika miji au majiji. Hali hii ndiyo inayoonesha upekee wa mandhari ya riwaya pendwa. Wasanii hutumia mandhari ya namna hii ili kukidhi malengo ya usukaji wa visa na maisha ya wahusika. Mandhari ya namna hii hubeba matukio kama vile ufujaji mkubwa wa fedha kwenye sehemu za starehe, kama vile baa, mahoteli makubwa na fukwe za bahari. Kwa mfano, kwenye riwaya ya *Salamu Toka Kuzimu* (Ben Mtobwa, 1987), kuna ufujaji mkubwa wa fedha unaofanywa na mhusika Joram na mpenzi wake. Vilevile, mandhari ya mijini yanaoneshwa kupitia tukio kama la uchezaji wa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 110 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kamari linalojitokeza kwenye riwaya ya *Simu ya Kifo* (Faraji Katalambula, 1965). Aidha, mandhari ya mjini au jijini yanathibitishwa na kuwapo kwa kampuni na mashirika makubwa. Kampuni hizi huajiri watu; wasanii huumba wahusika wenye vyeo kwa kuhusianisha na kampuni na mashirika hayo. Mfano mzuri ni mhusika *Kalulu* katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* (Mtobwa 1984). Huyu ni kiongozi katika kampuni mojawapo ya kusambaza dawa za Oxton. Mzee Jacobo kwenye *Simu ya Kifo* (Faraji Katalambula, 1965) ni mfanyakazi katika shirika la reli.

Mandhari ya mijini pia hudhihirika kupitia matumizi ya vyombo vya mawasiliano kufanikisha matukio ya ujambazi, ujasusi, uporaji na uhusiano wa kimapenzi. Mathalani, katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* (Ben Mtobwa, 1985), mhusika Kwame anatega chombo cha kunasa mawasiliano ofisini kwa Kombora. Chombo hiki kinamsaidia kunasa maongezi yote ya mipango ya kuwasaka wahalifu (Kwame na kundi lake). Kwa njia hii, Kwame na kundi lake wanang'amua mikakati ya kukamatwa, hivyo, wanafanikiwa kuwakimbia askari.

(f) Matumizi ya wanawake kama nyenzo ya mafanikio

Kwa ujumla, wahusika wakuu wa kiume wa riwaya pendwa husawiriwa wakifanikiwa katika mambo yao kupitia mbinu ya kuwatumia wanawake warembo. Warembo hao hutumiwa kwa njia za mapenzi, kuwa chambo cha kufanyia uhalifu, au chambo cha kumnasia adui. Mapenzi, kwa upande wake, huonekana kuwa jambo muhimu sana katika riwaya pendwa. Huonekana kwamba, upelelezi au shughuli yoyote inayofanyika haiwezi kusisimua wala kufanikiwa bila mapenzi. Katika riwaya za Aristablas Elvis Musiba, kwa mfano, mhusika Willy Gamba huwa na wasichana warembo ambao ndio wapenzi wake wanaomsaidia kufumbua mafumbo mazito na mitego mikubwa. Baadhi yao ni Zabibu kwenye riwaya ya *Njama*, Tete na Mwadi kwenye riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* na Nyaso kwenye riwaya ya *Hofu*.

(g) Uigaji wa mawazo na matendo

Riwaya pendwa nyingi za Kiswahili, hasa za miaka ya 1980, ni mwigo wa maandishi ya Kimagharibi pamoja na filamu za Kizungu na Kiasia zinazohusu upelelezi, ujasusi, uhalifu na mapenzi. Wasomaji wengi wameifanya riwaya pendwa kama kibadala au kijalizo cha filamu. Kwa mfano, Musiba kwenye riwaya zake, amemchora mhusika mkuu Willy Gamba, kwa kumpa ujuzi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa kupigana kininja katika mapambano dhidi ya majasusi. Kupigana kwa kufuata sheria za kininja, mara nyingi, ni mbinu zinazotumiwa na filamu za Kimagharibi na Kimashariki.

(h) Mtindo rahisi

Mara nyingi, riwaya pendwa hutumia mtindo wa masimulizi, na kwa kiasi kidogo, dialojia. Lugha yake ni rahisi na ya mazungumzo ya kila siku. Kuna matumizi ya lugha ya kisanaa pamoja na mafumbo ambayo wahusika wenyewe wanaweza kuyaelewa. Katika *Kikosi cha Kisasi*, kwa mfano, kikundi cha Willy Gamba kilikuwa kinatambuana kwa jina la KK. Vilevile, majasusi walikuwa wanakiita kikundi cha Willy Gamba kwa jina la "spea."

Zoezi la 4

(i) "Riwaya ni zao la fasihi simulizi." Jadili.
(ii) Eleza mchango wa mapinduzi ya viwanda katika kuzuka na kukua kwa riwaya.
(iii) Fafanua sifa za riwaya.
(iv) Jadili maendeleo ya riwaya ya Kiswahili baada ya Uhuru.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shughuli za kufanya

(i) Jadili maendeleo ya fasihi andishi nchini Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru.

(ii) Fafanua tofauti kati ya maigizo ya fasihi simulizi na tamthiliya ya fasihi andishi.

(iii) Jadili mielekeo miwili ya riwaya zilizoandikwa kipindi cha Azimio la Arusha.

(iv) Wafuatao hapo chini ni waandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Chambua mchango wa mwandishi mmojawapo katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

(a) Shaaban Robert

(b) Euphrase Kezilahabi

(c) Mugyabuso Mulokozi

(d) Mohammed Said Abdulla

(e) Eric Shigongo

(f) Gabriel Ruhumbika

(g) Zainabu Mwanga

(h) Penina Muhando

(v) Tofautisha dhana zifuatazo:

(a) Tenzi na tendi

(b) Ramsa na tanzia

(c) Tamthiliya na riwaya

(d) Mashairi ya kimapokeo na mashairi ya kisasa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 & 6 (KIWANDANI).indd 113 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Nne

Uhakiki wa kazi za fasihi

Utangulizi

Sura hii inahusu uhakiki wa kazi za fasihi. Vipengele ambavyo utajifunza ni dhana ya uhakiki, mhakiki wa kazi za fasihi, na misingi ya kuhakiki na kutathmini kazi za fasihi. Lengo la kujifunza mada hii ni kukuwezesha kupata ujuzi na maarifa kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi simulizi na andishi. Baada ya kujifunza mada hii, utaweza kuhakiki kazi za fasihi simulizi na andishi.

Uhakiki wa kazi za fasihi

Taaluma ya uhakiki ilianza zamani enzi za Plato (takribani miaka ya 428-348 k.k)mwanafalsafa wa zamani wa Kiyunani. Nchini Tanzania, taaluma hii ilianza kutumika zaidi miaka ya 1970, baada ya baadhi ya Watanzania kusoma taaluma ya fasihi. Miongoni mwao ni John Ramadhani na Farouk Topan. Wahakiki wengine walioendeleza taaluma hii ni Saifu Kiango, Tigiti Sengo, F.E.M.K Senkoro, Ndyanao May Balisidya, Mugyabuso Mulokozi na Mbunda Msokile.

Dhana ya uhakiki

Uhakiki ni taaluma ya uchambuzi na ufafanuzi wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi. Uchambuzi na ufafanuzi ndio unaoweza kuonesha ubora na udhaifu wa kazi ya msanii asilia. Uhakiki huwahusu watu wa aina tatu ambao ni wasanii asilia, wasomaji wa kawaida na wahakiki wenyewe.

Dhana ya mhakiki

Mhakiki ni mchambuzi na mfafanuzi wa kazi za fasihi zilizomo katika mazungumzo au maandishi kwa lengo la kubainisha fani na maudhui katika kazi hizo. Hufanya hivyo kwa kuongozwa na misingi ya nadharia fulani.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 114 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sifa za mhakiki wa kazi za fasihi

Mhakiki wa kazi za fasihi anatakiwa awe na sifa zifuatazo:

(i) Afahamu historia na siasa ya jamii inayohusika ili aweze kuelewa matatizo ya jamii hiyo.

(ii) Asome kazi mbalimbali za fasihi, tofauti na ile anayoihakiki, ili awe na ujuzi zaidi katika uwanja wa uhakiki.

(iii) Ajue historia na mazingira yaliyomkuza mwandishi au msanii.

(iv) Asome tahakiki za wahakiki wengine wa kazi za fasihi ili aweze kujiimarisha katika uhakiki.

(v) Awe mtu wa kusimamia ukweli; penye ubora aseme bayana, vivyo hivyo, penye udhaifu.

(vi) Asiongozwe na hisia zake tu anapohakiki kazi za fasihi.

(vii) Afahamu misingi na nadharia za uhakiki.

Dhima za mhakiki wa kazi za fasihi

Kumekuwa na mjadala kuhusu nafasi ya mhakiki wa kazi za fasihi. Mjadala huu umetokana na kuwapo kwa makundi mawili yanayopingana kuhusu nafasi ya mhakiki wa kazi za fasihi. Kundi la kwanza linasema kuwa wahakiki sio muhimu katika uwanja wa fasihi. Hii ni kwa sababu, wasanii ndio wahakiki wenyewe; hivyo, huweza kujikosoa na kurekebisha kazi zao mpaka wanaporidhika nazo. Mfuasi mmojawapo wa fikra za kundi hili ni Joseph Mbele (1993). Wanaongeza kuwa wahakiki huwa wanajipachika vyeo ambavyo hawastahili kwa kusema wao ni walimu wa msanii na msomaji. Hii inatokana na sababu kwamba wasomaji wa kazi za fasihi wana uwezo wa kusoma na kuelewa; hivyo, hawahitaji watu wa kuwafafanulia. Kila msomaji anaaminika kuwa na uwezo wa kuchambua kazi inayohusika, na uchambuzi hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mantiki hiyo, haitakiwi kumtegemea mhakiki ambaye naye ana mawazo yake kulingana na uwezo wake wa kuchambua na kufafanua kazi inayohusika.

Kundi la pili la wahakiki lina mtazamo tofauti na huo. Wafuasi wa kundi hili ni kama vile Samwel Mazigwa (1991), Mbunda Msokile (1993) na Saifu Kiango (1993). Hawa wanaona kwamba, msanii na mhakiki ni watu ambao wanahitajiana kwa sababu mhakiki ndiye anayeieleza na kuitambulisha kazi ya msanii kwa hadhira. Vilevile, mhakiki ndiye anayemtahadharisha mwandishi kuhusu makosa aliyoyafanya katika kazi yake na kumfanya awe makini zaidi katika kushughulikia kazi nyingine. Aidha, mhakiki ni kiungo muhimu kati ya jamii na msanii kwa sababu hutumia ujuzi wake wa kuchambua kazi ya sanaa ili kubainisha maadili,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 115 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ujumbe, msimamo na falsafa ya kazi hiyo kwa wanajamii. Wahakiki wanaamini kwamba mhakiki ni mwalimu wa jamii kwa kuwa humfundisha msomaji kuhusu yale yaliyomo katika kazi ya sanaa. Aidha, humweleza mwandishi kuhusu mambo yaliyomo katika kazi yake ambayo yanakubalika au hayakubaliki kwa jamii.

Kwa hiyo, kwa mtazamo wa kundi hili la pili, mhakiki wa kazi za fasihi ana dhima zifuatazo:

(i) Kuchambua kila kipengele cha fani na maudhui.
(ii) Kubainisha mafunzo yanayotolewa katika kazi za fasihi.
(iii) Kuhimiza na kushirikisha fikra za kihakiki katika kazi za fasihi.
(iv) Kukuza kiwango cha usomaji wa kazi za fasihi.
(v) Kumwelekeza msomaji ili apate maarifa zaidi.
(vi) Kufafanua nadharia zilizotumika katika kuhakiki kazi hiyo, ikiwa ni pamoja na kubainisha misingi bora ya uandishi wa kazi za fasihi.
(vii) Kuonesha uzuri na ubaya wa kazi iliyohakikiwa kwa lengo la kuelimisha jamii na waandishi wa kazi za fasihi.
(viii) Kubainisha falsafa na tamaduni za jamii na msanii.
(ix) Kubainisha ubora na mapungufu ya kazi za fasihi.

Mpaka hapa umejifunza kuhusu dhana ya uhakiki na mhakiki. Ifahamike kuwa maelezo ya kiuhakiki yaliyofanyiwa kazi hujulikana kama tahakiki.

Misingi ya uhakiki wa kazi za kifasihi

Misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi ni vigezo vinavyotumika katika kuhakiki kazi hizo. Vigezo vikuu vinavyotumika katika kuhakiki kazi za fasihi ni fani na maudhui.

Dhana ya fani

Fani ni moja ya sehemu kuu mbili za kazi ya fasihi zinazotumiwa na msanii kujenga kazi yake. Fani ni ufundi wa kisanaa anaoutumia mtunzi katika kuumba kazi yake. Kwa msingi huo, mhakiki hutumia vipengele vya fani katika kuhakiki kazi inayohusika. Baadhi ya vipengele hivyo ni *lugha, wahusika, mandhari, muundo* na *mtindo*.

Dhana ya maudhui

Maudhui ni mambo mbalimbali ambayo yanazungumziwa katika kazi za fasihi. Msanii hukusudia mambo hayo yaifikie hadhira yake. Maudhui ya kazi ya

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 116 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

fasihi huundwa na vipengele vingi, vikiwamo vya dhamira, mtazamo, falsafa, itikadi, msimamo, ujumbe, mafunzo na migogoro. Vipengele hivi hutumiwa na mhakiki katika kazi yake.

Uhusiano wa fani na maudhui

Kama ulivyokwishaona hapo juu, misingi mikuu miwili ya uhakiki wa kazi za fasihi ni *fani* na *maudhui*. Vipengele hivi vina uhusiano ambao umejadiliwa na wataalamu kadhaa kwa mitazamo miwili.

Mtazamo wa kwanza unaona kuwa fani na maudhui huweza kutenganishwa. Wanafasihi wenye mtazamo huu wanaona kuwa vipengele hivi huweza kujitegemea; na kwamba, si lazima viathiriane au kuingiliana. Wanaifananisha fasihi na sahani na chakula, au kikombe na maji. Katika kufafanua, wanaona maudhui kama chakula au maji; na fani kama chombo cha kubebea chakula au maji hayo. Kwa ufafanuzi wa mtazamo huu, tazama kitabu cha *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo* (Felician Nkwera, 1978). Dosari za mtazamo huu ni kushindwa kutambua dhima ya fani katika kujenga maudhui, na dhima ya maudhui katika kusanifu au kuibua fani.

Mtazamo wa pili unaona kuwa fani na maudhui ni vipengele visivyoweza kutenganishwa; kwamba, vipengele hivyo huibuana, huathiriana na kutegemeana. Wanafasihi wenye mtazamo huu huona kuwa kazi nzuri ya fasihi hujengwa na uwiano mzuri wa fani na maudhui. Hii ni kwa sababu mambo haya ni kama pande mbili za sarafu moja. Mtazamo huu tunaupata katika vitabu vya *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Kulikoyela Kahigi na Mugyabuso Mulokozi, 1982) na *Fasihi* (F.E.M.K. Senkoro, 2011). Mtazamo huu ndio unaotumiwa katika kitabu hiki kwa sababu vipengele vya fani na maudhui vinajengana na kukamilishana.

Vipengele vya uhakiki wa fani

Vipengele vya fani vinavyotumika katika kuhakiki kazi za fasihi ni lugha, wahusika, muundo, mtindo na mandhari. Yafuatayo ni maelezo kuhusu vipengele hivyo:

1. Lugha

Lugha ni kipengele muhimu sana katika kazi za fasihi, kwani hutofautisha kazi za fasihi na sanaa nyingine. Maudhui ya kazi ya fasihi yanaweza kuathiriwa na matumizi ya lugha. Lugha inayotumika katika fasihi ni ya kisanaa na ya kipekee hata kama itaonekana ni ya kawaida. Vipengele vya lugha vinavyotumiwa na mhakiki katika kuhakiki kazi za fasihi ni kama vifuatavyo:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Tamathali za usemi

Tamathali za usemi ni neno au vifungu vya maneno vinavyotumika kama kifananisho au kiwakilisho cha dhana fulani dhidi ya dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Hizi ni semi ambazo hutumiwa kwa maana maalumu kulingana na kazi inayohusika. Tamathali za semi zimegawanyika katika makundi makuu manne. Makundi hayo ni tamathali za mafumbo, tamathali za mlinganisho, tamathali za msisitizo na tamathali nyingine za semi.

(i) Tamathali za mafumbo

Msanii anatumia tamathali hizi kwa lengo la kuelezea jambo kinyume. Ifahamike kuwa ufundi wa kutengeneza fumbo hilo lazima uambatane na maana yenye uzito fulani katika tamathali inayohusika. Tamathali za mafumbo ni kama vile:

Dhihaka

Tamathali ya aina hii hubeba dharau. Hutumiwa na msanii kwa lengo la kumdunisha mhusika kwa kutumia mafumbo. Tazama mifano ifuatayo: "Yule mtu ni mchapa kazi kweli, kila siku njaa inapiga hodi nyumbani kwake"; au kumuita mtu rafiki ilhali ni adui. Mathalani, Mwalimu Nyerere alivyokuwa anamwita Idi Amini Dada "rafiki yangu," alikuwa anatumia dhihaka.

Tasifida

Hii ni tamathali inayotumiwa kwa lengo la kupunguza ukali wa kauli au matusi. Maneno yanayotolewa kwa tasifida huwa ni kinyume na maadili ya jamii inayohusika pale yanapotamkwa kama yalivyo. Tasifida hujumuisha majina mbadala yanayotaja sehemu za siri za binadamu pamoja na matendo yasiyotakiwa kufanywa hadharani. Tazama mifano ifuatayo:

- "Amejisaidia" badala ya "amekunya."
- "Ameaga dunia" badala ya "amekufa."
- "Uani" badala ya "chooni."
- "Kujifungua" badala ya "kuzaa" (kwa binadamu).

(ii) Tamathali za mlinganisho

Hizi ni aina za tamathali za semi zinazolinganisha vitu vyenye hadhi, sifa na umbile tofauti. Tamathali hizi ni kama vile:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 118 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tashbiha au Mshabaha

Tamathali hii hulinganisha vitu au mambo kwa kutumia maneno linganishi ya *kama, mfano wa, sawa na,* na *kama vile*. Mambo au vitu vinavyolinganishwa ni kama vile tabia, mwenendo, umbile au mtindo wa maisha. Tazama mifano ifuatayo:

- Yule jamaa ana usingizi *kama* pono.
- Amekuwa mrefu *mithili* ya twiga.
- Ni kigeugeu *mfano* wa popo.
- Bide ni *sawa* na sifuri.

Sitiari

Tamathali ya aina hii hulinganisha matendo, vitu na tabia ya vitu vyenye maumbile au hadhi tofauti bila kutumia maneno linganishi. Vitu hulinganishwa kana kwamba viko sawasawa, kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

- Ujana maji ya moto.
- Alikuwa koleo.
- Almasi ni roho yangu.
- Kiko ni mkaa.

Tashihisi

Hii ni tamathali ya usemi ambayo vitu visivyokuwa na uhai au uwezo wa kutenda hupewa uhai na uwezo wa kutenda kama kiumbe chenye asili ya kufanya hivyo au kiumbe chenye uhai. Angalia mifano ifuatayo:

- Giza lilizingira jiji zima.
- Kijiji kilitabasamu baada ya mvua kunyesha.
- Mifupa ya viungo vyake ilipiga kelele kwa mateso ya kunyooshwa.
- Mbingu zitashangilia kuwapokea watakatifu.
- Jua limetabasamu asubuhi na mapema.

(iii) Tamathali za msisitizo

Tamathali za aina hii husisitiza mambo mbalimbali katika kazi za sanaa. Baadhi ya tamathali hizo ni hizi zifuatazo:

Takriri

Ni ujirudiaji wa sauti, silabi au maneno yanayolingana katika kazi ya

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 119
17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

fasihi kwa lengo la kusisitiza au kutilia mkazo jambo fulani. Tazama mifano hii ya ujirudiaji wa maneno:

- Nikija, nikija, nikija utapona.
- Soma, soma mwanangu.
- Leo utanikoma, utanikoma nakwambia.
- Maisha ni magumu, ni magumu kwelikweli.

Tabaini

Hii ni aina ya tamathali za semi inayosisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani. Tazama mifano hii:

- Amekuwa mweusi si mweusi, mweupe si mweupe.
- Alikuwa mrefu, mfupi.
- Macho yanacheka, moyo unalia.
- Mwanzo wangu, ni mwisho wangu.
- Binadamu hupanga, Mungu hupangua.

(iv) Tamathali nyingine za semi

Kuna tamathali nyingine ambazo haziingii katika makundi yaliyotajwa hapo juu. Tamathali hizo ni:

Mubalagha

Tamathali hii hutia chumvi kuhusu tabia za watu, vitu au hali. Angalia mifano ifuatayo:

- Mtoto alilia mpaka akakauka.
- Ametoa machozi ya damu.
- Alisimama mpaka miguu ikaingia tumboni.
- Mji mzima ulihamia nyumbani kwake.

Ritifaa

Hii ni tamathali ya usemi ya kusemesha mtu au kitu kisichokuwapo. Mathalani, mtu huweza kuzungumza na mtu mwingine aliye mbali kana kwamba mtu huyo anamsikia. Tazama mfano wa shairi lifuatalo:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 120 17/09/2019 13:20

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Amina

1. Amina umejitenga, kufa umetangulia,
Kama ua umefunga, baada ya kuchanua,
Nakuombea mwanga, peponi kukubaliwa,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

2. Nilitaka unyanyuke, kwa kukuombea dua,
Sikupenda ushindike, maradhi kukuchukua,
Ila kwa rehema yake, Mungu amekuchagua,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

3. Majonzi hayaneneki, kila nikikumbukia,
Nawaza kile na hiki, naona kama ruia,
Mauti sijasadiki, kuwa mwisho wa dunia,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

4. Nasadiki haziozi, roho hazitapotea,
Twafuata uwokozi, kwa mauti kutujia,
Na wewe wangu mpenzi, peponi utaingia,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

5. Jambo moja nakumbuka, sahihi ninalijua,
Kuwa sasa umefika, ta'bu isikosumbua,
Kwayo nimefurahika, nyuma nilikobakia,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

6. Nimemaliza kutunga, kwa kukuombea dua,
Vumbi tena likiunga, roho likirudishiwa,
Mauti yakijitenga, mapenzi yatarejea,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

Shaaban Robert, *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1966:5)

Katika shairi hili, Shaaban Robert anaandika kana kwamba anawasiliana moja kwa moja na marehemu Amina (mkewe ambaye alikuwa analiliwa katika shairi hili baada ya kufariki).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 121 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mdokezo

Tamathali ya aina hii hudokeza kitu na kukiacha bila kukamilisha, aghalabu, kitu hicho huwa kinafahamika katika muktadha husika. Tazama mifano ifuatayo:

- Walipofika tu waka…
- Alimpiga, akamfunga kamba, kisha aka…
- Alimwangalia kwa dharau, hakusema zaidi ya…

Mjalizo

Hii ni tamathali ya usemi ambayo msanii huamua kutumia maneno yanayofuatana bila kuweka viunganishi isipokuwa alama ya mkato. Tazama mifano ifuatayo:

- Nilikimbia, nikachoka, nikalala.
- Niliamka, nikapiga mswaki, nikanywa chai.

Nidaa

Tamathali hii huonesha kushangazwa na jambo fulani. Tamathali ya aina hii huambatana na alama ya mshangao kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

- Mungu wangu!
- La hasha!
- Lo!
- Astaghafirullah!

Balagha

Hii ni tamathali ya usemi ambayo mtu huuliza jambo huku akifahamu jibu lake. Swali hilo huweza kuulizwa ili kuweka msisitizo, kubeza au kushangaa. Tazama mifano hii:

- Ni wewe kweli? (Kama mtu amekutana na rafiki bila kutarajia anaweza kuuliza swali kama hili).
- Mtu anaweza kuwa ameshika noti ya shilingi 10,000 halafu anajiuliza: Hii ni shilingi 10,000? (Mtu huyu hakuwa na matarajio ya kupata kiasi hicho cha fedha).

Majazi

Hii ni tamathali ya usemi ambayo wahusika wa kazi ya fasihi hupewa majina yanayoakisi wasifu au tabia zao. Aidha, majazi huhusisha majina ya mahali na mandhari. Mifano ya majazi tunaipata katika majina kama vile Majivuno, Karama na Jeta yaliyotumika katika riwaya ya

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 122 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kusadikika (Shaaban Robert, 1951) .

Mwigo (Tanakali)

Hii ni aina ya tamathali ya usemi ambayo huigiza mtu au kitu. Kuna aina kuu mbili za mwigo, nazo ni tanakali sauti na tanakali lafudhi.

Tanakali Sauti (Onomotopea)

Hii ni tanakali ambayo hutumika katika kuiga sauti za vitu mbalimbali kulingana na lengo na muktadha husika. Tazama mifano ifuatayo:

- Alikuwa akitembea huku malapa yake yakilia *pata pata pata*
- Moyo ulimdunda *tu! tu!tu!*
- Aligonga mlango *ngo! ngo! ngo!*

Tanakali Lafudhi

Hii ni aina ya tanakali yenye kuiga matamshi ya watu fulani wanaotumia lugha kwa namna fulani kwa lengo la ama kuonesha umahiri wa mhusika huyo katika matumizi ya lugha au kuonesha asili ya mhusika huyo. Tazama mifano ifuatayo:

- Pimdogo ameondoka (Pwani).
- Ntoto wa Nkuu wa Nkoa analia (Mtwara/Lindi).
- Mimi pana taka veve (Mhindi).

Taashira

Hii ni mojawapo ya tamathali za semi ambayo kwayo jina la sehemu ya kitu kimoja au la kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili. Tazama mifano ifuatayo:

- Jembe - mkulima/hodari wa kazi
- Mvi - uzee
- Kiti - uongozi
- Kichwa - akili nyingi/kiongozi

Tanabaha

Hii ni tamathali ambayo jina la mtu binafsi hutumiwa kwa watu wengine wenye tabia, mwenendo hali au kazi sawa na ya mtu huyo. Tazama mifano ifuatayo:

- Huyu ndiye Kikwete wetu (mtu anayetegemewa katika familia).
- Tunaye Kezilahabi mpya (Mtunzi chipukizi hodari sana).
- Messi katupatia ushindi mnono leo (mchezaji hodari ambaye uchezaji wake unafananishwa na wa *Leonel Messi)*.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 123 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Semi mbalimbali

Semi ni kipengele muhimu katika uhakiki wa kazi za fasihi. Umekwisha jifunza kuhusu semi katika sura ya pili kuwa, utanzu huu unajumuisha vipera kama vile methali, misemo, nahau, mafumbo, lakabu, misimu na vitendawili. Hivyo, uhakiki wa semi unapaswa kuzingatia jinsi vipera hivi vilivyotumika katika kazi husika.

(c) Taswira

Taswira au jazanda ni picha inayojengwa akilini mwa hadhira awe msikilizaji, msomaji au mtazamaji anapofuatilia kazi fulani ya fasihi (Kyallo Wamitila, 2008). Taswira hujengwa na utumiaji mzuri wa lugha. Msanii mzuri ni yule mwenye uwezo mkubwa wa kutumia taswira zinazoendana na kile anachokielezea. Kuna aina kuu tatu za taswira ambazo ni taswira za hisi, taswira za mawazo na taswira zinazoonekana.

Taswira za Hisi

Taswira za aina hii hujihusisha zaidi na mwili wa binadamu. Huweza kumfanya mtu awe na baridi, wasiwasi na msisimko wa furaha au woga. Kwa kawaida, taswira hizi hushughulikia hisi za ndani ya mwili wa binadamu. Tazama mifano ifuatayo:

- Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.
- Mshale wa uchungu ulipenya moyoni mwake ukamkaba koo hata asiweze kupumua vizuri.

Taswira za Mawazo/Kufikirika

Hizi ni taswira ambazo hujitokeza zaidi mawazoni na huweza kuganda akilini mwa mtu. Hizi ni taswira dhahania kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

- Alipofika nyumbani kwangu alijiona kama mtu aliye peponi.
- Alipoingizwa rumande alijihisi kama yuko kaburini.

Hakuna mtu ambaye amewahi kufika peponi au kaburini, bali tunawaza kuwa peponi ni mahali pazuri na kaburini ni pabaya.

Taswira za Vitu Vinavyoonekana

Hizi ni taswira ambazo hujengwa na vielelezo tunavyovijua na ambavyo tunaweza kuvishika kama inavyoonekana katika mfano huu.

- Alionekana kama **udongo** usiokuwa na rutuba.
- Wanaume nauliza mwafanyani? **Pakashume** jigeuza ni kwa nini?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 124

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maneno yaliyokoza yanajenga taswira zinazoonekana, na ambazo zinaweza kushikika. Udongo usiokuwa na rutuba hautoi mazao, na pakashume anawakilisha wanaume ambao hawatulii nyumbani.

(d) Matumizi ya ucheshi na utanzia

Ucheshi ni mbinu inayotumika katika kazi za sanaa ili kufurahisha na kuchekesha kupitia dhihaka, kejeli, utani na vijembe. Mara nyingi, ucheshi hujengwa na mambo mawili ambayo ni: mnato wa lugha au msigano wa kifikra kati ya kitu kilichosawiriwa katika sanaa na uhalisi unaojulikana kuhusu kitu hicho (Athumani Ponera, 2014). Mfano wa matumizi ya ucheshi tunaupata katika tamthiliya ya *Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe* (Edwin Semzaba, 1988). Humo kuna matumizi ya vifungu kama vile, "…sarawili yake kama kengele ya bomani…" na "…kwani mlango nao unahesabiwa?" Vifungu hivi vinaweza kuzua ucheshi kwa sababu vinabeba dhihaka. Suruali ya Ngoswe inabeuliwa kwa kufananishwa na kengele. Pia, kutokana na kukosa elimu kuhusu umuhimu wa sensa, mhesabiwa mmojawapo anauliza swali la kibeuzi kuhusu akina nani wanapaswa kuhesabiwa.

Kwa upande mwingine, utanzia hujengwa kupitia mateso, ulemavu (wa viungo au mifumo ya mwili), maradhi, balaa kama vile njaa, mafuriko, magonjwa na kimbunga. Kwa mfano, riwaya ya *Njama* inasawiri hali ya utanzia kupitia matukio mengi. Mojawapo ni la kifo cha mhusika Veronika Amadu. Msomaji anapokutana na kifo cha mpelelezi huyu anaweza kupata hisia za majonzi.

Fasihi huakisi jamii; hivyo, huakisi pia hali hizi mbili za utanzia na ucheshi ambazo ni za kawaida katika jamii. Hivyo, msanii mzuri ni yule mwenye uwezo wa kusawiri hali hizo katika kazi yake.

2. Wahusika

Wahusika ni viumbe au watu waliokusudiwa na mwandishi wawakilishe tabia za watu katika kazi ya fasihi. Wahusika huwakilisha tabaka fulani. Kwa mfano, Mfalme na Malkia katika riwaya ya *Kufikirika* (Shabaan Robert, 1967) wanawakilisha tabaka tawala, wakati Mwalimu anawakilisha tabaka tawaliwa, wanyonge, wenye busara na wasomi. Msomaji au msikilizaji anayetaka kumwelewa mhusika kwa kina, sharti ajiulize maswali yafuatayo:

(i) Mhusika anafanya nini?
(ii) Anasema nini?
(iii) Msimulizi anasemaje kumhusu mhusika?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 125 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Wahusika wengine wanasema nini kumhusu mhusika huyo ?
(v) Wewe kama msomaji au msikilizaji unamwonaje?
(vi) Uhusika wake ukoje katika kazi inayohusika (yaani, anabeba jukumu gani katika kazi husika?)

Vilevile, wasifu wa ndani na wa nje wa mhusika aliopewa na mwandishi husaidia kumfahamu mhusika. Wasifu wa nje unatokana na sifa za kimaumbile ambazo huonekana kwa macho. Wasifu wa ndani hutokana na tabia ya mhusika kupitia matendo na kauli zake. Jambo la kuzingatia ni kwamba, mhusika ni kiumbe kinachobuniwa na mwandishi kutokana na mahitaji ya kazi husika, na kwa kuzingatia uzoefu wake katika maisha. Mwandishi humchora mhusika wake kulingana na lengo lake.

Aina za wahusika

Wahusika huweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali. Katika kitabu hiki tunaainisha wahusika kwa kutumia vigezo viwili, navyo ni majukumu na tabia.

(a) Kigezo cha majukumu

Kigezo cha majukumu hugawanya wahusika katika aina mbili: wahusika wakuu na wahusika wadogo.

(i) Mhusika mkuu

Huyu ni mhusika anayejitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Hutokea akitenda mambo pamoja na kuzungumza na wahusika wengine. Mhusika huyu huweza kuwa kipaza sauti cha mwandishi kuhusu anayoyatetea au kuyalaani. Mwandishi humtumia mhusika huyu katika kujenga dhamira kuu ingawa hata msingi wa dhamira ndogo ni mhusika mkuu. Mfano wa mhusika mkuu ni Rashid katika riwaya ya *Kuli* (Shafi Adam Shafi, 1979). Kazi moja ya fasihi inaweza kuwa na mhusika mkuu zaidi ya mmoja. Kwa mfano, riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka* na *Ntulanalwo na Bulihwali* (Aniceti Kitereza, 1980) ina wahusika wakuu wawili ambao ni Myombekere na Bugonoka.

(ii) Wahusika wadogo

Hawa ni wahusika wanaomjenga mhusika mkuu. Hujitokeza hapa na pale katika hadithi huku wakimpinga au kumsaidia mhusika mkuu. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe*

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 126 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(Edwin Semzaba, 1988), wahusika wadogo ni Mazoea, Ngengemkeni Mitomingi, Mama Mazoea, Mamainda, Mzee Jimbi, Kifaruhande, Huzuni, Chapuuka, Mama wa Kwanza, Mama wa Pili, Mama Masikio na Mtoto. Wahusika wakuu na wadogo wanaweza kuwa bapa, duara, foili au kivuli kutokana na sifa au uwezo wa kuishi kulingana na matakwa ya mtunzi, ambaye ndiye anayeamua kama mhusika fulani aendelee kuishi au asitishe kuwapo kwake. Wakati mwingine, sifa au tabia hizi huchukuliwa na baadhi ya wanafasihi kama aina za wahusika.

(b) Kigezo cha tabia

Kigezo cha tabia hugawanya wahusika katika aina nne: wahusika bapa, wahusika duara, wahusika kivuli na wahusika shinda/foili.

(i) Wahusika Bapa

Hawa ni wahusika ambao hawabadiliki kivitendo na kitabia hata kama watakutana na mazingira tofauti. Kama ni wema, wataendelea kuwa wema, na kama ni wabaya wataendelea kuwa wabaya hadi mwisho wa hadithi. Mifano ya wahusika hawa ni Bi. Kirembwe katika *Kivuli Kinaishi* (Said Ahmed Mohamed, 1988) na Karama katika *Kusadikika* (Shaaban Robert, 1951). Wahusika wakuu au wadogo wanaweza kuwa wahusika bapa.

(ii) Wahusika Duara au Mviringo

Wahusika wenye tabia hii hubadilika kulingana na mazingira wanayokutana nayo. Hukua na hubadilika kimwili na kiakili, na maisha yao hutawaliwa na hali halisi ya maisha ya jamii. Mifano ya wahusika wenye tabia hii ni Rosa katika *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971), Shida katika *Shida* (May Balisidya, 1975) na Yasmin katika *Vuta N'kuvute* (Shafi Adam Shafi, 1999).

(iii) Wahusika Kivuli

Wahusika wa aina hii hutajwa tu katika kazi ya fasihi bila kutolewa maelezo ya kutosha. "Mwalimu Nyerere" katika riwaya ya *Zawadi ya Ushindi* (Ben Mtobwa, 1987) ni mfano wa mhusika kivuli. Wahusika wa aina hii hawaoneshi matendo yao bali hutajwa na wahusika wenzao au mwandishi mwenyewe.

(iv) Wahusika shinda/foili

Wahusika hawa wana sifa ya kutegemea wahusika wenye tabia ya

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 127 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

umviringo au wenye tabia ya ubapa. Ni wahusika ambao hawana maamuzi ya kwao peke yao. Maamuzi yao hutokana na wahusika wengine ambao huwatawala kiakili au kimawazo. Najum, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* (Mohammed Said Abdulla, 1957) na Aisha, katika *Hiba ya Wivu* (Zainabu Mwanga, 1984) ni mifano ya wahusika wa aina hii.

3. Muundo

Kama ulivyosoma katika sura ya kwanza, muundo ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi. Visa na matukio hayo huweza kujitokeza katika tanzu za ushairi, hasa katika tendi na baadhi ya tenzi, riwaya na tamthiliya. Kuna miundo ya aina kuu mbili, hasa katika tamthiliya na riwaya. Miundo hiyo ni msago na rejeshi. Mara nyingi, kazi za fasihi zinaundwa kwa kuzingatia sehemu tatu ambazo ni mwanzo, kati na mwisho.

(a) Muundo wa msago (moja kwa moja)

Huu ni muundo ambao visa na matukio hufuatana kwa mtiririko sahili, kuanzia kisa cha kwanza hadi cha mwisho. Riwaya ya *Kusadikika* (Shaaban Robert, 1951) na *Usiku Utakapokwisha* (Mbunda Msokile, 1990) ni mifano ya kazi za fasihi zenye muundo wa moja kwa moja.

(b) Muundo rejeshi (kioo)

Katika muundo huu, visa na matukio huchanganywa. Ni muundo usiopangilia kisa cha kwanza au cha pili au cha tatu kwa mfuatano sahili. Kisa chochote kinaweza kuanza ili mradi tu kisiweke mkanganyiko katika kuelewa mfuatano wa matukio. Mfano wa riwaya zenye muundo huu ni *Pesa Zako Zinanuka* (Ben Mtobwa 1984), *Pepo ya Mabwege* (Harrison Mwakyembe, 1980) na *Zawadi ya Ushindi* (Ben Mtobwa, 1992).

Hata hivyo, muundo katika ushairi unatazamwa kwa namna tofauti na riwaya na tamthiliya. Muundo wa ushairi hupambanuliwa kwa kuangalia idadi ya mistari katika beti, idadi ya beti na wakati mwingine vina na mizani. Kwa kuzingatia idadi ya mistari katika kila ubeti tunapata aina zifuatazo za mashairi kimuundo:

Tathnia ni shairi lenye mistari miwili kwa kila ubeti. Tazama mfano wa shairi lifuatalo:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 128 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hofu za Bin-Adamu

Kesho ni siku nyingine, hakuna mwenye kujua,
Mungu akipenda kesho, tuonane hapo kesho.

Kesho swali akilini, tunaweza kukiona,
Kwa mapenzi yake mola, kesho twaweza inusa.

Katu hatuwezi sema, kesho lazima ione,
Kesho yetu haifiki, sababu ujinga wetu.

Kijana Taifa la kesho, kwa nini isiwe leo?
Nani ajuaye kesho, wazee taifa la kesho.

Rose Mbijima, *Kurunzi* (2019)

Tathlitha ni shairi lenye mistari mitatu kwa kila ubeti. Tazama mfano wa shairi lifuatalo:

Makosa yetu

HALIZUKI somo bora, kuliko makosa yetu,
Kosa halina sogora, hulitenda kila mtu,
Zingatia kwa imara, kukosa tabia kwetu.

Kosa likija mapema, kuongoka si vigumu,
Hutengeza mambo vema, utakayo yakatimu,
Hapana kurudi nyuma, na kulegeza hatamu.

Kosa hukuza fikira, na mnyama huwa mtu,
Kisha huamsha mara, bidii na ari zetu,
Ria zetu hudorora, mpaka tukose kitu.

Kila kiumbe lazima, kosa lake kufahamu,
Ya kuwa ni sura njema, asome aihitimu,
Ndipo awapo mzima, fahamu kuwa timamu.

Shaaban Robert, *Masomo Yenye Adili* (1968)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 129 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tarbia ni shairi lenye mistari minne kwa kila ubeti kama inavyoonekana katika ubeti unaofuata hapa chini:

Usizae chokoraa

Alipenda kuitwa baba, mke akamtafuta,
Wana walifika saba, kwa malezi ya utata,
Hawakula na kushiba, uchumi ulizorota,
Watoto wa mtaani, matunda yenu wazazi.

Baba aliwakimbia, kuyakwepa majukumu,
Mama alifikiria, mwishowe akanywa sumu,
Nani angewapatia, mahitajio muhimu,
Watoto wa mtaani, matunda yenu wazazi.

Sakafuni walilala, darasa walitoroka,
Hawakujua pa kula, jamani waliteseka,
Hawakuzivaa ndala, mavazi yenye viraka,
Watoto wa mtaani, matunda yenu wazazi.

Cosmas Mushi katika Mkuki na Nyota, *Diwani ya Tuzo za Ushairi ya Ebrahim Hussein* (2016:144)

Takhmisa ni shairi lenye mistari mitano kwa kila ubeti. Tutazame shairi lifuatalo:

Hekalu limechafuka

Nimeshapoteza njia, yani sasa niko niko,
Sijui wapi sawia, panipasa kuendako,
Nipaamini kwa nia, sipate misukosuko,
Maisha yenye murua, muda wote ni vicheko,
Hekalu limechafuka.

Imani lipolalia, kwa sasa tena haipo,
Baada ya kujionea, uozo na michafuko,
Kwa siku yajizidia, hadi yazua mnuko,
Hewa yote hutibua, haifai kwa pumuko,
Hekalu limechafuka.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 130 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pale tunoaminia, utakatifu uliko,
Maombi panopitia, yafike kwa tuendako,
Aweze kuturidhia, na kutupa farijiko,
Leo pamechafukia, amani yenda mshuko.
Hekalu limechafuka.

Idd Mwimbe katika Mkulima na Nyota, *Diwani ya Tunzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein* (2016:153)

Tasdisa au **Sudusia** ni shairi lenye mistari sita kwa kila ubeti. Tazama mfano wa shairi lifuatalo:

Shetani, Rangi Rangile

Aa, awali sisi twanena, sisi sisi wananchi,
Ama kiza twakiona, ni kiza hiki hakuchi,
Mbaya wetu karudi, karudi tena mbichi,
Huu ukweli nanena,
Kweli siyo pirikichi,
Mbaya wetu karudi, shetani rangi rangile.

Ba, bahari tunaiona, bado haina shuwari,
Mawimbi yatatizana, mkondoni menawiri,
Tufani ni nana nana, katu hatuoni heri,
Roho atuminya sana,
Ka jeuri na kiburi,
Mbaya wetu karudi, shetani rangi rangile.

(Ally Mwalimu Rashid katika Mkuki na Nyota, *Diwani ya Tunzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein* (2016:166)

Sabilia ni shairi lenye mistari saba katika kila ubeti. Angalia ubeti ufuatao wa shairi.

Kuondoana Njiani

Kazi za sasa hasara, kwa jamii wafanyao,
Nyingi kukuru kakara, hazitimizi chajio,
Wenye nguvu wadorora, wako wapi wachumao?
Fanya kazi kwa imara, tajiri apate cheo,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 131 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kichwa kiote kipara, macho uvae vioo,
Huzidishwi mshahara, wala huna fanikio,
Tutatenda ndivyo sivyo, tuondoane njiani.

Shaaban Robert, *Kielezo cha Fasili* (1968)

Idadi ya mishororo inaweza kuongezeka kulingana na mtunzi anavyopendelea, na ikapewa majina mengine kama vile usaba, unane, ukenda na ukumi. Aidha, muundo hujumuisha idadi ya sura, mgawanyo wa sura katika sehemu ndogo ndogo, na matumizi ya vichwa vya habari katika sura. Waandishi wengine hutumia namba au nyota kutambulisha sura kuu na sehemu ndogo ndogo za sura inayohusika.

4. Mtindo

Mtindo ni jinsi msanii anavyotumia ufundi na hisia zake katika kujenga upekee wa utunzi wa kazi ya fasihi. Ufundi huo ndio unaofanya kazi yake ivutie na iwe tofauti na za watunzi wengine hata kama jambo linaloongelewa ni moja.

Vipengele vya Mtindo

Mtindo wa kazi za fasihi hujidhihirisha katika vipengele mbalimbali vya kazi hizo. Baadhi ya vipengele hivyo ni:

(i) *Utomelezi*: Humaanisha matumizi ya tanzu au vipengele vingine ndani ya utanzu mmoja. Mathalani, utomelezi huweza kufanywa kwa kupachika barua, nyimbo, shairi, au hotuba katika kazi inayoshughulikiwa. Mfano wa utomelezi ni matumizi ya ushairi ndani ya hadithi au barua ndani ya hadithi kama ilivyo katika *Njozi Iliyopotea* (Claude Mung'ong'o, 1978) na *Mtenda Hutendwa* (Rose Mbijima, 2019).

(ii) *Dialojia (majibizano)*: Hapa wahusika wanajibizana wao kwa wao. Ni mtindo wa kitamthiliya wenye kutofautisha tamthiliya na tanzu nyingine. Mtindo huu utaitwa mtindo mmojawapo kati ya mitindo iliyotumika katika kazi ya fasihi iwapo msanii atautumia katika utanzu mwingine tofauti na tamthiliya.

(iii) *Matumizi ya masimulizi na maelezo*: Huu ni mtindo maarufu unaopambanua utanzu wa riwaya kutoka katika tanzu nyingine. Wakati mwingine, mtindo huu hujitokeza katika tanzu nyingine tofauti na riwaya. Hali hii inapotokea huchukuliwa kama mtindo wa mwandishi.

(iv) *Matumizi ya nafsi*: Nafsi ni kitu muhimu sana katika kazi za fasihi. Nafsi hutupatia nafasi ya mwandishi na wahusika katika kazi fulani. Kuna nafsi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 132 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tatu ambazo hutumika katika kazi za fasihi. Nazo ni nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Msanii anaweza kutumia nafsi ya kwanza, hasa katika kazi zenye uhusiano wa karibu na historia yake. Hata hivyo, si kila kazi ya fasihi yenye mtindo wa aina hii huchukuliwa kama historia ya maisha ya mwandishi. Kuna baadhi ya kazi zenye mtindo huu ambazo zinaelezea vitu ambavyo havihusiani na maisha ya mwandishi. Nafsi ya kwanza hutumiwa na msanii kwa lengo la kuifanya hadhira ijihisi kuwa ni mshiriki katika yale yanayoongelewa na mwandishi. Nafsi ya pili huonesha kutohusika moja kwa moja kwa mwandishi juu ya mambo yanayozungumziwa ndani ya kazi inayohusika. Wakati mwingine, nafsi ya aina hii hutumiwa kama njia mojawapo ya kumwadilisha mtu fulani ambaye ni "wewe." Maadili hayo yanaweza kutolewa kwa njia ya maonyo au ushauri. Hata hivyo, ni kazi chache sana za riwaya zenye mtindo wa aina hii. Kazi nyingi zenye mtindo huu ni ushairi na tamthiliya. Nafsi ya tatu hutumika katika kazi ili kuelezea matendo au tabia ya mtu mwingine.

(v) *Mbinu ya kuhoji*: Hii ni mbinu inayotumiwa na msanii katika kuelezea mawazo yake kwa hadhira. Kunakuwa na hali ya kuhoji hata kama masuala yanayoongelewa yanaeleweka. Pamoja na malengo mengine, mbinu hii hutumiwa ili kumfikirisha msomaji au msikilizaji. Mbinu hii imetumika mwishoni mwa riwaya ya *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi, 1971).

(vi) *Matumizi ya barua*: Msanii anaweza kutumia mtindo wa barua katika kuandika kazi yake kama ilivyo katika *Barua Ndefu Kama Hii* (Mariama Bâ, 2009).

Kama ulivyojifunza katika sura zilizotangulia, mtindo ni dhana muhimu katika ushairi. Ifuatayo ni baadhi ya mitindo katika ushairi:

(i) *Mtindo wa kidato:* Baadhi ya mistari hufupishwa maneno yake au silabi zake tofauti na mistari mingine ambayo huwa na silabi au maneno mengi. Ufupishaji huu wa maneno au silabi katika baadhi ya mistari hufanywa kwa lengo maalumu. Kwa mfano, katika shairi la *Fumbua,* mstari wa mwisho una maneno mawili wakati mistari mingine ina maneno mengi. Mwandishi anasema:

Ama pindu pindua, nalo pindo lapindika,
Pinduo likiingia, mengine yanatukuka,
Baadhi yadidimia, kukidhi tunayotaka,
Kitendawili fumbua.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 133 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Theobald Mvungi, *Raha Karaha* (1982)

Mfano mwingine ni shairi la *Yanachanganya*:

Yanachanganya

Nina swali langu gumu, lakosa jibu la wazi,
Aje hapa mtalamu, alojawa na ujuzi,
Ninayo nyingi na hamu, kuupata na ujuzi,
Yanachanganya.

Babu ninamkumbuka, sasa hivi marehemu,
Babu aliimarika, kasemwa kila sehemu,
Babu maneno lisuka, litupa si binadamu,
Yanachanganya.

Nimejaribu shakiza, kwa waliofunga ndoa,
Li waweze kutujuza, nasi tupate kuoa,
Waniambie angaza, mambo yatakuwa poa,
Yanachanganya.

Vijana twapata tabu, tutafutao ni sisi,
Waweza pata aibu, tamaa zile za fisi,
Tukipiga mahesabu, tusitake ya wepesi,
Yanachanganya.

Penzi si halisi katu, roho zetu juu juu,
Mapenzi yaleta kutu, yasababisha makuu,
Mapenzi ni mkurutu, nakuwa vimbaumbau,
Yanachanganya.

Unaweza kudhania, kimwana umempata,
Mzuri kupindukia, hatoyaleta matata,
Mara ukastukia, mwingine kamfuata,
Yanachanganya.

Sio huko tu mjini, mapenzi kuwaadhibu,
Mpaka na vijijini, yatokea maajabu,
Uchawi wanaamini, waganga wanawatibu,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Yanachanganya.
Japo moyo waumia, tusichoke kusubiri,
Japo si tutakawia, tutulie kijasiri,
Japo fumbo latujia, tutawapata wazuri,
Yanachanganya.

Rose Mbijima, *Kurunzi* (2019)

(ii) *Kikufu:* Ni mtindo unaotumia neno la mwisho katika mshororo wa kwanza kuanzisha mshororo wa pili, neno la mwisho katika mshororo wa pili kuanzisha mshororo wa tatu, na neno la mwisho katika mshororo wa tatu kuanzisha mshororo wa nne. Ruwaza hii inaweza kuendelea iwapo utatunga shairi lenye idadi yoyote ya mishororo. Tazama mfano ufuatao:

Tusipuuze Elimu

Enyi wa bara na pwani, amkeni msilale,
Msilale amkeni, imeshapigwa kengele,
Kengele yenye maani, kwamba ni muda wa shule,
Shule haraka twendeni, elimu tujipatie.

Tujipatie elimu, tujuwe haya na yale,
Yale ya kule na humu, tuyasome vilevile,
Vilevile tufahamu, kuziganga kila ndwele,
Ndwele, ujinga ni sumu, tuviambae milele.

Milele bila kuchoka, tusome tuwe ka wale,
Wale waloelimika, kwa kutopuuza shule,
Shule kitu cha kushika, faidaze zipo mbele,
Mbele tusonge haraka, ujinga tusitawale.

Tusitawale kabisa, ujinga niwaambile,
Niwaambile kutosa, majini tusiuole,
Tusiuole kwa sasa, elimu tukamatile,
Tukamatile si kosa, tusipigeto kelele.

Kelele za debe tupu, hazifidi tangu kale,
Kale ujinga upupu, na hata sasa vivile,
Vivile tenga si kapu, na mafu si mai male,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 135 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Male mai kwapukwapu, yataka ujuzi tele.
Tele tujae shuleni, tuwahi elimu ile,
Ile ilo na thamani, hadi tufike kilele,
Kilele cha umakini, ja wapishi wa mchele,
Mchele kiwa shambani, mpunga ndo jinale.

Mathias Mnyampala, [Mh.] *Fasili ya Johari ya Mashairi* (1964);

Maneno yaliyopigiwa mstari yanadhihirisha matumizi ya kikufu kutokana na kushikamanisha mishororo na beti. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza, maneno msilale, kengele na shule yanashikamanisha mishororo minne ya ubeti huo. Pia, neno tujipatile linashikamanisha ubeti wa kwanza na wa pili.

(iii) Mtindo wa pindu: Hujidhihirisha pale ambapo neno au sehemu ya neno la mwisho katika kipande au mstari hurudiwa mwanzoni mwa kipande au mshororo unaofuata. Tazama mfano wa ubeti ufuatao:

Zuko

Tika kitupu hu**tika**, **tika** upya una**fuka**,
Uka huko uka**leni**, **leni** mapya kula**fuka**,
Fukara we mza**mani**, **ma'ni** mapya huta**taka**,
Takataka mawa**zoni**, **zoni** huna huku**shika**,
Shika - Mimi sishi**kani**, **kani**zo zapukutika.

Kulikoyela Kahigi, katika Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi, *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1982:79)

(iv) Mtindo wa kiitiko (kituo): Mstari wa mwisho hujirudiarudia kwa kila ubeti. Mfano mzuri ni shairi la *Kwetu ni Kwao kwa Nini?* Mwandishi anasema:

Mtu huuliza nini, kitu hiki ni cha nini?
Kitu hiki cha nani, na hiki kitu cha nini?
Nacho kinaitwa nini, na cha nani na kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

Na kwa nini cha nani, na chake kwa njia gani?
Jawabu liwe yakini, lisiwe purukushani?
Kwa nini sababu gani? kwao ni kwetu kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 136

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa nini kwao kwa nini, kuwe kwetu ni kwa nini?
Na kwetu pia kwa nini, kuitwa kwao kwa nini?
Kwa nini ina yakini, kwetu ni kwao kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

Mtu kwao huthamini, ijapokuwa jiweni,
Pia alale mtini, na baraza liwe chini,
Nile matunda porini, kuitwa kwenu kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

Saadani Kandoro, *Mashairi ya Saadani* (1972: 138-139)

(v) *Mtindo wa takriri:* Ni ujirudiaji wa neno au silabi unaofanywa kwa makusudio maalumu. Kwa mfano, takriri neno na takriri vina: shairi la *Msiba Uliotuangukia* lina takriri neno, ambapo neno 'wengine' limejirudiarudia katika beti mbalimbali. Tazama ubeti ufuatao:

Wengine tukakithiri kushangaa,
Wengine wakazidi kulialia,
Wengine wakazidi kutetemeka,
Maana tuliogopa kuanguka,
Wengine wakazidi zao ghadhabu,
Wengine wakazidi kuwa mabubu.

Kulikoyela Kahigi katika *Mashairi ya Kisasa* Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi (1973)

Kwa upande wa takriri vina, kuna shairi liitwalo "Nguo Ziteremsheni Yapungue Maasia" ambalo katika mistari mitatu ya kwanza lina takriri vina vya kati ***a*** na vina vya mwisho ***ni***. Angalia ubeti ufuatao:

Muovu aliyevaa, si yule asiye soni,
Alojiteremshia, si mkudia gotini,
Zuri ni zuri sikia, japo liwe kwa haini,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Kuvaa fupi si njia, na avae muumini,
Baya ni baya tambua, ingawa la uzunguni,
Hujahoji kwa hatua, bibi rudi kwa Manani
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 137 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kaluta A. Abedi, *Sheria za Kutunga Mashairi* (1954: 52-53)

(vi) *Mtindo wa mchoro au vielelezo:* Mpangilio wa mishororo katika beti pia huweza kudhihirisha mtindo fulani. Mishororo ya mtindo huu huweza kupangwa katika namna inayosawiri vielelezo au michoro. Tazama mfano wa mtindo wa mchoro wa L katika shairi *Maisha Mitihani*:

Maisha mitihani,
Usijiweke fichoni,
Pambana kijana,
Tama we kukana,
Maisha ni haya,
Majanga kwa kaya,
Famili zina pwaya,
Tuweze si kujikuna,
Shambani pambana,
Marafiki mlioshibana,
Mnapaswa kubebana, gurudumu kusukuma, mfike nyote pamoja,
Msipende kudundana, ninyi wote ni wa mama, msivifanye vihoja,
Msije fanya hiyana, kwa pamoja kujituma, ngazi ndefu kuzipanda,
Kazi kazi msichague, kazi kazi msibague, kazi kazi msikimbie.

Rose Mbijima, *Kurunzi* (2019)

5. Mandhari

Kama ilivyoelezwa katika sura ya kwanza mandhari inahusisha mahali ambapo matukio na visa katika kazi ya fasihi hufanyika.

Vipengele vya uhakiki wa maudhui

Uhakiki wa maudhui hujumuisha dhamira, mtazamo, msimamo, itikadi, falsafa, ujumbe na migogoro.

1. Dhamira

Ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Kazi ya fasihi inaweza kuwa na dhamira kuu na ndogo. Dhamira kuu ni wazo linalotawala katika kazi ya fasihi, ambalo mawazo mengine madogo madogo hujengwa kupitia kwake. Kazi moja ya fasihi inaweza kuwa na dhamira kuu moja au zaidi. Kwa mfano, dhamira kuu katika riwaya ya *Kuli* ni ukombozi wa kisiasa na kiuchumi. Dhamira ndogo ndogo ni

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 138 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mawazo yanayojitokeza katika kazi ya fasihi ili kujenga dhamira kuu. Mawazo haya hayana uzito kama zilivyo dhamira kuu. Kwa mfano, dhamira ndogo katika riwaya hii ni umoja na mshikamano, kujitoa mhanga na mapenzi.

2. Mtazamo

Mtazamo ni jinsi ya kuyaona mambo yanayotokea katika maisha. Aidha, mtazamo ni maoni ya mtu binafsi. Kila mtu ana namna au jinsi ya kuyatazama mambo yanayomzunguka katika maisha yake; namna hiyo huwa tofauti na ya mtu mwingine. Kuna aina mbili za mitazamo ambayo huwaongoza wasanii kutunga kazi na wahakiki kuhakiki kazi za kifasihi. Mitazamo hiyo ni mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu (kisayansi). Mtazamo wa kidhanifu ni ule ambao msanii huutazama ulimwengu kwa kudhania au kufikiri tu bila kuhusisha na uhalisi unaoweza kuthibitishwa. Kwa mfano, mdhanifu huweza kuutazama ulimwengu kama kitu kinachoweza kubadilika kulingana na matakwa ya Mungu. Hii inamaanisha kuwa, mabadiliko yanayoikumba jamii husababishwa na Mungu. Ulimwengu hautazamwi kama kitu dhahiri, hauoni kitu au tukio katika uhalisi wake. Mathalani, katika mtazamo huu, tukio la kuzuka kwa ugonjwa wa UKIMWI huangaliwa kama ni adhabu kutoka kwa Mungu. Mungu anawaadhibu wanadamu kwa sababu ya dhambi ya uzinzi. Kwa hiyo, wafuasi wa mtazamo huu hawajishughulishi kutafuta ukweli kwa kuzingatia uhalisi. Swali la kujiuliza hapo ni: Je, ni kweli wazinzi wote wanapata UKIMWI? Je, watoto wanaopata UKIMWI kutoka kwa mama zao ni wazinzi? Je, hakuna mtu ambaye hazini lakini anapata UKIMWI? Kwa kutafuta majibu ya maswali haya tunaweza kupata sababu kadhaa za kisayansi zinazoelezea namna UKIMWI ulivyoanza na unavyoambukizwa.

Mtazamo wa kiyakinifu ni mtazamo ambao msanii na mhakiki huyatazama mabadiliko ya mambo katika jamii kisayansi. Hii inamaanisha kwamba mabadiliko katika jamii huendana na hali halisi iliyopo katika jamii. Mabadiliko hayo yanaweza kuthibitishwa kwa hoja, mifano na sababu dhahiri. Mfano mzuri ni tukio la njaa ambalo linaweza kuthibitishwa kiyakinifu kutokana na ukame, uvivu au ufujaji wa mazao.

3. Msimamo

Kamusi Kuu ya Kiswahili (BAKITA, 2017) inafasili neno "msimamo" kuwa ni hali ya mtu kutetea jambo fulani bila kutetereka. Kutokana na fasili hii, dhana ya msimamo inaweza kuelezwa kuwa ni mwegamo wa maoni ya mtu kuhusu jambo. Hii inamaanisha kuwa, dhana ya msimamo hudhihirika vizuri zaidi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 139 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kupitia kuwapo kwa uwili au uwingi wa maoni, mtazamo au uamuzi. Hali hiyo ya uwingi au uwili husababisha kuwapo kwa pande tofauti. Hivyo, msanii au mhakiki huonesha kuegemea katika upande mmojawapo wa maoni, mtazamo, suluhisho au uamuzi.

Mara nyingi, msimamo alio nao msanii kuhusu jambo analolisimamia huwa haubadiliki. Msimamo wa msanii ndio unaosababisha kazi yake itofautiane na za wasanii wengine. Kwa mfano katika fasihi ya Kiswahili, kuna baadhi ya washairi wanaoamini kuwa ushairi ni lazima ufuate kanuni ya urari wa vina na mizani. Huo ndio msimamo wao kuhusu ushairi, na huuonesha kwa hoja kabambe za utetezi. Kwa upande mwingine, baadhi ya washairi wanaamini kuwa siyo lazima ushairi utawaliwe na kanuni ya urari wa vina na mizani.

4. Itikadi

Itikadi ni mawazo na imani kuhusu miongozo na mahusiano ya watu katika jamii. Itikadi huongoza na kuhalalisha au kuhoji matendo na mahusiano ya watu kwa lengo la ama kuyadumisha au kuyabadilisha. Mivutano ya kijamii hujidhihirisha katika migongano ya kiitikadi; ambapo kila kundi au tabaka huibua itikadi yake ili kutetea na kulinda maslahi yake. Hivyo, itikadi huweza kupotosha ukweli ili kulinda maslahi ya kundi fulani ndani ya jamii. Itikadi huweza kuwekwa katika mikondo mitano ifuatayo:

(i) Itikadi ya Kijadi: Hii ni imani yenye huzingatia nguvu asilia, visasili, ushujaa, miiko na laana. Itikadi hii hufungamana zaidi na mfumo wa ujima.

(ii) Itikadi za Ki-marx: Itikadi hii hutambua kuwa jamii imegawanyika katika makundi ya kitabaka yenye kupambana. Hatimaye, tabaka la wazalishaji litaupindua mfumo wa kibepari na kuasisi jamii isiyo na matabaka. Dola itasimamia uzalishaji kwa faida ya jamii nzima.

(iii) Itikadi ya Kijamaa: Hapa kinachozingatiwa ni umuhimu wa kukuza nguvu za uzalishaji mali kwa ushirikiano. Pia, kutumia dola ili kujitegemea na kujenga jamii yenye usawa.

(iv) Itikadi ya Kibepari: Msingi mkuu wa itikadi hii ni umilikaji binafsi wa nyenzo za uzalishaji mali kama mashamba makubwa na viwanda, na kutumia fedha (mtaji) kujipatia faida. Katika itikadi hii, kila kitu kinachofaa kuwa bidhaa hufanywa kuwa bidhaa. Aidha, itikadi hii husisitiza maisha na maendeleo ya mtu mmoja mmoja badala ya jamii nzima.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 140

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Itikadi ya Kiliberali: Katika itikadi hii ambayo ndiyo inayotawala katika mfumo wa ubepari, mwanadamu huambiwa kuwa ana uhuru wa kujichagulia atakayo na kufanya uamuzi; na anaweza kujiendeleza kwa juhudi yake mwenyewe hadi mwisho wa uwezo wake.

Zipo pia itikadi za kidini na kimaadili ambazo hatutazizungumzia hapa.

5. Falsafa

Falsafa ni tafakuri au mawazo ya kina kuhusu maisha. Falsafa inatumiwa na mtu kama nguzo muhimu ya kuyatazama maisha au kuvitazama vitu katika mtazamo mpana zaidi. Falsafa ya mwandishi huweza kubadilika kulingana na mazingira na jinsi anavyopambana na maisha. Hata hivyo, wapo waandishi wengine ambao falsafa zao huwa hazibadiliki. Mfano wa waandishi ambao falsafa zao hazijapata kubadilika ni Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Falsafa ya Shaaban Robert ni kwamba wema hushinda ubaya. Aidha, falsafa hii huenda sanjari na falsafa yake kuhusu maadili. Shaaban Robert anahimiza watu wawe na mwenendo mwema ili uwafae katika maisha yao ya duniani na ya ahera. Euphrase Kezilahabi kwa upande wake, anaona maisha hayana maana nje ya kuusaka ukweli usiofikika.

Falsafa inahusiana sana na mtazamo pamoja na msimamo. Hii inamaanisha kwamba, kupitia namna mtu anavyoyaona au kuyachukulia mambo (mtazamo) na jinsi anavyoonesha kuyaegemea au kuyatetea (msimamo), ndivyo undani wa mawazo yake kuhusu maisha unavyojidhihirisha. Falsafa ya kazi ya fasihi inatakiwa ichambuliwe kwa kuzingatia jinsi kazi hiyo ilivyoutazama ulimwengu na kueleza ukweli juu ya mambo mbalimbali. Hata hivyo, kuna uwezekano wa jamii kuwa na itikadi zaidi ya moja.

6. Ujumbe

Umekwishajifunza katika sura ya kwanza kuwa ujumbe ni mafunzo yanayotokana na dhamira zinazopatikana katika kazi ya fasihi. Ujumbe unaweza kuwa wazi au ukajitokeza kwa kificho. Ujumbe mmojawapo katika riwaya ya *Kusadikika* (Shaaban Robert, 1951) ni kuwa juhudi ni ngazi ya mafanikio; yaani ukitaka mafanikio sharti uyatafute kwa kufanya kazi kwa bidii. Vilevile, katika tamthiliya ya *Kilio Chetu* (Medical Aid Foundation, 1995) jamii inapata ujumbe kuwa ukahaba ni adui wa afya na maendeleo.

7. Migogoro

Hii ni hali ya ukinzani au kutoelewana ama ndani ya nafsi ya mtu au kati ya mtu na mtu au kati ya kundi moja na kundi jingine la watu. Migogoro katika kazi ya fasihi hutokana na tofauti za kimawazo na kimaisha baina ya wahusika au ndani

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 141 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya mhusika binafsi. Migogoro inaweza kuegemezwa katika siasa, utamaduni, uchumi na jamii.

Mara nyingi, migogoro ya kisiasa hutokana na kudai madaraka ambapo upande mmoja, mathalani wa watawaliwa, huona kuwa hautendewi haki na watawala wao. Hivyo, huamua kupambana nao kwa njia yoyote ile. Migogoro hii hujidhihirisha katika kazi mbalimbali za fasihi kama vile *Vuta N'kuvute* (Shafi Adam Shafi, 1999) ambacho kina mgogoro kati ya watawaliwa (Waafrika) na watawala (Wazungu). Migogoro ya kiuchumi hutokana na namna mali inavyogawanywa miongoni mwa wazalishaji. Kama mgawanyo au umilikaji mali hautakuwa sawa miongoni mwa wazalishaji, mgogoro utatokea. Mfano mzuri wa mgogoro huu ni ule unaojitokeza katika riwaya ya *Usiku Utakapokwisha* (Mbunda Msokile, 1990). Migogoro ya kiutamaduni inahusu masuala ya mila na desturi za jamii inayohusika. Tamthiliya ya *Hatia* (Penina Mhando, 1972) inaonesha mgogoro wa aina hii hasa pale ambapo Sembuli anatakiwa kula kiapo cha kijadi ili kujua kama anahusika na ujauzito wa Cheja. Sembuli anakataa kuapa kwa kutumia imani za kijadi, jambo ambalo linaleta mzozo kati yake na ndugu wa Cheja. Migogoro ya kijamii huhusu matatizo na mahusiano ya kijamii. Mfano mwingine wa mgogoro wa kijamii ni ule wa Herbert na Martha katika tamthiliya ya *Kwenye Ukingo wa Thim* (Ebrahim Hussein, 1988), ambapo Herbert na Martha wanakataliwa kuoana kwa sababu ya tofauti za makabila. Mgogoro wa nafsi hutokea pale mhusika mwenyewe anaposhindwa kukabiliana na hali halisi kutokana na matatizo binafsi aliyonayo. Katika riwaya ya *Kufikirika* (Shaaban Robert, 1967), kuna mgogoro wa nafsi wa Mfalme baada ya kukosa mtoto na katika *Mhanga Nafsi Yangu* (Said Ahmed Mohamed, 2012) mhusika mkuu, Afida, anakabiliwa na mgogoro wa utambulisho baada ya kuhamia Ulaya na kuolewa na Mzungu, na kushindwa kuishi katika jamii yake mpya.

Katika kutathmini kipengele cha migogoro, ni lazima mhakiki azingatie usuluhishi wa migogoro. Usuluhishi wa migogoro unatakiwa uwe ni ule wa kutoa fundisho kwa jamii ili iwe na mwenendo mzuri. Suluhisho linatakiwa kuwa chanya na lenye kuwatia moyo wasomaji kuelekea kwenye mafanikio.

Kufaulu na kutofaulu kwa mwandishi wa kazi za kifasihi

Kufaulu na kutofaulu kwa mwandishi wa kazi za kifasihi ni tathmini ambayo huwa inafanywa na mhakiki. Katika kufanikisha kipengele hiki, mhakiki anatakiwa atathmini vipengele vyote vya fani na maudhui. Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi vimeoneshwa kwa muhtasari katika kielelezo kifuatacho:

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 142 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo Namba 4.1 Vipengele vya uhakiki

Zoezi la 1

(i) "Uhakiki wa kazi za fasihi ni jambo lisilo na maana." Jadili dai hili.
(ii) Ni kwa namna gani vipengele vya fani na maudhui hujengana katika kuhakiki kazi za fasihi?
(iii) Kwa kutumia kazi mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili, jadili kudhihirika kwa dhana ya mtindo.
(iv) Fafanua matumizi ya lugha katika kazi mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili.

Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi
Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi huzingatia vipengele vya *fani* na *maudhui*.

Uhakiki wa fani katika kazi za fasihi simulizi
Sehemu hii inafafanua namna ya kuhakiki tanzu nne za fasihi simulizi na vipera vyake. Tanzu hizo ni *ushairi, hadithi, semi* na *sanaa za maonesho*.

1. Uhakiki wa ushairi
Ushairi wa fasihi simulizi hujitokeza katika *nyimbo, tendi, tenzi, mashairi* na *ngonjera* mbalimbali, na huwa na sifa zinazofanana. Sifa hizo ni pamoja na mishororo, vina, mizani na kibwagizo. Uhakiki wake huzingatia vipengele vilevile vilivyogusiwa katika fasihi andishi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 143 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Matumizi ya lugha

Uhakiki wa matumizi ya lugha huzingatia vipengele vyote vya lugha ya kishairi vinavyotumika. Lugha hii huwa na semi, tamathali za semi, taswira na ishara. Tazama mfano katika sehemu ya wimbo ufuatao:

Penzi Haligawanyiki

Kila nikipita, wageuza shingo, utadhani feni, bwana ee bwana x2
Kila nikipita, macho yakutoka, utadhani balbu, bwana ee bwana… x2

(*Bendi ya Vijana Jazz*, Miaka ya 1990)

Katika wimbo huu, kuna taswira ya mwanamume anayegeukageuka kumwangalia mwanamke anayepita. Mwimbaji wa wimbo analinganisha shingo ya mwanamume na feni inayozunguka. Vilevile, macho ya mwanamume yanalinganishwa na balbu, kwa namna anavyomwangalia huyo mwanamke. Pia, kuna takriri ya virai "kila nikipita" na "bwana ee bwana ee."

(b) Wahusika

Uhakiki wa wahusika wa kazi za kishairi hujielekeza kwanza katika kuwabainisha wahusika wenyewe. Katika kazi za kishairi, kama vile nyimbo, wahusika huweza kuwa mmoja au kundi la watu. Tazama mfano wa wimbo ufuatao:

Howa Mwana

Howa mwana, nyamaa silie,
Ukilia waniliza mie,
Machoziyo weka nisifie,
Watu waje wakushikilie.

Howa mwana, nyamaa silie,
Usilie sinikumbukie,
Uyatima wazee wafie,
Cheka mwana vilio vishie.

Wahusika katika wimbo huu ni Mama na Mtoto wake.

(c) Muundo

Uhakiki wa muundo wa vipera vya ushairi kama vile nyimbo, mashairi na tenzi unahusisha idadi na mpangilio wa mishororo katika beti, mpangilio wa

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 144

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vina, mizani, beti na kibwagizo. Kwa mfano, baadhi ya nyimbo au mashairi huwa na beti zenye mistari 3, 4, 5 na kuendelea. Hivyo, kutokana na idadi ya mishororo, tunapata miundo tofautitofauti kama ilivyojadiliwa katika utungaji wa kazi za fasihi simulizi.

(d) Mtindo

Uhakiki wa mtindo huzingatia vipengele vya kimtindo kama vile takriri, mkarara na nafsi mbalimbali vilivyotumika katika ushairi. Pia, kwa baadhi ya vipera, kama vile nyimbo, hutazamwa urefu au ufupi wa mishororo yake. Vipengele vingine vya kuhakikiwa ni namna gani mbinu mbalimbali kama vile makofi, vigelegele na mshindo, yaani uchezeshaji wa mguu mmoja au miguu yote hujitokeza katika uwasilishaji, pamoja na athari zake.

(e) Mandhari

Kama ulivyokwishaelezwa, Mandhari ni mazingira au mahali na wakati ambapo visa na matukio katika kazi ya fasihi hufanyika. Mandhari inaweza kuwa halisi kama ilivyo katika hadithi ya "Kisa cha Shemakumbi" (angalia ukurasa 35-39) au isiwe halisi (ya kufikirika) kama ilivyo katika hadithi ya "Nyoka hana miguu" (angalia ukurasa wa 42). Mandhari huchorwa kisanaa kulingana na ujumbe au dhamira ya msanii. Ujengaji mzuri wa mandhari hufanya kazi ya fasihi kuwa nzuri na yenye thamani kubwa.

2. Uhakiki wa hadithi

Uhakiki wa hadithi pia huzingatia vipengele kadhaa muhimu vya kifani ambavyo tumejifunza pia katika tanzu nyingine, navyo ni muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari.

(a) Muundo

Muundo wa hadithi za fasihi simulizi umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni mwanzo wa hadithi, kiini cha hadithi na mwisho wa hadithi. Ifahamike kuwa matukio ya sehemu hizi zote tatu huwa yanasimuliwa moja kwa moja.

- Sehemu ya mwanzo wa hadithi huwa kuna mianzo maalumu kama inavyoonekana hapo chini:

Fanani		**Hadhira**
Paukwa	-	Pakawa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 145 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hadithi! Hadithi! - Hadithi njoo…
Palitokeani - Naam twaibu
Baada ya hapo, fanani huendelea kusimulia "Hapo zamani za kale…"

- Sehemu ya kiini ni mahali ambapo matukio ya hadithi yenyewe huelezwa moja kwa moja.
- Sehemu ya mwisho wa hadithi huhitimisha masimulizi, kusuluhisha migogoro, na kuonesha funzo lililokusudiwa. Baadhi ya hadithi huishia na methali au maneno maalumu kama vile "Hadithi yangu imeishia hapo"au "Wakaishi raha mustarehe."

(b) Mtindo

Uhakiki wa mtindo wa hadithi hufanywa kwa kutazama namna mtunzi alivyotumia tanzu na vipera mbalimbali kama vile nyimbo, methali na majigambo. Pia, mtindo wa hadithi hujibainisha kwa kutumia takriri na uwezo wa fanani katika kubuni mbinu mbalimbali za usimulizi. Vilevile, mtindo hujibainisha katika matumizi ya nafsi; nafsi ya kwanza huifanya hadhira kuwa sehemu ya hadithi. Hii ni tofauti na jinsi nafsi nyingine zinavyotumika.

(c) Wahusika

Kuhusu uhakiki wa kipengele cha wahusika, hadithi za fasihi simulizi huwa na wahusika wa aina tano. Wahusika hao ni fanani, hadhira, binadamu, wanyama, mizimu na mazimwi, vitu pamoja na mahali.

- Fanani husimulia hadithi kwa kufanya matendo mbalimbali kama vile kuanzisha nyimbo, kupiga makofi, kuigiza milio ya wanyama na kubadilisha mbinu za usimulizi.
- Hadhira ni wasikilizaji ambao hushiriki kwa kusikiliza na kufanya matendo yanayosimuliwa kama vile kushiriki katika uimbaji, kupiga makofi na vigelegele. Hata hivyo, fanani na hadhira ni wahusika ambao hawamo ndani ya hadithi, lakini huhakikiwa kwa kuwa vitendo vyao huathiri mwenendo wa hadithi.
- Binadamu ni wahusika waliomo ndani ya hadithi. Wahusika hawa huwakilisha tabia na mienendo ya binadamu halisi. Mara nyingi, wahusika hawa hupewa majina ya jumla kama vile mtu mmoja, mfalme na vijakazi.
- Wahusika wanyama waliomo kwenye hadithi hupewa uwezo wa kutenda matendo yanayotendwa na binadamu. Mfano wa wanyama

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 146 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hao ni simba, sungura, kobe, nyani, fisi na tembo. Wahusika hawa wamepewa sifa za kudumu kulingana na tabia zao.

- Vitu na mahali pia ni wahusika wa fasihi simulizi. Hii ni kwa sababu huweza kuhuishwa na kupewa urazini kama binadamu. Kwa msingi huo, vitu huweza kutenda matendo kama binadamu. Mazimwi, mizimu, majini na miungu pia hupewa uwezo mkubwa katika baadhi ya hadithi, na huweza kuwakilisha wema na uovu. Wahusika hao huingiliana na wanadamu kwa namna chanya au hasi kwa kufanikisha au kukwaza harakati zao kulingana na hadithi husika.

(d) Mandhari

Uhakiki wa kipengele cha mandhari huelekezwa katika kuchunguza jinsi mandhari yalivyobainishwa katika hadithi za fasihi simulizi na kuyahusisha na wahusika na matukio yaliyomo. Mara nyingi, wahusika wanyama huoneshwa katika mandhari ya porini, msituni au shambani huku wakihusishwa na matendo au visa na matukio mbalimbali.

3. Uhakiki wa Semi

Uhakiki wa semi unapaswa kuzingatia jinsi vipera hivi vilivyotumika katika kazi husika.

(a) Uhakiki wa nahau

Uhakiki wa nahau hufanyika kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

(i) Matumizi ya lugha

Kwa kawaida, nahau hutumia lugha ya kificho kinyume na jambo linalotolewa. Kwa mfano, nahau ya *amepata jiko* ina maana ya ameoa au amepata mke. Lugha ya kiishara imetumika kuhusisha jiko na mke. Mke ndiye hupika na kumhudumia mumewe. Mfano mwingine ni nahau ya *amevaa miwani* yenye maana ya amelewa. Ishara inayodokezwa hapa ni kuhusu kuwapo kwa matatizo. Hivyo, wote, mvaa miwani na mlevi wana matatizo. Mvaa miwani ana tatizo la kutoona na mlevi ana tatizo la akili linalotokana na kilevi. Anayevaa miwani hafanyi hivyo makusudi; hivyo, kutumia ishara ya *kuvaa miwani* kwa mlevi ni kupunguza ukali wa maneno na kumsitiri mlevi ambaye anakunywa pombe na kulewa kwa makusudi.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI F.5 NA 6 (KWANDANI).indd 147

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Wahusika

Aghalabu, wahusika wa nahau huwa binadamu ijapokuwa hawabainishwi waziwazi. Hivyo hatuta wajadili hapa.

(iii) Muundo

Nahau huwa na muundo wa kisarufi, yaani mpangilio wake hutegemea aina za maneno. Muundo wa nahau, aghalabu, huanza na kitenzi na kufuatiwa na nomino. Tazama mifano ifuatayo:

- *Kifungua mimba* - mtoto wa kwanza
- *Kula mlungula* - kupokea rushwa
- *Kupiga soga/domo* - kuongea bila kufanya kazi
- *Kupiga mbizi* - kuzama majini

(iv) Mtindo

Mtindo wa nahau hutegemea lugha iliyotumika. Kwa kawaida, lugha ya nahau ni ile iliyosheheni picha na ishara nyingi. Nahau moja hutumia maneno yenye ishara tofauti zinazowakilisha maana moja. Katika kupata maana, haitakiwi kuangalia maana za neno mojamoja. Kwa mfano, maneno yanayounda nahau ya *kuvaa miwani* yakitafsiriwa kwa kutenganishwa, hayawezi kumaanisha hali ya kulewa.

(v) Mandhari

Baadhi ya nahau hudokeza mandhari zilimoibuliwa. Kwa mfano, nahau ya *kukalia kuti kavu* inaonesha kuwa imeibuliwa katika jamii ya wakulima wa minazi, ambapo mtu hawezi kukalia kuti kavu na kuwa salama. Hata hivyo, nahau hii hutumika katika mazingira yoyote kutegemeana na muktadha.

(b) Uhakiki wa methali

Uhakiki wa methali huzingatia vipengele vifuatavyo:

(i) Matumizi ya lugha

Methali hutumia lugha ya kisanaa na tamathali nyingi za semi. Tazama mifano ifuatayo:

- *Sitiari*: Mtoto wa nyoka ni nyoka.
- *Tashihisi*: Mbaazi ukikosa maua husingizia jua.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

- *Tashibiha*: Jambo usilolijua, ni kama usiku wa giza.
- *Tabaini*: Kukopa harusi, kulipa matanga.
- *Kejeli*: Uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti.

Methali nyingine hazitumii tamathali za usemi. Mfano wa methali za namna hii ni *Ng'ombe akivunjika mguu, hurejea zizini* na *Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo.*

(ii) Wahusika

Baadhi ya methali zina wahusika. Hata hivyo, kama ilivyo kwa nahau, wahusika wa methali hawajibainishi wazi lakini wapo. Kwa mfano, wahusika wa methali isemayo *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu,* wamebainishwa kwa kutumia nafsi, yaani kiambishi 'a' katika neno asiyesikia. Hapa, '**a**' inawakilisha mtu ambaye ni nafsi ya tatu umoja. Hata hivyo, kwa muktadha huu, ni mtu yeyote ambaye hafuati ushauri wa manufaa anaopewa na mtu anayefahamu vizuri kuhusu kitu anachokielekeza. Mkuu inawakilisha mtu mwenye uelewa kuhusu jambo linalotolewa ushauri.

(iii) Muundo

Kimuundo, methali zina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaweza kueleza matokeo chanya na sehemu ya pili ikawa hasi au kinyume chake. Pia, sehemu ya kwanza inaweza kuwa hasi na sehemu ya pili kuwa hasi. Tazama mifano ifuatayo:

- Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.
- Haba na haba, hujaza kibaba.
- Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.
- Ng'ombe akivunjika mguu, hurejea zizini.

Mfano wa kwanza hapo juu unaonesha kuwa sehemu ya kwanza ni hasi na sehemu ya pili ni hasi. Hii ni kwa sababu mtu anashindwa kuzingatia mambo mazuri anayoambiwa, matokeo anapata hasara ambayo ni sehemu ya pili. Katika mfano wa pili, sehemu ya kwanza ni chanya, vivyo hivyo kwa sehemu ya pili. Ni bora kutunza kitu hata kama ni kidogo kwa sababu kinaweza kukupa faida kubwa baadaye. Katika mfano wa tatu, sehemu ya kwanza ni chanya, ilhali sehemu ya pili ni

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 149 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hasi. Katika mfano wa nne, sehemu ya kwanza ni hasi na sehemu ya pili ni chanya. Hii ni kwa sababu ng'ombe kuvunjika mguu ni ishara ya mtu kupata matatizo. Kurejea zizini ni ishara ya kwenda mahali salama ambapo mtu anaweza kupata huduma.

(iv) Mtindo

Methali hujengwa kwa mbinu mbalimbali za kisanaa ambazo hupaswa kuhakikiwa. Baadhi ya mbinu hizo ni:

- Matumizi ya takriri: kwa mfano, katika methali isemayo *mla ni mla leo, mla jana kala nini?* Au *Ndo ndo ndo si chururu, chururu si ndo ndo ndo.*
- Matumizi ya taswira: kwa mfano, *paka akiondoka, panya hutawala.*
- Matumizi ya ufinyanzo: kwa mfano, *mkataa pema, pabaya panamwita*, badala ya mtu anayekataa mahali pema, mahali pabaya panamwita.

(v) Mandhari

Mandhari ya methali ni mahali ilipoibuliwa au ilipoanzia. Hata hivyo, kimatumizi, mandhari hutegemea mahali watu wanapoitumia. Kwa mfano, mandhari ya methali isemayo *mgaagaa na upwa hali wali mkavu* ni ya Pwani au sehemu zenye shughuli za uvuvi. Hata hivyo, methali hii huweza kutumika mahali popote kwa lengo la kuhamasisha watu kujituma kufanya kazi ya kujipatia kipato.

(c) Uhakiki wa vitendawili

Vitendawili ni aina ya semi zilizo katika fumbo, na ambazo hutolewa kwa njia ya swali linalohitaji jibu. Hivyo, uwasilishaji hutegemea pande mbili za watu, yaani, msemaji na msikilizaji. Uhakiki wake huzingatia vipengele vifuatavyo:

(i) Matumizi ya Lugha

Vitendawili hutumia lugha ya mafumbo na yenye tamathali za semi. Kwa mfano:

- *Taashira*: Mimi mjinga, nyama ninaacha ninakunywa mchuzi tu (*muwa*).
- *Tabaini*: Teke teke huzaa gumu gumu na gumu gumu huzaa teke teke (*mbegu za nafaka*).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 150 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

- *Tashihisi:* Saa yetu kadri inavyotembea ndivyo inavyopungua nguvu (*moyo*).
- *Taswira*: Nyumba yangu haina mlango (*yai*).

(ii) Wahusika

Vitendawili huwa na wahusika ambao hujengwa kimafumbo ili kuonesha uhalisi. Wahusika, aghalabu, hujumuisha watu, wanyama na vitu. Tazama mifano ifuatayo:

- Kuku wangu katagia mibani (*nanasi*);
- Wanangu hufukuzana kila siku lakini hawakutani (*magurudumu ya gari/ baiskeli).*

Katika mfano wa kwanza, wahusika ni *kuku* na *nanasi;* na katika mfano wa pili wahusika ni *wanangu* na *magurudumu ya gari au baiskeli.*

(iii) Muundo

Muundo wa vitendawili huwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza huwa ni swali na ya pili ni jibu. Katika sehemu ya kwanza, kunakuwa na mtegaji wa kitendawili ambaye huanza kwa kusema: "kitendawili…" na mteguzi hujibu "tega." Baada ya hapo, kitendawili hutegwa na kisha jibu lake hutolewa. Mteguzi akishindwa kutoa jibu sahihi, mtegaji huwa anadai kupewa kitu anachopenda kutegemeana na mazingira. Kitu hicho kinaweza kuwa mji, gari, nyumba, ng'ombe au shamba; akipewa anachokipenda, hutoa jibu sahihi.

(iv) Mtindo

Kuhusu kipengele cha mtindo, uhakiki unapaswa kuchunguza na kubainisha matumizi ya nafsi. Vitendawili huwa na matumizi ya nafsi mbalimbali kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

- Nimemfukuza sikumkamata (*kivuli*).
- Anachora bila kutumia akili (*konokono*).

Mfano wa kwanza umetumia nafsi ya kwanza umoja; na wa pili umetumia nafsi ya tatu umoja.

(v) Mandhari

Mandhari hujengwa katika hali ya fumbo; hujibainisha zaidi kupitia jibu la fumbo. Mfano mzuri ni kitendawili kinachosema "Kila nikienda safari haiishi" (njia). Katika sehemu ya swali, kuna mandhari ya safari,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 151 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yaani mtu yupo safarini. Pia, sehemu ya jibu lake inahusisha mandhari kupitia dhana ya njia. Majibu ya vitendawili, aghalabu, huathiriwa na mazingira. Kwa mfano, kitendawili "nyumba yangu nzuri lakini ina nguzo moja," kinaweza kuwa na majibu mawili tofauti. Majibu hayo ni "uyoga"na "mwamvuli." *Uyoga* ni jibu linaloweza kutolewa na watu wa jamii ambamo uyoga hupatikana, ilhali mwamvuli ni jibu linaloweza kutolewa na watu wanaoufahamu mwamvuli. Aidha, vitendawili huundwa kulingana na mazingira. Tazama mifano ifuatayo:

- Gololi mbili zinakwenda mbio (*macho*).
- Popoo mbili zavuka mto (*macho*).

Mfano wa kwanza unaonesha kitendawili kilichotungwa katika mazingira ambayo gololi zinapatikana au zinafahamika; na mfano wa pili unaakisi mahali linapopatikana tunda la popoo. Zamani katika jamii nyingi za Kiafrika, vitendawili vilitegwa usiku, tofauti na sasa ambapo vitendawili vinategwa mchana, hasa shuleni.

4. Uhakiki wa sanaa za maonesho

Imedokezwa katika sehemu zilizotangulia kuwa utanzu wa sanaa za maonesho una vipera vya kiutendaji. Vipera hivyo ni majigambo, miviga, vichekesho, ngoma, tambiko na michezo ya watoto. Kama zilivyo tanzu nyingine, uhakiki wa utanzu huu pia hufanywa kwa kuzingatia vipengele muhimu vya muundo, mtindo, wahusika, matumizi ya lugha na mandhari.

(a) Muundo

Uhakiki wa muundo katika sanaa za maonesho hutazama mfululizo wa uwasilishaji wa tukio linalohusika. Uwasilishaji wa matukio ya vipera vya sanaa za maonesho, aghalabu, huwa ni wa moja kwa moja. Kwa mfano, katika majigambo, mjigambi huanza kwa kujitambulisha (huu ni mwanzo wa tukio), kisha anaeleza tukio (hiki ni kiini cha tukio), hatimaye anamaliza na jinsi alivyoshinda (huu ni mwisho wa tukio). Hali ni hiyo hiyo kwa matambiko, ambapo watambikaji huanza kwa kupiga hodi, kiongozi hueleza lengo la tambiko (utangulizi), shughuli za utambikaji hufanyika, ambapo maombi na utoaji wa sadaka hufanyika (kiini) na, hatimaye, tukio la kuaga miungu na kutawanyika hufanyika (mwisho).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 152

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Mtindo

Kama ulivyosoma katika sura za nyuma, mtindo ni upekee katika utunzi au uandishi wa kazi ya fasihi. Vipengele vinavyochunguzwa katika mtindo ni uteuzi wa maneno na mbinu za usimulizi. Mbinu hizi huweza kuzingatia matumizi ya monolojia, dialojia, nyimbo na nafsi.

Kadhalika, kuna matumizi ya tanzu na vipera tofauti. Mathalani, kipera cha majigambo huambatana na nyimbo, vigelegele na ngoma. Vilevile, kuna matumizi ya nafsi, hususani nafsi ya kwanza umoja. Katika miviga, mara nyingi, nafsi ya tatu wingi na nafsi ya kwanza wingi ndizo zinazotumika zaidi. Hivyo, uhakiki wa mtindo katika sanaa za maonesho unapaswa kuvitazama vipengele hivi.

(c) Wahusika

Uhakiki wa wahusika wa vipera vya sanaa za maonesho huzingatia kuwa utanzu huu una wahusika ambao ndio watendaji. Wahusika hao ni wale waliomo kwenye mchezo (vichekesho) na huwa ni watu maalumu. Kwa mfano, wahusika kwenye miviga ni wazee wanaotenda matendo mbalimbali ya kuwapa vijana hadhi kutoka katika kundi la watoto kwenda kundi la watu wazima. Vijana wanahusika kwa kuangalia matendo na kusikiliza nyimbo na vyote vinavyofanyika ili wajifunze, hatimaye watekeleze. Vilevile, utanzu huu hujumuisha wahusika wasiokuwa binadamu, hususani kwenye kipera cha matambiko. Matambiko huwa na wahusika kama vile Mungu, mizimu na mapepo. Wahusika hawa dhahania ndio walengwa wakuu wa matambiko, yaani watambikaji wamejenga imani yao kwao. Watambikaji huamini kuwa shida zao zitatatuliwa na wahusika hao. Kipera cha majigambo huwa na wahusika wa aina tatu nao ni wajigambi, washiriki wa ngoma ya kujigamba na mpokeaji wa majigambo. Kama ni tukio la kupongeza mashujaa, mpokeaji anakuwa ni kiongozi wa jamii (kama vile machifu na watemi), tofauti na kwenye tukio la harusi ambapo mpokeaji anakuwa baba au mwakilishi wa baba wa bwana harusi.

(d) Matumizi ya lugha

Uhakiki wa matumizi ya lugha katika sanaa za maonesho hauna tofauti kubwa na uhakiki wa ushairi. Hii ni kwa sababu baadhi ya vipera vya utanzu wa sanaa za maonesho ambavyo ni majigambo, miviga, vichekesho,

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ngomezi, tambiko na michezo ya watoto hufanana na vile vya ushairi kwa kiasi kikubwa; hivyo, hata matumizi ya lugha yanafanana. Kwa msingi huo, lugha inayotumika kwenye sanaa za maonyesho kwa kiasi kikubwa ni ya kishairi. Lugha hii huwa na misemo kama vile methali, nahau na tamathali za semi.

(e) Mandhari

Mandhari ni sehemu au mazingira ambapo matukio yanatendeka katika kipengele chochote cha sanaa za maonesho. Wasanii huweza kutenda wakitumia mandhari halisi au ya kubuni, mbinguni au duniani, kutegemeana na kisa husika. Inaweza kuwa nyimbo, majigambo, vichekesho nk.

5. Uhakiki wa maudhui katika kazi za fasihi simulizi

Uhakiki wa maudhui unahusu uchambuzi wa mawazo yaliyomo katika kazi inayohusika na malengo ya kazi hiyo kwa jamii inayohusika. Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayojitokeza katika kazi za fasihi. Mawazo hayo hujumuisha vipengele vya dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa, kufanikiwa na kutokufanikiwa kwa mwandishi.

(a) Dhamira

Katika kuhakiki dhamira, ni vema kuchunguza mawazo au wazo lililomo katika kazi inayohusika. Mawazo yanayotolewa huweza kutofautiana kati ya jamii moja na nyingine au kipindi cha wakati mmoja na mwingine. Katika maigizo, dhamira huweza kuwa zaidi ya moja. Kwa mfano, igizo linaweza kuwa na dhamira za uchoyo na uvivu.

(b) Mtazamo

Mtazamo ni muono wa mtunzi kuhusu msuala anayoyajadili katika kazi yake, na namna anavyoiona jamii yake na migogoro yake. Mbali na msimamo wa msanii, mhakiki vilevile anatakiwa awe na mtazamo kuhusu masuala yanayojadiliwa na namna yanavyowasilishwa.

(c) Msimamo

Umekwishajifunza maana ya msimamo katika sura zilizotangulia. Mhakiki wa kazi za fasihi simulizi anatakiwa kubainisha mkito wa tafakuri kuhusu maisha unaowasilishwa katika kazi inayohusika. Pia awe na kitu dhahiri anachokiamini na anachoweza kukitetea.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBUERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 154 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Itikadi

Itikadi ni mawazo na imani kuhusu miongozo na mahusiano ya watu katika jamii. Itikadi huongoza na kuhalalisha au kuhoji matendo na mahusiano hayo kwa lengo la ama kuyadumisha au kuyabadilisha. Mivutano ya kijamii hujidhihirisha katika migongano ya kiitikadi, ambapo kila kundi au tabaka huibua itikadi yake ili kutetea na kulinda maslahi yake. Hivyo, itikadi huweza kupotosha ukweli ili kulinda maslahi ya kundi fulani ndani ya jamii. Itikadi huweza kuwekwa katika mikondo mitano kama ilivyojitokeza katika sura zilizotangulia.

(e) Ujumbe

Ujumbe ni taarifa au somo analolipata mtu kuhusu jambo fulani. Katika muktadha wa fasihi, ujumbe ni taarifa ambayo imo ndani ya dhamira na ina lengo la kuleta mabadiliko kwa jamii. Ujumbe ni mafunzo na maadili ambayo huwa yamekusudiwa kwa mtu au jamii inayohusika. Ujumbe huwa na dhima ya kubadili tabia au mwenendo fulani usioendana na maadili ya jamii inayohusika. Kwa mfano, matumizi ya nahau ya *kufa na kupona* yanalenga kutoa ujumbe wa kujituma ili kufanikisha malengo. Ujumbe huu unaweza ukamhusu mtu yeyote, yaani mtoto, kijana na hata mzee. Hivyo, katika kuhakiki kazi za fasihi simulizi ni vema kujiuliza maswali haya: Je, ujumbe uliotolewa unamhusu nani? Je, ujumbe huo una umuhimu gani? Je, ujumbe huo unasadifu mazingira gani?

(f) Migogoro

Migogoro ni ukinzani au kutokuelewana baina ya pande mbili zenye mawazo au maslahi fulani. Migogoro inaweza kuwa ya jamii na jamii, mtu na mtu au mtu na nafsi yake. Katika kazi za fasihi simulizi, migogoro hujitokeza katika tanzu zote. Wahusika hujengwa kwa migogoro ambayo ina lengo la kutoa mafunzo kwa jamii. Katika hadithi, kwa mfano, mara nyingi, mhusika sungura hujengwa kwa migogoro, hasa kutokana na tabia yake ya ujanja. Katika kuhakiki migogoro, ni vema kujiuliza maswali haya: Je, mgogoro uliojitokeza ni kati ya nani na nani? Chanzo cha mgogoro huo ni nini? Je, kuna suluhisho lililofikiwa? Je, suluhisho la mgogoro huo linakidhi? Linatoa funzo gani?

(g) Falsafa

Umekwishajifunza maana ya falsafa katika sura zilizotangulia. Mhakiki wa kazi za fasihi simulizi anatakiwa kubainisha mwelekeo wa tafakuri kuhusu maisha unaowasilishwa katika kazi inayohusika. Mfano wa mielekeo hiyo ni

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maadili au imani kuhusu maisha. Kwa mfano, methali inayosema *Mtaka yote kwa pupa hukosa yote,* ina falsafa ya kupinga choyo na tamaa iliyokithiri.

Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mtunzi wa kazi ya fasihi simulizi

Uhakiki wa kazi za fasihi hukamilika kwa kupima ubora na udhaifu wake. Upimaji huo una lengo la kuangalia ubora na udhaifu wa mambo yaliyosemwa na jinsi yalivyosemwa. Hivyo, mhakiki hujiuliza maswali yenye lengo la kuona uhalisi wa kazi iliyowasilishwa. Miongoni mwa maswali hayo ni: Je, kazi iliyowasilishwa inaendana na uhalisi wa jamii? Je, kazi hiyo ina ujumbe gani? Je, kazi hiyo inatoa suluhisho sahihi? Kufanikiwa kwa maudhui ya kazi za fasihi simulizi kunategemea muktadha wa matumizi ya kazi hiyo.

Kwa upande wa fani, ni vema kuangalia jinsi kazi inayohusika inavyowasilishwa. Mhakiki huchunguza vipengele vya lugha, mtindo, muundo, wahusika na mandhari kama vinatimiza malengo ya kazi hiyo na kuonesha uhalisi wa jamii. Fani huchunguzwa kwa kujiuliza maswali kama ifuatavyo: Je, semi zinazotolewa zina mvuto na zinaifanya kazi ya fasihi ikubalike? Je, semi hizo zinaifanya kazi hiyo iwafikie walengwa na inatimiza malengo ya kazi hiyo na kutimiza lengo lililokusudiwa? Kwa mfano, kufanikiwa katika ujumbe katika methali inayosema *Harakaharaka, haina baraka* kunategemea tukio na muktadha unaohusika. Mgonjwa anapoumwa, akacheleweshwa kupelekwa hospitali kwa kujikita katika methali hii, ni dhahiri mtumiaji wa methali atakuwa hajafanikiwa. Ikiwa anajenga nyumba, akajenga taratibu ili nyumba iwe imara, mtumiaji atakuwa amefanikiwa kuitumia methali hiyo inavyotakiwa.

Kusikiliza na kutazama kazi za fasihi simulizi

Kusikiliza kazi za fasihi simulizi kuna manufaa kwa mwanajamii yeyote; humwezesha mtu kupata maarifa mbalimbali ya maisha na kujifunza tamaduni za jamii nyingine. Kwa mfano, nyimbo za makabila mbalimbali zinafundisha utamaduni na namna ya kuishi maisha yanayokubalika katika jamii inayohusika. Vilevile, usikilizaji wa kazi za fasihi simulizi humsaidia mtu kubainisha miundo na mitindo mbalimbali ya lugha, na hivyo, kuwa mjuzi katika lugha inayohusika. Kusikiliza kazi za fasihi simulizi kunamwezesha mtu kujua mbinu mbalimbali za utunzi wa kazi za fasihi simulizi. Kimsingi, usikilizaji wa kazi za fasihi una umuhimu katika kuelimisha na kuburudisha. Msikilizaji hujengeka katika maadili ya jamii yake. Pia, hujifunza matatizo ya jamii yake na jinsi ya kukabiliana nayo. Katika kusikiliza, ni vizuri kuhakiki vipengele vya fani na maudhui katika kazi inayohusika. Baada ya kusikiliza, ni vizuri kupima ubora na udhaifu wa vipengele hivyo.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 156 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 2

(i) Chagua wimbo wa aina yoyote ya muziki wa Kiswahili; kisha hakiki vipengele vyake vya fani na maudhui.

(ii) Chunguza wimbo ufuatao, kisha hakiki vipengele vya fani na maudhui.

Ninachokipata

Kiitikio
Ninachokipata nagawana na wenzangu,
Masikini zaidi yangu,
Wenye dhiki kama mimi,
Walopoteza wazazi wao kwa ugonjwa wa UKIMWI,
Wale wenzangu na mimi wasojiweza kitandani,
Yaani wa leo wa kesho dua ninawaombea.

Moyo wangu wa mbigili, kila mtu wamchoma,
Awe na fedha kama sumu, awe fukara kama mimi,
Awe tajiri kama Lemaco, awe masikini kama yeye,
Lazima takuchoma.

Kilio changu mimi kwa niaba ya masikini,
Waliopoteza mama zao, kwa ugonjwa wa UKIMWI,
Waliopoteza baba zao, kwa ugonjwa wa UKIMWI,
Mayatima wote wapenda maendeleo kama Q-Chillah,
Kama baba Msofe na wengine.

Duniani duniani, tumekuja kutembea,
Ninachokipata mimi sitakula peke yangu,
Nitagawana na wenzangu hata kama ni kidogo,
Kwani kinanitosha mimi siko peke yangu,
Kwa niaba ya mayatima wote,
Duniani tunaimba wote si ndio?

(Wimbo wa "Ninachokipata" ulioimbwa na Abubakar Katwila (maarufu kama Q-Chillah, 2003)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 157 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uhakiki wa kazi za fasihi andishi

Baada ya kujifunza kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi simulizi, katika sehemu hii utajifunza misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi.

1. Uhakiki wa ushairi

Umekwishajifunza nadharia ya uhakiki wa fasihi, ambapo umejifunza misingi mikuu miwili ya uhakiki ambayo ni fani na maudhui. Aidha, umeona misingi hiyo inavyotegemeana na kukamilishana. Kupitia shairi lifuatalo, utajifunza jinsi ya kuhakiki shairi:

Mti unaocheza

(1) KUULIZA ni thawabu, wanenaji wamenena,
Jambo likikupa tabu, usilinyamaze sana,
Uliza wenye vitabu, na wajuao maana,
Ni nani anayeona, mti kucheza tarabu?

(2) Mti uchezao ngoma, nimepata kuuona,
Umefungwa mahazama, kama kwamba msichana,
Achezaye lele mama, kasoro kichwa hapana,
Ndivyo nilivyoona, nilipokwenda tazama.

(3) Kazi yake mwanadamu, kujua vitu majina,
Kuungama si haramu, maarifa hayo sina,
Ndipo nilipoazimu, kuuliza hadhirina,
Ili niambiwe jina, ambalo silifahamu.

(4) Mti unapewa maji, ingawa kinywa hauna,
Tena ni mtafunaji, wa vitu vigumu sana,
Nataka watambuaji, wanifunulie jina,
Linanisumbua sana, kutafuta kila mji.

(5) Huwa moja hata tatu, pembe za kuviringana,
Wanazitumia watu, kugonga kwa nguvu sana,
Nazo hulia tu! tu! tu!, pasipo kusikizana,
Hulishwa na wasichana, tena vitu vigumu tu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(6) Wala si mti mdogo, huo ninaousema,
Una kivimbo cha gogo, wala haukuachana,
Ukipewa ni mzigo, wa kutoa jasho sana,
Utajeni waungwana, katika nchi ya Digo.

(7) Nilifika hadi Bara, ambako wapatikana,
Watu walio busara, ya miti kila namna,
Nikatoa na ujira, ili niambiwe jina,
Walakini sikuona, pato ila ni hasara.

Shabaan Robert, *Koja la Lugha, (OUP* 1969: 8)

Vipengele vya fani

(a) Muundo

Muundo wa shairi hili ni tarbia kwa sababu kila ubeti una mishororo minne. Vina vya kati ni **bu**, **ma**, **mu**, **ji**, **tu**, **go** na **ra**.Vina vya mwisho ni **na**. Shairi limeundwa na mizani kumi na sita katika kila mshororo; yaani, kipande cha ukwapi kina mizani nane, na kile cha utao kina mizani nane pia.

(b) Mtindo

Mtindo wa shairi hili ni wa nafsi zote tatu. Matumizi ya nafsi ya kwanza ndiyo yaliyotamalaki. Nafsi hii imejitokeza katika beti mbalimbali kupitia maneno kama vile *nimepata* na *nilivyoona* (ubeti wa pili). Nafsi ya pili imejitokeza kupitia maneno au vifungu vya maneno kadhaa. Baadhi ya mifano yake ni *usilinyamaze* (ubeti wa kwanza), *ukipewa* ni *mzigo* na *utajeni waungwana* (ubeti wa sita). Pia, nafsi ya tatu imejitokeza kupitia maneno au vifungu mbalimbali vya maneno. Baadhi ya mifano yake ni *wamenena* (ubeti wa kwanza), *wanifunulie* jina (ubeti wa nne). Vilevile, kuna mtindo wa fumbo au kitendawili. Kupitia mtindo huu, mwandishi anawauliza wasomaji wake na kuwataka wamfunulie fumbo lake kwa kumpa jibu kuhusu *mti unaocheza ni mti gani?*

(c) Matumizi ya Lugha

Lugha iliyotumika ni nyepesi, wazi na inayoeleweka kwa urahisi kwa wasomaji wa viwango vyote vya elimu. Aidha, kuna matumizi ya lugha ya mkato kama ilivyojitokeza katika maneno *usilinyamaze* (usilinyamazie) na *nilipoazimu* (nilipoazimia). Zaidi, kuna matumizi ya lugha ya picha kama yalivyojitokeza katika maneno *una kivimbo cha gogo* (ubeti wa sita). Vilevile, mwandishi ametumia tanakali sauti ya *tu! tu! tu!* (ubeti wa tano).

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 159 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Wahusika

Wahusika waliotumika katika shairi hili ni wanenaji, wenye kujua au wenye vitabu, wenye busara, na wasichana. Wahusika hawa wote wanavaa uhusika unaosaidia kujenga masumbuko ya mhusika au mwandishi katika kusaka jibu la kitendawili chake.

Vipengele vya maudhui

Dhamira

Shairi hili ni la aina ya "Tambo." "Tambo" ni shairi lenye fumbo linalohitaji kufumbuliwa. Je, unafikiri jibu la fumbo hili ni nini?

Kutokana na jibu hilo unaweza kupata dhamira ya shairi.

Zoezi la 3

Hakiki fani iliyotumika kuumba shairi lifuatalo:

Bado

Bado, mnatunyonya, twavumiliya uchungu,
Bado, mwatunyang'anya, kisingizia Mzungu,
Bado, mnajifanya, eti mwancha Mungu!

Bado, ninazunguka, kila afisi mefika,
Bado, na sijachoka, ijapo minne miaka,
Bado, nasononeka, nguo viraka naweka.

Bado, sinayo kazi, ijapo nimehitimu,
Bado, yangu mavazi, ndio mizani muhimu,
Bado, yasema mwizi, jambazi lililohitimu.

Bado, ningelinaja, katika hii afisi,
Bado, ninayo haja, nataka kumuona bosi,
Bado, saga nangoja, nipate hiyo nafasi.

Bado, nina karani, macho ya mheshimiwa,
Bado, yuko kazini, angali anikaguwa,
Bado, ashika karu, ondoka watusumbuwa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 160 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bado, ninasimama, naunda yangu plani,
Bado, kimwana mafia, chanitazama ja nyani,
Bado, kinatahuma, najua shule ni nini?

Bado, wageni waja, Wazungu, Wahindi hawa,
Bado, waingia ndani, pasipokuzuiliwa,
Bado ni *waniwani*, na hongo bosi kupewa.

Bado, twasisitiza, mvae tai na suti,
Bado, tunawajuza, twataka watanashati,
Bado, tunakataza, kujua pasi ripoti.

Bado, hujafahamu, vyetivyo hatuvitaki,
Bado, ewe sanamu, kutusumbua huchoki,
Bado, u mahamuma, na hapa hatuwataki.

Bado, haujakamwa, ngoja askari waja,
Bado, haujazimwa, *spidi* hizo za lugha,
Bado, haujapimwa, mifupa ya kila moja.

Bado, haujaisoma, na hapa tuna walimu,
Bado, una ukoma, na dawa ziko muhimu,
Bado, hufanyi hima, ukaondoka hasimu?

Bado, hujaelewa, afisi hii si yako?
Bado, wajizuzuwa, twataka taabu zako,
Bado, hujaambiwa, ya kwamba kazi haiko?

Bado, haujakisoma, kibao kilicho wazi,
Bado, kipo chasema, RUDI HAKUNA KAZI,
Bado, haujanikoma, na hiyo yako kutuzi.

Bado, haujakubali, mwito wa raisi wetu,
Bado, na serikali, yataka zaraa yetu,
Bado, wataka mali, kwa kuwaibia wali.

Bado, ninakuonya, sirudi hapa kitwana,
Bado, wajidanganya, *bosie* utamuona,
Bado haujamanya, *bosie* si yako nana?

Kineene wa Mutiso katika *Mulika* 27 (2006:36-39)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 161 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Uhakiki wa hadithi fupi

Uhakiki wa hadithi fupi hautofautiani na wa tanzu nyingine za fasihi andishi kwa kuwa misingi ya uhakiki imekwishaelezwa. Sehemu hii inaeleza namna ya kuhakiki hadithi fupi. Hadithi fupi ya Euphrase Kezilahabi iitwayo "Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani" katika *Misingi ya Hadithi Fupi* (Mbunda Msokile , 1992) itatumika kama mfano.

Vipengele vya fani

(a) Muundo

Muundo wa hadithi hii fupi ni wa moja kwa moja. Hadithi fupi inaanza kueleza operesheni maalum ya kuondoa wazururaji kama vile makahaba, watu wenye ulemavu wa macho, wachawi, wauza baa na wauza karanga. Sehemu ya kati inaonesha utekelezaji wa operesheni hiyo chini ya uongozi wa Mkuu wa Polisi. Mwisho, hadithi fupi hii inatuonesha kushindwa kwa operesheni hii kutokana na mikakati mibovu. Hatimaye, Katibu Mkuu, Malyangu, anatafakari kuhusu haki za wanyonge walioitwa wazururaji.

(b) Mtindo

Mtindo wa hadithi fupi hii ni wa masimulizi. Nafsi ya tatu umoja na uwingi imetumika kwa kiasi kikubwa. Pia, mtunzi ametumia mtindo wa kutomelea wimbo katika hadithi fupi yake. Vilevile, ametumia mbinu ya ucheshi.

(c) Wahusika

Mhusika mkuu katika hadithi fupi hii ni Malyangu ambaye ni Katibu Mkuu. Wahusika wengine ni Mkuu wa Polisi. Vilevile, kuna kundi la wazururaji linaloundwa na walezi wa watoto, wafanyabiashara mbalimbali, walemavu, watu wasioona na wachawi.

(d) Matumizi ya lugha

Lugha iliyotumika ni ya kifasihi. Pia, ametumia kejeli kama vile "Wakajenga nyumba nzuri pale kijiji cha Mapinduzi kilipokuwa, wakapanda migomba mingi. Siku hizi magari mengi ya ST na SU yanafuatana kuelekea huko. Kisa? Vyeo!" (Kejeli kwa viongozi wanaomiminika kwa waganga wa jadi ili kufuata dawa za kulinda kazi na vyeo vyao). Pia, ametumia dhihaka. Mfano mmojawapo wa dhihaka ni "Wachawi wakazidi kupata sifa, wakaanza kuwa waganga, wakapata wateja wengi-wakatajirika." Dhihaka nyingine ni "maprofesa njia hawaioni, wenye ulemavu wa macho tumewashinda." Vilevile, mwandishi ametumia lugha nyepesi, yenye taswira, ya ucheshi, na yenye msamiati uliotoholewa.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 162 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Mandhari

Mandhari ya kijiografia ni jijini Dar es Salaam, hususani maeneo ya Oysterbay na kijiji cha Mapinduzi kilichopo Mbezi. Kuhusu mandhari ya kiwakati, hadithi fupi hii inazungumzia matukio ya miaka ya 1970 wakati uanzishwaji wa vijiji na vijiji vya ujamaa ulipokuwa umeshika kasi.

Vipengele vya maudhui

(a) Dhamira

Dhamira kuu inayojitokeza katika hadithi fupi hii ni uanzishwaji wa vijiji na vijiji vya ujamaa nchini Tanzania. Hadithi fupi hii ina matabaka makubwa mawili, tabaka la wenye nguvu na la wanyonge. *Tabaka la wenye nguvu* linaundwa na Katibu Mkuu (Malyangu), mawaziri na Mkuu wa Polisi. *Tabaka la wanyonge* linaundwa na makahaba, wauza nyama, wenye mahitaji maalumu, walezi wa watoto, wenye ulemavu wa macho, wachawi, wauza baa na wauza karanga. Hatimaye, tabaka la wanyonge linafanikiwa kulishinda tabaka la wenye nguvu, kwani wazo la kuwahamishia wanyonge hao kijijini lilishindwa kutokana na mikakati mibovu na utabaka.

(b) Ujumbe

Hadithi fupi hii inatupatia ujumbe kuwa ni vema viongozi wawe na mikakati imara wakati wa kuanzisha sera au programu za maendeleo. Aidha, tunapata ujumbe kuwa haki ya mtu, hata kama ni mnyonge, huwa haipotei, bali huweza kucheleweshwa.

(c) Mtazamo

Mwandishi ana mtazamo wa kiyakinifu kwa sababu ameyatazama matukio yaliyokuwa yanajiri wakati wa utunzi wa kazi husika na kuchambua changamoto zake kisayansi.

(d) Falsafa

Hadithi fupi hii inatupatia falsafa ya kuwa, wema daima huushinda ubaya. Kila mtu ana mchango katika maendeleo ya nchi, mradi apewe haki.

(e) Msimamo

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi. Hii ni kwa sababu ameonesha bayana haki za wanyonge, na jinsi wanavyoweza kuungana katika kutetea haki zao.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 163 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Mgogoro

Mgogoro unaojitokeza katika hadithi fupi hii ni wa kitabaka, kati ya tabaka la wenye nguvu na la wanyonge. Suluhisho la mgogoro huu ni ushindi wa tabaka la wanyonge dhidi ya mikakati mibovu ya viongozi.

Kufaulu na kutokufaulu kwa mwandishi kifani na kimaudhui

Mwandishi amefaulu kusawiri maudhui yanayoakisi hali halisi ya maisha ya jamii nyingi za Kiafrika. Pia, amefaulu kuonesha suluhisho sahihi la mgogoro mkuu ulioijenga hadithi fupi hii. Kwa upande wa fani, amefanikiwa kutumia mandhari halisi ya kijografia na ya kiwakati inayohusiana na kiini cha kazi yake. Pia, ametumia lugha nyepesi ya kueleweka na ya kisanii.

Kazi ya kufanya

Chagua moja kati ya hadithi fupi zifuatazo, kutoka katika kitabu cha Misingi ya Hadithi Fupi (Mh. Mbunda Msokile 1992) kisha hakiki dhamira na migogoro iliyomo:

(i) "Siri ya Bwenyenye " (Mugyabuso Mulokozi)

(ii) "Kijana Yule" (Mohamed S. Mohamed)

(iii) "Wasubiri Kifo" (Euphrase Kezilahabi)

(iv) "Kiumbe Mzito" (Mbunda Msokile)

3. Uhakiki wa riwaya

Uhakiki wa riwaya hautofautiani sana na wa tanzu nyingine za fasihi andishi ambazo ni ushairi, tamthiliya na hadithi fupi. Kwa vile misingi ya uhakiki imekwishaelezwa, sehemu hii inaeleza namna ya kuhakiki riwaya.

Kufikirika (Shaaban Robert, 1967) ni riwaya inayozungumzia nchi ya Kufikirika ambayo ilikuwa na watu waliokuwa wakiamini mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo zilijidhihirisha wazi kwa kupitia wahusika wake ambao ni *Mfalme, Malkia* na *Utu Busara* na ambazo kwa sasa hazikubaliki katika jamii. Mfano wa uchambuzi wa riwaya hii ni kama ifuatavyo:

Vipengele vya fani

(a) Muundo

Muundo wa riwaya hii ni wa moja kwa moja. Riwaya inaanza kwa kumwonesha Mfalme akiwa kwake bustanini na fikra alizonazo juu ya kutopata mrithi hadi anapotaka kuanza kutoa wazo lake kwa Waziri.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5&6 (KIWANDANI).indd 164 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Mtindo

Mtindo wa riwaya hii ni masimulizi yaliyo katika nafsi ya tatu umoja.

(c) Wahusika

Mhusika mkuu katika riwaya hii ni Mfalme. Wasifu wa ndani wa Mfalme ni usiri kwa mke wake, hajamshirikisha kuhusu tatizo la uzazi. Ana msongo wa mawazo. Wahusika wadogo ni Waziri na Malkia. Wengine ni Utubusara Ujinga hasara, Mtoto wa Mfalme, Mjinga, Mwerevu na waganga wa jadi.

(d) Matumizi ya lugha

Lugha iliyotumika ni ya kifasihi iliyojaa tamathali za semi na taswira. Tunapata tamathali ya semi kama vile tabaini. Kwa mfano, "…Magharibi jua lilitua, Mashariki mwezi ulitokeza." Vilevile, kuna taswira mbalimbali kama vile mlango wa fikra kwa maana ya kuonesha njia ya kutatua tatizo. Pia, kuna matumizi ya nahau kama vile "kuambaa nyayo elfu moja" (kufikiri kwa makini kabla ya kutenda).

(e) Mandhari

Mandhari ya riwaya hii ni bustanini, nyumbani kwa Mfalme wa Kufikirika. Mandhari haya yanaakisi hali zifuatazo: Mosi, mapumziko ambayo huambatana na mazungumzo ya hapa na pale. Pili, utajiri na uzuri wa nchi ya Kufikirika iliyojaa viumbe anuwai kama vile ndege.

Vipengele vya maudhui

(a) Dhamira

Dhamira kuu inayojitokeza katika riwaya hii ni uzazi. Tunauona upweke wa Mfalme kutokana na kutokuwa na mrithi. Hali hii inadhihirishwa na maneno yasemayo "Alitazama huku na huko akawa kama mahali pa jua hushikwa na mwezi au nyota juu ya mbingu, na mahali pa joto huja baridi, lakini nani atashika mahali pake akifariki!"

Baadhi ya dhamira ndogo ni masuala ya jinsia, ugumba, hasara au madhara ya ujinga na suala la utu. Mwanamke ameoneshwa kuwa ana nafasi ya kutekeleza majukumu makubwa katika jamii. Mwanamke ni mtendaji wa kazi mbalimbali. Kwa upande mwingine, Mfalme hakumshirikisha Malkia katika tatizo la uzazi, jambo ambalo siyo zuri. Uzazi ni suala la kifamilia; Mfalme alipaswa kumshirikisha Malkia ili kutatua tatizo lililokuwa likiwakabili kwa pamoja.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 165 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Ujumbe

Riwaya hii inatupa ujumbe kuwa tunapopatwa na matatizo tuwe na subira. Aidha, tutumie hekima katika kusaka utatuzi bila kuleta madhara.

(c) Mtazamo

Mwandishi ana mtazamo wa kijadi kwa kuamini kwamba tatizo la uzazi linalowakabili lingeweza kutatuliwa kwa kuwatumia waganga wa jadi.

(d) Falsafa

Mwandishi anaamini kwamba, ili kizazi kiendelezwe ni lazima awepo mrithi wa familia au ukoo. Hii inamaanisha kuwa maisha bila uzazi hayana maana.

(e) Msimamo

Mwandishi ana msimamo usiotetereka kuhusu thamani ya uzazi kwa mwanadamu.

(f) Mgogoro

Mgogoro wa riwaya hii ni wa kinafsi na wa kijamii wakati huo huo. Kinafsi, mfalme anakabiliwa na tatizo la kukosa mtoto ambaye atarithi ufalme atakapofariki. Mgogoro huu unatatuliwa na mtabiri Utubusara na Ujingahasara. Mgogoro wa kijamii unahusu mvutano kati ya maendeleo ya kisasa na ushirikina. Mgorogoro huu vilevile unatatuliwa na "mkulima mjinga" (Utubusara Ujingahasara) anayemshinda "mwerevu mjinga" - Mfanyabiashara katika mapambano ya kutumia Akili, na hivyo kutengua mila ya kuwatoa watu kafara wakati wa majanga.

Kufaulu na kutokufaulu kwa mwandishi kifani na kimaudhui

Mwandishi amefaulu kusawiri maudhui yanayoakisi hali halisi ya maisha ya jamii nyingi za Kiafrika. Hata hivyo, hajafaulu kuonesha suluhisho sahihi la mgogoro mkuu ulioijenga riwaya hii. Kwa upande wa fani, amefanikiwa kujenga wahusika kulingana na nafasi zao, lugha nyepesi ya kueleweka na ya kisanii.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 4

1. Chagua riwaya moja kati ya hizi zifuatazo, kisha hakiki vipengele vya kifani:
   - (i) *Janga Sugu la Wazawa* (Gabriel Ruhumbika)
   - (ii) *Hiba ya Wivu* (Zainabu Mwanga)
   - (iii) *Tata za Asumini* (Said Ahmed Mohamed)
   - (iv) *Kurwa na Doto* (Muhammad Saleh Farsy)
2. Chagua riwaya moja kati ya hizi zifuatazo, kisha hakiki vipengele vya kimaudhui:
   - (i) *Nagona* (Euphrase Kezilahabi)
   - (ii) *Mdunguaji* (Hussein Tuwa)
   - (iii) *Moto wa Mianzi* (Mugyabuso Mulokozi)
   - (iv) *Mirathi ya Hatari* (Claude Mung'ong'o)

4. Uhakiki wa tamthiliya

Katika sehemu hii, tamthiliya ya *Kinjekitile* (Ebrahim Hussein, 1969) itatumika kama mfano wa kuhakiki tamthiliya.

Tamthiliya ya *Kinjekitile* (Ebrahim Hussein, 1969) inazungumzia Vita vya Majimaji vilivyotokea miaka ya 1905-1907, ambapo mhusika Kinjekitile aliweza kuwashawishi watu kutumia maji aliyoyachanganya na dawa ili kujikinga na risasi za Wajerumani kwa imani kuwa watakapokuwa wanawashambulia risasi zitageuka kuwa maji. Mfano wa uchambuzi wa tamthiliya hii ni kama ifuatavyo:

Vipengele vya fani

(a) Muundo

Mwanzoni tunaona wananchi (Wamatumbi) wakitumikishwa na kuteseka katika mashamba ya Wajerumani. Kisha anatokea mganga (Kinjekitile) na kuwahamasisha watu kwa kutumia dawa ili waungane wapambane na kung'oa mkoloni. Wanafanya hivyo na kupambana lakini wanashindwa baada ya kugundua kuwa risasi za Wajerumani hazigeuki kuwa maji. Kinjekitile anakamatwa na kuteswa. Huu ni muundo wa moja kwa moja

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 167 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wenye mtiririko wa usababishana usiokuwa na urejeshi wala mchezo ndani ya mchezo.

(b) Mtindo

Mwandishi ametumia nafsi zote. Mfano wa matumizi ya nafsi ya kwanza ni *mimi, tujifundishe* na *nimedanganywa*. Matumizi ya nafsi ya pili ni *wewe, unaumwa* na *ulisema* na nafsi ya tatu ni *wamenidanganya* na *wanasema*. Aidha, kuna matumizi ya mbinu ya kuboji, mathalani, *Tukishinda vita tutakuwa watu wa Seyyid Said?* Vilevile, ametumia mtindo wa kishairi. Kwa mfano, *tuwe askari askari wetu wenyewe. Tukishakuwa na nguvu - nguvu zetu wenyewe...*

(c) Wahusika

Wahusika waliomo katika tamthiliya hii ni Kinjekitile, Bi. Kinjekitile, Bi Kitunda, Chausiku, Mnyapala, Askari, Mkichi, Wazee, Mngindo na Machela. Kinjekitile ni mhusika mkuu na kiongozi; anatoa majukumu kwa walio chini yake. Anaamini katika mizimu; ndiye alitoa dawa iliyotumika kama silaha na kinga dhidi ya risasi. Kitunda ni mhusika mdogo. Ni mtiifu, anapokea maelekezo kutoka kwa Kinjekitile.

(d) Matumizi ya lugha

Mwandishi ametumia lugha nyepesi na inayoeleweka. Aidha, ametumia tanakali lafudhi katika kuonesha asili ya wahusika. Maneno kama *tafazali* (tafadhali) na *kialabualabu* (kiarabuarabu) ni mifano michache ya tanakali lafudhi. Pia, msanii ametumia taswira ya kiishara katika kufikisha ujumbe wake. *Udongo mwekundu* ni taswira inayomaanisha watu weupe, wakoloni… wanasema *neno moja* kumaanisha kuwa na kitu kimoja (kushikamana). Taswira nyingine ni matumizi ya Seyyid Said ambaye anawakilisha ukoloni mamboleo. Pia, kuna matumizi ya takiriri kama vile, *askari askari wetu wenyewe* na *nguvu nguvu zetu wenyewe*. Takriri hizi zinasisitiza dhana ya "kujitegemea."

(e) Mandhari

Mandhari ya tamthiliya hii hayaoneshwi waziwazi, ila kutokana na mazungumzo na maudhui yenyewe, inaonekana kuwa mandhari yake ni maeneo ya Kusini mwa Tanzania ambako kulikuwa na Vita vya Majimaji. Pia, mandhari haya yanadokeza kuwa watu wako katika maandalizi ya vita yanayoashiriwa na maneno kama "silaha" na "bunduki."

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 168 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vipengele vya maudhui

(a) Dhamira

Dhamira tunayoipata katika tamthiliya hii ni mapambano dhidi ya ukoloni. Msanii anasema, kupitia kwa Kinjekitile: "*Tujifundishe njia za vita. Tujifundishe kutumia bunduki. Tujipange tuwe askari - askari wetu wenyewe. Tukishakuwa na nguvu - nguvu zetu wenyewe - ndio tupigane na udongo mwekundu.*"

(b) Ujumbe

Tamthiliya hii inatupa ujumbe kwamba umoja na mbinu bora ndiyo njia pekee ya kumshinda adui. Msanii anatumia dhana ya maji kama njia mojawapo ya kuwaunganisha watu ili waweze kupigana na mkoloni. Pia, anataka kuwaongoza katika mapambano na kuwafundisha mbinu bora za kupambana na adui ambaye ni mkoloni.

(c) Mtazamo

Kupitia kwa Kinjekitile, mwandishi ana mtazamo wa kisayansi kuwa maji (yaani imani) pekee hayawezi kuwa silaha na kinga dhidi ya risasi, bali inabidi maandalizi kamili ya vita yafanywe.

(d) Falsafa

Msanii anaamini kuwa katika maisha, umoja ni kitu muhimu sana katika kupata ushindi au kuleta maendeleo. Mafanikio hayawezi kupatikana bila kuchukua hatua sahihi. Kadhalika, neno likishazaliwa ni vigumu kulidhibiti; mtu huweza kuanzisha jambo zuri ambalo hatimaye huweza kumwangamiza mwenyewe.

(e) Msimamo

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi kwa sababu ana dhamira ya dhati ya kuikomboa jamii.

(f) Mgogoro

Katika tamthiliya hii, kuna migogoro mikubwa miwili: Wa kwanza ni mgogoro kati ya watawaliwa na wakoloni. Mgogoro huu unasababishwa na manyanyaso ya wakoloni dhidi ya watawaliwa. Mgogoro wa pili ni wa kinafsi ambao unampata Kinjekitile baada ya kugundua kuwa hata kama wakishinda vita, bado watakuwa chini ya ukoloni mamboleo. Suluhisho

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 169 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

la mgogoro kati ya wakoloni na watawaliwa ni watawaliwa kupigana na wakoloni.

Kufaulu na kutofaulu kwa mwandishi

Mwandishi amefanikiwa kuonesha dhamira ya ukombozi pamoja na dhamira ndogo zinazoendana na hali halisi ya maisha katika jamii. Kwa upande mwingine, njia ya kutumia imani kupambana huenda ilikuwa sahihi kwa wakati wake; lakini si njia sahihi katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia.

Mwandishi amefaulu katika vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha inayoeleweka na ya kisanii inayoendana na mandhari ya tamthiliya hii. Vilevile, ametumia mtindo wenye mbinu mbalimbali. Wahusika wamechorwa kulingana na nafasi zao. Kwa mfano, kiongozi anaonekana ana mamlaka, na anayeongozwa anatii.

Zoezi la 5

(i) "Kwa vile kila msanii na msomaji wa kazi za fasihi ni mhakiki, hakuna haja ya kuwa na mtu anayejiita mhakiki." Kubali au kanusha dai hili kwa hoja maridhawa.

(ii) Eleza tofauti baina ya mtindo na muundo katika kazi za fasihi.

(iii) Migogoro ndiyo roho inayoshikilia uhai wa kazi yoyote ya kifasihi. Huku ukitumia mifano kutoka katika riwaya au tamthiliya ya Kiswahili, jadili hoja hii.

(iv) Onesha uhusiano na tofauti ya dhana za mtazamo, msimamo na falsafa ya mwandishi?

(v) Chagua tamthiliya moja kati ya hizi zifuatazo, kisha hakiki vipengele vya kifani:

(a) *Nguzo Mama* (Penina Muhando)

(b) *Mkwava wa Uhehe* (Mugyabuso Mulokozi)

(c) *Nyerere na Safari ya Kanaani* (Emmanuel Mbogo)

(d) *Kivuli Kinaishi* (Said Ahmed Mohamed)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 170 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya Kufanya

1. Kusanya diwani tano za Kiswahili zilizochapishwa baada ya nchi za Tanganyika na Zanzibar kupata uhuru wao, kisha chunguza miundo na mitindo iliyotumika.
2. Kusanya hadithi fupi nne za Kiswahili, kisha chunguza jinsi zinavyosawiri dhamira ya ujenzi wa jamii mpya.
3. Kusanya tamthiliya tano za Kiswahili, kisha chunguza migogoro inayojitokeza pamoja na masuluhisho yake.
4. Kusanya riwaya tano za Kiswahili, kisha chunguza wasifu wa wahusika wakuu.

For Online Use Only

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tano
Usanifu wa maandishi

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kuhusu usanifu wa maandishi. Vipengele vya msingi vinahusu kutathmini aina ya matini pamoja na mbinu za kifani zilizotumika kuwasilishia maudhui.

Usanifu wa maandishi

Katika usanifu wa maandishi, thamani ya kazi ya fasihi huchunguzwa. Thamani ya kifasihi ni ubora ambao hadhira huuona na kuufaidi kutoka katika kazi ya fasihi. Ubora huo hutokana na namna mtunzi au msanii alivyoisanifu kazi yake. *Kwa hiyo, usanifu wa maandishi ni ufundi au ustadi wa kuandika kazi za fasihi kwa kuzingatia kanuni au taratibu zinazohusiana na matini yanayohusika.* Matini hayo yanaweza kuwa ushairi, hadithi fupi, tamthiliya au riwaya. Katika kutathmini usanifu wa maandishi, mambo yanayozingatiwa ni jinsi mwandishi alivyokidhi vipengele vya kisanaa na kimaudhui vya matini inayohusika. Vipengele hivi vikisukwa vizuri husaidia kujenga mvuto wa kazi inayohusika kwa hadhira.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kutathmini maandishi

Kuna mambo mbalimbali ya kuzingatia wakati wa kutathmini maandishi. Kabla ya kutathmini matini yoyote, mtathmini anapaswa kujiuliza maswali yafuatayo:

(a) Je, matini haya yana thamani ya kifasihi? Kama ipo, ni ipi?
(b) Je, maudhui ya matini haya yanahusu nini?
(c) Je, matini haya yametumia mtindo upi?
(d) Je, matini haya yametumia muundo upi?
(e) Je, matini haya ni ya utanzu upi?
(f) Je, matini haya yana wahusika? Ni wa aina gani?
(g) Je, matini haya yameandikwa kwa kuzingatia kanuni za utanzu unaohusika?
(h) Je, matini haya yana mandhari? Ni mandhari yapi au ya wapi?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Yafuatayo ni mambo ya msingi katika usanifu wa maandishi.

(a) Aina ya utanzu

Mtathmini wa usanifu wa maandishi anatakiwa kubainisha aina ya utanzu. Utanzu unaweza kuwa riwaya, ushairi, tamthiliya au hadithi fupi.

(b) Maudhui

Mtathmini anatakiwa kueleza wazo kuu la matini na ujumbe uliomo. Matini yanaweza kuhusu umaskini, siasa, dini au uongozi.

(c) Kanuni bora za uandishi

Mtathmini anapaswa kuangalia kama mwandishi amezingatia kanuni sahihi za uandishi au la. Kanuni hizo ni matumizi ya herufi kubwa na ndogo, alama za uandishi na matumizi ya namba kama yapo. Alama za uandishi huwa na maana na athari kubwa katika matini.

(d) Muundo wa matini

Kama ilivyofafanuliwa katika sura zilizotangulia, muundo huchunguzwa kulingana na umbo la utanzu husika. Muundo ni mpangilio wa mawazo na matukio yanayojitokeza katika mazingira fulani. Katika shairi, muundo hutegemea mjengo wa shairi. Muundo wa shairi huchunguzwa kwa kuzingatia idadi, mpangilio, na urefu wa mistari katika beti za shairi.

(e) Mtindo wa matini

Kama ilivyo katika muundo, mtathmini anatakiwa kuangalia mitindo iliyotumika katika matini zinazohusika. Mtindo ni upekee katika utunzi au uandishi wa kazi ya fasihi. Vipengele vinavyochunguzwa katika mtindo ni uteuzi wa maneno na mbinu za usimulizi. Mbinu hizi huweza kuzingatia matumizi ya monolojia, dialojia, nyimbo na matumizi ya nafsi. Katika ushairi, mtindo huchunguzwa kwa kuzingatia uzingativu wa kanuni za ushairi wa kimapokeo au ushairi wa kisasa. Kwa upande mwingine, matini yanaweza kufuata mtindo changamani.

(f) Matumizi ya lugha

Kipengele hiki kina uwanja mpana katika kupima ubora wa matini. Katika lugha, tunachunguza wepesi au ugumu wa lugha iliyotumika, matumizi ya tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa. Pia, kuna matumizi ya nahau, misemo na methali. Aidha, mtathmini achunguze matumizi ya picha, ishara, taswira, ujenzi wa taswira na matumizi ya ucheshi. Fauka ya haya, mtathmini anapaswa kuchunguza usanifu wa lugha, rejesta, uchangamani

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 173
17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa lugha na matumizi ya lugha za mitaani kama zipo. Katika mazingira mengine, mathalani fasihi ya watoto, mwandishi anaweza kutumia lugha nyepesi yenye michoro, katuni, picha na vielelezo vingine kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa wepesi zaidi.

(g) Wahusika na uhusika wao

Wahusika ni kipengele muhimu kwa sababu hutumika kufikisha dhamira au ujumbe unaopatikana katika matini teule. Katika riwaya au hadithi fupi, wahusika hutajwa bayana wakibeba matukio au kutambulisha mandhari ya kifasihi. Ujitokezaji huu huwa tofauti katika tanzu nyingine. Kwa mfano, katika tamthiliya, wahusika wanaweza kutajwa bayana au kutajwa katika makundi wakibainisha sifa, mienendo na matendo ya kila kundi. Katika ushairi, isipokuwa utendi, wahusika hawatajwi na mara nyingi, wanaweza kujengwa kitaswira. Mtathmini wa usanifu wa maandishi anatakiwa kuangalia jinsi mwandishi alivyowaumba wahusika na kuwabebesha majukumu katika matini yake.

(h) Mandhari

Mtathmini anatakiwa kubainisha mandhari yaliyotumika kwenye matini. Kama ulivyojifunza awali, mandhari ni sehemu na wakati ambapo matukio ya kifasihi yanafanyika. Mandhari hayo yabainishwe kama ni halisi au ya kubuni. Masuala mengine ya kuzingatia katika mandhari ni kuchunguza suala la wakati na mahali palivyo.

(i) Uwiano wa ujumbe na mbinu za kisanaa

Katika sehemu hii mtathmini wa kazi ya kisanaa hutathmini namna mbinu teule zilivyosaidia kufikisha au kutofikisha ujumbe. Kadhalika, mtathmini huchunguza upungufu wa mbinu hizo na kupendekeza mbinu nyingine.

Yafuatayo ni matini ya kisanaa kutoka sehemu ya shairi la "Kiswahili" pamoja na tathmini ya kiusanifu.

Kiswahili

Titi la mama // tamu, hata likiwa la mbwa,
Kiswahili naazimu, sifayo inayofumbwa,
Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
Toka kama chemchemu, furika palipozibwa,
Titi la mama // tamu, jingine halishi hamu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 174 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Lugha kama Kiarabu, Kirumi na Kiingereza,
Kwa wingi zimeratibu, mambo ya kupendeza,
Na mimi nimejaribu, kila hali kujifunza,
Lakini sawa na bubu, nikizisema nabezwa,
Titi la mama // tamu, jingine halishi hamu.

Kila mtu lugha yake, ndiye mtumishi mwema,
Lugha nyingine makeke, mviringo kuzisema,
Kila mkuu na pake, hana hadhi akihama,
Kiswahili nikuvike, joho lako la heshima,
Titi la mama // tamu, jingine halishi hamu.

Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua,
Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
Pori, bahari na mto, napita nikitumia,
Titi la mama // tamu, jingine halishi hamu.

Kiswahili kikikopa, lugha nyingine pia,
Ambazo zimenenepa, jambo hili hutumia,
Au sivyo zingetupwa, kwa kukosa manufaa,
Kiswahili kikikopa, si ila ndiyo tabia,
Titi la mama // tamu, jingine halishi hamu.

Shaaban Robert, *Pambo la Lugha* (1973)

Tathmini ya matini

Matini haya ni utanzu wa ushairi. Hili ni shairi la kimapokeo kwa sababu limezingatia urari wa vina na mizani. Kwa upande wa ufundi (usanifu), shairi hili limeundwa na beti tano, kila ubeti una mishororo minne na kibwagizo ambacho kinakaririwa kila ubeti. Vina vya kati vilivyotumika ni **mu**, **bu**, **ke**, **to**, na **pa/pwa**. Vina vya mwisho ni **bwa**, **za**, **ma** na **a**. Kila mshororo umeundwa na mizani kumi na sita. Mshairi ametumia nafsi ya tatu kwa kiwango kikubwa pamoja na nafsi ya kwanza. Mshairi ametumia lugha ya mkato. Kwa mfano, maneno "sifayo"(sifa yako) na "halishi" (haliishi). Aidha, ametumia lugha ya picha ambapo amelifananisha titi la mama na lugha. Ameonesha thamani ya titi la mama kwa kumtumia mnyama mbwa, akimaanisha kuwa, pamoja na kwamba wakati mwingine mbwa huonekana hana thamani kwa wanadamu, lakini huthaminiwa na

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 175 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mtoto wake. Hali ni hiyo kwa lugha ya Kiswahili, ambapo inaweza kuonekana haina thamani kwa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla lakini Watanzania tunatakiwa kuithamini. Mshairi ametumia misemo kama vile "Kila mkuu na pake, hana hadhi akihama" unaosisitiza umuhimu wa kukipa hadhi Kiswahili ndani ya eneo la watumiaji wa Kiswahili badala ya kuzipa hadhi lugha ngeni.

Wahusika hawakubainishwa wazi, ila inavyoonekana, mhusika mkuu ni mwandishi. Anaisifu lugha ya Kiswahili anaposema, "Lugha yangu taisifu." Wahusika wengine ni watu wasiokithamini Kiswahili. Mhusika mwingine ni lugha yenyewe ya Kiswahili. Mtunzi anaipa lugha hiyo hadhi ya "ubinadamu" kwa kutumia tashihisi "sifayo iliyofumbwa."

Ujumbe wa shairi hili unahusu lugha ya Kiswahili. Mshairi anaisifu lugha ya Kiswahili na kuiita lugha tukufu na yenye kuheshimika. Mshairi anahimiza watu kuthamini Kiswahili kama watoto wanavyothamini maziwa ya mama zao.

Zoezi la 1

1. Soma maghani yafuatayo ya Mrisho Mpoto yaitwao "Waite," kisha tathimini usanifu wa maghani haya.

Waite

Kiitikio

Waiteeeeee waiteeeee!!
Waite wakalishe chini,
Waite!
Watoe hofu kwanza aaaaaa,
Waite!
Waambie wao hawamo japo nao walikulaaaa eeeh
Waite x 10

Mjomba chutama, sisi ni waungwana;
Na muungwana akivuliwa nguo, mara nyingi huchutama.
Kuna baadhi ya michezo ukishindana peke yako, lazima uwe mshindi, lakini kwa mchezo ule uliwahitaji ili kukuongezea mashabiki na washangiliaji wenye sauti zisizokauka. Japo mwiba wa kujichoma hauna pole.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 176 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usitenganishwe na mtu wakati kuna ngalawa.

Walivyoanza mjomba hakuna aliyedhani,

Kwanza walifika mapema, mmoja wao akaandikisha jina lake kwa niaba ya wengine japo wote wana majina yao hayafanani.

Jina lako nani? Mimi.

Unatoka wapi? Kwetu.

Unakwenda wapi? Humu ndani.

Kikazi au binafsi? Nani, mimi aaaaa wakaingia!

Haujachelewa mjomba, waite.

Waiteeeeee ite waiteeeee!!x10

Mjomba ukipewa kazi ya kuosha maiti,
Siku zote wewe ni zaidi ya ndugu, wanaamini kwamba huwezi kuidhuru.
Waliingia wakajipanga kwa sauti zao,
Ya kwanza mpaka ya nne wakaanzisha mapambio, basi ikawa hivyo tu.
Watu wakilia kazi yao wanatoa pole, watu wakilia wanatoa pole.
Na waandishi kwa utashi wao wakaandika msiba umefana kweli!
Hakuna aliyelia nje ya *key*! he heheeeeeee!
Waite, mjomba; ushauri wangu, waite wakalishe chini watoe hofu kwanza.
Kisha waambie, muungwana hanuni kwa mashavu, hununa moyoni.
Wao hawahusiki, wala hawamo,
Waje tu kuwa mashahidi, kwa kuwa nao walikuwapo na walikula.
Ijapokuwa hawakujua umemtoa wapi mbuzi yule.
Ushahidi wao mjomba utakusaidia kwa vitu viwili: ya kwenye historia au kushinda kesi.
Siku zote mjomba mimi huwa nakuambia, anayekula kwa mikono miwili hawezi kushiba kamwe! *Never!*
Mimi pia nakumbuka kweli nilimuona, alikuwa mbuzi, tena mdogo tu, wala siyo ng'ombe kama wanavyodai.
Hii ni zawadi tunakupa, nenda ukale utukumbuke!
Utukumbuke!
Leo hii wanasema alikuwa ng'ombe mdogo,
Wengine eti oooho, kweli alikuwa mbuzi, lakini angekuwa, angekuwa ng'ombe.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 177 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mjomba, kuna aina tatu tu za kujibu maswali: swali kwa swali, swali kwa maelezo, swali kwa mkato.
Wajibu tu kwa mkato, alikuwa mbuzi mdogo tumemla akaisha! baaaasi!!!

Kiitikio
Waiteeeeee!
Waite wakalishe chini,
Waite!
Waite, watoe hofu kwanza aaaaaa
Waambie wao hawamo japokuwa walikula eeeh
Waite ite x10

2. Tathimini mbinu za kisanaa zilizotumika katika shairi lifuatalo.

Kifo cha Mende Wekundu
Na ujenge yako nyumba, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa na uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mipaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa ngumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu,
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake,
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

Euphrase Kezilahabi, *Karibu Ndani* (1988:33)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 178 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Tathmini kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata hapo chini:

Denge alipofika kwake, ilikuwa muda wa saa tisa. Alijinyoosha kitandani ili ajipumzishe, lakini wakati usingizi ulipokuwa ukimchukua taratibu, mlango uligongwa. Yasmin aliingia ndani na kusimama mbele ya mlango akitabasamu kama kawaida yake. Denge alisogea kwenye pembe ya kitanda akamwita, "Njoo ukae hapa." Yasmin alikaa ubavuni pa kitanda na baada ya kukaa tu, Denge alianza kumpapasa mapaja akimwuliza, "Ulikuwa wapi? Siku nyingi sikukuona.

"Niko wapi mimi au uko wapi wewe?" Yasmin aliuliza, "Kwa nini? Nilikuja Jumamosi usiku, Jumapili, Jumatatu, mwisho leo asubuhi nilikuja sikukukuta, ulikuwa wapi?"

Denge alimtazama Yasmin kama asiyemjali kitu na hapo Yasmin zilimpanda hamaki. "Unan'tazama huku unacheka, unacheka, unacheka nini kinachokuchekesha, mimi nakuuliza, wewe unan'tazama halafu unacheka, au umechoka na mimi ushapata haja yako sasa basi huna haja na mimi tena!"

"Kwa nini unasema hivyo Yasmin?"

"Nisiseme hivyo na nyinyi wanaume ndivyo mlivyo!"
"Vipi? Mnapomtaka mwanamke, mnaapa viapo vyote na mkishapata haja yenu basi. Si kweli. Si kweli gani, basi mimi leo nimekuja kukwambia mimi m..." Yasmin alisita akamtazama Denge.

"Wewe nini?" Denge aliuliza. "Mimi mjamzito."

Denge aliinuka kitandani, akakaa kitako uso umembadilika. "Unasemaje?" Yasmin alijilaza juu ya mapaja ya Denge naye alikuwa akizipapasa na kuzipuna nywele zake.

"Mbona umestuka?" Yasmin aliuliza.

"Sikustuka lakini nashangaa."

"Kinachokushangaza ni nini?"

Denge hakuwa na la kujibu, alinyamaza kimya kama mtu aliyeishiwa na maneno lakini Yasmin alikivunja kimya kilichokuwapo, "Leo unakwenda sinema?"

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 & 6 (KWANDANI).indd 179 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

"Sina fedha," Denge alijibu.

"N'takupa, mimi n'nazo."

Yasmin aliinuka na kukaa kitako, akachukua kikoba chake alichokuwa amekiweka juu ya meza. Alikifungua, akachomoa noti ya shilingi ishirini akampa Denge. "Mimi utanikuta nje ya sinema ya Malindi nakungoja."

Yasmin alipochomoa noti ya shilingi ishirini, kikaratasi kidogo kilidondoka kutoka ndani ya kile kifuko chake bila ya yeye mwenyewe kukiona. Denge naye hakukijali kikaratasi kile ila waliendelea na mazungumzo yao na baadaye Yasmin alikwenda zake.

Yasmin alipoondoka, Denge alikiokota kile kikaratasi kilichokuwa kimefinyangwa finyangwa. Alikikunjua taratibu na kwenye kikaratasi kile ziliandikwa nambari. Denge alishangazwa na nambari zile na hakujua zilikuwa nambari za nini. Alijiuliza ikiwa nambari zile ni nambari za gari, nambari za sanduku la posta au ni nambari za simu. Wivu ulianza kumjia na kufikiri labda Yasmin ana mwanamume mwingine anayeandikiana naye barua au anayepigiana naye simu. Alijaribu kuoanisha mambo mengi, shati alilomnunulia, shilingi ishirini alizomgawia, "Anapata wapi fedha?" alijiuliza. "Lazima ana mwanamume anayemhonga fedha nyingi na mimi ananilaghai tu," Denge aliwaza. Alifikiri jinsi Yasmin alivyobadilika kwa mavazi mazuri ya mitindo ya aina kwa aina anayovaa na manukato anayojipaka wakati anapokuja kwake, manukato ambayo harufu yake ilitosha kumfahamisha kwamba ni ya ghali. Aliyawaza maneno aliyoambiwa na Yasmin kwamba yeye yu mjamzito akihisi sasa amefikwa na matatizo, japokuwa hakuwa na hakika kwamba kweli Yasmin alikuwa na mimba. Aliamini kwamba baadhi ya wanawake wakati mwingine wana desturi ya "kutikisa kiberiti wasikilize mlio." Kwa hiyo, labda Yasmin alikuwa akimjaribu tu amsikilize atasema nini.

Jioni ile, Denge alienda kwenye miadi yake na Yasmin, kwa shingo upande akiwa na mchanganyiko wa mawazo na wivu, shaka na wasiwasi na aliomba kuche haraka haraka ili aanze uchunguzi wa ile nambari ambayo alihifadhi vizuri ndani ya mfuko wake wa suruali. Kutokuwa mshabiki wa sinema, kulimzidishia adha rohoni mwake na kwa muda wote walikaa ndani ya ukumbi wa sinema bila ya kuongea wala kuonesha ishara yoyote ya kuipenda au kuichukia filamu.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 180 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mchezo ulipomalizika, wakati wanaelekea nyumbani, Denge alibaki kimya ila Yasmin tu ndiye aliyekuwa akiuliza maswali "Mchezo mzuri?" "Umeupenda?" Hivi na vile.

Denge alikuwa akiguna tu kila alipoulizwa, "Humn," "Humn," "Humn." Hivyo ndivyo hali ilivyokuwa mpaka Denge alipomfikisha Yasmin nyumbani na yeye akaenda zake.

Siku ya pili, Denge alianza uchunguzi wa ile nambari na alihakikisha kwamba ile haikuwa nambari ya gari kwani ingelikuwa hivyo, basi nambari ile ingelianza na herufi fulani. Alikwenda mpaka kwenye kibanda cha simu na kuanza kukizungusha kigurudumu cha simu na alipomaliza kuzungusha nambari zote, sauti ya kike ilimjibu,

"*Police headquarters, can I help you!*"
Denge alishangaa lakini ile sauti ilimwuliza tena, "*This is Police headquarters, can I help you!*"
"*I am sorry wrong number,*" Denge alijibu na kuweka mkono wa simu chini taratibu.

Denge alifadhaika akawa hajui la kufanya amesimama nje ya kibanda cha simu akiwaza na kujiuliza, "Kuna uhusiano gani baina ya Yasmin na makao makuu ya polisi?" Inayumkinika Yasmin ana mwanamume huko."

Alijua kwamba polisi wanamtafuta sana lakini hakuwa na shaka na Yasmin hata kidogo kama angeliweza kutumiwa na polisi, kuwasaidia dhidi yake. "Lakini haidhuru, nitaupata ukweli," alijiliwaza.

Adam Shafi, *Vuta N'kuvute* (1999 uk-139-142)

Kwa kutumia kifungu cha habari cha hapo juu:

(i) Tathmini uzingativu wa kanuni za uandishi.
(ii) Tathmini matumizi ya lugha.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 181 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Tathmini jinsi lugha ilivyotumika katika tamthiliya ifuatayo:

HUKA (*anaanza kulia.*)

NGAHINYANA: Eeh! Ukweli unauma sasa...

MAMA HUKA: Aaa, Baba Huka, usimfikirie mtoto mambo mabaya.

NGAHINYANA: Hapana. Huyu mtoto amekwishaanza kuharibika. Mara nyingi, nimeandikiwa barua na babake mdogo kusema Huka hatulii, na wewe hukuamini ukasema wanaanza kumsingizia mtoto wako, mpaka tukagombana na aliyekuwa akitusomea barua zetu. (*Mara hodi inasikika*). Ehee! Sasa utaniona; nitamnyosha barabara. (*Anachukua fimbo yake iliyokuwa ikiegemea ukutani na anakwenda karibu na mlango na anainua fimbo kungojea ishuke mara tu apigaye hodi atakapoingia.*) Karibu. Fungua mlango.

MAMA HUKA : Hapana baba Huka! (*Anamshika lakini anasukumwa.*) Si vizuri.

NGAHINYANA: Sogea huko! (*Mgeni anaingia na fimbo ya mzee inashuka na kutua begani mwake*). Wewe ndiye...

PATA: (*Anaanguka kwa uchungu na barua alizozishika zinatapakaa chini.*) Ochehcheh! Mzee vipi? Nimekukosea nini? Ahaa (*Akainuka na kushika bega lake. Ndipo Ngahinyana anapogundua kosa lake. Huka baada ya kuona barua anatoka*).

NGAHINYANA: Oh! Pole sana mwanangu, sikujua kama ni wewe. Tulikuwa tunamtegemea mpumbavu mmoja. Lakini bahati yake. Pole sana mwanangu! (*Anasaidia kuokota barua*).

PATA: Loo! Pameuma. Pole tu haisaidii kitu. Mzee siku nyingine uwe na uhakika au la tutaogopa kukuletea barua zako. Unaonesha kuwa ni mkali sana!

NGAHINYANA (*Huku akicheka*): Ehe ... Ehee ... Wazee wakati mwingine huwa tuna hasira. Kuna barua yetu? Kutoka Dalisalaam?

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 182 17/03/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

PATA: Nadhani inatoka Dar es Salaam. (*Anapekuapekua barua hatimaye anaipata*). Hii hapa. Haya mzee nakwenda.

NGAHINYANA: Asante sana. Pole sana kwa kukupiga; nisamehe mwanangu.

PATA: Si kitu mzee. (*Anatoka*) Siku nyingine usinivizie nyuma ya mlango. Ningoje tuonane macho kwa macho. (*Anatoka*)

MAMA HUKA: (*Anacheka*): Hee ... he ... he ... Ooiii! Unaona sasa, nilikuambia mimi. Umempiga mtoto wa watu bure. Atapita kusema kila mahali.

NGAHINYANA: Basi na wewe ... (*Anachana barua na kuisoma.*)

MAMA HUKA: Inatoka kwa shemeji?

NGAHINYANA : Ee! *Anashtuka na kutoa macho*). Mh!

MAMA HUKA : Nini (*Anamsogelea.*)

NGAHINYANA : Mh. (*Huku akitikisa kichwa*). Sikiliza. (*Anasoma.*)

Kwa kaka mpenzi,

Natum... ma... ininy... temuwa... zi... makusu...dihasa... la...ku...waa... ndi... kiani... kuwa... aa... ri...fuma.. mbo .. fu .. lani... kuhu .. Huka. (*Anaendelea kusoma hivyo akikwamakwama*). Kwanza hakuchaguliwa kuendelea na shule. Pia, Huka, nasikitika, kuwaeleza, kuwa amebomoa nyumba ya watu. Nina maana amewagombanisha bi. na bwana Kambanga hata wameachana. (*Anaachia hapo. Anamwelekea Mama Huka*). Unaona jinsi mama yako anavyofanya. Tulikuwa tukisema sasa hivi. (*Anageuka kumwita Huka*). Unaona, alipofika yule kijana tu akatoweka. Alifahamu kuwa baba yake mdogo atatuandikia. (*Anaita tena*). Huka...Nikija huko, kweli nitakuchapa. Afadhali uje mwenyewe.

Ngalimecha Ngahyoma, *Huka* (1973)

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 183 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Faharasa

Amali Mambo ya kimila, kiimani, kiutamaduni na kisanaa yanayothaminiwa na kuzingatiwa na jamii

Bubwi Tamthiliya ambazo hazitumii maneno, bali hutumia vitendo au ishara

Balagha Hii ni tamathali ya usemi ambayo mtu huuliza jambo huku akifahamu jibu lake

Chuku Tamathali au mbinu inayotumika kwa kauli au tungo ambazo zimetiwa chumvi kwa lengo la kusisitiza au kuchekesha

Dhihaka Tamathali inayotumika kwa lengo la kumdunisha mhusika fulani kwa kutumia mafumbo

Dialojia Mbinu ya kisanaa inayotumia mazungumzo ya majibizano baina ya wahusika

Drama Maigizo yanayooneshwa jukwaani mbele ya hadhira

Falsafa Mwelekeo wa mawazo au tafakuri zinazopatikana katika kazi za sanaa

Fani Ufundi anaoutumia msanii katika kuwasilisha maudhui

Fasihi Andishi Aina ya fasihi inayotungwa na kuwasilishwa kwa njia ya maandishi

Fasihi Simulizi Aina ya fasihi ambayo uwasilishaji wa kile kilichokusudiwa hufanyika kwa njia ya mdomo; aghalabu, utunzi wake ni wa ghibu

Fasihi Sanaa inayotumia lugha kiufundi kuwasilishia masuala mbalimbali yanayomhusu mwanadamu na maisha yake

Foili Mhusika ambaye hawezi kufanya maamuzi yake mwenyewe kutokana na kuwategemea wahusika wengine kimawazo na kiakili, na aghalabu hutumika kumpambanua mhusika mkuu

Fumbo Usemi au kauli ambayo maana yake haitolewi waziwazi bali hufichwa

Futuhi Aina ya tamthiliya inayokusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema (Pia, tazama ramsa)

Hadithi fupi Simulizi ya kubuni inayosawiri tukio, tabia, mgogoro au kipengele fulani cha maisha kwa ufupi, kwa kawaida, hadithi fupi huwa na tukio moja au mawili na hutumia mawanda finyu

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hadithi Matukio yanayosimuliwa kwa mfuatano fulani wa kimantiki na kiwakati

Hekaya Ngano zenye visa visivyo vya kawaida vinavyoambatana na masaibu na pengine hata ujanja wa mhusika mkuu, ambaye huweza kuwa mtu au mnyama

Hurafa Ngano zenye wahusika wanyama tu ambao huwakilisha tabia na matendo ya binadamu kwa kurejelea masuala yanayopatikana katika jamii

Istiara Hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana iliyofichika. Kwa hiyo, maana huwasilishwa kwa njia ya mafumbo.

Itikadi Jumla ya mfumo wa mawazo, fikra au imani inayoongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha masuala mbalimbali

Kigano Hadithi fupi ya fasihi simulizi ambayo hutolewa kwa kutumia matumizi mapana ya jadi ili kuwasilisha maana

Kipera Kijitawi cha utanzu wa fasihi

Kisasili Hadithi inayoaminiwa kuwa kweli, inayoelezea chimbuko au asili ya jamii, ukoo au kundi fulani, na hufungamana na imani na miviga ya jamii

Kisasuli Hadithi yenye kueleza usuli na sababu za jambo, tukio au hali (yaani kwa nini jambo, tukio au hali iko kama ilivyo). Kisasuli hakina uzito mkubwa kama kisasili, na si lazima kiaminiwe na wanajamii.

Kitendawili Usemi mfupi wa mafumbo wenye kutumia lugha ya picha, tamathali na ishara katika kueleza jambo lililofichika

Lakabu Jina au majina ya nyongeza au ya kupanga (ambayo sio halisi) ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipa kutokana na sifa zao za kimaumbile, kinasaba, kitabia, kiujuzi au kimatendo

Lugha Njia ya mawasiliano ya kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Mfano: lugha ya maandishi, lugha ya masimulizi, lugha ya ishara, lugha ya alama na lugha ya vitendo

Maghani Tungo za kishairi zinazotongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji

Maigizo Sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuelimisha au kuburudisha

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 185 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

jamii

Majazi Tamathali ya usemi ambayo wahusika wa kazi ya fasihi hupewa majina yanayoakisi wasifu au tabia zao

Majigambo Masimulizi ya kujisifia au kujikweza kwa mtu kuhusu mambo anayoweza kuyafanya, aliyowahi kuyafanya au atakayoyafanya

Maleba Mavazi, vifaa na mapambo ya msanii anapokuwa jukwaani

Maudhui Jumla ya mambo mbalimbali yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ambayo yanajengwa na dhamira, mtazamo, falsafa, itikadi, msimamo, ujumbe, mafunzo na migogoro

Mdokezo Tamathali ambayo kwayo kitu fulani hudokezwa au huachwa bila kukamilishwa, aghalabu, kitu hicho huwa kinafahamika katika muktadha husika

Methali Semi za kimapokeo zenye hekima na busara zinazotumia sitiari kuelezea falsafa na uzoefu wa jamii fulani kwa muhtasari

Mhusika Bapa Mhusika ambaye habadiliki kulingana na wakati, mazingira au muktadha; yaani huonesha upande mmoja tu

Mhusika Duara Mhusika anayebadilika kulingana na wakati, mazingira au muktadha

Mhusika Kivuli Mhusika ambaye hutajwa tu katika kazi ya fasihi bila kutolewa maelezo ya kutosha

Mhusika Shinda Mtendaji au kiumbe anayetumiwa na fanani au mwandishi katika kazi ya fasihi ili kukamilisha jukumu fulani la kiploti na kumpambanua mhusika mkuu

Miviga Sherehe au shughuli za kijadi zinazofanywa na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka au katika muktadha maalumu

Monolojia Mbinu ya kisanii ambayo hutumia mtu mmoja anayejitokeza zaidi katika kusimulia hadithi. Pia, monolojia huweza kujitokeza wakati mhusika anapozungumza mwenyewe na nafsi yake

Msimu Usemi ambao huzuka kwa kipindi fulani kisha hutoweka. Msimu huambatana na matukio, mambo au shughuli zinazotokea katika jamii

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 186 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mtazamo Namna au jinsi mtu anavyochukulia kitu au jambo kisiasa au kiuchumi

Mtindo Kipengele cha kifani kinachohusu upekee au utofauti wa msanii unaojitokeza katika kazi ya fasihi na hutokana na matumizi ya lugha na vielelezo. Mtindo humtofautisha msanii mmoja na mwingine katika kazi moja na nyingine

Muundo Kipengele cha kifani kinachohusu umbo au mwonekano wa kazi ya sanaa

Muundo rejeshi Mpangilio wa visa na matukio wenye kuchangamana au kurejeleana

Muundo wa Msago Mpangilio wa moja kwa moja wa visa na matukio

Muundo Kipengele cha kifani kinachohusu umbo au mwonekano wa kazi ya sanaa

Mhusika mviringo Mhusika ambaye hubadilika au kukua kulingana na wakati, mazingira na muktadha

Nahau Misemo ya picha ambayo huwa na maana iliyofichika. Kwa kawaida huundwa na kitenzi na nomino

Nathari Utungo unaotumia lugha ya mjazo

Ngano Hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea na kuonya kuhusu maisha. Maudhui yake hujikita katika maadili, mahusiano na mwenendo ndani ya jamii

Ngoma Kipera cha sanaa za maonesho za jadi ambacho huhusisha uchezeshaji wa viungo vya mwili wenye mtindo na miondoko maalumu inayoambatana na muziki. Pia ni kifaa cha muziki kilichowambwa kwa ngozi

Ngomezi Fasihi itumiayo midundo ya ngoma ili kuwasilisha ujumbe

Ngonjera Mazungumzo au majibizano ya kishairi ya kusemwa yanayohusu mada fulani.

Nidaa Tamathali inayotumika kuonesha mshangao kuhusu jambo fulani

Nudhumu Istilahi inayotumika kujumuisha tungo zote za kishairi, yaani zinazozingatia urari fulani wa kisanaa

Ramsa Aina ya tamthiliya inayokusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema

Ritifaa Tamathali ya usemi inayotumika kuonesha hali

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KWANDANI).indd 187 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya kumsemesha mtu au kitu kisichokuwapo

Riwaya Hadithi ndefu ya kubuni itumiayo lugha ya kinathari (lugha ya mjazo) na yenye uchangamani wa visa, wahusika, mandhari na dhamira

Sabilia Shairi lenye mistari saba

Sanaaghibu Sanaa ambazo uzuri wake hujiegemeza katika hisia kutokana na ufundi wa lugha iliyotumika katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa

Sanaa Ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro, uchongaji, ufumaji na kadhalika

Sanifu Weka taratibu za lugha zenye kufuata kanuni zinazokubalika

Shairi Utungo wenye mishororo au mistari iliyogawanywa kwenye mafungu kadhaa unaoeleza au kuonesha kwa ufupi wazo au jambo au hisia fulani kuhusu binadamu na mazingira yake kwa lugha ya picha na mkato

Sitiari Tamathali ya usemi inayotumika kuonesha ulinganishi wa vitu au hali tofauti bila ya kutumia maneno ya ulinganishi

Soga Hadithi fupifupi za utani na ucheshi

Sokrate Mwanafalsafa wa Kiyunani aliyeishi 469-399 K.K

Taashira Tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumika kuwakilisha kitu kamili

Tabaini Tamathali za semi inayosisitiza jambo kwa kutumia maneno au kauli kinzani

Tahakiki Andiko linalochambua na kufafanua kazi fulani ya fasihi

Takhmisa Shairi lenye mistari mitano

Takriri Dhana inayotumika kuelezea hali ya kurudiarudia sauti, silabi, neno au maneno

Tamthiliya Mchezo ulioandaliwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani

Tanakali lafudhi Tamathali inayotumika kuonesha mwigo wa matamshi ya watu fulani wanaotumia lugha kwa namna fulani

Tanakali sauti Tamathali inayotumika kuonesha mwigo wa sauti za vitu mbalimbali kulingana na lengo na muktadha husika

Taniaba Tamathali ambayo kwayo jina la mtu binafsi hutumiwa kwa watu wengine wenye tabia, mwenendo hali au kazi

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI 5 NA 6 (KIWANDANI).indd 188 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sawa na ya mtu huyo

Tarbia Shairi la kimapokeo lenye mistari minne

Tarihi Hadithi zinazohusu matukio muhimu ya kihistoria

Tasdisa/Sudusia Shairi lenye mistari sita

Tashibiha Tamathali inayotumika kuelezea hali ya ulinganishi kwa kutumia maneno ya ulinganishi kama vile *kama, mithili ya, mfano wa, sawa na*, na mengine

Tashihisi Tamathali ambayo kwayo vitu visivyo na uhai na uwezo wa kutenda hupewa uwezo huo

Tasifida Lugha ya staha yenye lengo la kupunguza ukali au matusi katika kauli

Taswira Picha au jazanda inayojengwa akilini mwa hadhira anapoifuatilia kazi ya sanaa

Tathlitha Shairi lenye mistari mitatu

Tathnia Shairi lenye mistari miwili

Telemania Shairi lenye mistari tisa

Udhamini Hali ya kutoa fedha, mali au huduma ili kugharamia kazi ya fasihi

Uhakiki Dhana inayohusika na kuchambua, kufafanua, kufasili, kutathmini, na kueleza vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi

Ukumi Shairi lenye mistari kumi

Ushairi Utanzu wa fasihi simulizi ambao hutumia mizani, lugha ya mkato, lugha ya mafumbo na uimbaji au ughani ili kuwasilisha kwa hadhira maudhui yaliyokusudiwa

Utanzu Kundi linalojumuisha kazi mbalimbali za sanaa zenye kuchangia sifa fulani kuu

Utendi Utungo mrefu wa kishairi unaozungumzia kwa mapana matendo ya kihistoria ya shujaa. Mara nyingi utendi huwa na beti nyingi na mishororo mifupi na beti zenye kina cha bahari

Utenzi Utungo mrefu wa kishairi unaohusu mawaidha au masuala mengine ya kijamii

Utomelezi Matumizi ya tanzu au vipengele vingine katika utanzu mmoja

Wimbo Utungo wa kimuziki unaowasilishwa kwa kuimbwa na huzingatia mahadhi maalum

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Marejeleo Teule

Abasi, A. (1996). *Kuku, njiwa, kicheche, na hadithi nyinginezo.* Dar es Salaam: Readit Books.

Abedi, K. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau (EALB).

Abdulla, M.S. (1999). *Mzimu wa watu wa kale.* Nairobi: EALB.

Ajjemy, A. (1972). *Habari za Wakilindi.* Nairobi: EALB.

Andanenga, A. (2002). *Bahari ya elimu ya ushairi.* Peramiho: Benedictine Publications.

BAKITA. (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.

Bâ, M. (2009). *Barua ndefu kama hii.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Balisidya, M. (1975). *Shida.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press. (DUP).

Balisidya, M. (1987). "Tanzu na fani za fasihi simulizi." *Mulika* namba. 19 uk. 2-10.

Banzi, A. (1970). *Tamaa mbele.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House (TPH).

Banzi, A. (1972). *Titi la mkwe.* Dar es Salaam: TPH.

Brenn, E. W., & Johnson, F. (1921). *Mwaka katika mnyororo.* London: The Sheldon Press.

Bunyan, J. (1925). *Safari ya msafiri.* London: Society for the Promotion of Christian Knowledge (S.P.C.K).

Chachage, S. (1981). *Sudi ya Yohana.* Dar es Salaam: DUP.

Chachage, S. (2002). *Makuadi wa soko huria.* Dar es Salaam: DUP.

Diva, D.E. [Mf.] (1937-42) *Hadithi za Esopo I-III.* London: Sheldon Press.

Diva, D.E. (1949). *Msafiri katika nyumba ya sultani.* Pretoria: Gospel Publishers.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Eagleton, T. (1983). *Literary theory: An introduction*. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Farsy, M.S. (1960). *Kurwa na Doto*. Dar es Salaam: EALB.

Haggard, R. (1948). *Mashimo ya Mfalme Suleiman*. Arusha: Longman Tanzania.

Habwe, J. (2010). *Mizungu ya manabii na hadithi nyingine*. Nairobi: Phoenix Press.

Honero, N. (1980). *Matunda ya Azimio*. Dar es Salaam: DUP.

Hussein, E.(1971). *Mashetani*. Dar es Salaaam: Oxford University Press. (OUP).

Hussein, E. (1969). *Kinjekitile*. Nairobi: OUP.

Juma, M. (2012). *Diwani ya tuzo ya ushahiri*. Dar es Salaam: Mkuki na nyota Publishers.

Katalambula, F. (1965). *Simu ya kifo*. Nairobi: EALB.

Kahigi, K., & Mulokozi, M.M. (1979). *Kunga za ushairi na diwani yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Kandoro, S. (1978). *Ushahidi wa mashairi ya Kiswahili*. Nairobi: Longman.

Katama, M. (1973). *Ukiwa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa mistika*. Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (1974). *Cha mnyonge utakitapika hadharani*. Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Dar es Salaam: EALB.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwa maji*. Nairobi: EALB.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia uwanja wa fujo*. Nairobi: EALB.

Kezilahabi, E. (1976). *Dunia uwanja wa fujo*. Dar es Salaam: OUP.

Kezilahabi, E. (1978). "Utenzi wa ukombozi wa Zanzibar." *Mulika* Na. 14 uk. 45-51.

Kezilahabi, E. (1978). *Gamba la nyoka*. Dar es Salaam: EALB.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5&6 (KIWANDANI).indd 191 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kezilahabi, E. (1983). "Uchunguzi katika ushairi wa Kiswahili." *Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam: TUKI. uk. 145-165.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (1999). *Kaptula la Marx*. Dar es Salaam: DUP.

Khatibu, S. (1978). *Utenzi wa ukombozi*. Dar es Salaam: EAPH.

Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya fasihi simulizi*. Shungwaya: Nairobi.

Lihamba, A. (1985). *Hawala ya fedha*. Dar es Salaam: TPH.

Liwenga, V. (1978) *Nyota ya huzuni*. Dar es Salaam: TPH.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Massamba, D. (2003). "Utunzi wa ushairi wa Kiswahili." *Makala za semina ya kimataifa: fasihi III*. Dar es Salaam: *TUKI*. uk. 54-95.

Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa ushairi na diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: TPH.

Mazigwa, S. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*. Peramiho: Benedectines Publications.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publishers.

Mbatia, M. (2000). *Mwendawazimu na hadithi nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Mbele, J. (1993). "Mhakiki, uandishi na jamii" katika M.M. Mulokozi (Mh.) *Fasihi, uandishi na uchapishaji*. Dar es Salaam: DUP.

Mbijima, R. J. (2019). *Kurunzi*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mbijima, R. J. (2019). *Mtenda hutendwa*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa watumwa*. London: Sheldon Press.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mbogo, E. (1988). *Ngoma ya ng'wanamalundi*. Educational Services Center (ESC).

Mhando, P. (1972). *Hatia*. Nairobi: East African Publishing House (EAPH).

Mhando, P. (1984). *Lina ubani*. Dar es Salaam: DUP.

Mhina, G. (1977). *Mtu ni utu*. Dar es Salaam: TPH.

Mkuki na Nyota. (2016). *Diwani ya tuzo ya ushairi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Mnyampala, M. (1963). *Diwani ya mnyampala*. Dar es Salaam: EALB.

Mnyampala, M. (1964). *Fasili ya johari ya mashairi*. Dar es Salaam: Thakers.

Mnyampala, M. (1970). *Ngonjera za ukuta*. Dar es Salaam: OUP.

Mohamed, M.S. (1978). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: OUP.

Mohamed, S.A. (1980). *Dunia mti mkavu*. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Mohamed, S.A. (1980). *'Sikate tamaa*. Nairobi: Longman Kenya.

Mohamedi, S.A. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longman Kenya.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East African Education Publishers (EAEP).

Mohamed, S.A. (2013). *Posa ya Bikisiwa*. Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Musiba, A. (1986). *Njama*. Dar es Salaam: TPH.

Msokile, M. (1990). *Usiku utakapokwisha*. Dar es Salaam: DUP.

Msokile, M. (1992). *Kunga za fasihi na lugha*. Kibaha: EPD.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Kibaha: EPD.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki*. Nairobi: (EAEP).

Mtobwa, B. (1984). *Pesa zako zinanuka*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

Mtobwa, B. (1985). *Najisikia kuua tena*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

Mtobwa, B. (1987). *Ushindi*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muhando, P., & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na sanaa za maonyesho*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. (1997). *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Dar es Salaam: ECOL Publications.

Mung'ong'o, C. (1977). *Mirathi ya hatari*. Dar es Salaam: TPH.

Mung'ong'o, C. (1979). *Njozi iliyopotea*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. (Mh.) (1999). *Tenzi tatu za kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mulokozi, M. M., & Kahigi K. (1982). *Kunga za ushairi na diwani yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mutembei, A. (2006). "Nadharia ya fasihi simulizi na maendeleo katika sayansi na teknolojia." katika *Mulika Na. 27*. Uk. 1-17.

Mwakyembe, H. (1981). *Pepo ya mabwege*. Dar es Salaam: DUP.

Mwanakupona, M. (1858). *Utenzi wa mwanakupona*. Nairobi: EALB.

Mwengo, A. (1728). *Utenzi wa tambuka*. (Mswada) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mvungi, T. (1982). *Raha karaha*. Dar es Salaam: TPH.

Mvungi, T. (1985). *Chungu tamu*. Dar es Salaam: TPH.

Ngugi, G. (1961). *Nimelogwa nisiwe na mpenzi*. Nairobi: EAPH.

Ngahyoma, N. (1973). *Huka*. Dar es Salaam: TPH.

Ngomoi, J. (1975). *Ndoto ya Ndaria*. Nairobi: EAPH.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. (1976). "Fasihi" katika J. P. Mbonde (Mhariri). *Uandishi wa Tanzania: Insha*. Dar es Salaam: EALB.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na fasihi, sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI FASIHI F.5 & 6 (KIWANDANI).indd 194 17/09/2019 13:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

p' Bitek, O. (1973). *African's cultural revolution.* Nairobi: Macmillan.

Ponera, A. (2014). *Utangulizi wa nadharia ya fasihi linganishi.* Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ramadhani, J. (1975). "Ushairi" katika *Mulika* Na. 3. uk 1-8.

Richard, B. (2002). *Mkia wa chura.* Utah: LDS Publisher.

Robert, S. (1966). *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini.* Nairobi: Thomas Nelson and Sons Ltd.

Robert, S. (1991). *Kusadikika.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Robert, S. (1997). *Kufikirika.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Robert, S. (2010). *Mapenzi bora.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Robert, S. (2010). *Adili na nduguze.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Ruhumbika, G. (1992). *Miradi bubu ya wazalendo.* Dar es Salaam: TPH.

Saffari A, (1984). *Harusi*. Dar es Salaam: BCI Publishers.

Samwel, M. (2012). *Hadithi fupi: Nadharia, mbinu na mifano.* Iringa: Kasenyenda.

Sehoza, S. (1921). *Mwaka katika minyororo.* London: The Sheldon Press.

Seme, W. (1975). *Njozi za usiku.* Dar es Salaam: Longman.

Semzaba, E. (1988). *Ngoswe penzi kitovu cha uzembe*, Dar es Salaam: DUP.

Semghanga, F. (1988). *Teuzi za nafsi*. Dar es Salaam: DUP.

Sengo, T., & Kiango, S. (1975). *Hisi zetu 1 & 2.* Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi. Nadharia na tahakiki.* Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Shafi, A. (1979). *Kasri ya Mwinyi Fuadi.* Dar es Salaam: TPH.

Shafi, A. (1979). *Kuli*. Dar es Salaam: TPH.

Shafi, A. (1999). *Vuta n'kuvute.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

Steere, E. (1870). *Swahili tales*. London: Bell & Daldy Publisher.

Summers, H. (1989). "Literature" katika *The World Book Encyclopedia, Juz. 12:351-357.*

Taasisi ya Elimu Tanzania (1976). *Fasihi simulizi katika sekondari:* Dar es Salaam: DUP.

Topan, F. (1971). *Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili.* Nairobi: OUP.

Thomas, R. (2011). Taswira ya nyoka katika ngano za Kisambaa, Tasinfu ya umahiri katika Kiswahili M.A ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI. (1976). *Fasihi-simulizi ya Mtanzania: Vitendawili 1 na 2, Hadithi 1 na 2, Methali 1 na 2.* Dar es Salaam: TUKI.

Ugula, P. (1969). *Ufunguo wenye hazina.* London: Evans Brothers.

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa fasihi: misingi na vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publisher.

Wamitila, K. (2002). *Bin-Adam.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2010). *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi.* Nairobi: Focus Books.

Walibora, K. (2015) *Sasa nasikia sauti ya mama.* Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Waziri, A. (1944). *Kisa cha mwana wa mfame.* Nairobi: Moi University.

Wellek, R., & Warren, A. (1986). *Theory of literature.* Hormondsworth: Penguin Books.

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

ISBN 978-9987-09-024-2